Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 9 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatayo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2010

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2010/2012 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, naomba kulitaarifu Bunge kwamba Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda amesafiri kikazi kwenda Morogoro na inawezekana akarudi mchana wa leo. Kutokana hali hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza kuwa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji) atakaimu nafasi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hadi wakati huo. Ahsante. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Na. 383**

**Matatizo ya Maji Maji Kata ya Mbokomu**

**MHE. SUSAN J. LYIMO** aliuliza:-

Liko tatizo sugu la maji kwenye Kata ya Mbokomu hususan kwenye Vijiji vya Korini Kusini na Juu Tema pamoja na Vitongoji vyake ambalo halijapatiwa ufumbuzi.

(a) Je, ni lini tatizo hilo litatatuliwa?

(b) Kwa sababu vyanzo vya maji havikidhi mahitaji ya wakazi wa maeneo hayo: Je, Serikali haioni haja ya kuwa na vyanzo mbadala vikiwemo vile vya maji ardhini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo - Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa maeneo mengine ya nchi, Serikali inatekeleza programu ya Sekta ya Maendeleo ya Maji katika Halmashauri kupitia Mpango wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini. Katika mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Moshi iliidhinishiwa shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa vijiji 12 ambavyo vimechagua kutumia teknolojia ya mserereko *(Gravity Scheme)* kutoka kwenye mito ya maji iliyopo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 320.5 zimepokelewa na kazi zilizokwishafanyika ni usanifu wa miradi ya vijiji husika na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ambapo taarifa ya kazi hiyo iliwasilishwa kwa Waziri wa Maji ili kupata ridhaa ya kutangaza zabuni. Utekelezaji wa mradi huu unafanyika kwa *lot* tatu ambapo awamu ya kwanza inahusisha vijiji vya Korini Kaskazini na Korini Kusini vilivyoko katika Kata ya Mbokomu. Mradi huu ukikamilika, utaondoa tatizo la maji katika Kata ya Mbokomu na maeneo mengine ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Halmashauri imetenga shilingi milioni 704.7 kupitia mpango wa Sekta ya Maji kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji hivyo 12 vilivyochaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine inayotekelezwa ndani ya Halmashauri ni Kirua Kahe *Water Supply* ambapo ujenzi unatagemea kukamilika Desemba, 2011. Kutakuwa na *extension* tatu zitakazotekelezwa kuanzia Aprili, 2012. Katika mradi huu kuna makubaliano kati ya Halmashauri na Mhisani aitwaye KfW Shirika la Ujerumani ambalo litahisaini mradi huo kwa gharama ya shilingi bilioni 3.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa vijiji nilivyovitaja hapo juu walihamasishwa na kuelimishwa kuhusu uchangiaji wa ujenzi wa miradi ya maji na kuhusishwa kuchagua technolojia inayowafaa na watakayoweza kulipia gharama za uendeshaji ambapo vijiji vyote 12 vilichagua teknolojia ya serereko. Hivyo, kwa kutumia mbinu shirikishi, wananchi wenyewe wanapewa nafasi ya kuamua teknolojia inayowafaa kwa kuzingatia dhana au uchangiaji na huduma za maji katika jamii. Vyanzo vya maji vinavyotumika kwa sasa ni Mto Mrusunga na uwezo wa chanzo hiki ni lita 44 kwa sekunde.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu sana na hata Naibu Waziri wa kipindi kilichopita Mheshimiwa Chiza aliwahi kwenda miaka mitatu iliyopita na akaahidi tatizo hilo litakamilishwa, lakini mpaka leo bado na swali langu bado halijajibiwa kwa sababu nimeuliza ni lini tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi? Kwa hiyo, nilikuwa nataka jibu la hilo.

Pili, kwa kuwa mila na desturi za Wachaga ni pamoja na kufuga mifugo ya ndani, yaani hawatoi mifugo yao nje, na kwa maana hiyo, tatizo la maji ni kubwa sana, vile vile ikizingatiwa kwamba maeneo hayo kwa sasa hivi wazee wengi ndio wapo: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba tatizo hilo ni kubwa sana na kwa hiyo, inabidi wawapatie maji hasa ikizingatiwa Mto Mrusunga ambao ni chanzo kikuu kwa sasa hivi hauna maji kabisa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba Halmashauri ya Moshi inatekeleza huu mradi kupitia *program* ya maji na imefikia hatua nzuri na mpaka sasa wameshatangaza *tender* ili kuweza kupata mkandarasi atakayeendelea kujenga katika awamu ya kwanza. Nimesema kwamba tuna bahati kwamba Shirika la Ujerumani limekubali kufadhili mradi huu kwa shilingi bilioni 3.7 na watafanya kwa awamu. Kwa hiyo, nina uhakika katika muda mpaka tufikie 2015 tatizo hili la maji litakuwa limekwisha. Maeneo mengine tutaendelea kuyapanua jinsi uwezo wa fedha utakavyokuwa unapatikana.

Kuhusu Mto Mrugusunga ni kwamba maji ya mto ule yanatosha kwa kipindi cha masika. Lakini wakati wa kiangazi kuna tatizo la uharibifu wa mazingira, kwa hiyo, maji hupungua. Namwomba Mheshimiwa Lyimo asaidie pia kuhamasisha wananchi kuhifadhi mazingira ili tuwe na

maji endelevu na vyanzo vyetu vya maji viwe vinaweza kukidhi kwa muda wote wa mwaka mzima. *(Makofi)*

Na. 384

**Kupandishwa kwa Mipaka ya Wilaya**

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA** aliuliza:-

Kulikuwa na suala la kupindishwa kwa mipaka ya Wilaya wakati Wilaya ya Chato ikimegwa toka Wilaya kongwe ya Biharamulo hususan katika Kijiji cha Nyantimba na taarifa za awali zilipelekwa TAMISEMI.

Je, nini hatma ya suala hilo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa - Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 Serikali kupitia Tangazo Na. 337 ilitangaza kuundwa kwa Wilaya mpya ya Chato ambayo ilitokana na Wilaya mama ya Biharamulo. Mipaka ya Wilaya iliyowekwa ni ya asili kwa kutumia mito na milima. Aidha, tangazo hilo lilionyesha kuwa Kijiji cha Nyantimba ni kimoja na kipo katika Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 Serikali ilitoa tangazo la Serikali Na. 205 lilitangaza orodha ya vijiji vilivyokuwa vimesajiliwa na kuonyesha kuwa Kijiji cha Nyantimba kipo katika Wilaya zote mbili za Biharamulo na Chato isipokuwa tofauti pekee ni kwamba Kijiji cha Nyantimba kwa upande wa Biharamulo kina vitongoji vinne na kwa upande wa Wilaya ya Chato kina vitongoji vitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkanganyiko huu unatokana na tofauti iliyopo kati ya mpaka wa Wilaya na mpaka wa Jimbo la Uchaguzi la Chato. Serikali ilipoweka mpaka wa Wilaya ya Biharamulo na Wilaya mpya ya Chato haikuzingatia mpaka wa Jimbo, hivyo kuna sehemu ya Jimbo la Uchaguzi la Chato ambayo ilibaki upande wa Biharamulo na ni sehemu hii ambapo Kijiji cha Nyantimba kinapatikana.

Aidha, kuna makosa ya kiuchapaji ambayo yalifanyika katika matangazo ya Serikali ya kukitaja Kijiji cha Nyantimba kuwepo katika Wilaya zote mbili wakati siyo sahihi, kwani kipo kijiji kimoja tu cha Nyantimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, itawasilisha tena jambo hili kwa Tume ya Uchaguzi ili iweze kurekebisha mpaka wa Jimbo la Uchaguzi la Chato uendane na mpaka wa Wilaya ya Chato. Aidha, Serikali italifanyia pia marekebisho tangazo la Serikali Na. 205 ili kuondokana na kasoro zilizopo.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri ameonyesha kabisa kwamba Serikali imejichanganya na ilichapisha matangazo haya kimakosa:-

(a) Je, Serikali haoni kwamba kipengele cha kwanza cha tangazo la Serikali Na. 337 lilikuwa sahihi kwa kupatia kijiji hiki Wilaya ya Biharamulo?

(b) Kwa kuwa jopo la watalaam lilikaa na nyaraka zikaletwa TAMISEMI zikibainisha kabisa kijiji hiki kinapaswa kuwa Wilaya ya Biharamulo na siyo Chato: Je, haoni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kupitia nyaraka na kutoa tamko katika Bunge hili kwamba kijiji hiki kinapaswa kirudi Biharamulo na siyo Chato?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba *GN* hizi zote karibuni zimechanganya. *GN 337* yenyewe inagawa Wilaya ya Chato na Wilaya ya Biharamulo hiyo ni Wilaya. *GN 205* imegawa Vijiji na Kata. Napo hapo kuna mchanganyiko. *GN 190* ambayo imetaja Halmashauri ya Wilaya ya Chato Kijiji cha Nyantimba kiko katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato. Sasa kwa kuwa nyaraka zote hizi ziko TAMISEMI na kwa kuwa Kijiji cha Nyantimba sasa hivi kinapata huduma zote kutoka Chato, ni vyema na ni busara tukapitia zile nyaraka zote, lakini tukarudia pia kwa wananchi kuwauliza kwamba ni vyema wachague kwamba: Je, waende Biharamulo au Chato? Ikishindikana, ndipo hapo Serikali itaingilia kati ili kulitatua jambo hili moja kwa moja.

Na. 385

**Ujenzi wa Barabara ya Nzega – Tabora**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (k.n.y. MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA)** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya lami kutoka Mji wa Nzega – Tabora?

(b) Katika ujenzi wa barabara hiyo: Je, itahusisha ujenzi wa kilometa 10 za barabara ya lami kwenye barabara za Mjini Nzega na ni lini ujenzi utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrew Kigwangalla - Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tayari Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya lami kutoka Nzega hadi Tabora. Ujenzi wa barabara hii umegawanywa sehemu mbili zenye makandarasi wawili tofauti, Nzega – Puge (km 58.8) na Puge - Tabora (km 56.1). Makandarasi wote wawili wamekamilisha zoezi la kukusanya na kuandaa vifaa *(mobilization)* kujenga makambi ya miradi na kufunga mitambo ya kusaga kokoto na sasa wako katika awamu ya kusafisha eneo lote la ujenzi *(site clearance)* kwa kazi kubwa za udongo zinazofuatia.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya ujenzi wa barabara hii haihusishi ujenzi wa kilometa 10 za barabara zilizopo katika Mji wa Nzega ambapo zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mikataba ya Ujenzi katika barabara ya Nzega haihusishi zile barabara zilizopo katika eneo la Wilaya ya Nzega: Je, Serikali ina mpango gani kusaidia kuboresha barabara hizo ambazo ni muhimu sana kwa wananchi wa eneo hilo la Nzega? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zilizomo katika Mji wa Nzega kama nilivyosema katika jibu langu la msingi zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, lakini vile vile pamoja na kwamba barabara hii mpya haitahusisha ujenzi wa hizo kilometa 10 za barabara ndani ya Mji wa Nzega, napenda kumhakikishia Mheshimiwa na wananchi wa Nzega kwamba barabara hii mpya itabadilisha kabisa sura ya Nzega ikishakamilika kwa sababu kwanza barabara hii kubwa itaanzia/itaishia Mjini Nzega.

Pili, tunajenga *by pass* au barabara ya mchepuo kutoka kwenye barabara kuu inayotoka Singida kuja Shelui hadi Nzega yenye kilometa sita kuanzia sehemu moja inaitwa Kitangili na kuja mpaka sehemu inayoitwa Kazengwa kwenye barabara sasa mpaka ya kutoka Nzega kwenda Tabora na mtandao huu nina hakika utaipa Nzega sura mpya kabisa. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Kwa kuwa pia Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Singida Mjini – Ilongelo – Mtinko, Nkungi, Kidarafa mpaka Haidomu, na kwa kuwa kwa kuanzia aliahidi kutenga bajeti ya mwaka huu angalau kilometa 30 zianze kujengwa kwa kuwa kwenye bajeti hii haikuonekana: Je, Serikali inaweza kutuhakikishia bajeti ijayo watatenga kuanza kujenga kilomita 30 alizoahidi Mheshimiwa Rais kwa kuanzia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kabisa ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini kwa sababu alizotoa Mheshimiwa Rais kwa kipindi cha miaka mitano, ahadi tutaitekeleza katika kipindi hicho.

Na. 386

**Mpango wa Kujenga Barabara kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO** aliuliza:-

Ilani ya uchaguzi ya CCM (2010-2015) imeainisha kwamba barabara ya Makurunge – Matipwili – Saadani – Pangani – Tanga itajengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, mradi huo imefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo - Mbunge wa Chalinze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa Malindi – Mombasa – Lunga Lunga (Horohoro) kwa upande wa Kenya na Tanga – Saadani – Matipwili – Makulunge –Bagamoyo kwa upande wa Tanzania ni moja kati ya miradi inayotekelezwa chini ya ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na nchi za Tanzania na Kenya.

Mkataba wa kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni ulisainiwa tarehe 17 Januari, 2011 kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Kampuni ya Kihandisi ya *Aurecon AMEI* ya Afrika Kusini kwa gharama ya dola za Marekani (*USD* 2,294,646.25) ambazo ni fedha za msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu zinaendelea na zimepangwa kukamilika mwishoni mwaka mwaka 2012.

**MHE. SAIDi R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda niulize maswali madogo mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa barabara inayojengwa itapita sehemu ya Mto Wami kwenye Kijiji cha Matipwili na kwa kuwa wakazi wengi wa Kijiji cha Matipwili hulima ng'ambo ya pili ya Mto Wami, kwa hiyo, kulikuwa na juhudi za makusudi za kujenga *belly bridge,* yaani daraja linalojengwa kwa chuma. Nilitaka kufahamu na wananchi wanataka kufahamu kwamba: Je, mpango huu umeishia wapi?

Swali la pili, kwa kuwa pia wananchi wanafahamu kulikuwa na mazungumzo mahsusi baina ya Wizara mbili, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Maliasili na Utalii wa ama barabara hii ipite kwenye Hifadhi ya Taifa Saadani au ichepuke hifadhi na kupitia maeneo ya Gongo, Mkange na kadhalika. Je, Serikali inasemaje kwenye suala hili pia? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningemwomba Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala la ujenzi wa *belly bridge* kwa wakulima wa Wami atuletee tena kwa kuzingatia Kanuni ya 45 ya Kanuni zetu ili liweze kujibiwa vizuri na nina uhakika wenzetu wa TAMISEMI wanalielewa vizuri sana hilo swali.

Swali la pili kuhusu wapi barabara itapita, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya ujenzi wa barabara haujaanza, tunaanza na upembuzi yakinifu, upembuzi ambao una-*involve* utafiti wa kina wa mazingira na kuweza kuzingatia maeneo ya barabara

kupita. Naomba kumhakikishia tu kwamba masuala haya anayoyaeleza Mheshimiwa Mbunge ya kupitia katika hifadhi au kutokupitia yanazingatiwa kwa sasa hivi katika kipindi hiki cha upembuzi yakinifu na hatimaye katika usanifu wa kina.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Dodoma-Babati mwaka huu wafedha haikutendewa haki kwani takribani kilomita 160 hazikutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami na kwa kuwa abiria wengi wanaopita barabara hiyo wamekuwa wakiteseka, magari yao yanaharibikia njiani, hawafiki mwisho wa safari: Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatuambia ni lini barabara hiyo itakamilika kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Dodoma - Babati siyo kwamba haikutendewa haki, tumeizingatia katika bajeti hii vile vile kwa sababu tayari kama tulivyokwisha kusema na katika hotuba Waziri wa Ujenzi kwamba kipande cha barabara cha Dodoma - Mayamaya na kutoka Bonga kwenda Babati, ujenzi umeshaanza na makandarasi wapo na tayari katika mchakato wa kusaini mikataba kwa ajili ya pesa za ujenzi, kwa ajili ya kipande kilichobaki cha Mayamaya kwenda Bunga. Kwa hiyo, suala kwamba haikutendewa haki, kwa kweli halina msingi.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niulize swali dogo la nyongeza kuhusu barabara ya Dodoma - Babati. Kwa kuwa barabara nyingi zilizoko kwenye ahadi ya Rais huwa zinatengewa bajeti ndogo ndogo kwa miaka ya nyuma kwa barabara ya Dodoma - Babati kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 kwa kuona umuhimu wake, iliongezewa Shilingi bilioni 45. Sasa pamoja na ziada ya bajeti, bajeti ndogo ndogo zilizokuwa zinatengwa huko nyuma, ni kwa nini basi bajeti hizo za nyongeza na iliyotengwa mwaka huu isiendeleze kwa haraka barabaraba hasa hii ya Dodoma - Babati kwa kufuata umuhimu wake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongelea hapa mchakato wa ujenzi wa zaidi ya kilomita 11,300 wa barabara zote zilizopo nchini hapa ambazo zina umuhimu unaolingana. Kwa hiyo, suala la kutoa kipaumbele pengine kinachozidi barabara nyingine kwa barabara ya Dodoma – Babati, kwa kweli hilo angetuachia watendaji tuweze kulikamilisha. Hiyo barabara itajengwa kama ambavyo barabara nyingine zote tulizoahidi kwamba zitajengwa.

Na. 387

**Kuboresha kanda maalum ya kipolisi ya Tarime-Rorya**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Kutokana na kukithiri kwa uhalifu katika Wilaya ya Tarime na Rorya, Serikali ilianzisha Kanda Maalum ya Kipolisi ya Tarime Rorya ili kuzuia uhalifu na kurudisha amani na usalama katika maeneo yao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za Polisi na watumishi wengine na mpango huo utakamilika lini?

(b) Je, Serikali itaboresha lini Ofisi za Wilaya za Polisi za Nyamwaga, Sirari na Tarime Mjini ili ziwe na hadhi stahili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine - Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kujenga na kuboresha makazi ya askari nchi nzima. Zoezi hilo linatekelezwa kwa awamu kadri tunavyopata fedha kutokana na

bajeti ya Serikali, mikopo kutoka mashirika ya fedha na vyanzo vingine (kama michango ya wananchi na mashirika ya kimataifa). Na mpango huu ni endelevu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itajenga ofisi za Polisi Wilaya ya Tarime katika mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, Ofisi za Wilaya za Sirari, Nyamwaga zimepangwa kujengwa ifikapo mwaka 2015.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu ambayo hayaridhishi kwa kiasi kikubwa, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, licha ya Wilaya ya Tarime kuwa na Mkoa Maalum wa kipolisi wa Tarime - Rorya, bado kuna tatizo la mauaji, uhalifu, ujambazi na ujangili. Je, Naibu Waziri anasema nini? Haoni kabisa kwamba Kanda Maalum hiyo au Mkoa Maalum wa Kipolisi umeshindwa kazi yake?

Swali la pili, barabara ya Tarime inayopita Sirari mpaka Mwanza ina vizuizi vingi sana vya polisi takribani 42 na hao polisi badala ya kulinda mali ya wananchi wanawazuia wananchi wanaosafirisha mazao kutoka Mwanza kuelekea Tarime? Hali hii inasababisha rushwa kubwa sana, polisi wanapokea rushwa. Naibu Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na vizuizi hivyo 42?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya mauaji, uhalifu, wizi wa ng’ombe na kadhalika, haya ni masuala ambayo kwa kuwa Serikali tupitia Jeshi la Polisi tumejitahidi kadri tuwezavyo kukabiliana na hali halisi. Lakini ndiyo maana tunasema kwamba lazima pawepo na elimu ya kutosha kwa wananchi. Lakini pia pawe na ushirikiano mkubwa kati ya Jeshi la Polisi na wananchi na kama zitakuwepo taarifa na kama kutakuwa na mitandao ambayo inafanya mambo kama haya inajulikana, kwa kweli hatua zitachukuliwa. Lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba hawezi akasema kwamba hii ni kazi ya Polisi peke yake. Hii ni kazi yetu sisi sote na yeye akiwemo na wananchi husika wakiwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, anasema kwamba katika barabara alizozitaja yeye Mheshimiwa Mbunge, kuna askari wengi wanatoza rushwa na mengine na kadhalika. Hii tumekuwa tunaisema mara kwa mara, ni kwamba tunaomba ushirikiano na ningependa tuzungumze na Mheshimiwa Mbunge na kama kweli ana majina ya askari ambao wanafanya mambo kama hayo, hatutachelea kuchukua hatua. Kwa sababu hapa tumekuwa tunachukua hatua pale ambapo tumebaini kwamba askari wamekuwa wakienda kinyume na taratibu au mwenendo wao wa kazi na ikiwemo vitendo kama hivi vya kuchukua rushwa au vitendo vya kudhalilisha wananchi ama vitendo vya kuwanyang’anya wananchi mazao yao, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo kwamba askari wameshindwa au Jeshi la Polisi limeshindwa, lakini tunataka ushirikiano, ndiyo maana nazungumzia juu ya ulinzi shirikishi.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kanda hii maalum ya kipolisi ya Rorya na Tarime inao upungufu mkubwa sana wa vitendea kazi kama magari na pikipiki, na kwa kuwa kanda hii ya kipolisi imeonyesha upungufu mkubwa sana wa utendaji wa kazi kutokana na upungufu wa vifaa hivyo: Je, Wizara ina mpango gani wa kuipatia kanda hii ya Tarime na Rorya vifaa kama magari na pikipiki ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumekiri hata katika bajeti ambayo tumeitoa majuzi ni kwamba upo upungufu wa vitendea kazi na hii siyo katika maeneo ambayo ameyataja yeye, lakini pia yako maeneo mengi nchini ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa wamekuwa wakiyazungumzia. Namhakikishia kwamba kadri tutakavyokuwa tunapata fedha na uwezo utakavyokuwa unaruhusu, ndivyo tutakavyokuwa tunatoa vitendea kazi. Lakini kuhusu hali halisi ya Mkoa maalum huu wa Tarime - Rorya ni kwa sababu ya matatizo yao. Tutajitahidi kadri tuwezavyo kuupa kipaumbele.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mazingira ya kijiografia ya Wilaya ya Tarime yanafanana sana na yale ya Wilaya ya Tunduru kwa sababu Wilaya hizi zote ziko mpakani. Kwa kuwa tumekuwa tukichangia kwa maandishi na kwa kuongea hapa Bungeni juu ya mazingira magumu sana kwa nyumba za askari wa Wilaya ya Tunduru: Je, Waziri atakuwa tayari kuja mwenyewe Tunduru kujionea mazingira

magumu sana ya askari wetu wa Jeshi la Polisi na Magereza pale Tunduru ili aweze kufanya mipango yoyote ya fedha kuwanasua askari hawa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwamba matatizo aliyoyataja kwa maeneo ya mpakani yanatukabili kama nchi, kama Taifa na nitakuwa tayari, tutapanga, nitakwenda Tunduru na kwa kweli tulikuwa tumepanga tu. Kuna maeneo mbalimbali ambayo tulitaka tuyatembelee na kwa hiyo na Tunduru ikiwemo tuko tayari kwamba tutakwenda kutazama hali halisi.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu niulize swali dogo la nyongeza. Nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kama ana takwimu zozote za wananchi wa Wilaya ya Tarime ambao wameuawa na Jeshi la Polisi tangu kanda maalum ya Rorya na Tarime ilipoanzishwa. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni swali jipya. Kama Mheshimiwa Tundu Lussu anazungumzia *statistics,* kwa kweli siwezi kumpa *out of hand.* Tutalifanyia kazi na tutampatia.

Na. 388

**Ukarabati wa Majengo yaliyoko Laini Wete**

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI** aliuliza:-

Lengo la kuwapatia makazi Askari Polisi na Magereza ni kuwafanya waweze kutoa huduma zao vizuri. Majengo yaliyoko Laini Wete ambayo yalikuwa yamejengwa kwa malengo hayo, yako katika hali mbaya:-

(a) Je, ni lini ukarabati mkubwa utafanyika ili kuyaweka majengo hayo katika hali nzuri?

(b) Je, ni majengo mangapi katika eneo hilo ambayo yanakaliwa na askari husika na mangapi yameuzwa na kwa sababu zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Magereza, lipo Tanzania Bara tu na kule Zanzibar ni Chuo cha Mafunzo, kwani suala la Magereza siyo suala la Muungano.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa majengo yanayomilikiwa na Jeshi la Polisi tunao mpango wa kukarabati majengo ya zamani pamoja na kujenga majengo mapya kwa ajili ya Askari Polisi nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha. Mpaka kufikia mwaka 2015 tutakuwa tumekarabati majengo yote chakavu yakiwemo ya Laini ya Polisi Wete.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika laini hiyo, majengo yanayokaliwa na Askari Polisi ni saba. Sita yakiwa ya ghorofa moja na moja la ghorofa mbili na hakuna lilouzwa.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini napenda nimfahamishe kwamba, naelewa kwamba Magereza hayako Pemba wala Zanzibar isipokuwa kuna Chuo cha Mafunzo na ndiyo maana sikuuliza juu ya Gereza lililoko kule ambalo liko chini ya eneo hilo alilolizungumza. Nina swali moja ambalo nataka kupata ufafanuzi. Eneo lile la Laini, yako majengo ambayo siyo ya ghorofa: Je, majengo hayo hayako chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani?

Halafu ziko nyumba ambazo zimeanguka na zipo zilizojengwa ambazo hazimilikiwi na Askari wa Polisi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumesikia tetesi kuhusu hali ya majengo na kadhalika na Mheshimiwa Waziri amepanga baada ya kikao hiki cha Bunge, atafanya ziara huko Pemba na kutazama hali halisi na ningependa Mheshimiwa Mbunge labda angeweza kushiriki tuone hali halisi inayojitokeza pale na nini ambacho tunaweza tukafanya kwa upande wetu.

Kwa hiyo, nimwambie kwamba upo mpango Waziri mwenyewe kwenda kutazama hali halisi na mambo mengine kuhusu vitendea kazi. Kwa hiyo, ingekuwa jambo jema kama Mheshimiwa Mbunge angeweza kushiriki pale ili tuweze kuona tumepata ufafanuzi ama ufumbuzi gani kuhusu tatizo hili.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa suala hili la majengo ya askari wetu linaulizwa mara kwa mara na bado majibu ni yale yale, na kwa kuwa makazi haya hivi sasa askari mmoja anakaa na familia kwenye sehemu ambayo ina matatizo: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatupatia ukweli wa mambo kuhusu ratiba ya matengenezo ya sehemu zote ili tusiulize tena maswali kama haya ambayo kila siku yanaulizwa? Katika chumba kimoja anachokaa askari akae na familia na watoto wangapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mnyaa, anaelewa kwamba, hata sisi hali halisi ambayo tunaiona hairidhishi, haifurahishi, haipendezi. Tungeweza kufanya ambayo tungeweza kufanya hata jana, lakini tatizo na ndiyo maana majibu yanakuwa ni yaleyale kutokana na hali halisi ya kifedha amekuwanayo. Lakini kwa mujibu wa utaratibu ambao tumejiwekea na njia ambazo tunazibuni, mbali na bajeti ya Serikali kwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha, tunajitahidi kuona kwamba, ifikapo mwaka 2015 tunajipa programu hii mpaka mwaka 2015, kuona hali ya majengo hasa hali halisi wanavyoishi askari wetu, tunaipa kipaumbele kuona kwamba tunafanya mabadiliko yanayostahiki. Kwa sababu, hata sisi wenyewe hatufurahi kwa hali ambayo wanakuwanayo.

Na. 389

**Umeme Unaokwenda Buzwagi**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Serikali ilishakubali kushughulikia suala la umeme utakaokwenda moja kwa moja kwenye mgodi wa dhahabu wa Buzwagi, na utumike pia kwa matumizi ya kawaida kwa wananchi wa Wilaya ya Kahama, hususan Mji wa Kahama, ili kuondoa kabisa tatizo sugu la umeme kukatika mara kwa mara, lakini ni kitambo sasa tangu ahadi hiyo itolewe ndani ya Bunge na hakuna dalili zozote za utekelezaji wa ahadi hiyo.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya utekelezaji wa ahadi hiyo?

(b) Je, ni lini *TANESCO* itaanza kupeleka umeme kwenye maeneo ya Mhungula, Bukondamuyo, Mwime, Somu, Lugela na Mazense, maeneo yaliyomo ndani ya Mji wa Kahama ambao kwa muda mrefu wameomba kuunganishiwa umeme bila mafanikio?

(c) Je, ni lini tatizo sugu la kutounganishiwa umeme majumbani litakwisha licha ya kuwa waombaji wamelipa gharama zote na kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli - Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kujadiliana na wawekezaji wa *Barrick Gold Mines* ili kukubaliana nao jinsi ya kugharamia upanuzi wa kituo cha umeme cha Buzwagi, ili kukiwezesha kutoa umeme wa kutosha kukidhi mahitaji ya Mji wa Kahama

yanayokadiriwa kuwa *MW 6* na wakati huo huo kutoathiri upatikanaji wa umeme katika mgodi wao wa Buzwagi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, upelekeaji wa umeme kwenye maeneo yaliyomo ndani ya mji wa Kahama kutokea ulipo Mgodi wa Buzwagi, utahitaji ujenzi wa njia ya umeme yenye msongo wa *KV* 33 yenye urefu wa kilometa nane na uwekaji wa *Transformer* ya *220/33Kv.* Gharama yake inakadiriwa kuwa kama shilingi bilioni 10. Wizara yangu ikishirikiana na *TANESCO* itaendelea na jitihada za kutafuta fedha ili kuyapatia huduma ya umeme maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na maeneo mengine yasiyo na umeme katika Mkoa wa Shinyanga na nchini kwa ujumla.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ya kuridhisha ya upatikanaji wa vifaa kwa sasa, mwombaji wa umeme aliyelipia hupata huduma hiyo ndani ya muda unaostahili. Mwanzoni mwa mwaka 2010, *TANESCO* ilianza mpango wa kuboresha huduma zake kwa wateja iliyojulikana kama Mkataba wa huduma bora kwa wateja *(Customers Service Charter).* Kwa hiyo, iwapo kuna mwananchi aliyekwishaomba na kulipia bila kupatiwa huduma ya umeme, basi awasiliane na uongozi wa *TANESCO* ulio karibu naye kwa hatua zaidi.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo hayaashirii matumaini ya wananchi wa Mji wa Kahama, kufaidi matunda ya kuwepo kwa Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri katika jibu lake la swali langu (c) amesema kwamba, kuna Kitengo cha Huduma kwa Wateja pale Kahama; na kwa kuwa nimeuliza swali hili zaidi ya mara tatu ndani ya Bunge hili Tukufu, ni dhahiri kwamba, kitengo hicho hakifanyi kazi kama inavyotakiwa na badala yake, kazi hizo nizifanye mimi kwa wateja wa *TANESCO* kuja Ofisini kwangu mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kuja Kahama, angalau kwa siku moja kufanya hiyo kazi ya huduma kwa wateja na kuwapatia suluhu ya matatizo yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba haya makubaliano ya kuboresha ile *Sub-station* ya Buzwagi, yanachelewa kidogo. Baada ya Mgodi wa Buzwagi kuingia pale, Mji wenyewe wa Kahama na maeneo yale yanayozunguka ya Mwendakulima na Chapua kule na wapi, yameongezeka mahitaji yake, kwanza kwa wakazi wameongezeka, lakini pia na mahitaji ya umeme yameongezeka. Kwa hiyo, ukilinganisha na yale mahitaji ya 1980 wakati laini ilipoingia kutoka Ibadakuli mwanzoni, mahitaji yalikuwa ni *MW* mbili tatu. Sasa hivi ni *MW* 6. Lakini ni kweli anavyosema Mheshimiwa James Daudi Lembeli, unaoingia ni *MW* kama nne, kwa hiyo, haiutoshi, ndiyo maana inatokea kukatikakatika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, *solution* ni *Sub-station* lakini *solution* kubwa zaidi ni kupatikana kwa umeme wa *gridi* unatoka Shinyanga kupitia Shinyanga, kupitia Singida, ili Kanda yote ya Ziwa ipate umeme zaidi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Lembeli kwamba, hili la kupata *Sub-station* ya Buzwagi, tutalifanyia kazi, likamilike, lakini kwa upana zaidi ni kwamba, ni lazima tupate umeme wa ziada kwa Kanda nzima ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na mimi mwenyewe, tumepanga twende Kahama na maeneo yale yanayozunguka kwa kazi za ujumla tu za ziara za kikazi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa James Daudi Lembeli kwamba, nimeshakwenda Kahama mara mbili na itakuwa ni faraja kwenda mara ya tatu. Kama tutakwenda na wahusika wa *TANESCO* ili kuboresha hii *system* ya *Customer Service Charter* ambayo kwa sasa inatakiwa ifanye kazi vizuri kwa sababu, vifaa tayari vimeshafika Shinyanga.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Hivi karibuni Serikali imeongeza bajeti ya Wizara hii kwa shilingi bilioni 95 ili kukidhi tatizo la umeme kwa wananchi ambalo limekuwa tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, napenda kujua kwamba, kwa wale Watanzania ambao hawana umeme kabisa, watanufaikaje na nyongeza hiyo ya Wizara ya Nishati na Madini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza iliyopatikana kwenye bajeti, labda niseme tatizo la umeme la Tanzania tumeshalibaini kwamba, kwanza hili la *access* 14%, 15% ya Watanzania ndio wanaofikiwa na umeme sasa hivi. Lengo kwa miaka sita, saba ijayo ni kwenda kwenye 30%. Hii kazi siyo ya uzalishaji kwa maana ya *generation,* ni kazi kwanza *principaly,* ya uzambazaji. Kwa hiyo, hapo ndiyo maana nitasema nikilinganisha ile mwanzo wa swali kwenye swali la msingi, haya ni masuala ya kuboresha *Customer Service Charter* ya *TANESCO,* badala ya kuunganisha wateja kama 50,000 kwa mwaka. Wao wenyewe wamekadiria wafike kama wateja 200,000, ni changamoto kubwa. Lakini wakiweza kufika, hata wateja 100,000 au 120,000 kwa mwaka kwa muda wa miaka mitano au sita ijayo, tutafikia sehemu nzuri.

Na. 390

**Utekelezaji wa Mradi wa *Mcc* na *Rea***

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE** aliuliza:-

Miradi ya *MCC* na *REA* imefikia hatua nzuri ya utekelezaji na wananchi wanasubiri kwa shauku kubwa huko vijijini:-

(a) Je, ni lini miradi hiyo itaanza Wilayani Ludewa?

(b) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Ludewa kuhusu mpango wa kupeleka umeme katika vijiji vya Ludewa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe - Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *MCC* wa usambazaji wa umeme unajumuisha Mikoa sita ikiwa ni pamoja na Iringa, lakini Wilaya ya Ludewa haikupata mradi chini ya ufadhili wa Mpango huu. Wilaya ya Ludewa ilifikishiwa umeme kwa ufadhili wa Serikali yenyewe kupitia *TANESCO* ambapo mwaka 2008 Mradi wa kufikisha umeme Wilayani Ludewa ulianza kwa kupatiwa jenereta tatu zenye uwezo wa kuzalisha jumla ya *KW 1,270 (MW 1.2).* Majenereta hayo yalikusudiwa yafikishe umeme Ludewa Makao Makuu na maeneo yanayozunguka. Kwa sasa mahitaji ya juu kabisa ya umeme ya Mji wa Ludewa ni *KW 297.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kupeleka umeme katika vijiji vya Wilaya ya Ludewa upo chini ya mradi wa njia kuu ya usafirishaji umeme wa *KV 132,* kutoka Makambako hadi Songea. Katika mradi huo, kitajengwa kituo kikuu cha kupooza umeme chenye uwezo wa *KV 132/133* katika eneo la Madaba kwa ajili ya kusambaza umeme katika maeneo ya jirani kwenye Shamba la Ndolela na Vijiji vya Mundindi (Liganga), Shaurimoyo, Mkongobaki, Madindo, Muhoro Gereza la Ludewa na Ludewa Mjini. Vijiji vingine vitakavyofikiwa ni Lugalawa, Mlangali, Mkiu na Milo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya *KV 132* kutoka Makambako hadi Songea, yenye urefu wa kilometa 250. Njia za usambazaji umeme *KV 33* zenye urefu wa kilomita 900, usambazaji umeme mdogo na vituo vya kusambaza umeme kwa wateja na kuunga wateja wanaokadiriwa kuwa kama 8,500. Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa mradi wa Makambako – Songea, mpaka sasa ni kupatikana kwa mshauri mwelekezi

*(Consultant)* ambaye ni kampuni ya *SWECO International* kutoka Sweden, ambaye na yeye atateua Mkandarasi wa kutekeleza huo mradi, mradi utakamilika, unakadiriwa 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa mradi wa Mchuchuma awamu ya pili, unatarajia pia kuwa ni kichocheo kwa chanzo cha umeme ambacho kitaongeza upatikanaji wa umeme kwenye gridi ya Taifa na wakazi wa Ludewa. Aidha, kwa kuwa, kwenye sehemu ya miradi midogo midogo ya usambazaji wa mradi huu wa Makambako Songea, Vijiji vya Ludewa vimepangiwa kupatiwa umeme. Hakuna miradi ya *REA* iliyopangiwa kwa maeneo hayo.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri anaposema mradi huu utakuwa umekamilika, ifikapo mwaka 2014/2015, anamaanisha nini? Anawaambia nini wananchi wa Vijiji vya Ludewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa Vijiji vya Ludewa Kijijini na Luana, vipo jirani sana na Mji wa Ludewa, na sasa hivi umeme Ludewa upo mwingi. Mheshimiwa Waziri anaonaje, badala ya kusubiri huu umeme wa 2015, angalau vijiji hivi viwili vya Luana na Ludewa Kijijini, vipewe umeme? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Deo Filikunjombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilifu wa mradi huu una hatua mbili. Kwanza ni kutoka ile *transmission line* ya kutoka Makambako kwenda Songea na Songea pale ina-*branch,* kushoto inakwenda Namtumbo, kulia inakwenda Mbinga. Hiyo ni hatua ile ya *transmission line.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumesema kwamba pana kazi za usambazaji ili kuvifikia vile Vijiji na Miji ile midogo midogo inayozunguka pale, yenyewe ni hatua nyingine ambayo ina kilometa kama 900. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Deo kwamba, tutakachohimiza kwenye *terms of reference* kwa huyu Mshauri Mwelekezi wa *SWECO.* Ni kwamba, aambatanishe kwamba kazi hizi ziende sambamba, kwa sababu zinaweza kwenda sambamba. Hawa wanaweza kuwa wanapitisha laini kwa vijiji hivyo wakati njia kuu inapita ili *Sub-station* ikikamilika pale Madaba, waweze kuunganishiwa umeme badala ya kazi moja kusubiri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili ni kweli, mradi huu ulipofunguliwa Agosti, 2008 mimi mwenyewe nilikwenda, ninapafahamu vizuri. Mazingira ya pale *terrain* ya Ludewa pale Mjini na maeneo yanayozunguka ni ngumu kidogo kwa sababu pana milima milima. Lakini kule kwenye maeneo yanayozunguka huku ya Luano na Ludewa Vijijini, ni kweli kuna wateja wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelipokea hili. Tutajaribu kuangalia kama *REA* wanaweza, tulikuwanao siku hiyo Ludewa na wao wanafahamu maeneo. Tutajaribu kuangalia kwamba, kwa vijiji hivi viwili kabla ya ule mradi mkubwa haujaingia 2015 kama wanaweza kufanya kazi ambayo inakadiriwa kama Shilingi milioni 150 au Shilingi milioni 200 ya kupeleka umeme Luano na Ludewa Vijijini.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, tangu tumepelekewa jenereta katika Mji wa Kasulu na Kibondo, nimekuwa nikifuatilia kutaka kujua ni lini umeme utawaka katika Miji ya Kasulu na Kibondo? Mheshimiwa Waziri akanieleza kwamba, kufikia mwezi Julai, mwezi wa saba mwishoni, umeme utakuwa umewaka na leo ni tarehe 9 Agosti, 2011, Nilitaka nijue ni lini sasa umeme utawaka?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba, chini ya utaratibu tuliokuwa tumepanga au tumeelekezwa na *TANESCO,* umeme ulikuwa uwake mapema kidogo, lakini upatikanaji wa vifaa na ufikishaji wa vifaa Kasulu na Kibondo umekuwa mgumu kidogo. Wiki iliyopita tumepata taarifa kwamba *TANESCO* wamesema wanaendelea vizuri. Namwomba Mheshimiwa Josephine, tuwasiliane baadaye ili nipate taarifa ya leo, kwamba

kwa siku hii ya leo tarehe 9 Agosti, 2011 utekelezaji wa kazi hiyo umefikia wapi na utakamilika ndani ya muda gani?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujakwenda kwenye swali letu la mwisho la Wizara ya Katiba na Sheria kwa siku ya leo, naomba niwatangazie kwamba, Spika wetu - Mheshimiwa Anne Makinda, hayuko pamoja nasi leo, kwa sababu yuko ziara nchini Malawi, katika Bunge la Malawi ambako kuna Mkutano wa *Commonwealth Parliamentary Association,* unaohusisha Maspika wa Kanda ya Afrika. Kwa maana hiyo, kwa matatizo yoyote tuwasiliane. *(Makofi)*

Na. 391

**Marekebisho katika Sheria ya Ndoa**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza :-

Pamoja na Serikali kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali na kutunga Sheria mpya kwa zile Sheria zilizopitwa na wakati kama ilivyo Sheria ya Ndoa:-

(a) Je, Sheria ya Ndoa inasema nini juu ya matunzo na malezi ya watoto pale wazazi wanapoachana?

(b) Je, kiasi kilichopendekezwa kinakidhi matakwa ya matunzo ya watoto?

(c) Pamoja na kasoro hizo chache, lakini ziko kasoro nyingi ndani ya Sheria hiyo iliyopitwa na wakati : Je, Serikali haioni haja ya kuifanyia marekebisho au kutunga Sheria inayoendana na wakati tulionao sasa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu :-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta E. Kabati - Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ndoa, Sura Na. 29 ni Sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu kwa lengo la kusimamia masuala ya ndoa, haki ya mke na mume, kutengana au kuachana kwa wanandoa, nafuu ya wanandoa na mambo mengine yanayohusiana na ndoa, ikiwemo matunzo na malezi ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, Kifungu Na. 125 (1) na (2), Mahakama imepewa mamlaka ya kuamuru kama mtoto alelewe na baba au mama yake pindi wazazi wake wanapokuwa wameachana. Ama kama kuna mazingira tofauti yanayosababisha ulazima wa mtoto huyo kutokuwa chini ya malezi ya mazazi yeyote, Mahakama inaweza kuamuru kuwa mtoto huyo, alelewe na ndugu au chama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuamua ni nani amlee mtoto, jambo muhimu linalozingatiwa ni ustawi wa mtoto husika ikiwa ni pamoja na:-

(i) Matakwa/makubaliano ya wazazi;

(ii) Mapenzi ya mtoto kama anao uwezo wa kutoa mawazo yake mwenyewe;

(iii) Mila na Desturi za jamii ambayo wahusika wanaishi.

Aidha, Sheria inatoa dhana inayoweza kubadilika kwamba, kama mtoto yuko chini ya umri wa miaka saba, sharti awe chini ya malezi ya mama yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 129 cha Sheria ya Ndoa, kama hakuna makubaliano kati ya wanandoa, jukumu la kutunza mtoto ni la baba. Hata kama imeelekezwa kuwa mtoto alelewe na mama au mtu mwingine, matunzo ambayo mtoto anastahili kupewa ni pamoja na malazi, mavazi, chakula pamoja na elimu. Aidha, jukumu la kutunza na kuchangia matunzo ya mtoto huhamia kwa mama pale tu ambapo imethibitika kuwa baba amefariki, hajulikani aliko au hana uwezo wa kumhudumia au kumtunza mtoto.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria haijaweka kiwango maalum cha fedha kwa ajili ya matunzo ya mtoto. Hata hivyo, sheria inaelekeza kuwa kiwango kinachotolewa kwa ajili ya matunzo ya mtoto kizingatie uwezo na hali ya maisha ya mtu anayepaswa kulipia matunzo hayo. Iwapo Mahakama ina wasiwasi na mwenendo wa mtu anayeamriwa kutoa matunzo, inaweza kumuamuru mtu huyo kutoa kiasi cha fedha kitumike kama dhamana kwa ajili ya kuhakikisha ulipaji wa matunzo ya mtoto husika.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kupitia upya Sheria ya Ndoa kwa lengo la kuifanyia marekebisho. Kwa kutambua kwamba mambo ya ndoa yanahusisha mchanganyiko wa masuala ya kimila na kidini, Serikali iko katika mchakato wa kuandaa Waraka wa Serikali *(White Paper)* kwa ajili ya kukusanya maoni ya wananchi kwa nia ya kupata uwiano sawa wa mawazo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa ucheleweshaji wa kupitia sheria hiyo, umesababisha ongezeko la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, na kwa kuwa Serikali iko kwenye mchakato wa kuandaa *white paper*: Je, kwa sasa watoto hawa wanalindwa na sheria zipi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa maswali yake ya utetezi wa akina mama na watoto. Kwa sasa hivi ziko sheria ambazo pia zinamlinda mtoto. Sheria ya ndoa ikisomwa kwa pamoja na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 *(The Law of the Child)* kwa mfano, kifungu cha 44 kinafafanua vizuri zaidi kwamba mambo yanatakiwa yazingatiwe wakati Mahakama ikitoa *order* ya kumtunza mtoto. Mambo yaliyoandikwa katika kifungu cha 44 ni pamoja na, wanaangalia uwezo wa wazazi wote wawili, uwezo wa kifedha, hali ya maisha na haki za mtoto. Kwa hiyo, sheria ile ya mtoto pia inatoa ufafanuzi mzuri sana.

Kwa hiyo, Mahakama mara nyingi inasoma Sheria ya Ndoa, lakini pamoja na hayo, inasoma pia na Sheria ya Mtoto. Pia Sheria ya Makosa ya Jinai, yaani *penal code* pia kuna makosa yanayoainishwa pale na adhabu zake kuhusu matunzo ya mtoto. Kwa hiyo, sheria hizi bado zinamlinda mtoto na siyo zinamwachia tu mtoto.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sheria inasema kwamba ni jukumu la baba kumlea mtoto pale familia inaposambaratika, lakini kumekuwa na matukio mengi ya wazazi wanaume, yaani akina baba kuwadhuru watoto pale ambapo wanaachiwa. Kwa mfano, matukio ya kinababa kunyonga watoto, baba kubanika mtoto kwenye jiko la mkaa, yametokea, baba kuwachinja watoto ambayo imetokea Hanang; kutokana na matukio kama haya na akina baba wamekuwa waking'ang'ania kukaa na watoto: Serikali haioni sasa ni muda muafaka kabisa wa kuleta sheria haraka, tuibadilishe, ili inapotokea tatizo la wazazi kusambaratika, baba alazimike kutunza watoto wakiwa kwa mama kwa sababu ndiye mlezi mkuu wa watoto? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ukikumbuka yule baba naye amejinyonga kwa sababu ya kuzidiwa kipigo na mama. *(Kicheko)/(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali zuri la Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwamba kwenye *penal code,* kuna makosa hayo yameainishwa, mzazi ambaye anazembea kumlea mtoto, mzazi au mlezi ambaye anamfanyia mtoto matendo mabaya na adhabu yake imeainishwa katika *penal code* katika kifungu cha 35. Kwa hiyo, tukisoma hiyo Sheria ya Ndoa ni pamoja na sheria nyingine hizo nilizozitaja zinamlinda kabisa mtoto na adhabu zipo za kumtolea mtu yoyote yule ambaye hamtunzi mtoto kwa uzembe au kwa aina yoyote.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Sakaya, naomba tu uangalie kwenye *penal code* kifungu namba 166, 168 na 169 vyote hivi vinamlinda mtoto na sheria hizi zipo, zinatumika na wale ambao wanawafanyia watoto na wanapewa adhabu Mahakamani na jamii kwa ujumla. Jamani tuwe na moyo ule wa kupenda watoto, wengine wanafanya kwa makusudi, wengine wanafanya vibaya, lakini ni vyema mtoto wa chini ya miaka saba akalelewa na mama na siyo kulelewa na baba.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Eneo hili ni muhimu. Maswali mawili madogo ya nyongeza yataulizwa na Mheshimiwa Zaynabu Vullu na Mheshimiwa Anne Malecela.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa swali hili limeshaletwa ndani ya Bunge hili zaidi ya mara tatu, kwa awamu ya Bunge lililopita na kipindi hiki, pia limeshakuja zaidi ya mara mbili na mimi mwenyewe nimeshawahi kuuliza, na kwa kuwa sheria inamlinda mtu na sisi ndiyo tunaotunga hizo sheria na hasa ukizingatia sheria hii anayedhalilika na kunyanyasika sana ni Mwanamke na Mtoto: Je, Serikali iko tayari kushirikiana na mimi kuleta sheria hiyo humu ndani ili tuishughulikie haraka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mama na ninakerwa na hayo mambo ya uonevu kwa watoto, lakini Sheria hii ya Ndoa tumeifanyia utafiti kwanza. Tanzania ina mila tofauti, kwa hiyo, tulikwenda kwenye makabila mbalimbali kukusanya maoni yao. Baada ya kukusanya maoni, ndiyo maana tunaandaa hii *white paper* ili twende tena kwa wananchi kwa sababu sheria hii inatawaliwa pia na sheria za kimila na Sheria za Dini. Sasa tusipotengeneza hiyo *white paper* kupata maoni ya watu wengi zaidi tutakuwa tumetenda isivyo kwa Watanzania ambao wengine ni *matrinial* na wengine *partrinial*. Kwa hiyo, yote hayo yanazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi nakerwa, lakini naomba tuwe na subira, tuandike hiyo *white paper* iende kwa wananchi wa makabila yote ya Tanzania washiriki vizuri sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi mwenyewe nimefanya utafiti wa uhakika na nikaona kwamba *divorce* vyingi zinatolewa na kiwango ambacho baba anapaswa kulipa kumsaidia mama, lakini wanaume karibu wote wanaopitia *divorces* hizi na kupewa kiasi cha kulipa wengi wao hawalipi:

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka kipengele kikubwa kwamba kwa mwanaume ambaye hatatoa mchango wa kulea mtoto, achukuliwe hatua, ikiwa ni pamoja na kufungwa maisha? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ooh! Hii sasa kubwa tena. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna uzembe wa aina fulani kwa upande wa wanaume ambao mara nyingi hawapendi kutoa matunzo kwa watoto. Katika jibu langu la msingi, nimeeleza wazi kwamba, Mahakama ikiona mazingira ya huyo baba kutolipa, wanamwamuru kutoa dhamana pale Mahakamani ili mzazi awe anachukua fedha Mahakamani au kwenye Wizara ya Ustawi wa Jamii. Lakini vipo vifungu kwenye *penal code* kama nilivyosema, kifungu Na. 166, mzazi yeyote akizembea, amefanya kosa la jinai. Kifungu Na. 167, "mtu yeyote anayemtesa mtoto, amefanya kosa la jinai", adhabu zake ziko kwenye *penal code* kifungu Na. 35 wanasema kwamba, adhabu yako ni kifungo kisichozidi miaka miwili. Kwa hiyo, adhabu ipo kwa wale wanaofanya uzembe kwa njia moja au nyingine.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. Kipindi chetu cha maswali kimefikia mwisho na maswali yetu ya siku ya leo yamekwisha.

Sasa niendelee na matangazo ili tuendelee na utaratibu mwingine unaofuata. Kama kawaida tutaanza na matangazo ya wageni wetu wa siku ya leo ambapo walioko kwenye jukwaa la Spika ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Cyril Chami, Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Ndugu Joyce Mapunjo - Katibu Mkuu, ambaye ameambatana na mume wake Dkt. Mbwambo. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Pia wako Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wadau wa Sekta Binafsi pamoja na Wajasiriamali wote kutoka Viwanda na Biashara. Karibuni sana.

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami ambao ni Diwani wa Kata ya Uru Kaskazini - Ndugu Everist Mwambuli. Karibuni sana.

Pia Meneja wa *SACCOS* ya Walimu Wilaya ya Moshi Vijijini - Ndugu Bosco Simba, karibu. Katibu Ofisi ya Mbunge, Moshi Vijijini – Ndugu Martin Malya, karibu. Mpiga kura – Ndugu Filistine Willy Malya, na Meneja wa Benki inayoanzishwa ya wananchi wa Moshi Vijijini - Ndugu Kizito Primmy, ahsante sana na karibuni sana mwone kazi ya Mheshimiwa Mbunge wenu ambayo ni nzuri sana hapa Bungeni.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge Ukumbini ni pamoja na Wageni wa Mheshimiwa Lazaro Nyalandu - Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Madiwani 70 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Singida wakiongozwa na Mheshimiwa Celestina Yende - Mwenyekiti wa Halmashauri. Waheshimiwa Madiwani, aah, labda watakuwa *basement*. Baadaye watakapofika mtujulishe ili tuweze kutambua uwepo wao kwa sababu Bunge tunathamini sana Waheshimiwa Madiwani wanapotutembelea kujifunza kuona namna shughuli za Bunge zinavyoendelea. *(Makofi)*

Kwa ajili ya mafunzo, wako wanafunzi 70 kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma. Wasimame. Karibuni sana wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Jamhuri ya Dodoma pamoja na Walimu wenu mliofuatana nao, mjifunze shughuli za Bunge. Shule ya Jamhuri ni moja kati ya shule bora kabisa katika Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 30 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Kilutheri ya Emboko. Wanafunzi wa Emboko, karibu sana Dodoma. Karibuni Bungeni mjifunze namna Bunge lenu linavyofanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Bahati Ali Abeid ana watoto wake wapendwa Kurwa na Doto, popote walipo hebu wasimame. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Mheshimiwa James Lembeli – Mwenyekiti wa Kamati yake ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba Wajumbe wake, wakutane saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Lembeli – Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anawaomba Wajumbe wake wakutane katika Ukumbi Na. 219 saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa January Makamba - Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana wakutane katika Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa John Mnyika anawaomba Wabunge wote wa CHADEMA kuhudhuria kikao sa 9.00, kitakachofanyika ghorofa ya pili katika jengo la utawala Ukumbi Na. 219.

Waheshimiwa Wabunge, majuzi niliwatangazia kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa David Mchiwa Malole, amekwenda nchini Afrika ya Kusini. Mheshimiwa Malole kama upo, naomba usimame. Mheshimiwa Malole alikuwa ameitwa na *Omega Global University* ya Afrika Kusini ambako kule kwa kutambua kazi yake nzuri katika uongozi na ushiriki wa shughuli za wananchi, Chuo Kikuu kile kimemtunuku Mheshimiwa Malole Shahada ya Uzamivu *(Honorary Doctorate of Philosophy in Political Leadership)* Mheshimiwa Malole pamoja na shughuli kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika jamii na hasa katika Mkoa wa Dodoma, anamiliki shule ambayo amesomesha watoto yatima wengi na amefanya shughuli nyingi za kijamii ambazo zimetambuliwa na vyuo, kimoja wapokikiwa hiki. *(Makofi)*

Nitoa wito hapa kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wanafanya kazi nyingi na za maana sana ambazo zingeweza kutambuliwa na vyuo mbalimbali kwa shahada kama hizi. Nashangaa vyuo vyetu nchini havitambui shughuli za Wabunge walioko humu ndani, ni mpaka vyuo vya nje ndiyo vinaona mambo haya. Kwa hiyo, hii ni changamoto kwa vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Malole tunakushukuru na tutaweka utaratibu wa kutambua jambo lako hilo. Kwa hiyo, kuanzia sasa jamani Mheshimiwa David Mchiwa Malole, ni Dkt. David Mchiwa Malole. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Dkt. Joel Mwakyusa. Asante sana na karibu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, nitoe Mwongozo wa Spika na ninaomba tusikilizane. Kuhusu ufafanuzi wa utekelezaji wa Bunge wa Masharti ya Ibara ya 63(3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili ya Marejeo ya Sheria za Tanzania, Mwongozo huu unatolewa chini ya Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla aliomba Mwongozo wa Spika, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007 kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Spika, (nanukuu maneno yake), Ibara ya 63(3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inaongelea kuhusu wajibu wa Bunge wa kujadili mikataba. Sasa hapa nimeona kuna mikataba kama mitatu katika Wizara hii ya Uchukuzi ambayo imekuwa inajadiliwa. Wa kwanza ni Mkataba baina ya Serikali na *RITES*, wa Pili ni Mkataba wa *UDA* na wa tatu ni ule Mkataba baina ya Serikali na Shirika la *KADCO* kwa ajili ya ukodishaji wa kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sasa ninashindwa kuelewa, hii mikataba ilifikishwa Bungeni ikajadiliwa na kupitishwa na Bunge ili kutoa *go ahead* kwa Serikali kwenda kuitekeleza au la? Kama la, huo ni ukiukwaji wa Katiba au la? Mimi nashinda kuelewa, kwa sababu nimekuwa nikifuatilia, naona mikataba ya *Richmond, Dowans*, Madini na yote ni mikataba ya hovyo.

Mheshimiwa Spika, sasa: Je, hii mikataba inawajibika kupita Bungeni au haiwajibiki kupitishwa Bungeni? Naomba Mwongozo wako." Mwisho wa kunukuu maneno ya Mheshimiwa Kigwangalla ya siku hiyo.

Baada ya Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo hilo, nilimwelekeza kwamba Mwongozo aliouomba nitautoa baadaye. Waheshimiwa Wabunge ninapenda sasa nitoe Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla kwa kutoa maelezo mafupi ya ufafanuzi ili kumwezesha yeye pamoja na wananchi wote kwa ujumla na Waheshimiwa Wabunge ambao nao suala hili linawatatiza kupata uelewa mzuri wa suala hili.

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 63(3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imetamka ifuatavyo, na hapa ninanukuu: "Kwa Madhumuni ya

utekelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa" (Mwisho wa Kunukuu)

Maelezo ya ufafanuzi wa ibara hii ya Katiba ni kwamba Bunge limepewa madaraka ya kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano yenye masharti yanayohitaji iridhiwe na Bunge. Kwa maneno mengine, Bunge hili limepewa madaraka ya kuridhia Mikataba yote ya Kimataifa *(International Treaties, Protocols, Conventions),* inayoingiwa na Jamhuri ya Muungano kama nchi *(as a atate)* yenye masharti yanayotaka iridhiwe na Bunge.

Kutokana na ufafanuzi huo, siyo mikataba yote ya kimataifa inayoingiwa na Jamhuri ya Muungano kutakiwa kuridhiwa na Bunge, bali ni ile tu yenye masharti yanayohitaji iridhiwe na Bunge ndiyo ambayo huwasilishwa na Serikali Bungeni ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63 (3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeingia Mkataba wa Kimataifa ambao masharti yake yanahitaji uridhiwe na Bunge, Mwanasheri Mkuu wa Serikali huwasilisha kwa Katibu wa Bunge rasimu ya azimio pamoja na nakala za mkataba unaokusudiwa kuridhiwa ili ujadiliwe na kuridhiwa na Bunge. Kwa kuwa, jambo hili limekuwa likifanyika karibu katika kila Mkutano wa Bunge, hakuna ulazima wa kuelezea utaratibu unatumika kujadili na kupitisha Azimio la Bunge kwa mikataba ya aina hiyo. Mikataba yote ya ndani kama ile aliyoitaja Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla haihusiki kabisa na masharti ya Ibara ya 63 (3) (a) ya Katiba yanayohitaji kuwasilishwa, kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba nihitimishe mwongozo wangu kwa kueleza kwamba kuna utaratibu ambao ulishakubaliwa na Serikali, unaowawezesha Waheshimiwa Wabunge kuomba na kupata nakala za mikataba ya Kimataifa ambayo hairidhiwi na Bunge na pia nakala ya mikataba mingine ya ndani, yaani *Local Domestic Agreements* kutoka Serikalini kwa ajili ya shughuli za Kibunge.

Chini ya utaratibu huo ni kwamba Mbunge anayehitaji kuona masharti ya Mkataba fulani kwa ajili ya kazi zake za Kibunge, anatakiwa kuandika barua kwa Katibu wa Bunge kuomba apatiwe nakala za mkataba husika ili asome ambapo Katibu wa Bunge huomba nakala hiyo kwa niaba ya Mbunge, na Mbunge huyo akishasoma nakala hiyo hubaki mikononi mwa Katibu wa Bunge.

Huo ndiyo mwongozo wangu kuhusu suala hili. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu....

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Nitapokea miongozo baada ya dakika mbili tu. Naomba nimalize tangazo la mwisho.

Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu ana wageni wake kutoka Zchecoslovakia, wako kwenye *gallery* mahali fulani. Sasa sijui kama wanasikia lugha yetu! Karibuni sana Dodoma na karibuni katika Bunge. *(Makofi)*

Sasa kabla ya kuendelea, nimesikia miongozo kadhaa, ni mitatu ili nifunge dawati langu. Tutaanza na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na baadaya Mheshimiwa January Makamba na kisha Mheshimira Aden Rage na Mheshimiwa Idd Azzan atakuwa wa nne.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo kwa kupitia Kanuni za Bunge kifungu cha 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wanatakiwa kutoa uthibitisho juu ya kauli zao wanazozitoa. Kwa mfano, mimi kuna kauli niliyoitoa tarehe 4 Julai, 2011 hapa Bungeni, nikatakiwa kuthibitisha. Kwa kufuata Kanuni za Bunge nilithibitisha rasmi kwenye Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujua Mbunge anavyothibitisha kauli yake anahitaji kusubiri kwa muda gani ili Ofisi ya Spika iweze kumpatia uthibitisho kuhusiana na kauli yake. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo Kanuni ya 47 na masharti yake ni Kanuni ya 48 kuhusu jambo la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya nusu ya vituo vya kujaza mafuta nchini haviuzi mafuta, na hali kwa kadri tunavyoisikia ni mbaya, wapo watu wanaoshindwa kwenda kazini, biashara nyingine zimesimama kwa sababu mafuta hakuna. Mimi ninaamini hili ni jambo la dharura pale ambapo nchi haina mafuta kwa maana watu wanashindwa kununua mafuta na kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani kwamba jambo hili linapaswa kujadiliwa ili tupate taarifa ya kina ya Serikali kwamba tumefikaje hapa na ni kwa namna gani tunaondokana nalo leo kwa sababu taarifa zilizopo ni kwamba hata kwenye baadhi ya Mikoa magari ya kupeleka mafuta hayaendi na maghala ya kuhifadhi mafuta mengine hayatoi mafuta jana na leo. Hili ni jambo kubwa na la dharura kwa uchumi na usalama wa nchi na ninaamini kwamba Bunge ni lazima lizungumze. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Rage.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni namba 68 (7) naomba mwongozo wako. Kuna taarifa zimeandikwa katika vyombo vya habari leo kwamba Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikwenda *North Mara* kwa kufadhiliwa na ndege za *Barrick*. Ninaomba nipate mwongozo wako kwamba je, utaratibu huu ni sahihi? Kama siyo sahihi, ilikuwaje hata Waziri wa Mazingira naye akawemo kwenye huo msafara? La kushangaza zaidi, Mbunge anayetoka Tarime akaachwa uwanja wa ndege. Imekuwaje? Naomba maelezo.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 – 4 Agosti, 2011 kulikuwa na mjadala wa hotuba ya Waziri wa Uchukuzi. Pamoja na mambo mengi yaliyozungumzwa, lakini lilizungumzwa pia suala la uuzwaji kinyemela wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam, yaani *UDA*. Waheshimiwa Wabunge wengi walichangia na wengi wao walitaka hatua zichukuliwe kwa wale waliohusika. Wapo baadhi ya Wabunge walitaja na majina ya watu ambao wamehusika.

Mheshimiwa Naibu Spika Serikali ilitoa tamko kuhusu hatua zilizochukuliwa, lakini cha kushangaza, tarehe 5 Agosti, 2011 Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam alifanya kikao na waandishi wa habari na katika maelezo mengi aliyoyatoa, pia alizungumza kuhusu Waheshimiwa Wabunge kushindwa kutumia akili na badala yake wanatumia makalio yao kufikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii siyo kwamba tu imedhalilisha baadhi ya Wabunge, bali imedhalilisha Bunge zima, imewadhalilisha hata wananchi waliotuchagua kwamba Wabunge wao sasa hatutumi akili, bali tunatumia makalio kufikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni kinyume cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, naomba mwongozo wako kwa jambo kama hili linapotokea kwa mtu ambaye yuko nje ya Bunge hili na bahati mbaya mtu huyo ni kiongozi tena ni mkubwa na mwaka 2006 alipita Bungeni hapa akatuomba kura tumchague kuwa Mbunge wa Afrika Mashariki, lakini ni Meya wa Dar es Salaam. Kauli hii imetolewa na kiongozi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, ni hatua gani Bunge linaweza kuchukua kwa kauli kama hizi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Nilishafunga daftari langu baada ya kuwaandika wale wanne wenye miongozo. Nikishamaliza mwongozo, kama kuna taarifa tutaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nikiri kupokea miongozo minne ambayo, mitatu ninaomba dawati langu hapa lipewe muda ya kuishughulikia na ku-*report* kwenu baadaye kwa ufasaha. Ninaomba mwongozo alioutaka Mheshimiwa Magdalema Sakaya, tutatoa majibu kwa ufasaha hapa baadaye. Mwongozo alioutaka Mheshimiwa Ismail Rage tutatoa majibu kwa ufasaha baadaye, lakini vilevile mwongozo wa Mheshimiwa Idd Azzan tutatoa maelezo ya nini kifanyike.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa baada ya kuwaomba wenzangu hawa wawe na uvumilivu, naomba tushughulikie mwongozo wa Mheshimiwa January Makamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ambaye yeye ametumia Kanuni ya 47 ambayo nitaisoma.

Kanuni ya 47(1) inasema; "Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo ambalo ni la dharura na muhimu kwa umma." Ndiyo Kanuni aliyoitumia.

Kwa maneno mengine, Mheshimiwa Mbunge anachoniambia na kunishawishi ni kwamba nisimamishe shughuli za Bunge, tushughulikie shughuli hii kwanza ambayo ameipendekeza. Sasa hili ni ombi zito na kwa kweli tunafahamu kabisa kinachoendelea katika sekta hii ya mafuta nchini, ni *crisis* kubwa kabisa kwa uchumi wa nchi yetu na maisha ya watu wetu, lakini Waheshimiwa Wabunge mnafahamu kwamba kama kiongozi, sina mamlaka ya kufanya jambo hilo bila kushauriana na Kamati ya Uongozi ya Bunge kwa udharura ule ule ambao umeelezwa na Mheshimiwa Makamba.

Kwa jinsi hiyo basi, nawaomba Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge tukutane kwenye ukumbi wa Spika sasa hivi kwa ajili ya kuzingatia ombi hili la dharura na baadaye tutawajulisha namna tutakavyoshughulika nalo jambo hili.

Kwa maelezo hayo basi, naomba nimwite Mheshimiwa George Simbachawene - Mwenyekiti wa Bunge ili aweze kuendeleza shughuli zilizo mbele yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makaridio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 20100/2012

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara...

**MWENYEKITI:** *Order please*! Mnaotoka, tafadhali mtoke taratibu na Waheshimiwa Wenyeviti mnakwenda kwenye kikao sasa hivi mtoke kwa utaratibu. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa tena kuiongoza nchi kwa kipindi cha pili cha miaka mitano. Hii inadhihirisha imani kubwa walionayo wananchi kwa

Mheshimiwa Rais na Chama cha Mapinduzi kwa sera zake nzuri za kukuza uchumi na kuongeza kipato cha wananchi. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Tisa wa Afrika wa Uwekezaji *(9th Africa Investment Forum 2011, "Accelerating East African Investment and Accessing a Market of a Billion People")* uliofanyika tarehe 17 hadi 19 Aprili, 2011 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulikuwa jukwaa muhimu la kutangaza fursa za uwekezaji, kuimarisha biashara Barani Afrika hususan Tanzania na kujenga ubia mpya katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa ziara yake aliyoifanya Wizarani kwangu tarehe 1 Aprili, 2011. Nachukua fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa tutaendelea kuzingatia miongozo na maelekezo aliyoyatoa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha, nampongeza kwa kuhamasisha uhifadhi wa mazingira yanayozingatia maendeleo endelevu katika Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa namna ya pekee nawapongeza Mheshimiwa Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawatakia mafanikio mema katika kutekeleza shughuli za kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa Katavi (CCM), kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mbunge na hatimaye kuteuliwa tena na kuthibitishwa na Bunge kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Njombe Kusini (CCM) na pia kwa kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai - Mbunge wa Kongwa (CCM), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na wewe Mwenyekiti na wenyeviti wenzako wawili wa Bunge hili kwa kuaminiwa na Bunge letu na kupewa nyadhifa mlizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote, pamoja na Naibu Mawaziri, kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge na pili kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa hizo. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani aliyonayo kwetu kwa kututeua mimi na pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu - Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM) kuongoza na kusimamia majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru kipekee kabisa wapigakura wa Jimbo langu la Moshi Vijijini kwa kunichagua kwa mara nyingine kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu. Binafsi, nawashukuru kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote nikiwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Nawaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa dhati kwa kipindi hiki katika kuleta maendeleo na ustawi wa Jimbo letu. Aidha, namshukuru mke wangu, watoto, ndugu zangu na Watanzania kwa ujumla kwa upendo na ushirikiano ambao wameendelea kunipa na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa -

Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini (CCM) akisaidiwa na Makamu wake, Mheshimiwa Mhandisi Stella M. Manyanya - Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), kwa ushauri wao wenye ubunifu na maelekezo wakati wa kujadili muhtasari wa makadirio ya matumizi ya Wizara hii. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja na michango ya Kamati imezingatiwa katika hotuba ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano tunaoupata katika kuwasilisha Miswada mbalimbali ya Sheria na mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwahakikishia kuwa mchango na ushauri wenu utazingatiwa ili kuhakikisha kuwa malengo tuliyojiwekea yanafikiwa kwa manufaa na ustawi wa nchi yetu na jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa Jimbo la Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake fasaha na inayoonyesha mafanikio ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne. Pia, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo - Mbunge wa Jimbo la Kilosa (CCM) kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa uchumi wetu ikiwa ni pamoja na malengo ya Bajeti ya Serikali. Bajeti hiyo imelenga kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa kuzingatia utekelezaji wa MKUKUTA II, Kilimo Kwanza na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuzishukuru Wizara na Taasisi za Serikali na wadau wote, hususan Asasi za sekta binafsi zikiwemo Baraza la Kilimo Tanzania, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania, Chama cha Wadau wa Ngozi na Mazao yake, Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania, Baraza la Taifa la Biashara, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Chama cha Wafanyabiashara Wanawake na Vikundi vya Biashara Ndogo, kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na Masoko ambazo Wizara yangu inazisimamia. Aidha, ninawashukuru wananchi kwa ushirikiano waliotupa katika kipindi chote kilichopita. Ni matumaini yangu kuwa wataendeleza ushirikiano ili kuchangia maendeleo ya Sekta na Uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ambao ni Naibu Waziri - Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Katibu Mkuu - Bibi Joyce K. G. Mapunjo, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Shaaban R. Mwinjaka na Wakuu wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, nawashukuru wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kujituma katika kutekeleza majukumu yao. Vilevile, ninawashukuru wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya hotuba hii ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, ukurasa wa 47 – 53 hususan Ibara ya 49, 50, 51, 52, 53 na 54 yamewekwa malengo ya maendeleo endelevu ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015. Napenda nichukue fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Wizara umezingatia utekelezaji wa maelekezo ya Ilani. Mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZA),* Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* na Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeendelea kutenga maeneo maalumu ya uwekezaji katika Mikoa yote nchini. Maeneo haya yatawekewa miundombinu ya msingi ili kuvutia sekta binafsi kujenga viwanda na kufanya biashara katika maeneo hayo.

Hatua hiyo itapunguza changamoto ya upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wanaotaka kuanzisha viwanda nchini. Aidha, kupitia sheria za Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZ)* na Maeneo Maalumu ya Uwekezaji *(SEZ),* Serikali imebainisha vivutio mbalimbali ikiwa ni pamoja na nafuu za kodi ili kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia inaandaa utaratibu wa kuanzisha Kituo Kimoja cha Huduma za Uwekezaji *(One Stop Services Centre)* katika eneo maalumu la uwekezaji la Benjamin William Mkapa, kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma zote muhimu zinazohusika na uwekezaji wa viwanda. Wizara inaendelea kushirikiana na taasisi zinazohusika na utoaji wa mikopo hususan Benki ya Raslimali Tanzania *(TIB)* ili kurahisisha upatikanaji wa mitaji ya kuwekeza katika viwanda na biashara. Wizara kupitia *SIDO* na *TanTrade* imeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali mbalimbali kuhusiana na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora ili kuweza kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuinua uwezo na kuimarisha ujuzi unaohitajika viwandani, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, Benki ya Dunia na Chuo Kikuu cha *GRIPS* – Tokyo ilitoa mafunzo yajulikanayo kwa jina la *KAIZEN* yenye lengo la kuongeza tija, ufanisi, usimamizi wa shughuli za viwanda na kuongeza ubora wa bidhaa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wajasiriamali 113 wenye viwanda vya nguo na mavazi waliopo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Programu hiyo ilikuwa ya majaribio *(pilot).*

Matokeo ya programu hiyo ambayo ndiyo iliyoiinua Sekta ya Viwanda kwa nchi za Japan, Taiwan, Korea, Malaysia, Singapore, China, nchi za Ulaya na Amerika ya Kaskazini yamepata mwitikio mkubwa. Wizara imekamilisha Mkakati wa *KAIZEN* utakaohusisha sekta ndogo zote za viwanda *(sub sectors).* Serikali ya Japan itafadhili programu hiyo kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania ili kujenga na kuimarisha stadi kwa ajili ya shughuli za viwanda kupitia Programu ya *KAIZEN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu wa ngozi *(leather technologists),* Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam *(DIT)* inaendelea na ufufuaji na uendelezaji wa Chuo cha Teknolojia ya Ngozi cha Mwanza *(TILT).* Jitihada hizo zimewezesha kuanza mafunzo ya muda mfupi ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi kuanzia mwezi Julai, 2011 na baadaye mafunzo ya muda mrefu katika fani ya *leather technologists* baada ya ukarabati wa majengo kukamilika. Vilevile, *Tanzania Gatsby Foundation (TGF)* wanashirikiana na *College of Engineering and Technology (CoET)* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuanzisha mafunzo ya wataalamu wa nguo *(textile technologists).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje, Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya *EPZ* na *SEZ* kwa kuipa nguvu ya kisheria *EPZA* kusimamia Mfumo wa *SEZ*. Kwa kutumia Mfumo wa *SEZ*, wawekezaji katika sekta mbalimbali za uchumi wanaotaka kuuza bidhaa katika masoko ya nje na ya ndani wataweza kuwekeza kupitia mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia programu za *EPZ* na *SEZ,* Wizara imetenga maeneo mbalimbali nchini hususan yale ya mipakani kwa lengo la kutumia fursa za biashara za mipakani. Maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Singida, Shinyanga na Tanga. Maeneo haya yatatumika kama vitovu vya kujenga viwanda vya kuongeza thamani mazao na kuuza nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuimarisha Kifedha Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* ili kiwe Chombo Madhubuti cha Kuchochea Mapinduzi ya Viwanda Nchini kwa Kutoa Mikopo ya Muda Mrefu na Riba Nafuu kwa Wawekezaji Wakubwa, wa Kati na Wadogo Nchini Kote

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa programu za kusaidia upatikanaji na udhamini wa mikopo ya kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo

ambapo andiko la programu mbili za kushirikiana na *TIB* na *SIDO* limekamilika. Programu ya mikopo kupitia *TIB* inaitwa *Industrial Development Support Loan (IDSL)* ambayo inalenga Serikali kutoa ruzuku ya asilimia tano ya riba inayotozwa na *TIB*. Programu ya pili ni ya kupitia *SIDO* inayoitwa *Industrial Credit Guarantee Initiative (ICGI)* ambapo *SIDO* itatakiwa kutoa dhamana ya mikopo midogo itakayotolewa na *NMB* kwa wajasiriamali. Utekelezaji wa programu hizi unategemea upatikanaji wa fedha za Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwekeza katika Mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na Viwanda vya Kemikali na Mbolea katika Kanda za Maendeleo kikiwemo Kiwanda cha Mbolea aina ya Urea Mkoani Mtwara na kuwezesha Kiwanda cha Minjingu kuzalisha mbolea bora ya *NPK* na *MPR* ili kufikia lengo lililowekwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi za muda mrefu zilizofanywa na Wizara kupitia *NDC* za kuvutia wawekezaji katika miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, mwekezaji katika miradi hii alipatikana mwezi Januari 2011, ambaye ni Kampuni ya *Sichuan Hongda Corporation Limited* ya China. Majadiliano ya awali yalifanyika mwezi Januari, 2011 na majadiliano ya mkataba wa ubia yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma unahusisha uzalishaji wa umeme wa Megawati 600 ambao utatumika katika uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya chuma na chuma ghafi na bakaa kuingizwa kwenye gridi ya Taifa.  Kwa kuanzia na chuma ghafi tani milioni moja kwa mwaka kitazalishwa ambacho kitatumika kuzalisha bidhaa mbalimbali za chuma *(iron and steel products)* nchini.  Katika uzalishaji huo, yatapatikana pia madini adimu ya *Vanadium* na *Titanium* ambayo yana thamani kubwa zaidi kuliko chuma chenyewe. Aidha, utekelezaji wa miradi hiyo ambayo itakwenda sambamba na uhakiki wa makaa ya mawe, uchorongaji na upembuzi yakinifu kwa mradi wa chuma unatarajiwa kuanza mwaka 2011/2012. Mwekezaji huyo atawekeza kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni tatu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya chuma na makaa ya mawe kwa mfumo unganishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Serikali imekuwa na juhudi za kuanzisha kiwanda cha mbolea kwa kutumia gesi asili Mkoani Mtwara. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa juhudi hizo zimepata mafanikio ambapo mwezi Februari, 2011 mwendelezaji wa mradi wa gesi asili ya Mnazi Bay, Kampuni ya *Wentworth Resources Limited (WRL)* ambayo imenunua hisa za *Artumas Energy (T) Ltd* ameonyesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa mbolea.

*WRL* inaendelea na uandaaji wa upembuzi yakinifu na uchimbaji wa visima zaidi vya gesi ili kupata malighafi ya kutosha ya kuzalisha mbolea aina ya *Urea* na kemikali ya *Methanol* kwa matumizi ya viwanda. Kwa upande mwingine, Kampuni ya *Minjingu Mines and Fertilizer Ltd. (MMFL)* inayozalisha mbolea aina ya *Minjingu Rock Phosphate (MRP),* imefanya upanuzi wa Kiwanda ambao umeongeza uwezo wa uzalishaji kutoka tani 75,000 kwa mwaka hadi tani 100,000 za *MRP*.  Aidha, mbolea itakayozalishwa sasa itakuwa aina ya *NPK* ambayo ina ubora zaidi kuliko ya *MRP* baada ya kiwanda kuongeza naitrojeni katika idadi ya malighafi zake za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu suala la kuimarisha uzalishaji mali viwandani kwa kuvifufua na kuviendeleza kwa teknolojia ya kisasa viwanda vyote ambavyo viliuzwa huko nyuma kisha kutelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji na tathmini ya mwaka 2007/2008 wa viwanda vilivyobinafsishwa ulibainisha kuwepo mafanikio kwa baadhi ya viwanda na mashirika yaliyobinafsishwa ambapo mashirika 42 kati ya 74 yalitekeleza mikataba kama ilivyokubalika na kuwekeza zaidi ya kiwango cha mikataba.

Aidha, viwanda na makampuni 15 yaliwekeza chini ya kiwango kilichokubalika katika mikataba ya ubinafsishaji, na hivyo utendaji ni wa kulegalega. Mengi ya hayo ni yale yaliyobinafsishwa kupitia utaratibu wa kuwauzia wafanyakazi na menejimenti *(Employee Management Buy-Out-MEBO).* Aidha, ilibainika kwamba viwanda 17 wawekezaji wameshindwa kuvifufua na hivyo vimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya viwanda vinavyoendelea na uzalishaji saba vilivyobadilisha biashara ya awali kutokana na sababu mbalimbali zikiwepo ushindani katika soko la bidhaa zilizokuwa zinazalishwa awali. Viwanda hivi vinaendelea vizuri na vinazalisha bidhaa bora tofauti na za awali. Aidha, mashirika na viwanda 17 vilivyofungwa ni kutokana na kuwekeza kwa kiwango ambacho hakikidhi mahitaji na hivyo bidhaa zilizozalishwa zikashindwa kuhimili ushindani.

Tathmini hiyo ilibainisha pia kuwa baadhi ya viwanda vimeongeza uzalishaji na hata kukuza mchango katika pato la Taifa ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira na kutumia teknolojia ya kisasa. Mifano ya baadhi ya viwanda vinavyofanya vizuri ni pamoja na *Tanzania Breweries Ltd, Tanzania Cigarette Company Ltd, Tanzania Portland Cement Company Ltd, Tanga Cement Company Ltd, Mbeya Cement Company Ltd, Tanzania Distillers Company Ltd, 21st Century Textiles Mills Ltd, ALAF, East African Cable (T) Ltd, Nampack Tanzania Ltd, Dar Brew (T) Ltd., TANELEC Ltd, Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd, Tanzania Steel Pipes na NAMERA Group* (Sunguratex).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa muda umepita tangu uperembaji wa kwanza ulipofanyika na kutokana na sababu kwamba taarifa iliandaliwa na kutoa mapendekezo ya jumla ya hatua za kuchukuliwa kwa wale ambao hawajafufua viwanda na mashirika waliyouziwa, mwezi Juni, 2011 Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na *Consolidated Holdings Corporation (CHC)* iliunda kikosi kazi kwa lengo la kufanya uchambuzi wa kina zaidi na kutoa mapendekezo yanayotekelezeka kwa kuzingatia masharti yaliyomo kwenye mikataba ya mauzo, hasa kwa kuzingatia kwamba viwanda hivi vinafufuliwa na kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kuboresha vivutio kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi mbalimbali zilizopo nchini vikiwemo Viwanda vya nguo, ngozi, usindikaji matunda, mbogamboga na usanifu wa madini ya vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kukuza uwekezaji kwenye viwanda vya kuongeza thamani katika mazao, Wizara imeendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha ili kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji. Vivutio hivyo ni pamoja na misamaha mbalimbali ya kodi kwa wawekezaji wanaozalisha bidhaa na kuuza nje kupitia mfumo wa *EPZ*; kuandaa maeneo na kuyawekea miundombinu ya msingi kama maji, umeme, barabara kama ilivyofanyika katika eneo la Uwekezaji la Benjamin Wiliam Mkapa na kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kupunguza muda wa kusajili makampuni yanayowekeza katika maeneo ya *EPZ*, muda wa kutoa leseni na muda wa kufungua na kufunga biashara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ipo katika hatua za awali za kuwezesha upatikanaji wa mikopo maalumu kwa wajasiriamali katika usindikaji wa mazao ya kilimo kwa kutumia programu za *Industrial Development Support Loans (IDLS)* kupitia Benki ya Raslimali Tanzania *(TIB)* na *Industrial Credit Guarantee Initiative (ICGI)* kupitia *SIDO*. Hatua nyingine ni pamoja na kuandaa na kuwasilisha mapendekezo ya sekta mbalimbali katika vikao vya kujadili marekebisho ya mfumo wa kodi ili kuwa na ushindani wa haki kati ya bidhaa za viwanda vya ndani na zile zinazoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea kubainisha maeneo ya uwekezaji ya *EPZ* na *SEZ* na kuhamasisha uwekezaji ndani ya maeneo hayo. Kwa ujumla, mpaka sasa viwanda 44 vinavyozalisha bidhaa chini ya *EPZ* vimeanzishwa. Viwanda hivi vimewekeza jumla ya mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 650 na vimetoa ajira 13,000 za moja kwa moja. Aidha, ujenzi wa miundombinu katika eneo maalumu la uwekezaji la Benjamin William Mkapa *Special Economic Zones (BWM-SEZ)* umekamilika ambapo viwanja 14 katika eneo hilo vimetolewa kwa wawekezaji. Mbali na maeneo ya awali ya *Millenium Business Park* (Dar es Salaam), Hifadhi *EPZ* (Dar es Salaam) na Kisongo *EPZ* (Arusha), maeneo mapya yaliyoanzishwa na sekta binafsi ni *Global Industrial Park* Mkuranga (Pwani), Rusumo *Falls SEZ* (Kagera) na inayoendelea kujengwa ya *Kamal EPZ Industrial Park*, Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Kamal Group* inaendeleza eneo la *EPZ* lenye ukubwa wa ekari 300 ambapo ujenzi wa miundombinu ya msingi umekamilika kwa asilimia 80. Tayari Makampuni manne yameshaanza kujenga viwanda katika eneo la *Kamal EPZ Industrial*

*Park*. Kati ya viwanda hivyo, ni kiwanda kikubwa cha kuzalisha chuma kitakachogharimu kiasi cha dola za Kimarekani milioni 222. Kiwanda hiki kitakuwa miongoni mwa viwanda vikubwa na vya kisasa vya uzalishaji wa chuma katika Afrika ambapo kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 700,000 kwa mwaka na kuajiri zaidi ya wafanyakazi 5,000 wa moja kwa moja. Uzalishaji unatarajiwa kuanza katikati ya mwaka 2012.

Vingine ni Kiwanda cha Kusindika mazao ya kilimo cha *Kamal Agro Ltd* kinachotarajiwa kuanza uzalishaji Desemba, 2011; kiwanda cha kusafisha mafuta machafu cha *Kamal Refinery Ltd* kitakachoanza uzalishaji mwezi Novemba, 2011; Kiwanda cha kuzalisha gesi ya *Acetylene* ya kutumika viwandani cha *Kamal Acetylene Ltd* ambacho kilianza uzalishaji mwishoni mwa mwezi Juni, 2011 na Kiwanda cha kuzalisha mbegu bora kwa kutumia bioteknolojia ya *Kamal Seeds Ltd.* Aidha, Makampuni mbalimbali makubwa kama *S. S. Controls Ltd., Lotus Packaging Ltd., Accumen Holding Ltd., U.K Cable Ltd.; Lotus Battery Ltd.* na *Lotus Appliances Ltd*. yamethibitisha nia ya kuwekeza katika eneo la *Kamal Industrial Estate EPZ.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekta binafsi kupitia Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania *(Leather Association of Tanzania - LAT)* imeendelea kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya bidhaa za ngozi nchini. Mkakati huo unaotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo *(Livestock Development Fund),* una lengo la kukuza uwezo wa viwanda vya ndani ili kusindika ngozi zote hapa nchini badala ya kuuza nje zikiwa ghafi. Kwa sasa vipo viwanda nane vya kusindika ngozi vyenye uwezo wa kusindika futi mraba milioni 73.9. Hata hivyo, uzalishaji halisi ni futi za mraba 34.3 sawa na asilimia 46.41 ya uwezo wa viwanda hivyo. Pamoja na uwezo mdogo wa uzalishaji, thamani ya mauzo ya ngozi zilizosindikwa na kuuzwa nje ya nchi yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 6.8 mwaka 2009 hadi Shilingi bilioni 8.4 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 23.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Sekta Ndogo ya Ngozi inaendelea kuimarika, kwani tumeanza kuona bidhaa za ngozi sokoni na hata ajira kuongezeka kutoka wafanyakazi 520 mwaka 2009 hadi 1,150 mwaka 2010. Mafanikio mengine yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mkakati huo ni pamoja na kufanyika kwa mafunzo ya usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa Mikoa 15 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Arusha, Kagera, Kilimanjaro, Iringa, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Singida, Shinyanga, Tabora na Tanga. Hadi sasa, jumla ya washiriki 500 wamepata mafunzo hayo na wanaendelea na utengenezaji wa bidhaa za ngozi na usindikaji wa ngozi vijijini kwa kutumia njia za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ilikipatia Kituo cha *SIDO* Dodoma mashine 25 za uzalishaji wa bidhaa za ngozi. Mashine hizo zinatumika kutoa mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa wajasiriamali ili hatimaye waweze kuanzisha viwanda vyao vidogo vidogo, ili kujiajiri na kutoa ajira kwa wengine. Kituo hiki nilikizindua tarehe 18 Juni, 2011 na wakati huo wa uzinduzi, wajasiriamali 17 walikuwa wanaendelea na mafunzo. Kituo hiki kimeshatoa mafunzo kwa wajasiriamali 74 ambao wameanzisha viwanda vidogo saba kwa kujiunga kwenye vikundi vya uzalishaji, viwili tayari vimeandikishwa na vitano viko katika mchakato wa uandikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea na zoezi la kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi mbalimbali ya maendeleo ya viwanda hapa nchini. Uandaaji na uainishaji wa fursa za uwekezaji na miradi ulipewa kipaumbele katika Kanda za Maendeleo za Mtwara, Kati na Kaskazini. Aidha, Wizara inatekeleza Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda na Mpango Kabambe unaolenga kuziendeleza sekta ndogo za viwanda kwa kuainisha sekta za kipaumbele. Sekta hizo ni pamoja na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo yatakayozalishwa katika kanda hizo kwa ajili ya malighafi za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukanda wa Kaskazini, sekta za kipaumbele ni za kuzalisha nguo, nyama, ngozi na bidhaa za ngozi, maziwa na bidhaa zake, matunda na mbogamboga. Katika Ukanda wa Kati, kipaumbele ni uzalishaji wa mafuta ya kula, ngozi na bidhaa zake, nguo, saruji na vifaa vingine vya ujenzi vikiwemo nondo na mabati. Katika Ukanda wa Mtwara,

kipaumbele ni viwanda vya korosho, chuma na bidhaa za chuma, saruji, mbolea, na kemikali ambazo zinatokana na gesi asili. Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC),* Balozi za Tanzania na wadau wengine itaendelea kuzitangaza fursa hizo kwa lengo la kupata wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini *(MUVI)* yenye lengo la kuongeza ufanisi wa mlolongo wa thamani wa bidhaa za mazao ya alizeti, mihogo, mifugo, matunda na nyanya ili kuimarisha kipato cha mzalishaji na hatimaye kupunguza umaskini. Katika mwaka 2010/2011, Mikoa sita iliyoainishwa katika programu hii ilichagua Wilaya zitakazokuwa katika mpango huo. Wilaya hizo ni Iringa Vijijini, Kilolo na Njombe kwa Mkoa wa Iringa; Simanjiro, Hanang na Babati kwa Mkoa wa Manyara; Sengerema kwa Mkoa wa Mwanza, Bagamoyo, Rufiji na Mkuranga kwa Mkoa wa Pwani; Songea Vijijini, Namtumbo na Mbinga kwa Mkoa wa Ruvuma; Kwimba na Ukerewe kwa Mkoa wa Mwanza na Muheza, Korogwe, Kilindi na Handeni kwa Mkoa wa Tanga.

Baadhi ya shughuli nyingine zilizotekelezwa katika Wilaya hizo ni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji na uimarishaji wa vyama/vikundi vya wazalishaji na wakulima, kuimarisha mifumo ya usambazaji wa mbegu bora na pembejeo, kuwaelimisha wakulima dhana ya kilimo cha biashara, kuanzisha majukwaa ya kuratibu shughuli za sekta za mazao yaliyochaguliwa, na kuanzisha na kuendeleza mifumo unganishi ya masoko *(market linkages).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuongeza mchango wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwenye Pato la Taifa, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa programu mbalimbali zikiwemo Muunganisho Ujasiriamali Vijijini *(MUVI)* na Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja *(ODOP).* Programu hizo zinalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na usindikaji wake kwa lengo la kukuza uzalishaji na kujenga uchumi imara ambao hatimaye utaweza kuchangia katika Pato la Taifa kutoka asilimia 33 ya sasa na kufikia asilimia 40 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya teknolojia mpya 312 zimetafutwa kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya miradi ya uzalishaji. Aidha, *SIDO* kupitia vituo vyake vya uendelezaji wa teknolojia vilivyopo Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Lindi na Kigoma iliwezesha utengenezaji wa mashine mpya za aina mbalimbali 506 na vipuri 1,622 na usambazaji kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kutoa elimu na kuwajengea uwezo wakulima wa kusindika mazao kabla ya kuyauza kama vile usindikaji wa asali, utengenezaji wa mvinyo, utengenezaji wa juisi pamoja na ufungashaji wa bidhaa kwa kutumia teknolojia ya TBS.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali kwa Wajasiriamali ili kuwaimarisha katika kuendesha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na ufugaji na utengenezaji wa mizinga ya nyuki, usindikaji na ufungashaji wa asali ambapo wafugaji wa nyuki wapatao 566 walipata mafunzo hayo. Aidha, wasindikaji 20 wa zao la alizeti kutoka Mji wa Makambako Mkoani Iringa walibainishwa na kuunganishwa na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).* Vile vile, jumla ya wajasiriamali 15,722 kupitia kozi 564 wamepata mafunzo yaliyowawezesha kupata maarifa na stadi za kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusaidia kukuza na kuboresha bidhaa za wajasirimali wadogo, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* imeweza kuwaunganisha Wajasiriamali wadogo na makampuni makubwa na za kati ambapo wajasiriamali 58 waliunganishwa na makampuni ya *Nyanza Mine Tobacco Authority; Prume Timber Ltd; Intermec Engineering; Wilddersun Safaris Ltd; Lake Victoria Sardins; Misanga Mini Supermarket; SAUT University; Katapala Engineering Safari Co. Ltd; Mohamed Enterprises; Lavena* na *U-Tum Supermarkets* katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Rukwa na Tabora. Hatua hii imewasaidia wajasiriamali wadogo kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuweza kupata masoko kwenye makampuni hayo makubwa na ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara imefanya jitihada mbalimbali katika kuijengea uwezo SIDO, licha ya kuwa na bajeti ndogo mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2010/2011, Serikali imeweza kupeleka baadhi ya maofisa wa *SIDO* katika mafunzo na semina mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kitaalamu wa kuwahudumia wajasiriamali wadogo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara imeweza kukamilisha mapitio ya majukumu, kazi na Sheria Na. 28/1973 iliyoanzisha *SIDO* ili kuboresha utendaji wa Shirika. Hatua inayofuata ni Serikali kuridhia mapendekezo yaliyotolewa na Mtaalamu Mwelekezi na ushauri mbalimbali uliotolewa na wadau wa Sekta hiyo. Aidha, Serikali imeendelea kuongeza mtaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali Wadogo *(NEDF)* ili kuhudumia wajasiriamali wengi zaidi. Mfuko huo ulianzishwa na Serikali mwaka 1994 kwa mtaji wa shilingi milioni 800. Serikali imekuwa ikichangia fedha za Mfuko kiasi cha shilingi milioni 500 kila mwaka kutoka mwaka 2006/2007 hadi 2010/2011. Kiwango cha juu cha ukopeshwaji kilikuwa Sh. 500,000/= ambacho kilirekebishwa mwaka 2008 hadi kufikia shilingi milioni 2.5 kwa shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara kupitia *SIDO* imekamilisha ujenzi wa jengo la kongano *(industrial clusters)* ya usindikaji wa vyakula Kemondo Mkoani Kagera na kukarabati majengo ya kongano Kigoma kwa bidhaa zitokanazo na zao la mchikichi. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na sekta binafsi katika kutenga na kuendeleza maeneo kwa ajili ya wenye viwanda vidogo na biashara ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa zikiwemo fursa za masoko ya *AGOA, EBA*, China, Japan, Canada na India ili kukuza biashara ya nje kwa kiwango kikubwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Wizara imeendelea kuhamasisha jumuiya ya wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko zilizopo ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kwa kutoa taarifa hizo kupitia taasisi zinazowawakilisha wafanyabiashara, kuwaunganisha kutoka nje katika mikutano ya ana kwa ana na kupitia warsha mbalimbali za kikanda. Aidha, mauzo ya bidhaa kwenye masoko hayo ya upendeleo yamekuwa yakiongezeka. Kwa mfano, mauzo katika soko la China yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 491.9 mwaka 2009/2010 hadi shilingi bilioni 908.3 mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la asilimia 84.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo katika soko la India yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 242.5 mwaka 2009 hadi shilingi bilioni 312.9 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 29. Mauzo katika soko la Marekani kupitia mpango wa *AGOA* yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 1.8 mwaka 2009 hadi Dola za Kimarekani milioni 2.1 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 16.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali kwa kutoa mafunzo na mbinu mbalimbali za kuyafikia masoko ya nje yaliyotolewa kwa njia ya warsha na semina. Mafunzo hayo yamekuwa yakiendeshwa kwa vikundi kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO),* Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade).* Mafunzo yaliyotolewa yalihusu biashara kwa ujumla na mauzo nje *(Train for Trade and Export Readiness).* Mafunzo hayo yalifanyika katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam na kushirikisha jumla ya wajasiriamali 55. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wajasiriamali kujua masharti na mahitaji ya soko hususan viwango vya ubora wa kimataifa ili kuziwezesha bidhaa husika kumudu ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishasema hapo juu, majadiliano ya Ubia wa Uchumi *(Economic Partnership Agreement -EPA)* kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* yameendelea tangu pande hizi mbili zilipotiliana saini ya awali *(initialing)* Mkataba wa Mpito wa *EPA (Framework for Economic Partnership Agreement-FEPA)* tarehe 27 Novemba, 2007 mjini Kampala- Uganda. Kuanzia mwezi Juni, 2010 kasi ya majadiliano ilipungua kutokana na tofauti zilizojitokeza kwa pande zote mbili na hasa Jumuiya ya Ulaya pale

iliposhindwa kukubaliana na matakwa ya msingi ya *EAC* hasa suala la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo.

Nchi wanachama wa *EAC* wanataka Jumuiya ya Ulaya kuongeza misaada ya kifedha zaidi ya zile zinazotolewa chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya hiyo *(EDF)* ili kuzisaidia nchi za *EAC* kutatua changamoto za uzalishaji duni, miundombinu na vikwazo vingine visivyo vya kiushuru ili kunufaika na fursa za masoko zilizotolewa na Jumuiya ya Ulaya jambo ambalo *EU* hawakubaliani nalo.

Aidha, *EU* imeweka masharti kwa nchi za *EAC* baada ya kusainiwa kwa mkataba wa *EPA*. Masharti hayo ni pamoja na kuzuia kuongeza kodi kwa bidhaa zitakazouzwa katika soko la *EU* na kutoa upendeleo sawa kwa *EU* pale nchi za *EAC* zitakapoingia makubaliano na nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi na kuzipa fursa zaidi ya zile ilizotoa kwa *EU*. Nchi za *EU* wanataka nchi za *EAC* kabla ya kuchukua hatua yoyote ile ya kuongeza kodi kwenye bidhaa watoe taarifa kwa *EU* kupitia Baraza la *EPA* litakaloundwa na ambalo litakuwa linakutana mara moja kila baada ya miaka miwili.

Kutoza kodi baadhi ya bidhaa na hasa bidhaa ghafi kunalenga kushawishi uongezaji thamani bidhaa na hivyo kukuza viwanda vya ndani na hatimaye kuongeza ajira na kupunguza umaskini. Masharti hayo yanazinyima nchi za *EAC* kuwa na uhuru *(policy space)* wa kuamua mambo yao yenye kuleta maendeleo. Tofauti hizi zilisababisha kusitishwa kusainiwa kwa mkataba wa mpito wa *EPA-FEPA*. Majadiliano ya *EPA* yataendelea ili kuondoa tofauti zilizojitokeza kwa lengo la kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2011 ili kuwezesha kusainiwa kwa mkataba kamili wa *EPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeingia katika hatua ya tatu ambayo ni ya Soko la Pamoja kati ya hatua tano za mtangamano ambazo ni Eneo Huru la Biashara, Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Sarafu na Shirikisho la Kisiasa. Itifaki ya Soko la Pamoja ilisainiwa rasmi na Wakuu wa nchi za Jumuiya tarehe 29 Novemba, 2009 na utekelezaji wake ulianza rasmi tarehe 1 Julai, 2010.

Hatua ya Soko la Pamoja inategemewa kuongeza zaidi fursa za masoko ya biashara ya huduma, soko la mitaji, uhuru wa watu kuingia nchi wanachama na kuanzisha shughuli za kiuchumi na uhuru wa kufanya kazi popote katika nchi wanachama. Kwa kutambua fursa zitokanazo na Soko la Pamoja, Wizara kwa kushirikiana na asasi zinazowawakilisha wafanyabiashara kama *TCCIA, CTI, TPSF, VIBINDO* na *TAFOPA* imeendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kuzichangamkia fursa hizo kwa lengo la kuongeza kipato na hatimaye kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kupunguza gharama za kufanya biashara katika Jumuiya za *EAC* na *SADC*, nchi wanachama zimefanya utafiti wa Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru *(Non Tarrif Barriers - NTBs)* katika kila nchi. Kutokana na matokeo ya utafiti, ili kuondoa vikwazo Wizara kwa kushirikiana na wadau imeunda Kamati ya Kitaifa itakayofanya kazi ya kuainisha, kufuatilia na kutoa taarifa ya vikwazo vilivyopo na vinavyojitokeza na kupendekeza njia ya kuvitatua.

Vilevile, nchi wanachama wa Jumuiya hizi zimeunda Kamati ya Kikanda ambayo inajumuisha Waratibu wa Kamati za Kitaifa *(National Focal and Enquiry Points)* ambayo inaratibu hali ya Vikwazo Visivyo vya Kiushuru katika nchi wanachama na kupendekeza hatua za kuviondoa. Wajumbe wa Kamati hizo vilevile wamepatiwa mafunzo ya namna ya kupashana habari kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya utafiti wa kina kuhusu maeneo yanayoongeza gharama za kufanya biashara nchini. Baada ya utafiti, mpango maalumu *(road map)* unaoeleza vikwazo vilivyopo na njia ya kuvitatua uliandaliwa.

Aidha, kila mdau anayehusika na utekelezaji wa mapendekezo ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini alishirikishwa na kupewa taarifa kwa utekelezaji. Maeneo ambayo yanafanyiwa kazi ni pamoja na kupunguza muda wa kusajili kampuni, majina ya biashara, kupata leseni za biashara, kupunguza vizuizi vya barabarani *(road blocks),* kurahisisha utoaji wa mizigo bandarini, kurahisisha taratibu za kuvuka mipakani na kupunguza muda wa kupata vibali vya kuendesha shughuli za uwekezaji kama vile vibali vya ujenzi *(building permit).* Maeneo ya kipaumbele ambayo yamefanyiwa kazi ili kupunguza gharama za kufanya biashara pamoja na kurahisisha taratibu za kupata leseni za biashara katika Mamlaka ya Halmashauri kwa kutenganisha mahitaji ya mipango miji na afya kwenye maombi ya leseni za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Afya na Mipango Miji watatekeleza majukumu yao ya usimamizi wa afya na mipango miji bila kufungamanishwa na maombi ya leseni za biashara kama ilivyokuwa hapo awali. Maeneo mengine yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na kuwezesha kupatikana kwa baadhi ya huduma za usajili wa makampuni na majina ya biashara katika mtandao wa kumpyuta (tovuti ya *BRELA- www.brela-tz.org*).

Aidha, tovuti hii ina taarifa zote za huduma ikiwa ni pamoja na fomu zote zinazohitajika katika kupata huduma zitolewazo na *BRELA*) na kuanza kutolewa kwa huduma za udhibiti kwa pamoja katika bandari na vituo vya mipakani *(one stop centre)* kwa kuzifanya taasisi za udhibiti kama vile *TBS, TFDA,* Wakala wa Vipimo, Wakaguzi wa mimea na mifugo zitafanya kazi kwa pamoja na kuwa na ofisi katika jengo moja zitaanza kutolewa. Idadi ya vizuizi vya barabarani vimepunguzwa na kubakiza vile vinavyohusu mizani za barabarani, usalama na vituo vya *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TanTrade* ina mpango wa kuanzisha vituo vya biashara vya kanda kwa kuanzia na mikoa ya Arusha, Mbeya na Mwanza. *TanTrade* tayari imefanikiwa kupata jengo la kupanga *NSSF*, Mwanza kwa ajili ya kituo cha biashara Kanda ya Ziwa na taratibu zinafanyika ili kupata fedha za kulipia kodi ya pango na kupata kibali cha kuajiri watumishi kwa ajili ya ofisi hiyo mpya. Kwa vituo vingine, taratibu zitaendelea kufanyika kadri uwezo utakavyoruhusu.

Wizara kwa kushirikiana na *TanTrade* ilihamasisha wajasiriamali kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam na Maonesho ya Kisekta. Pia, iliwahamasisha na kuwawezesha kushiriki Maonesho ya *Nairobi International Trade Fair, African Commodity Exhibition (ACE)* Yiwu, China, Maonesho ya Kimataifa ya Msumbiji, Maonesho ya Kimataifa ya Malawi na Maonesho ya *EXPO* 2010 yaliyofanyika Shanghai, China. Aidha, katika maonyesho ya mwaka huu nchi 17 zilishiriki pamoja na makampuni ya nje 364, wakati mwaka 2010 makampuni ya nje yaliyoshiriki ni 216, hili likiwa ni ongezeko la washiriki 148. Washiriki wa ndani walikuwa 1100 ukilinganisha na washiriki 995 mwaka 2010. Nafurahi kuliarifu Bunge lako kuwa Maonesho yamefikia viwango vya juu vya ubora kimataifa kwa kutunukiwa cheti safi kutoka Shirikisho la Maonesho ya Biashara Duniani *(UFI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na utafiti wa masoko kwa kufuatilia mienendo ya bei ya mazao makuu ya chakula na biashara kwa lengo la kupanua wigo wa mahitaji na kuwapatia wazalishaji bei nzuri zaidi. Bei ya mkulima kwa mazao makuu ya biashara yakiwemo kahawa aina ya arabika, chai, pamba, mkonge na korosho iliongezeka kwa viwango tofauti.

Aidha, bei ya mlaji kwa mazao makuu ya chakula hususan mahindi, mchele, ngano, ulezi na mtama ilipungua na bei za maharage, uwele na sukari ziliongezeka katika msimu wa mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na bei za msimu wa mwaka 2009/2010. Kutokana na ongezeko kubwa la bei ya sukari, Serikali iliingilia kati kwa kutoa bei elekezi na maelekezo maalumu kwa wazalishaji na wasambazaji wa sukari nchini kusambaza na kuhakikisha kuwa bei ya mlaji haizidi kiasi cha Sh.1,700/= kwa kilo. Serikali pia ilipunguza kiwango cha ushuru wa kuagiza sukari toka nje ya nchi ili kupunguza makali ya bei ya sukari nchini. Hata hivyo, ufanisi haukuwa kwa asilimia 100 kwa sababu ya wafanyabiashara wa rejareja*(retailers)* wenye tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imefanya utafiti kuwezesha kupata soko kwa tumbaku ya Tanzania nchini China na Uturuki. Wafanyabiashara kutoka nchini China wameonyesha nia ya kununua tumbaku hiyo. Wizara

inafanya pia juhudi za kuwezesha tumbaku ya Tanzania kuingizwa katika orodha ya bidhaa zinazoruhusiwa kuuzwa nchini China bila ushuru na ukomo *(duty free quota free)* kupitia Mkataba Maalumu wa Upendeleo *(Special Preferential Tariff Agreement)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uanzisha programu ya kuwa na utambulisho wa kitaifa kwa bidhaa Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Utafiti wa Viwanda *(TIRDO)* na Sekta Binafsi kwa kuhusisha kikamilifu vyama vya wenye viwanda na wafanyabiashara nchini kutoka Tanzania Bara na Visiwani *TPSF, CTI, TCCIA*, *ZNCCA, TAHA, TWCC, Tea Association of Tanzania, Cashewnuts Processors Association,* na kadhalika, imewezesha upatikanaji wa huduma ya usajili wa kutumia nembo za mistari *(bar codes)* na huduma nyingine zinazotolewa na Kampuni ya Kimataifa ya *GS1* yenye Makao Makuu huko Brussels, Ubelgiji. Majukumu yaliyofanywa ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kuhusu utayari wa Tanzania kama nchi kuingia katika mfumo huo, kutoa mafunzo kwa wadau, kuitisha Mkutano wa Kitaifa wa Wadau na kuwezesha kuanzishwa kwa chombo kitakachosimamia na kuratibu utoaji wa *bar codes* hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imekubalika kuwa kati ya nchi zitakazotoa nembo za utambuzi wa bidhaa *(bar codes)* kwenye kikao cha *GS1 General Assembly 2011,* kilichofanyika tarehe 14 - 19 Mei, Paris, Ufaransa na kuifanya Tanzania kuwa mwanachama wa *GS1.* Haya ni mafanikio makubwa kwa nchi yetu, kwani wenye viwanda na wafanyabiashara wetu hasa wajasiriamali watapata huduma hii hapa nchini kwa bei nafuu badala ya kufuatilia huduma hii nchini Kenya na Afrika ya Kusini. Hii itasaidia sana kukuza mauzo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na huduma hii ya nembo ya utambuzi *(bar codes)*, tumewezesha uanzishwaji wa chombo kitakachosaidia huduma ya vifungashio *(packaging)* hapa nchini *Tanzania Institute of Packaging*. Huduma hii ilizinduliwa hapa nchini tarehe 3 Agosti, 2011 ambapo Rais wa *World Packaging Authority* alishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hizi mbili, *bar codes* na *packaging* ni muhimu sana katika maendeleo ya viwanda, biashara na masoko. Serikali haifanyi bishara lakini inalo jukumu la kuiwezesha sekta binafsi ili iweze kutoa bidhaa bora na hivyo kushindana katika masoko ndani na nje ya nchi. Kwa misingi hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kwa kupitia vyama vya wenye viwanda na wafanyabishara *(TPSF, ZNCCIA, CTI, TCCIA, TAHA, ACT na TWCC)* kuhakikisha kuwa huduma hizi mbili zinakidhi malengo yaliyotarajiwa na kuwanufaisha wadau wote na kuhakikisha huduma zote muhimu katika kuendeleza Viwanda na Biashara zinapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo, sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi zisizo za Kiserikali na Taasisi za Elimu ya Juu imekamilisha Mkakati wa Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo. Waraka wa Baraza la Mawaziri kutoa taarifa ya utekelezaji umeandaliwa. Katika kurahisisha utekelezaji wa Mkakati huo, Wizara imetafsiri Sera ya Masoko ya Mazao ya kilimo kwa lugha ya Kiswahili na uandishi wa mkakati katika lugha rahisi *(popular version)* umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Miundombinu ya Masoko ya Mikoa na kuanzisha masoko katika vituo vya mipakani ili kukuza biashara ya ndani na kikanda Wizara kwa kupitia Mradi wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo *(DASIP)* imefanya makubaliano ya kujenga masoko sita katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara na Shinyanga. Masoko hayo yatajengwa katika mipaka ya Manyovu, Mtukula, Murongo, Kabanga na Sirari na pia Bandari Kavu ya Isaka Wilayani Kahama. *DASIP* inakamilisha mpango wa kumpata mshauri mwelekezi wa kuandaa michoro na gharama za ujenzi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Programu ya *Market Infrastructure, Value Addition and Rural Financing (MIVRF)* itajenga masoko manne ya mipakani na maghala kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za mazao ghalani. Programu hiyo itaanza kutekelezwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, Wizara kupitia Mipango ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* na Mradi wa *DASIP* inaendelea na ujenzi wa masoko ya mazao ya kilimo katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha ujenzi wa masoko ya kimataifa katika miji midogo ya Segera na Makambako, Wizara iliingia mkataba na Chuo Kikuu cha Ardhi kama Mshauri Mwelekezi kuandaa Mpango Kamambe *(Master Plan)* ya masoko hayo. Mshauri Mwelekezi huyo amekamilisha rasimu ya Mpango huo. Uchambuzi wa awali wa Mpango huo umefanywa na Wizara na maoni yamewasilishwa kwa Mshauri Mwelekezi ili ukamilishwe. Aidha, changamoto zilizojitokeza za upatikanaji wa eneo la kutosha huko Makambako zimepatiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Iringa. Ujenzi wa masoko hayo utategemea upatikanaji wa fedha/wawekezaji. Wizara itaendelea na juhudi za kutafuta fedha kutoka kwa wawekezaji au kupitia miradi ya maendeleo hususan ile inayolenga kufanikisha azma ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Vituo vya Pamoja vya Mipakani *(One Stop Boarder Posts)* ili kurahisisha ufanyaji biashara na nchi jirani kwa kupunguza muda unaotumika kukamilisha taratibu za watu na mizigo kuvuka mpakani, pia kuwawezesha wafanyabisahara wetu kutumia vizuri fursa tulizonazo katika mipaka yetu. Katika kufanikisha zoezi hilo, utafiti wa mahitaji ya ujenzi wa Kituo *(needs assessment)* upande wa Tanzania (kwa Kituo cha Tunduma) umekamilika kwa kushirikiana na *Trade Mark E.A*. Hatua hizo ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano kati ya Serikali yetu na Serikali ya Zambia ya kujenga Kituo cha Pamoja katika mpaka wa Tunduma/Nakonde. Aidha, utafiti kama huo umefanyika kuwezesha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mpakani mwa Tanzania na Burundi eneo la Kabanga/Kobero na majadiliano kati ya pande hizo mbili yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetembelea maeneo ya mipaka kwenye vituo vya Kabanga, Kasumulu, Mtukula, Namanga, Rusumo na Tunduma ili kutathmini urahisi wa kufanya biashara na nchi jirani na pia kuhamasisha uanzishwaji wa mfumo wa utendaji kazi wa pamoja *(One Stop Centre)* kwa Taasisi za Umma zinazosimamia Sheria za Biashara Mipakani. Taasisi mbalimbali hususan Mamlaka ya Mapato, Wakala wa Vipimo, Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya Chakula na Madawa na Wakaguzi wa Mazao ya Kilimo na Mifugo watawezeshwa kufanya kazi kwa pamoja ili kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kuwatafuta katika maeneo mbalimbali. Lengo ni kurahisisha ufanyaji biashara kwa kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za biashara kwa kupunguza muda wa kukagua na kuidhinisha bidhaa kupita mipakani.

Aidha, Kamati za ufuatiliaji kazi pamoja mipakani *(Joint Border Committee - JBC)* zimekwishaundwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania imepewa jukumu la kuongoza Kamati hizo katika kila mpaka. Katika utekelezaji wa mfumo wa utendaji kazi wa pamoja, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, na Taasisi za *TBS, TFDA, TRA* na *WMA* zimekwishapewa Ofisi ya Pamoja katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kurahisisha utaratibu wa uingizaji na utoaji wa mizigo nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, Wizara pia imetembelea masoko ya mipakani ya Kasanga, Kasesya, Kasumulu, Kipili, Kirando na Tunduma na kutoa elimu kwa wajasiriamali kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara na mbinu za kufanya biashara kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa. Aidha, wataalamu walisaidia wajasiriamali kuanzisha vikundi na kuvisajili, ambapo jumla ya vikundi 40 vilisajiliwa *BRELA* kutoka katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* iliendesha warsha ya urasimishaji biashara pamoja na taratibu nyingine za ufanyaji biashara kwa wajasiriamali katika kanda ya Kaskazini mjini Moshi mwezi Mei, 2011, ambapo wajasiriamali 21 walisajili majina ya biashara. Mafunzo haya yataendelezwa katika kanda zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje na Mpango Unganishi wa Biashara, rasimu ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Biashara *(Trade Sector Development Programme - TSDP)* imewasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo *(Development Patners-DPs)* ambao wanatarajiwa kuchangia fedha kwenye mfuko *(Mult-donor Basket Fund)* utakaotumika katika utekelezaji wa Programu hiyo. Hadi sasa nchi ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (Sida) imeonesha nia ya kuchangia kwenye Mfuko wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa *TSDP* itaanza kwa:-

(a) Kutekeleza miradi inayolenga kuimarisha uwezo wa Serikali kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa programu;

(b) Kuwezesha utekelezaji wa mkakati na mpango kazi wa kitaifa wa kuendeleza biashara ya maua, matunda na mbogamboga kupitia Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Maua, Matunda na Mboga (*National Horticultural Development Strategy)*;

(c) Kuboresha huduma katika sekta ya utalii kwa kuainisha na kupanga madaraja ya mahoteli ya kitalii *(Classification and Grading of Accomodation Establishments)* kwa kufuata mfumo wa kimataifa katika Mikoa ya Arusha na Manyara kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar; na

(d) Kurazinisha sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa viwango vya mazao ya chakula na mifugo *(Sanitary and Phytosanitary-SPS-standards)* vinavyolenga kulinda afya za binadamu, wanyama na mimea na kujenga uelewa wa wauzaji wa bidhaa nje ya nchi kuhusu hakimiliki *(Intellectual Property Rights-IPRs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ununuzi wa bidhaa za ndani kwa kupitia kauli mbiu ya ‘Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania’, Wizara imetayarisha Waraka wa kuvikuza, kuviendeleza na kuvilinda viwanda vya ndani ambapo kauli mbiu hiyo inasisitizwa ili kufikia lengo la kuendeleza sekta ya viwanda nchini.

Kauli mbiu hiyo inakwenda sambamba na uboreshaji na ufungashaji wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali hapa nchini. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania limetoa mafunzo ya ubora wa bidhaa na ufungashaji bora kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati *(SMEs) 292* katika Mikoa ya Iringa, Manyara, Mtwara, Singida na Tanga. Sampuli za bidhaa 359 zilipimwa katika maabara za *TBS*. Aidha, wajasiriamali 55 walipewa leseni za kutumia alama ya ubora ya ‘*TBS’* kwa bidhaa za maji, unga wa mahindi, mvinyo, mafuta ya alizeti, mikate, jibini, nyama, achari, asali, sabuni ya maji, sabuni za kuogea, siagi, jamu, juisi na chaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha na Kupanua Wigo wa Biashara Mtandao Katika Ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa,Wizara imeandaa Mfumo wa Usajili wa Shughuli za Biashara *(software)* kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA).* Mafunzo ya matumizi ya mfumo huo yalitolewa kwa Maafisa Biashara na Wataalamu wa mifumo wa Halmashauri za Majiji, Miji, Manispaa na Wilaya 24.

Aidha, Kompyuta 24 pamoja na vifaa vyake *(accessories),* zilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri hizo. Uteuzi wa Wasajili *(Registrar)* katika Halmashauri za Wilaya unafanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Aidha, Wizara imefanya Mkutano na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya 24 kuhusu Sheria ya Business *Activities Registration Act - BARA* ili kurahisisha usimamizi wa utekelezaji wa Sheria hiyo. Pamoja na juhudi hizo za Wizara, *BRELA* imeweka huduma mbalimbali katika tovuti yake *www.brela-tz.org* ikiwa ni pamoja na taarifa zote za huduma zitolewazo na *BRELA* pamoja na fomu zote zinazohitajika katika kupata huduma zinazotolewa na *BRELA* .

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imekamilisha rasimu ya makubaliano kati yake na *TCCIA* kushirikiana katika kutoa huduma saidizi kwa wateja hadi katika ngazi ya Wilaya kwa kuwa tayari wana mfumo wa kiteknolojia unaowasiliana katika Wilaya 95. *BRELA* imeanza kutembelea baadhi ya vituo vya *TCCIA* kwa lengo la kujionea hali halisi ya zana za kufanyia kazi, na pia kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ili wafahamu uwepo wa huduma hizo katika Ofisi za *TCCIA* zilizo karibu nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mazingira ya biashara nchini, Wizara imetenganisha utaratibu wa kupitisha fomu za maombi ya leseni za biashara kwa Maafisa Mipango Miji na Maafisa Afya ili kuwarahisisishia wafanyabiashara kujipatia leseni za biashara na

hivyo kuongeza wigo wa kurasimisha biashara. Hatua hizo zimechukuliwa katika kipindi hiki cha mpito ambapo Wizara inaendelea na maandalizi ya kuanza utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BARA). Utekelezaji wa Sheria hiyo unategemewa kuanza mara baada ya kukamilisha maandalizi katika Wilaya zote nchini. Maandalizi hayo yamepangwa kukamilishwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imeendelea kuhamasisha wazalishaji kutumia njia mbalimbali za mawasiliano zikiwemo simu za kiganjani ili kupata taarifa za masoko katika maeneo wanayoishi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kupitia kwa Wakusanya Taarifa za Masoko walioko katika Halmashauri na Mikoa, tumeendelea kusambaza taarifa za masoko na hivyo kuwezesha kuwepo kwa njia mbalimbali za mawasiliano hususan magazeti, mtandao wa kompyuta *(internet),* redio na luninga.

Wizara imetoa mafunzo kwa wakusanya taarifa za mifugo na mazao ya kilimo kuhusiana na ukusanyaji, usambazaji na jinsi ya kupata taarifa za masoko kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu *(SMS)* ili nao wawaelimishe wadau katika maeneo yao. Sambamba na jitihada hizo tayari makampuni ya simu za mkononi yakiwemo *Vodacom* na *Airtel* yameanzisha huduma hiyo na hivyo kufanya upatikanaji wa taarifa hizo kuwa rahisi zaidi. Aidha, majadiliano yamefanyika kati ya wadau na makampuni ya simu za kiganjani na kuweka mikakati ya ushirikiano katika kukusanya na kusambaza taarifa za masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha taratibu za kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* na Mamlaka hiyo imeanza kutekeleza majukumu yake. Kurugenzi ya kushughulikia Maendeleo ya Biashara ya Ndani imeundwa na tayari imetembelea Mikoa saba na Wilaya 44 ili kubainisha bidhaa zinazozalishwa, bei, ubora, mfumo wa biashara uliopo na changamoto za biashara ya ndani na kuanza kuandaa Mkakati wa Kuboresha Soko la Ndani. Mamlaka pia, imefungua Ofisi yake huko Zanzibar. Uzinduzi rasmi wa Mamlaka hiyo ulifanyika tarehe 01 Julai, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuendeleza utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania imetoa Leseni kwa maghala 27 yenye daraja “A”, “B” na “C” kwa ajili ya kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kufikia msimu wa 2010/2011.

Maghala yaliyopewa leseni hizo yana ujazo wa kuanzia tani 200 hadi 60,000. Maghala hayo yapo katika maeneo mbalimbali yanayotekeleza mfumo kwa mazao ya alizeti, kahawa, korosho, mahindi, mpunga, pamba na ufuta. Aidha, kiasi cha tani 120,062 za korosho ziliuzwa kupitia mfumo huo kwa msimu wa 2010/2011 ikilinganishwa na tani 61,000 msimu wa 2007/2008. Kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, wakulima wameweza kujipatia mikopo kutoka *NMB, CRDB Bank* na *Kilimanjaro Cooperative Bank (KCB)* kama ifuatavyo:-

Shilingi bilioni 20.66 zilitolewa na *NMB* msimu wa mwaka 2009/2010 na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 42.9 msimu wa mwaka 2010/2011; *CRDB Bank* walitoa mikopo ya kiasi cha Shilingi billioni 45.92 mwaka 2009/2010 na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 66.17 msimu wa mwaka 2010/2011. *KCB* msimu wa mwaka 2009/2010 ilitoa mikopo ya kiasi cha Shilingi bilioni 2.96 na msimu wa mwaka 2010/2011 imetoa Shilingi bilioni 2.16. Vilevile, uboreshaji wa miche ya mikorosho umeendelea kuleta tija katika uzalishaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, Wizara kupitia Mradi wa *District Agricultural Investment Project* imefanya tathmini ya maghala 74 yaliyojengwa katika maeneo ya mradi huo kwa mikoa ya Kagera, Mwanza na Shinyanga na hatua inayofuata ni kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi kwa zao la mpunga na pamba kwa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga pamoja na zao la kahawa kwa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Miundombinu ya Masoko ya Mikoa na Kuanzisha Masoko Mpakani kama vile Karagwe, Kigoma, Holili, Horohoro, Namanga, Sumbawanga, Taveta na Tarakea, Wizara inaratibu uanzishwaji wa Vituo vya Pamoja vya Mpakani

ili kurahisisha biashara na nchi jirani kwa kupunguza muda unaotumika kukamilisha taratibu za kuvuka mpaka. Katika kufanikisha zoezi hilo, yafuatayo yamefanyika. Makubaliano ya ushirikiano wa kujenga Kituo cha Pamoja katika Mpaka wa Tunduma/Nakonde yamefikiwa kati ya Tanzania na Zambia. Vilevile, utafiti wa mahitaji *(needs assessment)* ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja Tunduma umefanyika kwa kushirikiana na *Trade Mark EA* kupitia *DFID*. Aidha, hatua za kufanya utafiti kama huo katika kituo cha mpakani cha Kabanga zimeanza. Wizara ina mpango wa kufanya utafiti kama huo katika vituo vya mipakani vya Daraja la Umoja (Tanzania na Msumbiji), Holili (Tanzania na Kenya) na Kasumulo (Tanzania na Malawi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni na kutekeleza mikakati ya masoko ya ndani, kikanda na Kitaifa, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imeanzisha Jukwaa la Wadau wa Masoko ya Mazao ya Kilimo *(Agricultural Marketing Forum)* kwa lengo la kuwakutanisha wadau wa kuendeleza masoko ya mazao ya kilimo. Mkutano wa Pili wa Wadau ulifanyika na kuainisha maeneo yatakayoshughulikiwa na Jukwaa hilo ikiwa ni pamoja na uendeshaji wake. Wizara imeziwezesha na kufanya kazi kwa karibu na taasisi zifuatazo:

Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania *(MVIWATA), Tanzania Horticulture Association (TAHA), Horticultural Development Council of Tanzania (HODECT), Agricultural Council of Tanzania (ACT), Rural Livelihood Development Company (RLDC), Tanzania Agricultural Market Development Trust (TAGMARK),* Bodi za Mazao na Vyama vya Ushirika. Mafanikio ya ushirikiano huo ni pamoja na kuandaliwa kwa Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani *(Horticulture Development Strategy),* kuwashirikisha katika maandalizi ya Mkakati wa Masoko ya Mazao, Maandalizi ya Mkakati wa Mfumo Mpana na Unganishi wa Taarifa za Masoko na kufanya mapitio ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa pamoja.

*Mheshimiwa Mwenyekiti,* katika kuimarisha udhibiti wa bidhaa duni *(substandard)* toka nje ya nchi, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania imeendelea kuongeza mtandao wake kwa kufungua ofisi nyingine moja ya kukagua ubora wa bidhaa zinazoingia Tanzania kupitia mpaka wa Namanga. Uanzishaji wa ofisi hiyo unafanya jumla ya ofisi za TBS kufikia tano ambazo ni Horohoro, Bandari ya Tanga, Sirari, Holili na Namanga. Kwa sasa, tathmini inafanyika kwa ajili ya kufungua Ofisi katika mipaka ya Mtambaswala, Mtukula, Rusumo na Tunduma. Aidha, Shirika liliendelea kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nje *(batch certification).* Hadi Juni, 2011, Shirika lilikwishatoa vyeti 2,123 vya ubora wa bidhaa zilizotoka nje ukilinganisha na lengo la vyeti 2,200 sawa na asilimia 97.

Katika kutekeleza mfumo huo Shirika hushirikiana kwa karibu sana na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).* Vilevile, *TBS* inatarajia kuanzisha utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinakotoka kabla ya kuingiza nchini *(Preshipment Verification of Conformity to Standards – PVoC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwalinda wajasiriamali, Wizara kupitia Tume ya Ushindani imeendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa bandia katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu *(Inland Container Depots).* Vilevile, Tume imeendelea kufanya ukaguzi katika maghala na maduka mbalimbali katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro, Musoma, Mwanza, na Singida. Katika ukaguzi huo, Tume ya Ushindani ilifanikiwa kukamata na kuteketeza bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 824.7 kwa kipindi cha 2010/2011. Bidhaa zilizokamatwa na kuteketezwa ni pamoja na vipuri vya magari, betri *(dry cell),* betri za pikipiki, vifaa vya umeme, vifaa vya muziki, redio, runinga, jenereta za umeme na kalamu. Aidha, kupitia Baraza la Ushindani, Wizara imeendelea kupokea na kuamua rufani kutokana na maamuzi ya Tume na ya Mamlaka za Udhibiti kwa wale ambao hawakuridhika na maamuzi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mipango ya Sekta kwa mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayolenga kukuza, kuendeleza na kulinda viwanda vya ndani ambapo kumekuwa na mafanikio ya kuridhisha yanayoweza kupimwa kwa vigezo vya ukuaji wa Sekta ya Viwanda na mchango wake katika pato la Taifa, kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa viwandani na kuongezeka kwa ajira na mauzo ya bidhaa za viwandani. Katika kipindi cha mwaka 2010, ukuaji wa Sekta ya Viwanda uliendelea kuwa chanya ambapo ulifikia asilimia 7.9.

Ukuaji huo umepungua kidogo kwa asilimia 0.1 kutoka asilimia 8.0 mwaka 2009 hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la mdororo wa uchumi ulioikumba dunia mwaka 2008 na kufikia kilele mwaka 2009. Aidha, mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa nao uliongezeka kutoka asilimia 8.6 mwaka 2009 na kufikia asilimia 9.0 mwaka 2010. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani. Hata hivyo, kasi ya ukuaji na mchango wa Sekta ya Viwanda kwa pato la Taifa haukuongezeka kama ilivyotarajiwa, kutokana na athari za mgao wa umeme ambao ulisababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji na hivyo baadhi ya viwanda kusimamisha au kupunguza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ambavyo uzalishaji uliongezeka katika kipindi cha mwaka 2010 ni pamoja na uzalishaji wa unga wa ngano ulioongezeka kutoka tani 368,885 mwaka 2009 na kufikia tani 388,905 mwaka 2010, ambalo ni ongezeko la asilimia 5.4. Uzalishaji wa konyagi uliongezeka kutoka lita 10,201,000 mwaka 2009 hadi kufikia lita 12,972,843 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 27.2, pombe ya kibuku uliongezeka kutoka lita 16,141,000 mwaka 2009 hadi kufikia lita 20,753,530 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 28.6, uzalishaji wa bia uliongezeka kutoka hektolita milioni 2.84 mwaka 2009 hadi kufikia hektolita milioni 5.15 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 81.3.

Aidha, uzalishaji wa mabati uliongezeka kutoka tani 50,664 mwaka 2009 na kufikia tani 66,231 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 30.7, uzalishaji wa betri uliongezeka kutoka betri milioni 78 mwaka 2009 hadi kufikia betri milioni 93 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 19.2 ambapo uzalishaji wa sigara uliongezeka kutoka sigara bilioni 5,831 mwaka 2009 hadi bilioni 6,170 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Vilevile, uzalishaji wa chuma uliongezeka kutoka tani 34,793 mwaka 2009 hadi tani 43,882 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 26.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa saruji uliongezeka kutoka tani 1,940,845 mwaka 2009 hadi tani 2,312,055 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Uzalishaji huo uliongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na upanuzi wa viwanda vyote vitatu vya saruji nchini na kuongezeka kwa mahitaji ya saruji katika Sekta ya Ujenzi. Kiwanda cha *Tanzania Portland Cement Co. Ltd* kimeongeza uwezo wa uzalishaji kutoka tani 700,000 hadi 1,400,000; *Tanga Cement Co. Ltd* kutoka tani 500,000 hadi 1,200,000; na *Mbeya Cement Co. Ltd* kutoka tani 250,000 hadi 350,000. Kwa ujumla, hadi kufikia mwaka 2010 uwezo wa uzalishaji *(installed capacity)* wa saruji kwa viwanda vyote vitatu uliongezeka kwa asilimia 102.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010, Sekta ya Nguo na Mavazi imeendelea kuimarika kutokana na matumizi ya teknolojia ya kisasa pamoja na uongezaji wa mitaji kwa Viwanda kama vile *Polytex (21st Century), Sunguratex (NAMERA Group), Mwatex, NIDA*, Kiwanda cha *A - Z* (Arusha) cha kuzalisha vyandarua na *Mazava Fabrics Production Ltd*. (Morogoro) cha kuzalisha mavazi yanayouzwa zaidi Soko la *AGOA*. Kwa ujumla Sekta ya Nguo na Mavazi imekuwa na ongezeko la uzalishaji kufikia mita za mraba 120,000,000 mwaka 2010 ikilinganishwa na mita za mraba 91,501,000 zilizozalishwa mwaka 2009. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 31.1

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hali ya sekta ya Viwanda vya Kusindika Ngozi na bidhaa za ngozi inaendelea kuimarika, tathmini iliyofanyika inaonyesha kwamba uwezo uliosimikwa *(installed capacity)* wa viwanda vyote nane vya usindikaji ngozi nchini ni futi za mraba milioni 73.9 wakati uwezo halisi uliotumika *(capacity utilization)* kwa mwaka 2010 ni futi za mraba milioni 39.7 ikilinganishwa na futi za mraba milioni 37.3 mwaka 2009. Kushuka huko kulitokana na changamoto mbalimbali zilizoikumba Sekta ya Viwanda vya ngozi ikiwepo ya mdororo wa uchumi ulioikumba dunia.

Aidha, kwa upande wa ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha *wet-blue* mauzo yake nje ya nchi yalipungua kutoka tani 5,831 mwaka 2009 hadi tani 5,504 mwaka 2010 (sawa na upungufu wa asilimia 5.6). Hata hivyo, thamani ya mauzo ya ngozi hizo zilizosindikwa yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 6.8 mwaka 2009 hadi Shilingi bilioni 8.4 mwaka 2010 (sawa na ongezeko la asilimia 23.5). Ongezeko hili lilisababishwa na kupanda kwa bei za ngozi zilizosindikwa katika soko la nje mwaka 2010. Aidha, baadhi ya viwanda vimeanza kusindika ngozi hadi kiwango cha kati *(crust leather)* na cha mwisho *(finished leather)* kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi hapa nchini.

Viwanda vya bidhaa za ngozi navyo vimeendelea kuimarika kutokana na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa ikiwemo mafunzo ya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa vikundi vya wajasiriamali nchini. Ajira kwenye Sekta ya Ngozi imeongezeka kutoka wafanyakazi 520 mwaka 2009 hadi wafanyakazi 1,150 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa kuhamasisha uwekezaji wa viwanda ndani ya nchi kwa kuwashirikisha wawekezaji na wajasiriamali wa Kitanzania ulifanyika mwezi Machi, 2011, ambapo baadhi ya Watanzania wameonesha nia ya kuanzisha viwanda. Mfano, Kampuni ya *Yuko's General Supplies Ltd* (Kiluvya, Kibaha) inatarajia kuanzisha kiwanda cha kutengeneza viatu, Kampuni ya *Covenant Investment Agency* inatarajia kuanzisha kiwanda cha kusindika ngozi Dar es salaam, Kampuni ya *Tanmbuzi Co. Ltd* inatarajia kuanzisha Kiwanda cha Usindikaji wa ngozi Mkoani Kilimanjaro na *Afro Star (T) Ltd* inatarajia kuanzisha pia kiwanda cha usindikaji wa ngozi. Wizara itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha inakamilika na kuwezesha usindikaji wa ngozi zote zinazokusanywa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inakamilisha Programu Maalumu ya Uanzishwaji na Uendelezaji wa Maeneo Maalumu ya viwanda kama mpango mmojawapo wa kuhamasisha na kuchochea uwekezaji wa viwanda vya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi nchini. Maeneo hayo yatajulikana kama Vijiji vya Viwanda kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji wa viwanda vidogo na vikubwa. Programu hii kwa mapana yake ina mikakati mitatu ambayo ni:

(i) Mkakati wa Kuanzisha na Kuendeleza Vijiji vya Viwanda kama maeneo maalumu kwa ajili ya kuhamasisha na kuchochea uwekezaji wa viwanda vya bidhaa za ngozi na usindikaji wa ngozi nchini;

(ii) Mkakati wa Kuendelea Kuimarisha na kujenga Uwezo wa Kisekta na wa kiushindani katika soko; na

(iii) Mkakati wa Kuwezesha Sekta Kuyafikia na Kuyakuza Masoko ya Bidhaa za Ngozi zinazotengenezwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji katika kiwanda cha *General Tyre (EA) Ltd (GTEA)* ulisimama mwezi Septemba, 2007 kutokana na ukosefu wa fedha za uendeshaji. Serikali imeendelea kufanya majadiliano na mbia mwenza, kampuni ya *Continental AG* tangu mwishoni mwa mwaka 2008 na hadi sasa majadiliano hayo hayajahitimishwa kutokana na masharti magumu yaliyowekwa na mbia mwenza.

Masharti hayo ni pamoja na kuitaka *GTEA* kuuza matairi yatakayozalishwa nchini Tanzania katika nchi za Uganda na Burundi pekee; *Continental AG* kutowekeza ndani ya *GTEA* kwa vile siyo shughuli ya msingi ya *Continental AG* na deni la *Continental AG* la *USD* milioni 3.321 linalodaiwa *GTEA* kulipwa kabla ya kufikia muafaka wa kutumia alama yake ya biashara ya *General*. Kutokana na msimamo wa *Continental AG*, na kwa kuzingatia umuhimu wa kiwanda hiki katika uchumi wa Taifa, Serikali imekusudia kukabidhi kiwanda hiki *NDC* ili iweze kutafuta mwekezaji mahiri ili kiwanda kifufuliwe kwa kutumia malighafi ya mpira unaozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* imeendelea kuweka msukumo katika kuhamasisha uwekezaji ambapo wawekezaji wameendelea kujitokeza kwa miradi mbalimbali chini ya *NDC*. Miradi hiyo ni pamoja na makaa ya mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na mradi wa magadi *(soda ash)* wa Ziwa Natron; na miradi mingine ikiwemo uanzishaji wa kiwanda cha mbolea Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuzalisha chuma ghafi *(sponge iron)* unaofahamika kwa jina la “Kasi Mpya” utatumia madini ya chuma ya Maganga Matitu (sehemu ya Liganga) na makaa ya mawe ya Katewaka (karibu na Mchuchuma) katika Wilaya ya Ludewa.

Mradi huo unatarajiwa kuzalisha chuma ghafi tani 330,000 kwa mwaka ambacho kitatumika kuzalisha chuma cha pua *(steel billet)* tani *250,000* kwa mwaka na umeme *(captive power)* wa MW 25. Mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya *Maganga Matitu Resources Development Limited (MMRDL*) ambayo ni kampuni ya ubia kati ya *NDC* kwa niaba ya Serikali ambayo inamiliki hisa asilimia 25 na mwekezaji, Kampuni ya *MM Steel Resources Public Limited Company* inayomiliki hisa asilimia 75. Kwa sasa Kampuni hiyo inakamilisha uchorongaji ili kubaini ubora na uwingi wa chuma na makaa ya mawe katika eneo la mradi na zoezi linatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2011. Ujenzi wa mgodi wa chuma, mgodi wa makaa ya mawe na kiwanda cha kuzalisha *sponge iron* unatarajiwa kuanza mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara imepewa jukumu la kutekeleza nguzo namba saba ya azma ya Kilimo Kwanza ambapo Sekta ya Viwanda inapaswa kuwa kichocheo cha kuleta Mapinduzi ya Kijani hapa nchini.

Malengo makuu ya nguzo hiyo ni kuendeleza viwanda vya usindikaji ili kuongeza thamani mazao ya kilimo na mifugo na kuhakikisha upatikanaji wa zana na pembejeo za kilimo. Ili kutekeleza azma hiyo, katika mwaka 2010, Wizara iliendelea kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vinavyohusika na usindikaji na utengenezaji wa pembejeo na zana za kilimo. Aidha, kupitia Mamlaka ya *EPZ* viwanda vinane vya kusindika mazao na kutengeneza vifungashio vya mazao vimepewa leseni wakati viwanda 20 vya usindikaji mazao na vitano vya kutengeneza pembejeo na zana za kilimo vilionyesha nia ya kuwekeza kupitia *TIC* katika mwaka 2010. Kwa ujumla wawekezaji 168 walionyesha nia ya kuwekeza katika uanzishaji viwanda ambapo 18 vipo chini ya *EPZA* na 150 chini ya *TIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mkakati Unganishi wa kuendeleza Sekta ya Viwanda na inakamilisha Mpango Kamambe wa kutekeleza Mkakati huo. Mpango Kamambe huo umebainisha programu na miradi mbalimbali itakayotekelezwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uwezo wa Wizara, uimarishaji wa miundombinu, uendelezaji wa sekta za kipaumbele hususan usindikaji wa mazao, uendelezaji wa sekta binafsi, uhaulishaji wa teknolojia, upatikanaji wa mitaji na uimarishaji wa masoko. Utekelezaji wa Mkakati huo unakwenda sambamba na juhudi za kuanzisha viwanda vya kipaumbele vya mbolea na saruji katika mwambao wa pwani ya Mtwara, uendelezaji wa *SEZ* katika pwani ya Bagamoyo na uendelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga ili kujenga viwanda vya msingi kwa maendeleo ya Sekta ya Viwanda na sekta nyingine za uzalishaji.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Gatsby Trust (TGT)* inaandaa mkakati wa sekta ndogo ya nguo na mavazi kama moja ya sekta za kipaumbele. Lengo ni kuhakikisha viwanda vya ndani vya nguo vinasindika angalau asilimia 70 ya pamba inayozalishwa hapa nchini kutoka asilimia 30 ya sasa. Azma ya Wizara ni kuhakikisha nguo zinazalishwa na mavazi kushonwa kwa ajili ya soko la ndani na la nje hususan soko la *AGOA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi za muda mrefu zilizofanywa na Wizara kupitia *NDC* za kuvutia wawekezaji katika miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga, mwekezaji katika miradi hii alipatikana mwezi Januari, 2011, ambaye ni Kampuni ya *Sichuan Hongda Corporation Limited* ya China na majadiliano ya mkataba wa ubia yanaendelea. Mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma unahusisha uzalishaji wa umeme wa MW 600 kwa ajili ya uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya chuma na chuma ghafi na bakaa kuingizwa kwenye gridi ya Taifa. Tani milioni moja za chuma ghafi zitazalishwa kwa mwaka kiasi ambacho kitatumika kuzalisha bidhaa mbalimbali za chuma *(iron and steel products)* nchini. Katika uzalishaji huo, yatapatikana pia madini adimu ya V*anadium* na *Titanium* ambayo yana thamani kubwa zaidi kuliko chuma chenyewe. Kwa mfano, kiasi cha mashapo kinachotoa tani moja ya chuma inayouzwa katika soko la dunia kwa Dola za Kimarekani 600, pia kinatoa madini hayo ya *vanadium* na *titanium* yenye thamani ya Dola za Kimarekani 882.

Utekelezaji wa miradi hii ambao utakwenda sambamba na uhakiki wa makaa ya mawe, uchorongaji na upembuzi yakinifu kwa mradi wa chuma unatarajiwa kuanza mwaka 2011/2012 baada ya majadiliano ya mkataba wa ubia kukamilishwa na mkataba kusainiwa. Mwekezaji huyo

atawekeza kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni tatu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya chuma na makaa ya mawe kwa mfumo unganishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Magadi *(Soda Ash)* wa Ziwa Natron unatarajiwa kuzalisha tani 500,000 za Magadi kwa mwaka. *NDC* inaendelea kukamilisha tafiti za ziada za kisayansi kuhusu Kemia, Haidrolojia, Ekolojia na *Hydrodyanamics* ya Ziwa Natron, baada ya wadau kuonyesha wasiwasi juu ya utafiti wa athari za mradi katika mazingira na jamii ambao ulikwishakamilika. Aidha, utafiti kuhusu upatikanaji wa magadi katika eneo mbadala mbali na Ziwa huko Engaruka Wilayani Monduli, unaendelea. Utekelezaji wa mradi huo utahitaji uboreshaji wa miundombinu ya reli kati ya Tanga na Arusha, ujenzi wa reli mpya kati ya Arusha na Ziwa Natron (km 132) na upanuzi wa Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Kange, Tanga na *TAMCO*, Kibaha yanafanyiwa *Cadastral Survey* ili kuonyesha mipaka ya viwanja, miundombinu, na kadhalika na hivyo kuvutia wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda mbalimbali. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katikati ya mwezi Agosti, 2011 kwa upande wa eneo la Kange wakati kwa upande wa *TAMCO* zoezi lilikwishakamilishwa ambapo usanifu wa miundombinu hususan barabara na mfumo wa maji safi na taka vinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2011 ili kutoa nafasi kwa wawekezaji waliokwishawasilisha maombi yao *NDC* kujenga viwanda. Viwanda vinavyotarajiwa kuanzishwa ni vya magari, kuongeza thamani mazao ya kilimo na vya nguo. Vilevile, eneo la *Kilimanjaro Machine Tools* lililoko Wilaya ya Hai lilipata mwekezaji isipokuwa kutokana na mdororo wa uchumi kasi yake ya kuanza shughuli za uzalishaji ilipungua na bado hajaanza hadi sasa. Kutokana na kuchelewa huko, *NDC* tayari imekwishampa notisi ya kutengua mkataba ili kuachana naye na kuanza utaratibu wa kumpata mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* inaendelea na mazungumzo na mwekezaji aliyebainishwa ili kuanzisha mradi wa kilimo cha mashamba makubwa ya mtama mtamu katika Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani kwa ajili ya kuzalisha malighafi ya kuzalisha *ethanol* na nishati kutokana na mabua ya mtama huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* imeendelea kuibua na kunadi fursa za uwekezaji katika kanda za maendeleo za Mtwara na Kati, kwa mfano, uendelezaji wa uongezaji thamani mkaa wa mawe na madini ya chuma katika ukanda wa Mtwara na madini ya *nickel* katika ukanda wa Kati. *NDC* inajishughulisha pia na mikakati ya utekelezaji wa miradi mihimili katika ukanda wa Kati. Aidha, *NDC* imeendelea kunadi *heavy capacity ferry* na Bandari ya Mtwara kwa uendelezaji na upanuaji kwa ajili ya kuibua fursa nyingine katika ukanda wa maendeleo wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuzalisha umeme wa MW 50 hadi 300 kwa kutumia nguvu ya upepo huko Singida *(Singida Wind Power Project-SWPP)* unatekelezwa kwa ubia kati ya *NDC* na Kampuni ya *Power Pool East Africa Ltd (PPEAL).* Upembuzi yakinifu wa mradi umekamilika na Serikali imewasilisha maombi ya awali ya mkopo nafuu *(preferential loan)* katika Benki ya *Exim* ya China na mazungumzo yanaendelea. Mradi huu unategemewa kuanza kutekelezwa mwishoni mwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* iko katika hatua za mwisho za kupata kibali kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* cha kutekeleza mradi wa kusafisha dhahabu kwa njia ya kikemia baada ya kufanya utafiti wa athari ya mradi katika mazingira na jamii *(ESIA).* Aidha, tafiti za njia bora ya usafishaji wa dhahabu kwa kutumia kemikali uko katika hatua ya mwisho ya kukamilisha michoro ya mitambo ya kusafishia dhahabu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* imeingia ubia na Kampuni ya *Pacific Corporation East Africa (PCEA)* na kuunda Kampuni ya ubia ya *TANCOAL Energy Ltd* kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mbalawala na Mhukuru huko Mbinga. Kampuni hiyo inamilikiwa na *NDC* kwa asilimia 30 na *PCEA* kwa asilimia 70. Mradi huu unahusu uchimbaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya viwandani na uzalishaji wa umeme kwa kuanzia na MW 400 kwa ajili ya kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Uzalishaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya viwanda utaanza mwishoni mwaka 2011, ambapo ujenzi wa kituo na kuzalisha umeme utaanza mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* pia inasimamia ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kibaiolojia za kuua viluilui vya mbu wanaoeneza malaria kwa kutumia teknolojia kutoka Cuba. Kiwanda hicho kitakachozalisha lita milioni sita za dawa kwa mwaka kinajengwa katika eneo la Viwanda la *TAMCO*-Kibaha, Mkoani Pwani. Ujenzi wa Kiwanda husika hadi kukamilika utagharimu Dola za Kimarekani milioni 22.3, katika fedha za kigeni na Shilingi bilioni tano katika fedha za Kitanzania, ambapo asilimia 75 ya fedha za kigeni imeshalipwa. Maandalizi ya ujenzi wa kiwanda yamekamilika na ujenzi umeanza mwezi Juni, 2011 na utakamilika Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Viwanda vipya na uendelezaji wa Viwanda katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* kwa kiasi kikubwa vimechangia ongezeko la ajira katika Sekta ya Viwanda. Kwa mfano, katika maeneo ya *EPZ* ajira iliongezeka kutoka wafanyakazi 9,300 mwaka 2009 hadi wafanyakazi 13,000 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 30. Kwa ujumla, idadi ya wafanyakazi walioajiriwa katika viwanda vikubwa na vya kati walikuwa 107,267 mwaka 2009 na kuongezeka hadi wafanyakazi 108,340 mwaka 2010. Katika ajira hizo, viwanda vilivyoongoza ni vya kusindika mazao ya chakula (44,365); ufumaji na ushonaji (11,988); na tumbaku na sigara (6,883).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya *EPZ* imekamilisha zoezi la kubainisha maeneo ya *EPZ* na *SEZ* katika Mikoa. Mikoa iliyotoa maeneo ni Arusha hekta (1600); Iringa (hekta 200); Kagera (hekta 2600); Kigoma (hekta 3000); Kilimanjaro (hekta 463); Lindi (hekta 100); Manyara (hekta 530.87); Mara (hekta 1360); Mbeya (hekta 500); Mtwara (hekta 2600); Mwanza (hekta 3500); Morogoro (hekta 2000); Pwani (hekta 9081); Ruvuma (hekta 2033); Shinyanga (hekta 1040); Singida (hekta 2000) na Tanga (hekta 1363). Maeneo haya yataendelezwa kwa awamu na kwa kushirikisha sekta binafsi. Juhudi za kupata maeneo katika Mikoa ya Tabora, Dodoma na Rukwa zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya *EPZ* ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha Kituo cha Utoaji Huduma *(One Stop Services Centre)* katika eneo la *Benjamini William Mkapa Special Economic Zone*. Tayari mawasiliano na taasisi, wadau zikiwemo *TRA, NEMC* na Uhamiaji yamefanyika ili kuipatia *EPZA* maofisa watakaotoa huduma katika kituo hicho. Aidha, majengo ya kituo hicho yamekamilika na tayari yamewekwa samani, na kuunganishwa na mfumo kasi wa mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai 2010 Baraza la Mawaziri lilitoa maamuzi ya kufanyia Sheria za *EPZ* na *SEZ* marekebisho ili kuiwezesha Mamlaka ya *EPZ* chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia pia mfumo wa *SEZ* ambao hapo awali ulikuwa unasimamiwa na iliyokuwa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji. Urekebishaji wa Sheria hizo mbili ulipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2011 na Kanuni za Sheria ya *SEZ* zinaandaliwa. Kukamilika kwa Kanuni za Sheria ya *SEZ* kutatoa fursa ya kuanza kutumika kwa mfumo wa *SEZ* na hivyo kuvutia wawekezaji wengi zaidi katika eneo la *SEZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *SEZ* la Bagamoyo lenye ukubwa wa hekta 9,081 litaendelezwa kwa mfumo wa *satellite town* na utakaohusisha pia uendelezaji wa Bandari ya Mbegani na ujenzi wa uwanja wa Ndege katika kijiji cha Zinga. Hatua zilizofikiwa katika kuendeleza eneo hili ni kama ifuatavyo:

(a) Zoezi la uainishaji mipaka, upimaji na upigaji wa picha za anga tayari limekamilika;

(b) Eneo la Bagamoyo *SEZ* tayari limetangazwa katika *government gazette* kama eneo maalum la mradi;

(c) Upembuzi yakinifu umekamilika;

(d) Uthamanishaji wa maeneo ya mashamba makubwa ya Pimbini, Kitopeni, Kidagoni na Mareale umekamilika;

(e) Uthamanishaji wa maeneo mengine ya wananchi upo katika hatua za mwisho (wataalamu wa Wizara ya Ardhi wanamalizia uthamanishaji wa sehemu iliyobaki); na

(f) Pamoja na juhudi za kutafuta Shilingi bilioni 53 za fidia ya eneo zima ambazo zimekuwa zikiendelea, ufumbuzi bado haujapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Mamlaka ya *EPZ* inaendelea na taratibu za kuandaa Mpango Kamambe ya eneo zima. Baada ya kuandaliwa kwa Mpango Kamambe, wawekezaji binafsi na Mifuko ya Pensheni itahamasishwa kukodisha vitalu katika eneo hilo na kujenga miundombinu ya uzalishaji. Aidha, tayari makampuni manne (4) yameonesha nia ya kuendeleza miundombinu ya viwanda katika eneo hilo. Makampuni hayo ni *Turkuaz Ltd* kutoka Uturuki; *Blue Rock Ltd* kutoka Marekani; *Kamal Group Ltd* kutoka India na *Industrial Park Ltd* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa kujenga miundombinu na viwanda vya uzalishaji katika maeneo ya *EPZ*.

Kutokana na uhamasishaji huu makampuni ya *Kamal Group* (Zinga, Bagamoyo), *Global Industrial Park* (Mkuranga, Pwani) na Rusumo *Falls SEZ* (Kagera) yamepewa leseni za kujenga miundombinu ya msingi katika maeneo mapya ya uwekezaji ambayo yameanza kuvutia viwanda vya uzalishaji.

Aidha, Kiwanda cha *Mazava Fabrics and Production E.A Ltd* kimeongeza uzalishaji wa nguo katika eneo la *EPZ* Msamvu Mkoani Morogoro. Kiwanda hiki kinatengeneza nguo za michezo aina ya Alleson, Puma, Adidas na kadhalika kwa ajili ya soko la *AGOA* na Ulaya na kimeajiri wafanyakazi 1,500. Idadi hii inatarajia kufikia wafanyakazi 2,500 ifikapo mwezi Septemba, 2011 na itaongezeka kufikia 5,000 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo awali katika mwaka wa fedha 2010/2011 Mamlaka ya *EPZ* ilikamilisha ujenzi wa eneo maalumu la uwekezaji la *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (BWM-SEZ).* Jumla ya wawekezaji 14 wamepewa viwanja vya kujenga viwanda katika eneo hilo ambapo kwa sasa viwanja vyote vilivyotengwa vimetolewa kwa wawekezaji.

Wawekezaji waliojenga viwanda katika eneo hilo ni *Tembo Agro Ltd* (Oman); *Harvest Africa Ltd* (Tanzania); *The Great Export Co. Ltd* (Tanzania); *Paperkraft International Ltd* (Tanzania); *Labotrix Group (T) Ltd* (China); *Quality Pulse Exporters Ltd* (India); *Steel One Ltd* (Tanzania); *Konectt Industries Ltd* (India); *Rising Electronics Ltd* (Tanzania); *DZ Card Africa Ltd* (Thailand); *Somani Agro Exports Ltd* (Tanzania na Uingereza); *Tube LTD* (Tanzania na China); *Kastan Industries Ltd (*Korea na Marekani); *Rehmat Beverages and Food (Tz) Ltd* (Oman).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kupitia Mamlaka ya *EPZ* iliendelea na uhamasishaji wa uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya uwekezaji ya *EPZ* na *SEZ* kwa kutumia njia mbalimbali kama vipeperushi, mabango, majarida, tovuti ya Mamlaka na matangazo kwenye vyombo mbalimbali vya habari (magazeti, luninga, radio n.k) na kwa njia ya kushiriki katika maonyesho na makongamano ya kibiashara yanayofanyika ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia wawekezaji wengi.

Aidha, Mamlaka ya *EPZ* imekuwa inatoa mada kuhusu umuhimu na fursa zilizoko chini ya *EPZ* na *SEZ* kwa wajumbe wa Halmashauri na Mabaraza ya Madiwani katika Wilaya za Bagamoyo, Kigoma, Manyara na Meru kuchangamkia fursa hizo. Kutokana na uhamasishaji huu, idadi ya wawekezaji imeongezeka kutoka 18 mwaka 2008 hadi 44 mwaka huu ambapo mtaji umefikia Dola za Kimarekani milioni 650 na yameuza nje bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 350 na kutoa ajira za moja kwa moja 13,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Wizara imekuwa ikitekeleza mipango na mikakati mbalimbali ikiwa na lengo la kuindeleza Sekta. Katika utekelezaji

huo, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa *SIDO* katika uwezeshaji wa kitaalamu na mitaji, kuboresha huduma za ugani na ushauri.

Mheshijmiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa ushirikishwaji wa wananchi unakuwepo, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa na Halmashauri mbalimbali imekuwa ikianisha na kutenga maeneo kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ajira na kuongeza kipato kwa wajasiriamali vijijini, Wizara kupitia *SIDO* iliendelea kupeleka miradi mbalimbali ya uzalishaji mali vijijini. Katika mwaka 2010/2011, miradi mipya 237 ilianzishwa na kufikia miradi 2,743 kutoka miradi 2,506 mwaka 2009 hili ni ongezeko la asilimia 9.5. Huduma za ugani na ushauri ziliongezeka kutoka wajasiriamali 47,356 mwaka 2009 hadi kufikia wajasiriamali 55,356 mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la asilimia 16.9.

Aidha, huduma za mafunzo mbalimbali za wajasiriamali na biashara ziliongezeka kutoka wajasiriamali 28,619 mwaka 2009 na kufikia wajasiriamali 38,583 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 34.8. Mafunzo mengine yalitolewa kwa wahunzi ambapo idadi iliongezeka kutoka 6,519 mwaka 2009 na kufikia wahunzi 7,039 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wajasiriamali walioshiriki kwenye maonesho mbalimbali nje na ndani ya nchi iliendelea kuongezeka kwa asilimia 18.4 kutoka 8,254 mwaka 2009 na kufikia 9,772 mwaka 2010/2011. Aidha, washiriki kwenye maonesho hayo waliweza kuuza bidhaa zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 480. Upatikanaji wa mitaji pia uliongezeka, kufikia shilingi bilioni 5.026 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikitekeleza programu na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuiendeleza sekta hii. Hii ni pamoja na utekelezaji wa programu ya Muunganisho Ujasiriamali Vijijini (MUVI), mkakati wa Wilaya moja bidhaa moja *(ODOP),* programu ya usindikaji wa vyakula inayofadhiliwa na Serikali ya Korea ya Kusini na mikataba kati ya *SIDO* na Shirika la Viwanda Vidogo India ambao utekelezaji wake utajikita kwenye teknolojia ya habari pamoja na uimarishaji wa viatamizi vya biashara na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya jitihada mbalimbali za kuongeza uwezo wa *SIDO* katika uwezeshaji wa kitaalamu na mitaji. Juhudi hizo ni pamoja na uanzishwaji wa Mfuko wa Kitaifa wa Kuwaendeleza Wajasiriamali Wadogo *(NEDF)* mwaka 1994. Toka mfuko ulipoanzishwa hadi kufikia mwezi Machi, 2011 Serikali ilikwishawekeza jumla ya shilingi bilioni 4.8.

Aidha, mfuko ulikuwa umepokea jumla ya maombi 145,435 yenye thamani ya shilingi bilioni 75 ambapo jumla ya maombi 51,019 yenye thamani ya shilingi bilioni 26 yaliidhinishwa na kuwezesha upatikanaji wa ajira 153,185. Kiasi hicho ni kikubwa kuliko fedha zilizokwishawekezwa na Serikali kwa sababu mfuko huo unaendeshwa kwa mfumo wa mzunguko *(revolving). (Makofi)*

Katika mwaka 2010/2011, jumla ya wajasiriamali 5,976 walipewa mikopo ya thamani ya shillingi billioni 5.26 na mikopo hiyo iliwezesha kupata ajira za watu 6,458. Katika mikopo hiyo, asilimia 42 ilitolewa kwa wanawake ambao wengi wapo vijijini. Katika kipindi hicho marejesho yalikuwa ni asilimia 91.4. Kwa ujumla mfuko huu umesaidia kuboresha vipato kwa wananchi na kuchochea ujasiriamali mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara imekamilisha zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Taarifa kamili imekamilika na inatarajiwa kuzinduliwa mwezi Septemba, 2011 kwa ajili ya kutumiwa na wadau mbalimbali. Aidha, Serikali kupitia *SIDO* imeendelea kutoa huduma za ushauri na ugani ambapo jumla ya wajasiriamali 20,755 walipata huduma za ushauri katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji. Aidha, *SIDO* imeendelea kutoa huduma za ugani zikilenga maeneo mbalimbali ya kiufundi ambapo zilitolewa huduma katika viwanda vidogo 1,247 katika wilaya mbalimbali hapa nchini na kati ya hivyo 237 vilikuwa viwanda vipya. Hili ni ongezeko la asilimia 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* imeweza kuhamasisha mafundi wadogo kuhudhuria mafunzo ya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi na kuwezesha kozi 20 kuendeshwa katika mikoa 15 nchini. Kozi zilizoendeshwa ziliwashirikisha wajasiriamali 336 ambapo 117 sawa na asilimia 35 walikuwa wanawake. Mafunzo haya yamewezesha miradi 102 kuanzishwa ambapo 70 ni ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi na 32 ya usindikaji ngozi. *(Makofi)*

Aidha, kozi 11 za usindikaji wa vyakula zimeendeshwa kwa wajasiriamali 198 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Mtwara na Mwanza. Pia, kozi moja ya wataalamu elekezi 21 imeendeshwa ili kuweza kutoa fursa kwa wasindikaji kupata mwongozo wa usindikaji kupitia wataalamu hawa. Aidha, mashine na vifaa vya usindikaji wa vyakula zilizopokelewa kutoka Korea Kusini zitawezesha vituo vya mafunzo ya usindikaji vyakula vya Dar es Salaam na Morogoro kuwa na uwezo mzuri wa kutoa mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo umewezesha uanzishaji wa viwanda vipya 237 vijijini na kutengeneza ajira mpya 5,089 katika mwaka 2010/2011. Asilimia 86 ya viwanda vilivyopata huduma hiyo ni vya usindikaji wa vyakula vya aina mbalimbali. Aidha, majengo kumi yamekarabatiwa katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Shinyanga na Tanga. Vilevile, wajasiriamali wabunifu 37 wamepata nafasi katika majengo yaliyoandaliwa chini ya mradi wa kiatamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya majengo 87 yenye nafasi ya kutosha miradi midogo 520 yamejengwa kwa ushirikiano na sekta binafsi. Uendelezaji huo umefanyika katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha na kuwawezesha wajasiriamali wadogo kuweza kuyafikia masoko ya ndani na nje ya nchi, Serikali imekuwa ikiboresha vituo vyake vya kusambaza habari kwa ajili ya kuyajua masoko na sehemu muhimu za kufanyia biashara. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara kupitia *SIDO* imeweza kufanya ukarabati wa majengo na manunuzi ya vifaa kwa ajili ya vituo vya habari 15 katika mikoa mbalimbali hapa nchini ili kurahisisha upatikanaji wa habari za kimasoko na biashara za ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa vipaumbele vya pekee katika maonesho ya bidhaa mbalimbali zawa jasiriamali wadogo katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa ili kuweza kuwapa fursa ya kujifunza na kuuza bidhaa na huduma wanazozalisha. Katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia *SIDO* imewezesha kufanyika kwa maonesho matano ya kikanda ya bidhaa za wajasiriamali wadogo. Kanda hizo ni Kanda ya Mashariki, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kusini. Aidha, jumla ya wajasiriamali 1,214 walishiriki na kufanikiwa kuuza bidhaa zenye thamani ya shilingi milioni 480. Pia, *SIDO* iliwezesha wajasiriamali 442 kushiriki katika maonesho ya Sabasaba na Nanenane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2010/2011, Serikali kupitia *SIDO* imeweza kutoa mafunzo ya ujuzi wa kutengeneza majiko sanifu ya kutumia mkaa kidogo na taka za randa za mbao kwa wajasiriamali 30 katika mikoa ya Iringa na Mtwara. Pia, *SIDO* imeweza kuandaa makongamano 40 ya uhamasishaji wa utengenezaji na utumiaji wa majiko sanifu, mitambo ya majiko yatumiayo kinyesi cha mifugo na taka za randa za mbao katika mikoa yote nchini. Vilevile, mafunzo ya kuongeza ujuzi katika eneo la uhunzi yalitolewa kwa wahunzi 520 yakilenga kuboresha ubora wa bidhaa zao na kuhimili ushindani wa kibiashara ambapo mikoa ya Mtwara, Shinyanga na Iringa ilinufaika na mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, *SIDO* ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 15,722 kupitia kozi 564 zilizoendeshwa katika mikoa mbalimbali. Vilevile, *SIDO* ilitekeleza utaratibu wa kujenga uwezo wa wajasiriamali wadogo 10,976 kwa kushirikiana na *TPSF* kupitia programu ya *Business Development Gateway (BDG)* ambao walishiriki katika ushindanishaji wa mipango ya biashara na kufanya tathmini ya miradi iliyopitishwa. Hii inafanya wajasiriamali waliopata mafunzo kati ya 2005/2006 na 2010/2011 kufikia 39,181. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 thamani ya mauzo ya bidhaa nje imeongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 3,294.7 mwaka wa fedha 2009/2010 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 4,296.8 kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 30.4. Mauzo ya Tanzania yameongezeka kutoka shilingi bilioni 3,753 mwaka fedha 2009/2010 hadi kufikia shilingi bilioni 5,191 mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 1,438 sawa na asilimia 38.3. *(Makofi)*

Aidha, manunuzi ya bidhaa kutoka nje pia yameongezeka kutoka shilingi bilioni 8,447 mwaka fedha 2009/2010 na kufikia shilingi bilioni 11,119 mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2,672 sawa na ongezeko la asilimia 31.6. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia *(traditional commodities)* iliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 559.0 mwaka 2010/2011 kutoka dola za Kimarekani milioni 479.6 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 16.5. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia *(non-traditional products)* iliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 3,177.3 mwaka 2010/2011 kutoka dola za Kimarekani milioni 2,376.1 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 33.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/2011 thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka kwa asilimia 90.3 hadi dola za Kimarekani milioni 963.9 kutoka dola za Kimarekani milioni 506.5 mwaka 2009/2010. Mauzo ya bidhaa za viwandani yalichangia asilimia 30.3 ya mauzo yasiyo asilia kwa mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na asilimia 21.3 mwaka 2009/2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ongezeko la mauzo nje lilichangiwa na kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara ikiwa ni pamoja na mwamko uliotokana na uhamasishaji wa fursa za masoko na kupungua kwa mdororo wa uchumi duniani. Aidha, kupanuka kwa fursa za masoko mfano yale ya China na Jumuiya ya Afrika Mashariki yote kwa pamoja yamechangia ongezeko la biashara nchini katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ambapo thamani ya mauzo ya Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kwa asilimia 70.6 kutoka dola za Kimarekani milioni 263.8 mwaka 2009/2010 hadi dola milioni 450.0 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo zaidi nchini Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mauzo kwa nchi ya Kenya iliongezeka kwa asilimia 67.6 kufikia dola za Kimarekani milioni 297.3 mwaka 2010/2011. Mauzo ya bidhaa kwa nchi ya Kenya yalichangia asilimia 66.1, Rwanda asilimia 12.2, Burundi asilimia 11.3 na Uganda ilichangia asilimia 10.4. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikua na ziada ya dola za Kimarekani milioni 164.8 mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 46.7 mwaka 2009/2010. Hivyo, Watanzania tuondoe hofu ya kumezwa na Kenya na badala yake tuongeze bidii ili badala ya kuwa soko la wenzetu, tuendelee kuwauzia bidhaa kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia zikiwemo China, Japan, India, Hong Kong na Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 29.0 hadi dola za Kimarekani milioni 1,200.2 kutoka dola 930.3 milioni mwaka 2009/2010. Kwa mara nyingine Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie kuwa mauzo yetu ndani na nje ya nchi yatazidi kuongezeka kwa kupata huduma za *bar codes* na *packaging. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majadiliano ya Kimataifa ya Duru la Doha, Tanzania na nchi nyingine maskini duniani zimeendelea kutetea msimamo wa nchi maskini wa kutaka majadiliano yakamilike mapema iwezekanavyo na kuhakikisha kuwa maslahi yanayolenga maendeleo ya nchi maskini yanazingatiwa. Msimamo wa Tanzania na nchi nyingine maskini duniani ni kushinikiza kupunguzwa na hatimaye kuondolewa kwa ruzuku kubwa zinazotolewa na nchi tajiri kwa wakulima wao na kufanya bidhaa zetu zitokanazo na kilimo kutohimili ushindani katika masoko ya nchi tajiri. *(Makofi)*

Aidha, shinikizo la kupatiwa misaada ya kifedha na kiufundi limeendelezwa na hatimaye kuwezesha walau kupata kiasi kidogo cha fedha. Mojawapo ni fedha zilizopatikana na kuwezesha kufanya mapitio ya Sheria ya *Anti-Dumping* inayolenga kudhibiti biashara ya ushindani usio wa haki. Aidha, Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Ulaya *(EDF)* umefadhili zoezi la kuandaa Sera ya Taifa ya Haki Miliki ambapo imetoa mchango wa kiasi cha takriban shilingi milioni 130. Juhudi

zinaendelea ili kushinikiza kuongezewa fedha zaidi na hasa kupitia mfuko wa *Aid for Trade* ili kukabiliana na changamoto zikiwemo za uzalishaji duni na kuboresha miundombinu ya masoko.

Vilevile mafanikio mengine ni pamoja na Tanzania kupunguziwa madeni yake na hata kusamehewa katika maeneo mengine. Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya madogo, bado nchi tajiri hazijaonesha waziwazi dhamira ya kukubaliana na misimamo inayolenga maslahi ya kundi la nchi maskini duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato wa hatua ya pili ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni kuanzishwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja. Kama nilivyokwishaelezea awali, mazungumzo ya kuanzishwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja yalikamilika na utekelezaji wa Itifaki hiyo ulianza rasmi mwezi Julai, 2010. Hatua nyingine zilizoendelea ni ukamilishwaji wa viambatisho kwenye Itifaki ya Soko la Pamoja mwezi Februari, 2011. Viambatisho hivyo vilihusu sekta ndogo za ujenzi na masuala ya ufundi, afya na huduma za jamii, michezo na utamaduni, huduma za utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* ambayo sasa ni eneo huru la biashara, Tanzania imeendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya *SADC* kwa kuendelea kupunguza viwango vya ushuru wa bidhaa kwa lengo la kufikia asilimia sifuri ifikapo mwaka 2012 ili kuwezesha kuingia hatua ya pili ya Umoja wa Forodha na hili linafanyika kwa nchi zote wanachama wa *SADC.* Hatua ya eneo huru imechangia kuongezeka kwa biashara kati ya Tanzania na nchi wanachama za *SADC.*

Ninayo furaha tena kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2010/2011 thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za *SADC* iliongezeka kwa asilimia 67.0 kutoka dola za Kimarekani milioni 374.2 mwaka 2009/2010 hadi dola za Kimarekani milioni 625.1 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa *SADC* na mchakato wa kuanzishwa kwa Itifaki ya Biashara ya Huduma. Lengo la Itifaki hii ya Biashara ya Huduma ni kuwezesha nchi wanachama kufunguliana milango katika sekta hii na hivyo kupanua zaidi wigo wa fursa za masoko. Majadiliano yapo katika hatua za awali na Wizara ya Viwanda na Biashara inaratibu majadiliano haya kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji wa vituo vya biashara vya London na Dubai, Wizara inaendelea kuviimarisha kwa kuvipatia vitendea kazi kama vile samani za ofisi na kuimarisha mawasiliano. Vilevile kuviongezea uwezo kifedha kadri Wizara inavyopata fedha. Kituo cha Dubai kiliratibu ushiriki wa kampuni ya *Classic Homecare Furniture* kwenye maonesho ya mbao yaliyofanyika kuanzia tarehe 5 - 7 Aprili, 2011 *Airport Expo Center* -Dubai ambapo Kampuni ilifanikiwa kupata *order* za kuuza milango ya mbao na vilevile kupata machine na vifaa vya kuboresha utendaji wa kiwanda.

Aidha, Kampuni ilipata mashine ya kusindika vumbi la mbao kuwa mkaa wa kupikia ili kuondosha tatizo la uchafuzi wa mazingira. Kampuni ya *MAM Foodstuff LLC* ya Dubai ilikuja Tanzania ili kutatua matatizo yanayokwamisha uuzaji wa matunda hususan maparachichi kutoka Tanzania kwa kushirikiana na *Technoserve* na *Frank Horticultural and Timber Crops.* Sababu kubwa inayokwamisha uuzaji huo ni gharama kubwa ya usafiri wa ndege toka Tanzania. *Technoserve* wanafuatilia kupata punguzo la bei toka shirika la ndege la *Emirates*. Kituo pia kilitoa ushauri kwa Kampuni ya *Arabian Resources* ambayo watashirikiana na *TCCIA* kuandaa maonesho makubwa ya kilimo na kongamano la uwekezaji kwenye kilimo litakalofanyika mwezi Mei, 2012 *Mlimani City,* Dar es Salaam.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Fedha ipo katika mchakato wa kuanzisha vituo vya biashara nchini China na Marekani kwa lengo la kukuza mauzo nje na kuvutia wawekezaji. Tayari Serikali ya China pamoja na Benki ya Dunia wameonesha nia ya kusaidia kuanzisha kituo hicho nchini China na tayari Serikali ya China imetenga eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inashikiri kikamilifu kwenye mchakato wa kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara *(Grand FTA)* litakalojumuisha Kanda za *COMESA, EAC* na *SADC*. Hatua mbalimbali zimefikiwa ikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano *(Memorandum of Understanding – MoU)* na *roadmap.* Kukamilika kwa eneo huru kubwa la biashara la Kanda hizi tatu za *COMESA, EAC* na *SADC* kutasaidia kupanuka kwa soko la bidhaa zetu na pia litasaidia kupunguza tatizo la mwingiliano wa Kikanda *(multiple membership)* na hivyo kuwezesha biashara kufanyika bila vikwazo. Wakuu wa nchi za Kanda hizi wameshaidhinisha kuanzwa kwa majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mkakati Unganishi wa Biashara Tanzania *(TTIS)* imeunda Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Biashara *(Trade Sector Development Programme-TSDP)* kupitia mfuko maalumu *(Multi Donor Basket Fund)* ambao utashirikisha washirika wetu wa Maendeleo *(Development Partners)* katika kuchangia mfuko huo. Utekelezaji wa programu hiyo unategemea kuanza rasmi katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa, nchi ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa *(SIDA)* imeonesha nia ya kuchangia kwenye mfuko. Aidha, Mkakati wa Zanzibar wa Kuendeleza Mauzo Nje *(Zanzibar Export Development Strategy-ZEDS)* ambao umetayarishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeonekana kuwa unakidhi mahitaji ya *Diagnostic Trade Integration Study (DTIS)* iliyotakiwa ifanyike Zanzibar chini ya Mkakati Unganishi wa Biashara Tanzania *(TTIS)* na hivyo hakuna haja ya kufanya *DTIS* tena kwa madhumuni ya kujumuisha masuala ya Zanzibar katika programu ya *TSDP. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na ushirikiano mkubwa na wenzetu wa Zanzibar kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pamoja na *Zanzibar Chamber of Commerce and Agriculture (ZNCC).* Wizara ilitayarisha mwelekeo *(Road Map)* kwa kupitia programu ya *TTIS* tuliweza kugharimia mafunzo juu ya Usimamizi wa Miradi *(Project Life Cycle Management)* kwa wadau wa *TTIS* Zanzibar kama sehemu ya maandalizi ya *TSDP.* Kamati za Taifa ya Uendeshaji *(Trade Integration National Steering Committee)* na Kamati ya Wataalamu *(TTIS Technical Committee)* ziliendelea kutekeleza majukumu yao katika mkakati huu wa *TTIS* kwa kufanya vikao na kutoa maelekezo kwa Wizara kwa ajili ya utekelezaji wa yale yaliyokubaliwa katika vikao hivyo. Pia wajumbe kutoka sekta za umma na binafsi kutoka Zanzibar waliingizwa katika Kamati hizo ili kuziimarisha katika kushughulikia biashara za nje kama moja ya masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ilifanya zoezi la kufuatilia miradi ya majaribio *(pilot projects)* iliyotekelezwa na wavuvi katika Mikoa ya Dodoma na Iringa na pia wanenepeshaji wa mifugo kibiashara katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Miradi yote imeonesha mafaniko makubwa na kuleta matokeo chanya *(positive impact)* kwa wavuvi na wafugaji/wanenepeshaji mifugo walioshiriki katika miradi husika. Hali kadhalika, Wizara ilifuatilia mradi uliotekelezwa na *TAHA,* ambao pia ulionesha kuwa na matokeo chanya na mafanikio makubwa kwa wakulima wadogo wadogo wa mboga mboga na matunda katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kwa ujumla kumekuwa na unafuu wa bei ya mlaji kwa mazao makuu ya chakula. Wastani wa bei ya jumla ya mahindi kwa gunia la kilo 100 ilishuka kutoka shilingi 42,133 mwaka 2009/2010 na kufikia shilingi 34,247 mwaka 2010/2011 ikiwa ni punguzo la asilimia 18. Aidha, bei za mchele, ngano, ulezi na mtama zilishuka pia. Bei ya mlaji kwa maharage ilipanda kutoka shilingi 105,092 hadi shilingi 109,537 kwa gunia la kilo 100 sawa na ongezeko la asilimia nne. Kupanda na kushuka kwa bei ya mazao makuu ya chakula kulitokana na hali halisi ya ugavi na mahitaji katika soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010, wastani wa bei ya mkulima kwa mazao ya kahawa, chai, pamba, mkonge na korosho uliongezeka. Aidha, bei ya kuuzia nje iliongezeka kwa mazao ya chai na kahawa aina ya Arabika ambapo wastani wa bei ya kahawa ya aina ya Arabika ilipanda kutoka dola za Kimarekani 2.98 kwa kilo mwaka 2009 hadi 3.45 mwaka 2010 na katika kipindi hicho wastani wa bei ya chai ilipanda kutoka dola za Kimarekani 2.40 hadi 2.91.

Hata hivyo, wastani wa bei ya kahawa aina ya Robusta ilishuka kutoka dola za Kimarekani 2.02 kwa kilo mwaka 2009 hadi dola 1.57 mwaka 2010, na wastani wa bei ya mkonge pia ilishuka kutoka dola za Kimarekani 1,209 kwa tani mwaka 2009 hadi dola za Kimarekani 908 kwa tani mwaka 2010. *(Makofi)*

Aidha, mwenendo wa bei za bidhaa nyingi za viwandani unaonyesha kuwa bei zilipanda. Bei ya rejareja ya sukari ilipanda kutoka wastani wa shilingi 1,500 hapo mwaka 2009 hadi kufikia shilingi 1,600 mwaka 2010 kwa kilo. Bei hiyo ilipanda zaidi katika robo ya kwanza ya mwaka 2011 hadi kufikia shilingi 2,000 hapo Machi 2011. Hata hivyo, kufuatia jitihada mbalimbali za Serikali kwa kushirikiana na wadau husika, bei hiyo imeshuka na kuwa kati ya shilingi 1,600 na shilingi 1,800 kwa kilo moja katika maeneo mengi. Bei ya rejareja ya saruji ya mfuko wa kilo 50 katika masoko mbalimbali nchini ilikuwa kati ya shilingi.12,500 na shilingi 17,400 mwezi Desemba 2009 na kupanda na kuwa kati ya shilingi 13,046 na shilingi 19,000 Desemba, 2010. Vilevile bei ya bati la geji 30 ilishuka kutoka kati ya shilingi12,500 na shilingi 17,722 mwezi Desemba, 2009 hadi kufikia kati ya shilingi 11,000 na shilingi 17,061 mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kumekuwa na ongezeko la bei ya mifugo (ng'ombe, mbuzi na kondoo). Wastani wa bei ya jumla ya ng'ombe daraja la pili iliongezeka kutoka shilingi 389,696 mwaka 2009 hadi shilingi 393,853 mwaka 2010 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia moja. Aidha, bei ya ng'ombe daraja la tatu ilishuka kutoka shilingi 285,470 mwaka 2009 hadi shilingi 285,359 mwaka 2010 sawa na anguko la asilimia 0.04. Bei ya mbuzi ilipanda kutoka shilingi 37,458 hadi shilingi 38,805 wakati bei ya kondoo ilipanda kutoka shilingi 32,677 hadi shilingi 34,333 katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa taarifa za masoko umeendelea kuboreshwa na kupanuliwa katika kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na bidhaa za viwandani hususan za saruji, mabati na nondo. Taarifa za masoko ya mazao zinaonesha kuwa masoko yameongezeka kutoka masoko 93 katika mwaka wa fedha 2008/2009 hadi masoko 104 mwaka 2010/2011. Pia, minada ya mifugo imeongezeka kutoka minada 46 mwaka 2009 hadi minada 53. Taarifa hizo husambazwa kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa njia ya magazeti, luninga, tovuti, mtandao wa *internet* na ujumbe wa simu za kiganjani. Taarifa za bei ya mazao makuu ya chakula husambazwa kwa wadau mara tatu kwa wiki na taarifa za bei ya mifugo hukusanywa na kusambazwa mara moja kwa wiki. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia pamoja na wadau wengine ipo katika hatua za mwisho kukamilisha Mkakati wa Kuanzisha Mfumo Mpana na Unganishi wa Taarifa za Masoko kwa masoko ya ndani na nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeshirikiana na taasisi binafsi ikiwemo *Nuru Infocom Ltd.,* makampuni ya huduma za simu, vyombo vya habari na magazeti kuwahabarisha wananchi juu ya taarifa muhimu za biashara na masoko ili waweze kufanya maamuzi muafaka katika uzalishaji, usindikaji na uuzaji wa mazao na bidhaa zao. Taarifa hizo hujumuisha bei kwa kila aina ya zao, madaraja, masoko na ugavi kwa upande wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya matumizi ya taarifa za masoko imefanywa sanjari na jitihada za kuanzisha mkakati wa mfumo mpana na unganishi wa taarifa za masoko. Tathmini ilibaini umuhimu wa kuongeza jitihada za usambazaji wa taarifa hususan vijijini kwa njia za kisasa zaidi kama matangazo ya redio, ujumbe wa simu za kiganjani na mbao za matangazo. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa banda la kudumu katika viwanja vya Maonesho ya Wakulima Nzuguni Dodoma ili kufanikisha utangazaji wa majukumu ya Wizara, bidhaa/teknolojia zinazozalishwa na Taasisi zetu pamoja na huduma wanazotoa kwa wakulima na wananchi wengine wakati wa Maonesho ya Nanenane. Aidha, wajasiriamali pamoja na taasisi nyingine binafsi za wazalishaji wa bidhaa za kilimo na mifugo waliwezeshwa kushiriki katika maonesho ya Sabasaba na ya wakulima Nanenane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha uwezo wa halmashauri na manispaa wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wakusanya taarifa za masoko ya mazao ya kilimo na mifugo walioko katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji 114 kwa upande wa mazao makuu ya chakula na 52 ya mifugo. Aidha, vitendea kazi

vimeendelea kutolewa kwa ajili ya kuwezesha na kufanikisha ukusanyaji wa taarifa hizo. Uboreshaji zaidi unaofanywa ili taarifa hizo zitumwe na kusambazwa kwa njia ya ujumbe kwa njia ya kisasa zaidi ikiwemo ujumbe wa simu ya kinganjani *(sms).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania kwa kutumia mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani umewezesha ubora wa mazao yaliyohifadhiwa ghalani kuongezeka na kuwezesha wakulima kulipwa bei inayolingana na ubora. Kwa mfano, katika Mkoa wa Pwani zaidi ya asilimia 80 ya korosho ziliuzwa kama daraja A msimu wa 2010/2011, ikilinganishwa na hapo awali ambapo korosho zote kutoka mkoa wa Pwani na Tanga ziliuzwa kama daraja B. Mfumo huu pia ulionesha ongezeko la korosho zilizokusanywa katika maghala kutoka tani 72,492 mwaka 2009/2010 hadi tani 120,139 mwaka 2010/2011.

Aidha, Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani umewezesha matumizi ya vipimo sahihi katika ununuzi wa mazao. Kwa upande wa bei ya wakulima, Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani umewawezesha wakulima kupata bei nzuri ikilinganishwa na wale waliouza nje ya mfumo huo. Kwa mfano, wakulima waliotumia mfumo kwa zao la ufuta Mkoani Lindi msimu wa 2010/2011, walipata wastani wa shilingi 1,400 kwa kilo ikilinganishwa na shilingi 1,000 kwa kilo kwa wakulima waliouza nje ya mfumo. Aidha, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani umewezesha bei ya korosho daraja la kwanza kuongezeka kutoka shilingi 800 kwa kilo bei dira hadi kufikia wastani wa shilingi 1,600 kwa kilo msimu wa 2010/2011, ikilinganishwa na shilingi 700 bei dira na bei ya wastani 1,428 kwa msimu wa 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani imeendelea kutolewa kwa wakulima na viongozi mbalimbali katika mikoa ya Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Shinyanga na Singida kwa njia ya semina na mikutano. Bodi imeshiriki pia katika maonesho mbalimbali yakiwemo ya Nanenane, Sabasaba, Wiki ya Utumishi wa Umma na Wiki ya Ushirika. Aidha, matangazo ya kalenda na vipeperushi kwa ajili ya kuhamasisha wadau na kutoa elimu yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani umeendelea kusisitiza ubora wa mazao ghalani kwa kuhakikisha vifaa vya kudhibiti ubora vinapatikana kwenye maghala ambapo ni njia mojawapo ya kuongeza thamani na kivutio tosha kwa wanaotaka kusindika mazao husika. Bodi imekuwa ikihimiza wajasiriamali kufungua viwanda vidogo vya kuongeza thamani karibu na maghala hasa kwa mazao ya alizeti, mahindi na mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Leseni za Maghala imehamasisha Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi kushiriki katika uendelezaji wa miundombinu, mfano, maghala na barabara. Mabenki ya *NMB, CRDB Bank* na *TIB* yamekubali kushiriki katika kutoa mikopo ya ujenzi wa miundombinu iliyotajwa. Aidha, *NMB* na *CRDB Bank* wamekubali kutoa mikopo kwa vyama vya msingi kwa ajili ya ujenzi wa maghala katika mikoa ya Singida na Pwani. Pia mabenki haya yametoa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa mazao. Mikopo iliyotolewa ni pamoja na shilingi bilioni 20.66 zilitolewa na *NMB* msimu wa 2009/2010 na kuongezeka hadi shilingi bilioni 42.9 msimu 2010/2011; *CRDB Bank* walitoa mikopo ya kiasi cha shilingi billioni 45.92 mwaka 2009/2010 na kuongezeka hadi shilingi bilioni 66.17 msimu 2010/2011. *KCB* msimu wa 2009/2010 ilitoa mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 2.96 na msimu wa 2010/2011 imetoa shilingi bilioni 2.16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Leseni za Maghala, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mamlaka ya Soko la Mitaji na Hisa *(Capital Markets and Securities Authority CMSA),* Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanza kufanya matayarisho ya uanzishaji wa Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* hapa nchini. Maandalizi ya *concept paper* yamekamilika. Aidha, timu ya maafisa wa Serikali iliyoundwa kuratibu maandalizi haya inashirikiana na taasisi za Kimataifa hususan *UNCTAD* na Benki ya Dunia kuandaa *road map* ya uanzishaji wa soko la bidhaa nchini. Jitihada zinafanyika ili kuwezesha kutembelea baadhi ya nchi zilizofanikiwa katika kuendesha soko la bidhaa ikiwa ni pamoja na nchi za Afrika ya Kusini, Ethiopia na India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala inaendelea kuhimiza ujenzi wa maghala mapya yatakayojengwa yawe na ujazo usiopungua tani 3,000 na kuongezea uwezo maghala yaliyopo pale inapowezekana ili yaweze kuwa na ujazo huo. Hii itasaidia hasa pindi kutakapokuwa na soko la bidhaa ambapo mnunuzi anaweza kupata mazao mengi kwenye kituo kimoja, pia kuwezesha maghala yawe na vifaa vyote vya kitaalamu ili iwe rahisi kuyaunganisha na soko la bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maghala yapatayo 27 yamepewa leseni msimu wa 2010/2011. Aidha, kulingana na Ssheria Nambs 10 ya mwaka 2005 ambayo inawataka waendesha maghala wote kusaini hati ya kinga *(performance bond)* na Bodi ya Leseni ya Maghala, akaunti imefunguliwa katika benki ya *CRDB* ambapo waendesha maghala wanaweka fedha za kinga kulingana na utaratibu wanaopewa. Kiasi cha shilingi 100,235,919 zimeshaingizwa katika akaunti hiyo na shilingi 55,098,418 zimeshalipwa kama fidia kwa wanaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Leseni za Maghala kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazosaidia katika utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani zimekusanya maoni kutoka kwa wadau kuhusu maeneo yenye utata au mgongano katika Sheria Namba 10 ya 2005 na Kanuni zake, pia kuangalia sheria nyingine zenye mahusiano ya kiutekelezaji na mfumo mzima. Kazi hiyo inafanyika kwa kutumia vikundi kazi *(working groups)* vilivyoundwa baada ya mkutano wa wadau. Aidha, Bodi imewasiliana na Chuo cha Ushirika Moshi kwa lengo la kuangalia namna ya kuanzisha mitaala mbalimbali kwa wadau. Kinachotakiwa kufanyika ni kuona jinsi walimu wa Chuo hicho watakavyopata elimu kuhusu mfumo huu ili waweze kuandaa mitaala na kufundisha. Wizara imejadiliana na *Natural Resource Institute (NRI)* ya Uingereza ambao wana utaalamu katika eneo la Mfumo wa Stakabadhi ili kuweza kuwafundisha walimu kutoka Chuo cha Ushirika Moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara nchini *(TanTrade)* iliandaa Maonesho ya 34 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Maonesho hayo yaliendelea kuwa kivutio kikubwa kwa washiriki wa ndani na nje ikilinganishwa na Maonesho ya nyuma. Idadi ya waoneshaji iliongezeka kutoka 2,103 mwaka 2009 hadi 2,150 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Kati ya hao, washiriki 1,800 walikuwa wa ndani ya nchi na washiriki 350 walitoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yameendelea kutumiwa na nchi mbalimbali shiriki kama jukwaa la kutangazia biashara zao. Kumekuwapo na ongezeko la nchi shiriki kutoka 23 mwaka 2009 hadi 27 mwaka 2010. Katika Maonesho hayo, maulizo ya biashara kwa ajili ya soko la nje *(export enquiries)* yalikuwa dola za Kimarekani milioni 196.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 199.1 kwa mwaka 2009, huo ukiwa ni upungufu wa asilimia 1.56. Upungufu huo umetokana na mtikisiko wa kiuchumi wa dunia na uwepo wa upungufu wa makampuni yaliyotaka kuagiza bidhaa toka hapa nchini. Kadhalika, maulizo ya bidhaa kutoka nje ya nchi yalikuwa dola za Kimarekani milioni 197.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 132.7 mwaka 2009, hilo likiwa ni ongezeko la asilimia 48.0. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kupungua kwa mauzo ya papo kwa papo kutoka takribani shilingi bilioni 25.4 mwaka 2009 hadi takribani shilingi bilioni 25.0 mwaka 2010. Kupungua kwa mauzo haya kumetokana na mwamko wa washiriki kuyatumia maonesho haya kwa ajili ya kutafuta biashara endelevu badala ya kufanya mauzo ya papo kwa papo. Pamoja na hali hiyo, katika mikutano ya kibiashara ijulikanayo kama *business to business meetings* iliyofanyika wakati wa maonesho, makampuni 67 kutoka nje na ndani ya nchi yalishiriki. Katika mikutano hii kulikuwa na maongezi ya kibiashara ya thamani ya shilingi milioni 608.95 zikijumlisha uwekezaji katika sekta ya kilimo, mahitaji ya bidhaa za nguo, ngozi na nyuzi za pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TanTrade* iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya *Expo 2010* Shanghai ambapo washiriki 23 wakiwemo *TTB, TIC, TANAPA* na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro walishiriki katika kunadi vivutio vya utalii, kutangaza maeneo ya uwekezaji na kuonesha bidhaa zao. Maonesho China yaliyodumu kwa muda wa miezi sita yaliyojulikana kama *Expo 2010* Shanghai yaliyofanyika nchini China. Kaulimbiu ya maonesho hayo ilikuwa ni Mji Bora Maisha Bora

*(Better City Better Life)* na Tanzania ilitumia fursa hiyo kutangaza miradi tisa iliyoendana na kaulimbiu hiyo pamoja na vivutio vya utalii, utamaduni na uwekezaji. Banda la Tanzania lililojengwa kwa mandhari ya Kitanzania lilikuwa kivutio kwa watembeleaji pamoja na wageni na viongozi mashuhuri kutoka Tanzania na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TanTrade* imeanza kutekeleza jukumu la uratibu wa biashara ya ndani kwa kufanya utafiti katika mikoa na wilaya zote za Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi pamoja na mipaka iliyopo katika Kanda hizo. Katika utafiti huo, *TanTrade* ilikutana na viongozi wa mikoa, wilaya, tarafa, kata, vijiji pamoja na wazalishaji mbalimbali katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Madini na Maliasili ili kubaini bidhaa zinazozalishwa, wingi wake, ubora, mfumo wa masoko, bei na kutambua changamoto zinazowakabili wazalishaji. Utafiti huo ulibaini changamoto mbalimbali zikiwemo za kutokuwepo mfumo wa masoko, miundombinu hafifu hususan ya barabara kufika maeneo ya uzalishaji, bei ndogo za bidhaa zinazozalishwa, ubora hafifu wa baadhi ya bidhaa na vikwazo mbalimbali vikiwemo vya ushuru katika maeneo ya mipakani mwa Tanzania na nchi jirani. Mapendekezo ya mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo yamewasilishwa kwa mikoa husika kwa hatua zaidi na *TanTrade* inaendelea kufanya kazi na Uongozi wa Mikoa na Wilaya ili kushirikiana katika kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* iliendelea na majukumu ya uwekaji viwango vya ubora wa bidhaa na usimamiaji wa utekelezaji wa viwango hivyo. Pamoja na viwango vinavyohusu sekta mbalimbali, Shirika lilikamilisha viwango muhimu vya vigae, ubora wa huduma za nishati, uwezo wa vifaa au mifumo kufanya kazi bila mwingiliano na sumaku umeme katika mazingira, mafuta ya kula, maziwa, nguo, ubora wa maji, matairi ya magari, vifaa vya ujenzi, zana za kilimo kama vile matrekta, majembe, plau, matrekta ya kusukuma kwa mikono *(power tillers)* na mashine zinazotumika katika kilimo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2011, Shirika lilikuwa limetayarisha viwango vya Taifa 1,427 katika sekta mbalimbali yaani kilimo na chakula, nguo, kemikali, uhandisi, mazingira na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango limeendelea na juhudi za kutoa mchango muhimu katika Sekta ya Ufungashaji wa Bidhaa kupitia Kituo cha Ufungashaji *(Packaging Technology Centre)* ambacho kwa sasa hivi kipo katika hatua ya majaribio ya awali. Aidha, Shirika liliendelea na utoaji wa mafunzo ya ufungashaji bora kwa wajasiriamali wadogo na kati *(SMEs)* wapatao 140 katika mikoa ya Iringa, Mtwara, Rukwa na Tanga. Kituo kitakapoanza kazi rasmi, kitatoa huduma za kupima sampuli za viwanda vya ufungashaji kwa lengo la kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kuhakiki vifungashio *(packaging materials)* kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika linaendelea na juhudi za kuziwezesha maabara zake kupata umahiri na kufikia viwango vya upimaji vya Kimataifa *(laboratory accreditation).* Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako kuwa tarehe 4 Novemba 2010, Kamati ya pamoja ya *SADCAS* na *SANAS* iliipatia Maabara ya Shirika ya Ugezi Cheti cha Umahiri wa Utendaji wa Kazi zake *(laboratory accreditation)* katika Nyanja ya upimaji wa ukubwa *(dimensional).* *(Makofi)*

Pia, Maabara ya Chakula *(food microbiology)* nayo ilipata Cheti cha Umahiri wa Utendaji kazi zake *(laboratory accreditation)* katika upimaji wa vijidudu kwenye vyakula na maji vinavyosababisha maradhi kama vile homa ya matumbo *(typhoid),* kipindupindu (*cholera),* kuumwa tumbo na kuhara (*E.coli*) na magonjwa yaambatanayo na majipu *(staphylococci).* *(Makofi)*

Aidha, maabara za Shirika za Uhandisi Umeme, Uhandisi Mitambo na Uhandisi Ujenzi zimekamilisha miongozo ya ubora kulingana na kiwango cha kimataifa *ISO/IEC 17025* na tayari imekaguliwa na imeidhinishwa. Wakati wowote maabara hizo zitafanyiwa ukaguzi wa awali wa kuthibitisha umahiri wa upimaji wa nyaya za umeme, nondo na simenti. Kupata umahiri kwa maabara hizo, kutawahakikishia walaji ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa nchini. Pia watunga sera watakuwa na uhakika wa kutolea maamuzi ya majibu yaliyopatikana kutoka katika maabara zilizohakikiwa umahiri wake. Vilevile hatua hizo zitapanua masoko ya bidhaa zetu ndani na nje, kwani taarifa za upimaji na ugezi zitakazotolewa na Shirika zitatambulika Kimataifa na hivyo kuongeza kukubalika kwa bidhaa za Tanzania duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* inashirikiana na mashirika mengine ya viwango Kikanda na Kimataifa katika uwekaji wa viwango. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Shirika linaendelea kushirikiana na mashirika ya viwango ya Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda kuweka viwango vya Afrika Mashariki. Nafurahi tena kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2011, jumla vya viwango vya Afrika Mashariki 1,222 vilikamilishwa katika nyanja za uhandisi, vyakula, nguo na kemikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Tanzania kupitia programu ya MKUKUTA limesaidia kuinua ubora wa bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa na wajasiriamali wadogo na wa kati *(SMEs).* Hadi kufikia mwezi Machi 2011, jumla ya leseni 63 zilikuwa zimetolewa kwa viwanda vya wajasiriamali wadogo na wa kati *(SMEs)* baada ya kuthibitishwa kuwa vinazalisha kulingana na viwango vya Kitaifa ambavyo huwaruhusu kutumia alama ya ubora wa bidhaa *TBS* kwa bidhaa zifuatazo, mkate, mafuta ya kujipaka mwilini, siagi, chaki, spageti, asali, jibini, juisi, mvinyo, vibamba *(paving blocks),* unga na achari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika liliendelea na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa viwanda vyote hapa nchini kwa nia ya kuvisaidia viweze kuzalisha bidhaa zenye ubora. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Shirika limeweza kutembelea jumla ya viwanda 176 vya wajasiriamali wadogo kama ifuatavyo, Dodoma 18, Kilimanjaro 17, Lindi 4, Manyara 19, Mbeya 15, Morogoro 16, Mtwara 5, Rukwa 32, Ruvuma 17 na Tabora 33. *(Makofi)*

Shirika limeendelea kuboresha miundombinu yake kwa kufungua ofisi ya kukagua ubora wa bidhaa zinazoingia Tanzania kupitia mpaka wa Namanga. Aidha, maandalizi yameanza kwa ajili ya ufunguzi wa ofisi ya Tunduma. Kwa sasa tathmini inafanyika kwa ajili ya kufungua ofisi katika mipaka ya Mtambaswala, Mtukula na Rusumo. Kwa upande wa vifaa vya kisasa vya maabara, katika mwaka 2010/2011 Shirika limenunua vifaa vya kupimia ubora wa saruji na upimaji wa chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika pia liliendelea kusimamia utekelezaji wa viwango vya Taifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora *(certification schemes).* Aidha, Shirika lilitoa jumla ya leseni 1,199 za ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda 762 vya humu nchini. Leseni za ubora wa bidhaa hutolewa na *TBS* kwa wazalishaji wanaotimiza masharti ya ubora wa bidhaa zikiwemo zile zinazogusa afya na usalama wa walaji, mazingira na uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Shirika liliendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Bidhaa Duni Kutoka Nje ya Nchi ambapo leseni 2,100 za ubora wa bidhaa zilitolewa ikilinganishwa na leseni 661 za mwaka 2009/2010. Vilevile Shirika linaendelea na jitihada za uanzishwaji wa utaratibu wa upimaji wa ubora wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja Tanzania *(Pre-shipment Verification of Conformity to Standards)* na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwanzoni wa mwaka wa fedha 2011/2012. Zabuni kwa ajili ya kuwapata wazabuni ilikwishatangazwa na kufunguliwa ambapo uchambuzi wa maombi hayo unafanywa. Katika kutekeleza mfumo huo, Shirika hushirikiana kwa karibu sana na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo na Mizani imeendelea kukagua na kuhakiki vipimo vinavyotumika katika biashara ili kumlinda mlaji. Jumla ya vipimo 807,719 vinavyotumika katika biashara vilikaguliwa ikilinganishwa na vipimo 739,842 vya mwaka 2009/2010. Hilo ni ongezeko la asilimia tisa. *(Makofi)*

Aidha, zaidi ya ukaguzi unaofuata ratiba, ukaguzi wa kushitukiza umefanyika mara nyingi zaidi katika mikoa yote. Jumla ya wafanyabiashara 4,738 walipatikana na makosa kwa kukiuka Sheria ya Vipimo. Hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kufilisiwa *(compounding)* na kushitakiwa mahakamani. Idadi ya watu waliofilisiwa kwa kukiuka matumizi ya vipimo ni 7,028 na jumla ya kesi 12 zipo mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa elimu kwa umma, Wakala wa Vipimo kwa mwaka 2010/2011 imeshiriki katika Maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Wiki ya Utumishi wa Umma, pamoja na ya wajasiriamali yaliyotayarishwa na *SIDO*, Dar es Salaam. Katika maonesho hayo

ilipata nafasi ya kuelimisha wazalishaji matumizi sahihi ya vipimo na namna nzuri ya ufungashaji wa bidhaa wanazozalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala imepanua wigo wa kazi zake kutoka vipimo vilivyozoeleka kama mizani na pampu za mafuta kwa kuanzisha upimaji wa malori ya mchanga, kokoto na matenki yanayotumika kuhifadhi mafuta ya kuendeshea mitambo na nishati *(storage tanks for petroleum products).* Jumla ya malori ya mchanga na kokoto 1,246 yalipimwa katika kipindi cha mwaka 2010/2011 lengo likiwa ni kupima malori 1,440. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imerekebisha Kanuni za Sheria ya Vipimo kupitia Tangazo la Serikali *(Government Notice)* Na.144 la tarehe 17 Novemba, 2010 ili kuiwezesha Serikali kufahamu kwa usahihi zaidi kiasi cha mafuta yanayoingizwa nchini kwa madhumuni ya kuondoa udanganyifu uliokuwa unafanywa na baadhi ya waagizaji wa mafuta na hivyo kuwezesha nchi kupata kodi stahiki. Baada ya marekebisho hayo, Wakala pia imeweza kupima matenki makubwa 177. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* imesajili makampuni 7,058 kutoka makampuni 5,278 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 33.7, majina ya biashara 14,866 kutoka majina ya biashara 11,127 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 33.6, leseni za viwanda 105 kutoka leseni za viwanda 92 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 14.1 na alama za biashara na huduma 1,652 kutoka alama za biashara na huduma 1,724 mwaka 2009/2010.

Pia idadi sawa ya hataza 22 ilitolewa katika kipindi cha miaka miwili. Aidha, ili kuweza kutoa huduma kwa urahisi na kwa ubora zaidi, *BRELA* inaboresha mfumo wa utoaji wa huduma kwa mfumo wa kielektroniki. Tayari mfumo wa usajili kwa njia ya kisasa *(Registration Information Management System - RIMS)* umetengenezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani na kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Aidha, taratibu za upekuzi wa majina *(name search)* umeboreshwa na kuwekwa kwenye tovuti ya *BRELA* ili kumwezesha mdau yeyote kupata huduma hiyo popote alipo *(on-line)*. *BRELA* imeweka huduma mbalimbali ndani ya tovuti yake ya *www.brela-tz.org* ikiwa ni pamoja na kuweza kupata fomu zote za usajili popote, Katiba ya kampuni iliyorahisishwa *(Simplified MEMART),* maelekezo juu ya majina yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imefanya mazungumzo na *TCCIA* ili kushirikiana nao katika kutoa huduma saidizi kwa wateja hadi katika ngazi ya Wilaya kwa kuwa tayari wana mfumo wa kitekinolojia unaowasiliana katika wilaya 95. *TCCIA* watatoa huduma za kuwasaidia waombaji wa kusajili majina ya biashara na makampuni ambazo siyo za kisheria. Rasimu ya makubaliano *(MOU)* ya kutekeleza azma hiyo imekwishaandaliwa. *BRELA* imeanza kutembelea baadhi ya vituo vya *TCCIA* kwa lengo la kujionea hali halisi ya zana za kufanyia kazi na pia kutoa elimu kwa wajasiriamali ili wafahamu uwepo wa huduma hizo katika ofisi za *TCCIA* zilizo karibu nao. Aidha, *BRELA* ipo kwenye mazungumzo na *TRA* ili iweze kutoa huduma ya *TIN* kwa wateja mara wanaposajili makampuni na majina ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imefanya semina na warsha mbalimbali mikoani na jijini Dar es Salaam, imeshiriki maonesho ya Wiki ya Utumishi, Sabasaba, Nanenane na Siku ya Miliki Ubunifu Duniani. Maonesho haya husaidia kuelimisha juu ya shughuli za Wakala kwa wadau wote. Aidha, Wakala umetoa vipeperushi, vitabu vidogo vidogo na makala mbalimbali kwenye vyombo vya habari. Pia iliitisha mkutano wa vyombo vyote vya habari mwezi Februari, 2011 kuelezea uboreshaji mbalimbali uliokwishafanyika katika kuwafikia wadau nchi nzima kwa kutumia mtandao. Wakala pia hufanya ukaguzi kwenye maeneo ya biashara kuangalia na kuelimisha juu ya utekelezaji wa sheria za biashara na kutembelea viwanda. Hilo limefanyika Arusha, Dodoma, Kigoma, Manyara, Mbeya, Moshi, Mwanza, Songea na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala imefanya semina mbalimbali za wadau kwa kushirikiana na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani *(WIPO)* ambapo *branding strategy* itasaidia kuwezesha mazao

kama kahawa, chai, karafuu na mchele kuuzwa kwa bei nzuri kwenye masoko ya nje. Mkakati huu humsaidia mzalishaji na/au muuzaji nje ya nchi wa bidhaa zenye utambuzi wa pekee kufuatilia thamani halisi ya bidhaa anayozalisha ama kuuza nje ya nchi ambayo watumiaji wa bidhaa hiyo watakuwa tayari kuilipa. Aidha mkakati huu hupunguza sana ama kuondoa kabisa wizi wa thamani za bidhaa unaofanywa na madalali katika magulio ya bidhaa hizo ndani ya nchi. Kwa mfano, nchi ya Ethiopia imeutumia kikamilifu mkakati huu katika kuboresha thamani ya bidhaa ya kahawa ya nchi hiyo. Hivi sasa kahawa ya Ethiopia ni miongoni mwa kahawa maarufu sana duniani na inajulikana hivyo kwa kutumia mkakati huo. Vilevile wavumbuzi na *innovator* katika taasisi za *TIRDO, SIDO, COSTECH* na Vyuo Vikuu wamehamasishwa kuhusu matumizi bora ya miliki ubunifu kwa kuanzisha na kutumia kituo kilichopo *COSTECH (Tanzania Intellectual Property Advisory Service and Information Centre – TIPASIC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za kuandaa Mkakati wa Miliki Ubunifu, ilionekana kuna haja kwanza kufanya tathmini ya miliki ubunifu *(IP Audit).* Kamati ya Kitaifa *(National IP Audit Steering Committee)* iliyojumuisha wadau wote muhimu iliundwa na Kamati imefanya tathmini ya namna *IP Audit* itakavyotekelezwa. Wizara kwa kushirikiana na *BRELA* inafanya maandalizi ya kupata rasilimali watu na fedha kwa ajili ya kufanya tathmini hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Mashirika ya Miliki Ubunifu Kikanda na Kimataifa ya *African Regional Intellectual Property Organization (ARIPO)* na *World Intellectual Property Organization (WIPO)*. Wizara hulipa michango ya kila mwaka kwa mashirika yote mawili. Kwa *ARIPO, BRELA* inapata ada kwa kila hataza na alama ya biashara iliyosajiliwa *ARIPO* na mwombaji kuomba miliki ubunifu wake ulindwe hapa Tanzania. Katika mwaka huu, *BRELA* ilishiriki katika mikutano mbalimbali katika ngazi za Kikanda na Kimataifa ambayo inawezeshwa ama na *WIPO, ARIPO* na/au asasi nyingine za Kimataifa. Aidha, *BRELA* ilihudhuria Mkutano Mkuu wa Baraza la nchi Wanachama wa *WIPO* huko Geneva, Switzerland na mkutano uliofanyika Istambul, Uturuki ambapo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara alihudhuria pamoja na Mwenyekiti na Mjumbe mmoja wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imekuwa inatafuta jengo au eneo la kujenga ofisi zake zitakazowezesha kuwahudumia wateja na zilizo na mazingira mazuri ya utendaji wa kazi. *BRELA* imetenga fedha takriban shilingi bilioni tatu za kuanza kujenga jengo lake. Hadi sasa bado eneo la kujenga jengo la ofisi halijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, *COSOTA* imeendelea kutoa huduma mbalimbali ikiwemo usajili wa wanachama na kazi zao. Jumla ya wanachama 2,215 walisajiliwa kati ya hao watunzi na wasanii wa kazi za muziki ni 1,142, wachapishaji na wazalishaji wa kazi za muziki ni 35, watunzi na waigizaji wa kazi za maigizo ni 309, wachapishaji na wazalishaji wa kazi za maigizo ni 18, watunzi wa kazi za maandishi ni 669 na wachapishaji wa kazi za maandishi ni 42. Aidha, jumla ya kazi 9,461 zilisajiliwa zikiwemo kazi za muziki 8,202, maigizo 423 na maandishi 836.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* inaendesha zoezi la ukusanyaji wa mirabaha kutokana na matumizi ya kazi za muziki na filamu (maonyesho ya umma) katika mahoteli, baa, migahawa, kumbi za disko na majumba ya starehe. Katika mwaka 2010/2011 jumla ya shilingi 162,795,000.00 zimekusanywa, ambapo jumla ya leseni 746 zimetolewa kwa wamiliki wa maeneo husika. Makusanyo hayo yamegawanywa kama mirabaha na kunufaisha jumla ya watunzi na wasanii 1,142 wa fani ya musiki na filamu. Vilevile *COSOTA* imeanza zoezi la ukadiriaji wa mirabaha kutoka kwenye mabenki, makampuni ya simu na mashirika ya utangazaji. *COSOTA* inawasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ili kupata taarifa zitakazorahisisha zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti uharamia nchini, kesi 27 dhidi ya wakiukaji wa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki zilifunguliwa na kesi hizo zinaendelea katika Mahakama za Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Moshi na Singida. Kwa kushirikiana na *Multichoice (DSTV)* na polisi, kesi dhidi ya wanaokiuka taratibu za usambazaji wa matangazo zimefunguliwa katika mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga, Singida na Tabora. Baadhi ya kesi hizo zimeishatolewa hukumu na

watuhumiwa kulipa faini na kesi nyingine zinaendelea. Vilevile *COSOTA* imepokea migogoro 71 ya hakimiliki kati ya hiyo migogoro 44 imesuluhishwa na usuluhishi wa migogoro iliyobaki bado unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *COSOTA* na wadau mbalimbali likiwemo Shirika la *Rulu Arts Promoters* kwa ufadhili wa *BEST Advocacy Component* na *UNESCO* inafanyia marekebisho Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999. Aidha, maafisa wa *COSOTA* kwa kushirikiana na wataalamu wa sheria wanaendelea na zoezi la kurekebisha Kanuni za Utoaji Leseni kwa Matumizi ya Kazi za Muziki na Filamu za mwaka 2003 na kuandaa Kanuni za Ukusanyaji wa Mirabaha kutokana na uzalishaji na utoaji nakala za kazi za maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Ushindani imeendelea kusimamia ushindani kwa kudhibiti muungano wa makampuni *(mergers and acquisitions)* ambao unaathiri ushindani katika biashara. Kwa kipindi cha 2010/2011, Tume imepokea na kushughulikia maombi 19 ya muungano wa makampuni ikilinganishwa na maombi ya makampuni matano na yote kuridhiwa katika kipindi cha 2009/2010. Maeneo yaliyohusika ni pamoja na maduka makubwa *(supermarkets),* mawasiliano, mafuta ya petroli, utalii, kilimo na taasisi za fedha. Kati ya maombi 19 yaliyowasilishwa, Tume imeridhia muungano wa makampuni 13 bila masharti na makampuni mawili kwa masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010/2011, Tume imeendelea kufanya tafiti katika sekta mbalimbali za kiuchumi kwa lengo la kubainisha masuala ya kiushindani. Kupitia utafiti, Tume huweza kubainisha masuala ya kisera, kanuni na taratibu zinazoweza kuathiri ushindani na hivyo kuiwezesha Tume kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003. Katika mwaka 2010/2011, Tume imekamilisha tafiti katika sekta ndogo za saruji na tumbaku na matokeo ya utafiti yanafanyiwa kazi. Aidha, Tume inaendelea kufanya tafiti katika Sekta za Ujenzi, Sukari, Kahawa, Pamba, Mbolea, Benki, Bima, Mabati, Madawa na Vinywaji Baridi.

Aidha, Tume imekamilisha utafiti katika Sekta ya Sukari. Tafiti hiyo pamoja na mambo mengine ililenga kubainisha mahusiano yaliyopo kati ya wahusika mbalimbali katika Sekta ya Sukari hususan mahusiano baina ya wazalishaji wa ndani na waingizaji wakuu wa sukari kutoka nje ya nchi ili Serikali iweza kuchukua hatua stahiki. Utafiti umebainisha kuwa makampuni yanayoingiza sukari toka nje ya nchi yanaruhusiwa pia kununua na kusambaza sukari inayozalishwa na viwanda vya ndani. Utafiti umependekeza ziwekwe taratibu za kutenganisha wanunuzi na wasambazaji wa sukari inayozalishwa katika viwanda vya ndani na wale wanaoagiza sukari toka nje ya nchi ili kuimarisha ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Ushindani *(Fair Competition Tribunal - FCT)* lilikuwa na kesi sita zilizokuwa zinaendelea kusikilizwa ambazo zilisajiliwa mwaka 2009/2010. Aidha, Baraza lilisajili kesi mpya kumi na moja na hivyo kufanya idadi ya kesi za kusikilizwa katika kipindi cha 2010/2011 kuwa 17. Hadi kufikia mwezi Aprili 2011, kesi 11 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi na kesi sita zilikuwa katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Lengo la Baraza ni kesi kusikilizwa kwa miezi isiyozidi sita tangu tarehe ya kusajiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* Baraza la Ushindani limeweza kutekeleza malengo yake ya kujenga uwezo zaidi katika kushughulikia kesi kwa kupata mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yalihusisha wajumbe wote wa Baraza na Wafanyakazi watano ambapo walijifunza juu ya sekta zinazosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* na taratibu zinazofuatwa na Mamlaka hiyo katika kutatua migogoro. Aidha, Wajumbe wanne wa Baraza wamehudhuria mafunzo juu ya *better regulation, energy, water, communications and transport* kwenye taasisi ya *Public Administration International (PAI)* nchini Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Ushindani limeweza kutoa elimu kwa umma juu ya kazi zake kwa njia mbalimbali kama vile kuandaa kipindi cha Lijue Baraza la Ushindani ambacho kinarushwa mara nne kwa wiki kwenye vituo vya luninga vya Shirika la Habari la Tanzania *(TBC)* na

*ITV.* Katika vipindi hivyo, umma unaelimishwa pia juu ya taratibu za kufuata wakati wa kusajili na kusikiliza kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, pamoja na kusikiliza kesi za rufaa, Wizara kupitia Baraza na Tume ya Ushindani iliweza kuchambua Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 na kubainisha mapungufu yanayosababisha taasisi hizo zisifanye kazi kwa ufanisi uliokusudiwa. Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo yapo katika hatua za mwisho ili yafikishwe Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha tena kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)* ilikamilisha uundaji wa trekta dogo aina ya *CFT 22 (CAMARTEC FASTRUCKTOR)* lenye *horse power 22 (HP22)* linalofaa kwa matumizi mbalimbali *(multi-purpose tractor).* Tayari *CAMARTEC* imetengeneza matrekta sita ya awali katika karakana yake. Matrekta hayo yalifanyiwa majaribio huko Chanika, Dar es Salaam, Mlandizi Pwani, Dakawa na Gairo Morogoro na kuonesha mafanikio makubwa. Rasimu ya upembuzi yakinifu na Mpango wa Uwekezaji Kibiashara *(Business Investment Plan)* kwa ajili ya uzalishaji wa matrekta hayo na zana mbalimbali kibiashara vimeandaliwa. Makusudio ni kuanzisha Kampuni ya kuzalisha matrekta hayo na zana za kilimo katika eneo la *Kilimanjaro Machine Tools Complex,* Moshi ifikapo Januari, 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *CAMARTEC* iliendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kueneza Matumizi ya Teknolojia ya Biogesi Ngazi ya Kaya *(Tanzania Domestic Biogas Programme – TDBP)* chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania na Uholanzi. Hiyo ni Programu ya Kitaifa ya miaka mitano iliyoanza kutekelezwa mwaka 2009 kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa madhumuni ya kuibua sekta endelevu ya *Biogas* kwa kujenga mitambo 12,000. Programu hii ilizinduliwa rasmi tarehe 26 Machi, 2011 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal. *TDBP* imeeneza mitambo 1,000 ya *Biogas* katika mikoa 11 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Pwani, Ruvuma, Singida na Tanga. Aidha, waashi 490, wasimamizi 42 na watumiaji 367 wa teknolojia ya *Biogas* walipata mafunzo juu ya ujenzi wa mitambo, usimamizi na udhibiti wa ubora na matumizi mazuri ya teknolojia ya *Biogas.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Taasisi yake ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo *(TEMDO)* ilikamilisha ubunifu na uendelezaji wa mashine mbalimbali za kusindika kahawa, za kutengeneza bidhaa za ngozi na mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji. Aidha, Taasisi ya *TEMDO* imeendelea kuboresha mashine za kusindika matunda, asali, karanga, kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya upepo na kutengeneza mkaa unaotokana na taka za mbao, vumbi la mkaa na mabaki ya mimea *(briquettes).* Mashine hizo zilihaulishwa kupitia *SIDO* ambayo inazitengeneza na kuzisambaza kibiashara nchini. Vilevile mtambo wa kutengeneza *briquettes* ulihaulishwa kupitia Shirika la Mzinga. Mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za upepo umefungwa Arusha kwa majaribio zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kutoa mchango kwenye sekta ya afya na utunzaji wa mazingira, Taasisi ya *TEMDO* imeboresha kiteketezi cha taka ngumu zikiwemo za hospitali *(solid/hospital waste incinerator).* Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), *TEMDO* imefunga kiteketezi hicho katika Chuo cha Mafunzo na Tiba Muhimbili, Hospitali za Mawenzi, Kibong'oto, Masama, Kisiki, Hai, Ngarenaro, Kisongo na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Utumiaji wa viteketezi hivyo umepunguza uagizaji wa vifaa hivyo kutoka nje ya nchi na hivyo kuokoa fedha za kigeni. *TEMDO* itahaulisha teknolojia hiyo kupitia Shirika la Mzinga ili zitengenezwe na kusambazwa nchini kibiashara. Natoa wito kwa wazalishaji taka ngumu hususan za hatari kama za hospitali kutumia viteketezi vinavyotengenezwa na *TEMDO* ili kupunguza athari za uchomaji onyo wa taka hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utafiti la Maendeleo ya Viwanda nchini *(TIRDO)* kwa kushirikiana na Kampuni ya *Intermech* ya Morogoro liliunda mashine ya kukamua na kusafisha mafuta ya mawese yenye ubora na viwango vinavyokubalika. Mashine hizo zitasaidia wazalishaji wa mafuta ya mawese kuondokana na njia zisizo na ubora katika kukamua mafuta kama vile

kutwanga, njia ambayo inapoteza muda na hutoa mafuta yasiyo na ubora. Majaribio yaliyofanywa kwa mashine hiyo yalionesha ufanisi mzuri ambapo uwezo wa kukamua mafuta ni kilo 100 za mbegu za mchikichi kwa saa. Pia mafuta yaliyokamuliwa na kusafishwa na mashine hiyo yalipimwa na ubora wake ukabainika kuwa na viwango vya mafuta ya mawese ya kula vinavyosimamiwa na Shirika la Viwango la Tanzania *(TBS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIRDO* imetengeneza mashine za kusindika vyakula na matunda *(hammer mill, juice extractor),* ambazo zimetumia malighafi zisizo na madhara kwa walaji na zinazokubalika Kimataifa kama vile chuma cha pua *(stainless steel).* Aidha, katika hatua ya awali Shirika limeendeleza ujenzi wa majengo ya viatamizi *(incubators)* vya teknohama na usindikaji wa mazao ya kilimo kwa ajili ya kuinua viwanda na wajasiriamali. Pia *TIRDO* imetengeneza makaushio yanayotumia teknolojia ya ukaushaji kwa kutumia jua ambapo makaushio 17 wamesambaza kwenye vijiji 17 vya mikoa ya Mtwara na Lindi chini ya ufadhili wa *FAO.* Vilevile Shirika limebuni kaushio kubwa linalotumia nishati ya jua lenye uwezo wa kukausha kilo 150 za muhogo kwa siku. Kaushio hilo litatumika kukaushia unga wa muhogo wenye ubora wa viwango vya Kimataifa. Majaribio yanaonesha kuwa unga unaokaushwa una kiwango cha unyevu kinachotakiwa cha asilimia 12.95 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 13 wa kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limeendelea na shughuli za kuimarisha maabara ya mazingira ili kupata hadhi ya Kimataifa ya uhakiki *(accreditation)* pamoja na kuongeza vifaa vya kuboresha uwezo wa maabara wa kufanya kazi. Hiyo ni pamoja na kununua *flue gas analyzer* ya kisasa yenye uwezo wa kupima gesi zaidi ya kumi, kuvifanyia *calibration* vifaa vilivyopo na pia kurekebisha upungufu ambao umejitokeza wakati wa tathmini ya awali. Aidha, maabara imefanya ukaguzi wa ndani kabla ya tathmini kutoka kwa wakaguzi wa nje. Vilevile Shirika limechukua hatua za awali katika kuhakiki maabara ya vifaa vya kihandisi ili iweze kufikia viwango vya Kimataifa. Hatua hizo ziliwezesha utengenezaji wa machapisho ya ubora wa maabara na uboreshaji wa vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limetoa mafunzo kwa wazalishaji bidhaa kuhusu Mfumo wa Ufuatiliaji *(treaceability)* kama njia ya kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia katika masoko zinatimiza masharti na viwango vinavyohitajika katika masoko hayo hususan bidhaa za vyakula. Mfumo wa ufuatiliaji umeainishwa katika Sheria Na. 178/2002 ya Vyakula ya Nchi za Ulaya *(EU Food Law No. 178/2002),* ambayo inahitaji kila bidhaa ya chakula iweze kufuatiliwa tangu shambani hadi kwa mlaji. Hilo ni sharti kuu ambalo ni lazima litekelezwe. Katika kuwezesha bidhaa za Tanzania kuingia katika soko la Ulaya, *TIRDO* imetoa mafunzo kuhusu Mfumo wa Ufuatiliaji kwa wasindikaji 3,574 katika bidhaa za asali, chai, kahawa, korosho, mifugo na samaki na pia kwa viongozi wa Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Lengo ni kuimarisha na kuboresha uwezo wa wazalishaji kuweza kuzalisha bidhaa bora na salama. Pia Shirika lilisaidia wajasiriamali wa kahawa kuweza kutumia Teknolojia ya Kompyuta ya Mfumo wa Ufuatialiaji *(Computerized Traceability System).* Teknolojia hiyo inawasaidia wajasiriamali kuendeleza uuzaji nje mazao ya chakula na biashara kwa kufuata viwango vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusaidia bidhaa za Tanzania kuingia katika masoko mbalimbali, Wizara kupitia *TIRDO* ilihamasisha sekta binafsi kuhusu umuhimu wa ufuatiliaji wa bidhaa *(traceability)* na matumizi ya mfumo wa utambuzi wa bidhaa wa *GS1* unaotumia nembo za mistari *(bar codes).* Jumla ya makampuni 120 katika Kanda za Ziwa, Kusini, Kaskazini na Dar es Salaam yalihamasishwa na kufanyiwa mafunzo ya mfumo wa ufuatiliaji na mfumo wa Kimataifa wa utambuzi *(GS1). TIRDO* kwa kushirikiana na *SIDO* na sekta binafsi hususan *TCCIA, TPSF, ZCCIA, ACT, CTI, TWCC* na *TAHA* iliwezesha kukubalika kuanzishwa kwa shughuli na huduma za *GS1* hapa nchini. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maombi hayo yamekubaliwa mwezi Mei, 2011 na maandalizi ya kuwezesha kuanza kutolewa kwa huduma hii nchini yamefikia hatua nzuri na inatarajiwa kuwa huduma hii itaanza kutolewa kabla ya kufika mwezi Septemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi zilizofanywa na *TIRDO* na wadau wengine kama ilivyoelezwa hapo awali, Tanzania imepata usajili wa *GS 1* na kuruhusiwa kutumia mfumo wa utambuzi wa bidhaa *(bar codes)* ambao wajasiriamali wa hapa nchini wamekuwa wakiupata toka nchi za Kenya, Afrika Kusini na Denmark kwa gharama kubwa. Pia sekta binafsi watapatiwa

mafunzo ya kuelewa na kutumia mifumo ya elektroniki ya biashara duniani kama vile *Electronic Product Coding (EPC)* na *e-commerce.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida nyingi za kuwa na Mfumo wa Utambuzi wa Bidhaa kwa kutumia *bar codes* kwani ni rahisi kujumuisha taarifa nyingi za kuwezesha kutambua bidhaa, nchi zilikozalishwa, mfumo wa uzalishaji, ubora na usalama wa bidhaa na ufuatiliaji wa bidhaa *(traceability).* Hivyo mfumo huo unafanya wanunuzi kuwa na uhakika wa usalama wa bidhaa wanazonunua na zinakotoka. Aidha, mfumo huo husaidia katika uboreshaji wa uthibiti wa mfumo wa usambazaji na kulinda thamani ya jina la bidhaa. Pia kiuchumi mfumo wa ufuatiliaji husaidia kuokoa biashara isiporomoke kwa kuwa na kumbukumbu bayana zilizohifadhiwa katika mlolongo wa ufuatiliaji. Mfumo huo utasaidia wazalishaji wadogo hadi wakubwa kuuza bidhaa zao kwenye maduka makubwa ya bidhaa *(supermarkets)* ya ndani na pia kurahisisha bidhaa zetu kupenya katika masoko ya nje ikiwa ni pamoja na yale ya kikanda *(EAC* na *SADC)* na masoko ya kiupendeleo kama *AGOA* na *EBA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 *TIRDO* kwa kushirikiana na asasi isiyo ya Kiserikali ilihamasisha matumizi ya TEKNOHAMA na kuwasaidia wajasiriamali kupata masoko ya bidhaa za mazao ya kilimo yaliyosindikwa. Aidha, juhudi hizo zimeiwezesha *TIRDO* kuwafikia wajasiriamali 172 kutoka vikundi 79 katika mikoa ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Lindi na pia kuwajengea tovuti ambazo zitatangaza bidhaa zao Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti*, TIRDO* imetoa mafunzo yaliyolenga kuboresha bidhaa za uyeyushaji chuma kwa mafundi 13 kutoka viwanda nane. Mafunzo yalitolewa pia kwa viwanda vya kufua vyuma katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Ruvuma na Kilimanjaro na kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuweza kuboresha bidhaa zao. Aidha, Shirika lilitoa mafunzo ya uchomeaji vyuma kwa mafundi na wajasiriamali 40 katika Manispaa ya Iringa. Vilevile Shirika katika mwaka 2010/2011 limeendelea kupima na kutoa ushauri kwa wenye viwanda kuhusu uchafuzi wa mazingira utokanao na uzalishaji na njia za kuzuia uchafuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika mwaka 2010/2011, *TIRDO* imetengeneza makaushio 41 ya matunda, mboga na samaki na kusambazwa kwa njia ya kufundisha vikundi katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mara, Mwanza, Mtwara na Pwani. Wajasiriamali wapatao 534 wa mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Morogoro, Pwani na Ruvuma wamefundishwa uzalishaji wa uyoga na Shirika limetengeneza matembe 26 ya kukaushia tumbaku katika mkoa wa Ruvuma. Wajasiriamali 326 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Morogoro, Mtwara, Pwani, Ruvuma na Tanga wamepata mafunzo ya kusindika matunda, unga bora wa mihogo usio na sumu *(cynanide)* na nyanya. Mashine 25 za usindikaji zimesambazwa katika mikoa hiyo. Wazalishaji na wasindikaji katika viwanda 38 wamepewa mafunzo kuhusu Mfumo wa Ufuatiliaji *(traceability)* kama njia ya kuhakikisha kuwa bidhaa zinazouzwa ndani na nje ya nchi zinatimiza masharti ya viwango vya juu. Aidha, wajasiriamali 147 wa Kyela walifundishwa jinsi ya kutengeneza mafuta bora ya mawese. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Duniani *(UNIDO)* iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza sekta ya viwanda nchini. Moja ya maeneo yaliyofaidika ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalamu katika masuala yanayohusu uchambuzi na maandalizi ya sera na mikakati ya maendeleo ya viwanda, kutekeleza programu ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda kwa kutumia mfumo wa mlolongo wa thamani, kutoa mafunzo ya teknolojia na uzalishaji wa bidhaa bora kwa wajasiriamali pamoja na teknolojia za kisasa zinazohusika na usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuwawezesha wajasiriamali hao kukua kiteknolojia na kiuzalishaji na hivyo kuzalisha bidhaa bora zilizoongezwa thamani na zinazouzika ndani na nje ya nchi. Aidha, Shirika lilitekeleza programu mbalimbali zenye lengo la kusaidia upatikanaji wa nishati jadidifu *(renewable energy)* sambamba na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 130 na wenye viwanda juu ya uzalishaji unaozingatia uhifadhi wa mazingira*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 jumla ya wajasiriamali wapatao 300 walipata mafunzo ya ubanguaji wa korosho sambamba na kupewa msaada wa mashine ndogo 240 kwa ajili ya kufanya ubanguaji wa awali wa korosho katika Wilaya za Masasi na Tandahimba mkoani Mtwara. Kupitia utaratibu wa *One UN,* unaotekelezwa na Mashirika ya

Umoja wa Mataifa kwa kutoa huduma pamoja, *UNIDO* ilitoa mashine za kisasa kwa ajili ya kukamua ufuta katika Wilaya ya Ruangwa Mkoani Mtwara. Usimikaji wa mashine hizo umekamilika na majaribio ya awali yamefanyika na kuonesha matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uboreshaji wa nishati vijijini, programu za *UNIDO* ziliwezesha vijiji vinne vya mfano ambavyo ni Nyangao (Lindi), Ilagala (Kigoma), Tanga na Zanzibar kupata teknolojia na mafunzo ya utumiaji wa mitambo midogo ya uzalishaji nishati mbadala na jadidifu kwa matumizi ya uzalishaji. Aidha, mitambo midogo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua, taka na mabaki ya mimea ilisimikwa katika mikoa ya Kigoma, Lindi na Tanga. Matumizi ya nishati mbadala yanawezesha uendeshaji wa miradi ya maendeleo, kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira pamoja na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi *(mitigate climate change). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kimeongeza kiwango cha udahili kutoka jumla ya wanachuo 7,007 kwa mwaka 2009/2010 hadi kufikia wanachuo 10,704 katika mwaka 2010/2011 ambalo ni ongezeko la asilimia 53. Udahili kwa mwaka 2009/2010 kwa kila Kampasi ulikuwa ni 4,069 (Dar es Salaam), 2,108 (Dodoma) na 830 (Mwanza) ambapo kwa mwaka 2010/2011 udahili kwa kila kampasi ulikuwa ni 5,878 (Dar Es Salaam), 3,080 (Dodoma) na 1,746 (Mwanza). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* imeendelea kuboresha Kampasi ya Dar es Salaam, ambapo ujenzi wa Jengo la Vipimo na Mizani upo katika hatua za mwisho ili kukiwezesha Chuo kudahili wanachuo wengi zaidi katika fani ya vipimo na mizani na kuimarisha mafunzo katika fani hiyo muhimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mafuzo ya vipimo na mizani kwa vitendo, Chuo kimenunua mashine na vifaa vingine kwa ajili ya maabara ya vipimo na mizani chuoni. Vifaa hivyo vimenunuliwa kupitia mradi wa *Marching Grant* uliokuwa ukisimamiwa na Mfuko wa Uendelezaji wa Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF)* ambapo jumla ya vifaa vyenye thamani ya dola za Kimarekani 197,727.04 vilinunuliwa. Aidha, Chuo kimepata vifaa mbalimbali vya kufundishia na kusomea kwa msaada wa *TPSF.* Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta 412, viti 412 na meza 206, *laptop* 35, *projectors* na *projection screens* 20 na viyoyozi 20. Jumla ya thamani ya vifaa hivyo ni dola za Kimarekani 865,717 sawa na shilingi 1,302,038,368.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la *TIRDO* ilifanya tathmini katika viwanda vya kusindika ngozi kuhusu uchafuzi wa mazingira. Viwanda sita vya ngozi katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro na Pwani vilitembelewa na sampuli za maji taka yanayotokana na shughuli za usindikaji wa ngozi yalifanyiwa uchunguzi katika maabara za *TIRDO.* Uchunguzi huo ulisaidia kubainisha viwango vya viini vya uchafuzi wa mazingira vinavyotokana na shughuli zao za uzalishaji. Ushauri ulitolewa kwa viwanda hivyo kuhusu matumizi ya teknolojia mbadala za uzalishaji zinazozingatia utunzaji wa mazingira. Vilevile kwa kupitia maonesho ya Kitaifa kama Wiki ya Viwanda Duniani, Sabasaba na Nanenane Wizara imeendelea kutoa elimu na mafunzo juu ya Sera ya Taifa ya Mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na Kanuni zake kwa wadau wa Sekta ya Viwanda kwa lengo la kuzijua na kuzitekeleza. Aidha, Wizara imeendelea kushiriki katika kufanya tathmini ya mazingira katika miradi mipya ya viwanda pamoja na miradi iliyoanzishwa bila kufanya tathmini hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea na jitihada za kutoa mafunzo kuhusu mbinu za kupambana na kuthibiti rushwa. Elimu hiyo ilitolewa kwa umma kupitia maonesho mbalimbali ya Kitaifa kama vile Sabasaba, Nanenane na Wiki ya Utumishi wa Umma. Pia mafunzo yalitolewa kupitia vikao vya idara, vitengo na taasisi zake ambayo hufanyika kwa wastani kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, watumishi waliothirika na UKIMWI walipata mafunzo ya jinsi ya kutunza afya zao. Pia Wizara iliendelea kutoa huduma ya lishe, virutubisho *(food supplements)* na usafiri kwa waathirika waliojitokeza. Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ziliendelea kukumbushwa umuhimu wa kujali afya za wafanyakazi likiwemo suala la elimu mahala pa kazi ya kupambana na maambukizi mapya ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilikuwa na jumla ya watumishi 213 waliokuwa kwenye orodha ya mishahara na iliajiri watumishi wapya watatu ambao walipangwa na Sekretarieti ya Ajira. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, Wizara haikufikia malengo yake iliyojiwekea ya kuajiri watumishi kumi na nane kulingana na ikama ya mwaka 2010/2011.

Aidha, kwa kipindi hicho Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 11 ili kujaza nafasi mbalimbali kwa lengo la kukidhi Miundo ya Utumishi *(Scheme of Service)* na pia kuziba nafasi zilizoachwa wazi kutokana na kustaafu utumishi wa umma, kuacha kazi na kuhamishwa. Katika kipindi hicho hicho, Wizara iliweza kusomesha jumla ya wafanyakazi 25 kulingana na Mpango wa Mafunzo wa Wizara. Kati ya hao, 15 walikwenda mafunzo ya muda mrefu na kumi ya muda mfupi kwenye vyuo vya ndani na nje ya nchi. Vilevile Wizara ilitumia mfumo wa wazi wa mapitio na tathimini ya utendaji kazi kwa watumishi *(Open Performance Appraisal System-OPRAS)* wakati wa kupandisha vyeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mipango ya Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, zipo changamoto za jumla zilizojitokeza wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa sekta hii ambazo zinahitaji ushirikishwaji wa sekta mbalimbali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Changamoto zinazoikabili Wizara hii ni Wizara na taasisi zake kutengewa na kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake, upatikanaji wa fedha za fidia kwa maeneo yaliyobainishwa kwa ajili ya uwekezaji chini ya *EPZA,* upatikanaji wa umeme wa uhakika na maji, kuwa na miundombinu imara kama vile barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, mifumo ya taarifa, maghala na *cold rooms* kwa ajili ya usafirishaji wa malighafi, bidhaa na nyenzo yenye kuwezesha sekta shindani ya viwanda na biashara na kukabiliana na msukosuko wa soko la mitaji, soko la fedha na uchumi wa dunia ambayo kwa kiasi kikubwa imesababisha upungufu wa uwekezaji na mauzo nje. *(Makofi)*

Pia kuwezesha upatikanaji wa mitaji na teknolojia sahihi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, usindikaji na kuongeza thamani na ubora wa mazao na bidhaa zitakazowezesha kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje, kuwezesha upatikanaji wa wataalamu bingwa na wa kutosha katika nyanja za viwanda, biashara, masoko na viwanda vidogo na biashara ndogo, kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, Biashara na Masoko, kuwezesha ushindani wa haki katika soko, utoaji wa elimu ya biashara na ujasiriamali kwa Watanzania walio wengi, upitiaji wa Sheria zilizopitwa na wakati na kusimamia utekelezaji wake na upatikanaji wa masoko ya uhakika na yenye masharti nafuu kwa bidhaa na huduma zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji na kufanya biashara.

Katika mwaka 2011/2012, malengo ya sekta ya viwanda, biashara, masoko na viwanda vidogo na biashara ndogo ni pamoja na kuweka kipaumbele katika utekelezaji na ukamilishaji wa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, malengo ya sekta ya viwanda ni kuendeleza uhamasishaji wa uwekezaji na kutoa kipaumbele kwa viwanda vinavyoongeza thamani mazao ya kilimo, kuendeleza utekelezaji wa Mkakati Unganishi na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda Nchini hususan kuandaa miradi na mikakati ya sekta ndogo za viwanda, kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vipya vya kusindika ngozi na bidhaa za ngozi. Hii itakwenda na programu mahsusi inayolenga kujenga miundombinu *(industrial villages/clusters)* itakayowezesha viwanda vidogo na vya kati *SME* kuongeza uzalishaji wa bidhaa za ngozi nchini na kuendeleza utoaji wa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi na ubora wa bidhaa za viwanda ikiwa ni pamoja na uzalishaji unaozingatia hifadhi na kulinda mazingira katika shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani.

Pia kuendelea na ushiriki katika ukamilishaji wa Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na nchi wanachama wa Jumuiya nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* kuanza maandalizi ya awali ya kufanya sensa ya

viwanda Tanzania. Sensa kama hiyo kwa mara ya kwanza ilifanyika mwaka 1989. Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO,* Ofisi ya Takwimu ya Taifa *(NBS),* sekta binafsi na wadau wa maendeleo itaendelea na majadiliano ya kuona namna ya kutekeleza kazi hiyo ifikapo mwaka 2013 na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma ghafi na chuma cha pua kwa kutumia chuma cha Liganga ambapo uchorongaji na uandaaji wa upembuzi yakinifu utaanza mwaka huu wa fedha, ujenzi wa Mgodi wa Chuma, Mgodi wa Makaa ya Mawe na Kiwanda cha kuzalisha chuma ghafi *(sponge iron)* unatarajiwa kuanza mwaka 2012 na uzalishaji wa chuma ghafi unatarajiwa kuanza mwaka 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kasi mpya, ikiwa ni pamoja na kukamilisha uchorongaji na upembuzi yakinifu ifikapo Desemba, 2011 na kuanza ujenzi wa Mgodi wa Chuma, Mgodi wa Makaa ya Mawe na Kiwanda cha kuzalisha chuma ghafi mwaka 2012, kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe wa Ngaka Kusini (Mbalawala na Mhukuru huko Mbinga) na kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kibaiolojia za kuua viluwiluwi vya mbu wa Malaria *(TAMCO* - Kibaha).

Pia kuendelea na usindikaji mazao ya kilimo *(agro-processing of rubber, sweet sorghum, meat processing),* kupitia *NDC* ambayo imejipanga kutekeleza miradi hiyo kwa njia ya ubia kati yake, wawekezaji na wakulima wadogo, kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kutokana na upepo huko Singida, kukamilisha zoezi la ubainishaji wa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* katika Mikoa mitatu iliyobaki ya Dodoma, Rukwa na Tabora, kukamilisha taratibu za uanzishaji Mfumo wa Kituo cha Utoaji Huduma *(One Stop Service Centre)* kwa wawekezaji katika eneo la *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone,* kukamilisha uandaaji Mfumo wa *SEZ,* ili usajili wa wawekezaji kupitia mfumo huo uanze kutumika na kukamilisha uandaaji wa Mpango Kamambe *(Master Plan)* katika eneo la kipaumbele la *Bagamoyo SEZ* na kuanza ujenzi wa miundombinu ya msingi kwa kushirikiana na sekta binafsi. *(Makofi)*

Pia kuendelea na uhamasishaji wa wawekezaji wa kujenga miundombinu na wa kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* na kwa kushirikiana na *UNIDO* kuendelea kusaidia maendeleo ya sekta ya viwanda kwa kutoa kipaumbele katika mafunzo yanayolenga kuongeza ujuzi kwa wazalishaji, kusaidia utambuzi wa teknolojia sahihi za uzalishaji, uhaulishaji wa teknolojia, uchambuzi wa sera, uendelezaji wa nishati jadidifu, biashara na upatikanaji wa masoko, taarifa za viwanda na usimamizi wa Sera ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, malengo ya sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo ni kuendeleza zoezi la uperembaji na tathmini ya utekelezaji wa sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo, kuongeza kasi ya upatikanaji na usambazaji taarifa zinazohusiana na sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani katika maeneo walioko wajasiriamali hasa vijijini, kutafuta utaratibu wa kuzalisha kwa wingi teknolojia zinazofaa na kuzisambaza kwa watumiaji, kutoa ujuzi maalumu wa kuzibadilisha rasilimali hasa mazao ya kilimo, misitu na mifugo kuwa bidhaa, kujenga miundombinu itakayowafanya wajasiriamali hasa wa vijijini kupata sehemu za kufanyia kazi na kujenga misingi ya kusaidia utengenezaji wa bidhaa mpya kutokana na mawazo ya wajasiriamali. *(Makofi)*

Pia kutoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara, kuwawezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara na kutengeneza sehemu za kuonesha bidhaa zao, kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapodhihirika kuhitajika na kujenga uwezo wa uzalishaji wa zana za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, malengo ya sekta ya biashara ni kuendelea kusimamia na kutekeleza Mikataba na Itifaki mbalimbali ambayo Tanzania imeridhia chini ya makubaliano kati ya nchi na nchi *(bilateral),* kikanda na ile ya Kimataifa, kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara wa Wilaya, Manispaa na Majiji kuhusu fursa za masoko ya nje ikiwa ni pamoja na sheria na kanuni za kuingia masoko hayo hususan yale ya upendeleo yanayotolewa chini ya mpango wa *AGOA, EBA,* nchi kama Canada, China, India na Japan na yale ya Kikanda

na Kimataifa kwa mfano *SADC* na *EAC,* kusimamia taratibu na sheria za biashara chini ya makubaliano ya *WTO* ikiwa ni pamoja na maadili ya ushindani katika uchumi ili kuliwezesha Taifa kuhimili changamoto za biashara ya Kimataifa na kuweka sera, sheria, kanuni na taratibu za kukuza na kuimarisha ulinzi na haki za uvumbuzi na ubunifu *(intellectual property rights)* na kuendelea kuimarisha mahusiano kati ya nchi na nchi *(bilateral),* kikanda na yale ya kimataifa kwa lengo la kuendelea kukuza fursa za masoko kwa bidhaa zetu.

Pia kutekeleza Mkakati Maalumu wa Kukuza Mauzo Nje (*Export Development Strategy - EDS),* kuongezea thamani mazao, bidhaa na huduma nje ya nchi ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini, kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ili kuhakikisha inaendana na mfumo wa utandawazi katika nyanja za kibiashara, kuendelea kuimarisha vituo vya Biashara vya Tanzania vilivyopo London na Dubai na kupeleka Waambata wa Biashara nchini China na Marekani, kuendeleza majadiliano ya Ubia wa Uchumi kati ya *EAC* na *EU* na kuendelea kushiriki majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Kanda za *COMESA, EAC* na *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, malengo ya sekta ya masoko ni kukamilisha mkakati wa mfumo mpana na unganishi wa taarifa za masoko unaolenga kukuza biashara ya ndani na mauzo nje, kukusanya, kuhifadhi, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko kwa wadau kwa njia za kisasa zaidi ili kuwajengea uwezo wazalishaji na wafanyabiashara kuzalisha zaidi na kuuza katika masoko yenye bei shindani, kuendeleza vituo vya pamoja vya mipakani vya Tunduma/Nakonde na Kabanga/Kobero, kuendelea kuboresha miundombinu ya masoko hususan masoko, magulio, maghala na barabara za vijijini, kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini na kuanzisha soko la bidhaa. *(Makofi)*

Pia kukuza matumizi ya mfumo wa utambuzi wa bidhaa kwa kutumia nembo za mistari *(bar codes)* unaoratibiwa na Shirika la Kimataifa la *GS1* lenye Ofisi zake huko Brussels Ubelgiji, kuendeleza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, kutekeleza Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BARA), kufanya tafiti za masoko ya mazao na bidhaa na kutangaza bidhaa za Tanzania kupitia maonesho ya ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Mamlaka ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* itafanya yafuatayo:-

Kwanza kuendelea na utafiti wa mfumo wa biashara ya ndani katika Mikoa na Wilaya zote nchini ili kuandaa mapendekezo yatakayowezesha kuundwa kwa Mfumo wa Masoko wa Kitaifa utakaosaidia kuongeza uzalishaji na kuwa na masoko endelevu ya bidhaa hapa nchini. Pili, kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajasiriamali katika vituo vya Zanzibar na Mwanza.

Tatu, kuratibu uandaaji wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Maonesho ya Kisekta, Tamasha la miaka 50 ya Uhuru, pamoja na uratibu wa maonesho ya kimataifa na nchi za Kenya, Rwanda, Malawi na China na nne, kuimarisha Ofisi ya Zanzibar ili iweze kusaidia juhudi za kukuza sekta ya biashara Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Tume ya Ushindani imepanga kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kutangaza shughuli za Tume kwa umma ili kuongeza *compliance,* pili, kumuelimisha na kumlinda mlaji, tatu, kuboresha elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kama radio, luninga na magazeti kuhusiana na bidhaa bandia na madhara yake kwa binadamu na mali zake, nne, kupambana na kudhibiti makampuni yanayokula njama kwa pamoja kwa kupanga bei, na kwa kudhibiti kiasi cha bidhaa inayopelekwa kwenye soko *(output restrictions between competitors)* na nne, kufanya uchunguzi wa masoko na kusikiliza kesi za ushindani. *(Makofi)*

Tano, kufuatilia na kuidhinisha muungano wa makampuni, sita kuongeza mafunzo kwa rasilimali watu wa Tume jinsi ya kutumia mifumo mbalimbali kama *ASCUDA++(TRA)* na *IPM tool (WCO)* ili kuwezesha Tume ya Ushindani kupambana na bidhaa bandia kwa ufanisi zaidi, saba, kuboresha mahusiano na Taasisi nyingine za Serikali kama *TRA, TFDA,* Polisi, *TBS* na Ofisi ya

Mawanasheria Mkuu wa Serikali kupitia vikao vitakavyopangwa na Tume kwa mujibu wa Kanuni ya Alama za Bidhaa ya mwaka 2008 na kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji litatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia maslahi ya mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye Tume ya Ushindani, Mamlaka za Udhibiti na Serikali kwa ujumla;

(ii) Kuendelea kupokea na kusambaza habari na maoni yenye maslahi kwa mlaji;

(iii) Kuanzisha Kamati za Mlaji za Mikoa na Sekta na kushauriana na kamati hizo; na

(iv) Kushauriana na wenye viwanda, Serikali na jumuiya nyingine za walaji katika mambo yenye maslahi kwa mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Ushindani litatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusikiliza kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa Ushindani katika soko na Udhibiti wa Bidhaa na Huduma;

(ii) Kujenga uwezo zaidi wa Baraza katika kushughulikia kesi hizo;

(iii) Kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza katika Uchumi; na

(iv) Kwa kushirikiana na Tume ya Ushindani, kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Shirika la Viwango kwa mwaka 2011/2012 ni:-

(i) Kutoa mchango muhimu katika sekta ya ufungashaji wa bidhaa kupitia Kituo cha Ufungashaji *(Packaging Technology Centre)* ambacho kwa sasa hivi kiko katika hatua ya majaribio ya awali. Kituo kitatoa mafunzo ya huduma za kupima sampuli za viwanda vya ufungashaji kwa lengo la kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kuhakiki vifungashio (packaging materials) kwa bidhaa zile zinazotoka nje ya nchi;

(ii) Kuendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri *(laboratory accreditation)* ili kuongeza kukubalika kwa bidhaa za Tanzania katika soko la kimataifa;

(iii) Kuanza utekelezaji wa utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini *(Preshipment Verification of Conformity to Standards – PVoC).* Utaratibu huo utasaidia Tanzania isiwe jalala la bidhaa hafifu kutoka nje ya nchi;

(iv) Kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Serikali vikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania *(TFDA),* Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA),* Tume ya Ushindani *(FCC)* na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenye ubora unaokubalika;

(v) Kuongeza idadi ya utoaji wa leseni kutoka leseni 100 kwa mwaka hadi kufikia leseni 120 katika mwaka 2011/2012;

(vi) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini kote kuhusu viwango vya udhibiti wa ubora wa bidhaa na vyeti vya ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje zinatarajiwa kuwa 2,800 kwa mwaka 2011/2012; na

(vii) Kuendelea na upimaji sampuli za bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Wakala wa Vipimo kwa mwaka 2011/2012 ni:-

(i) Kuanza uhakiki wa vipimo vingine vinavyotumika kwa biashara kama vile mita za umeme, mita za maji na mitungi ya gesi ya kupikia;

(ii) Kuimarisha Kitengo cha Vipimo Bandarini *(WMA Ports Unit)* ili kiweze kutoa huduma kwa makampuni yanayoagiza mafuta kwa ufanisi zaidi;

(iii) Kuendelea kukagua usahihi wa bidhaa zilizofungashwa *(quantities in pre-packed goods)* zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini na pia kutoka nje ya nchi;

(iv) Kufanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa ujenzi wa Jengo la Wakala *(Vipimo House)* ambalo litakuwa na ofisi za Makao Makuu ya Wakala, maabara za kisasa, na pia litatumika kama kitega uchumi;

(v) Kufanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa ujenzi mpya na wa kisasa (eneo la kupimia magari yanayosafirisha mafuta) katika eneo la Wakala huko Misugusugu, Pwani;

(vi) Kukamilisha taratibu za utungaji wa Sheria mpya ya Vipimo *(Legal Metrology Act*) ili kukidhi matakwa ya sasa ya biashara na pia kuzingatia maridhiano yaliyofikiwa na nchi kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya vipimo;

(vii) Kukamilisha taratibu za kusitisha matumizi ya mizani ya rula *(steel yard)* katika ununuzi wa zao la pamba;

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuongeza vitendea kazi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kitaalam na vyombo vya usafiri imara na vya kutosha kwa ofisi zote ili kuhakikisha huduma za Wakala zinawafikia walaji/wadau wengi zaidi, kwa haraka na ufanisi zaidi; na

(ix) Kutekeleza programu ya elimu kwa umma ili kuongeza uelewa wa matumizi ya vipimo sahihi kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni kwa mwaka 2011/12 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha uingizaji wa taarifa zote za makampuni na majina ya biashara kwenye mfumo wa kompyuta ili kurahisisha na kuboresha taratibu za utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo ya kiteknolojia;

(ii) Kupanua wigo wa watumiaji wa huduma na kupeleka huduma hizo karibu na wateja. *BRELA* kwa kushirikiana na *TCCIA* itatekeleza mpango wa kutoa baadhi ya huduma zake wilayani;

(iii) Kuhamasisha na kuelimisha watumishi na watumiaji wa huduma za Wakala, ili kuharakisha urasimishaji wa biashara;

(iv) Kuendeleza elimu juu ya umuhimu wa matumizi bora ya Miliki Ubunifu ili kuwawezesha wananchi kutumia fursa zilizopo katika rasilimali hizo kukuza uchumi wao na kupambana na umaskini;

(v) Kukamilisha upitiaji wa sheria za Miliki Ubunifu, Majina ya Biashara, Leseni za Viwanda na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002, ili iweze kwenda na mabadiliko yanayoendelea sasa hivi duniani;

(vi) Kuendelea na mpango wa kuandaa Mfumo Mkakati wa Miliki Ubunifu Tanzania *(Intellectual Property Strategy Framework);*

(vii) Kuimarisha ushirikiano uliopo katika eneo la miliki ubunifu na mashirika ya nje kama vile Shirika la Miliki Ubunifu la Kanda ya Afrika *(African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO)*, Shirika la Miliki Ubunifu la Dunia *(The World Intellectual Property Organization - WIPO)* na Shirika la Biashara Duniani *(World Trade Organization - WTO);*

(viii) Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi na nchi (bilateral arrangements) katika maeneo ya Miliki Ubunifu na maeneo mengine ambayo *BRELA* inayasimamia;

(ix) Kutekeleza Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BARA) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa *(Local Government Authority);* na

(x) Kupata kiwanja au jengo kwa ajili ya Ofisi za Wakala kwa ajili ya utoaji huduma na kuiwezesha Wakala kutumia teknolojia ya kisasa katika kutoa huduma zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Kipindi cha mwaka 2011/2012, *COSOTA* imejipanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha masuala ya Hakimiliki, na kutumia kila nafasi ya kushirikiana na vyombo vya habari katika uhamasishaji;

(ii) Kuanzisha matumizi ya stika zenye namba, zijulikanazo kama *HAKIGRAM*, katika usambazaji wa kanda na *CD* za kazi za muziki na Filamu, ili kuwawezesha wanunuzi wa kazi hizo kutofautisha kati ya kazi halali na bandia;

(iii) Kutoa elimu kwa wauzaji wa kanda na wanunuzi kuhusu *CD* na mikanda bandia;

(iv) Kusajili makampuni ya uzalishaji na usambazaji wa kanda na *CD*, uchapishaji na mashirika ya utangazaji yaliyopo ili kutoa miongozo ya kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki;

(v) Kukusanya mirabaha na kutoa leseni kwa mashirika ya utangazaji, mabenki na makampuni ya simu;

(vi) Kuandaa marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi ya mwaka 1999;

(vii) Kuendelea kusuluhisha migogoro na kufungua kesi dhidi ya wakiukaji wa Sheria na wanaogoma kulipia mirabaha;

(viii) Kurekebisha viwango vya mirabaha ili viweze kulipika na kuendana na wakati; na

(ix) Kufanya mikutano na vyama vya wafanyabiashara mikoani juu ya utekelezaji wa Sheria ya Hakimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi ya Leseni za Maghala itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika maeneo yote yanayotekeleza mfumo hapa nchini;

(ii) Kukuza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi katika maeneo na mazao mengine;

(iii) Kuimarisha mfumo ili utumike kikamilifu katika soko la bidhaa *(commodity exchange);*

(iv) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi za Leseni Ghalani kwa wakulima na wadau wengine;

(v) Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao; na

(vi) Kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo ya ununuzi wa mazao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara *(CAMARTEC, TIRDO* na *TEMDO)* zimejipanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendeleza uboreshaji, uundaji na uanzishwaji wa uzalishaji kibiashara wa matrekta madogo aina ya *CFT 22* na zana zake; kuendesha mafunzo kwa mafundi, waendesha matrekta na wasimamizi wao;

(ii) Kuendeleza utafiti wa ufuaji umeme kwa kutumia teknolojia ya *biogas;*

(iii) Kuendeleza uundaji wa mashine za kusindika mazao ya kilimo;

(iv) Kuendelea na uhaulishaji wa teknolojia mbalimbali zilizobuniwa na taasisi za utafiti. Hii itatekelezwa sambamba na kutoa huduma katika viatamizi vilivyopo kwenye taasisi za utafiti;

(v) Kutoa mafunzo na kuhamasisha wajasiriamali kwa kutumia viatamizi vya teknolojia mbalimbali;

(vi) Kubuni na kuendeleza machinjio ya kisasa yenye gharama nafuu pamoja na teknolojia za kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mabaki ya mifugo;

(vii) Kubuni na kuendeleza teknolojia za kurejesha taka za mijini *(municipal solid waste recycling technologies);*

(viii) Kuendeleza utoaji huduma za kihandisi viwandani kwa lengo la kuongeza uzalishaji, ubora wa bidhaa, kuhifadhi mazingira na matumizi bora ya nishati;

(ix) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ili viwanda vya ngozi nchini vipunguze uchafuzi wa mazingira;

(x) Kukamilisha mchakato wa kuhakiki na kuboresha maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi ili viweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(xi) Kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa mazao (*traceability);*

(xii) Kuendelea kusaidia utendaji wa Kampuni ya GS 1 kama mshauri wa kiufundi chini ya uendeshaji wa sekta binafsi; na

(xiii) Kuendelea kutoa huduma viwandani zinazolenga matumizi ya TEKNOHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Chuo cha Elimu ya Biashara kinalenga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali wadogo wadogo ili kuwasaidia kufanya biashara zao kisasa zaidi;

(ii) Kuaandaa mpango wa kuendesha mafunzo kwa wajasiriamali katika Kampasi zake za Dodoma na Mwanza ili kuwafikia wajasiliamali wengi;

(iii) Kuandaa mitaala ya kozi ya ujasiriamali katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada; na

(iv) Kuandaa michoro katika kiwanja cha Nzunguni (Dodoma) na Kiseke (Mwanza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kutekeleza mikakati inayohusu masuala ya utunzaji wa mazingira pamoja na programu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira viwandani na taasisi za Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kupambana na kudhibiti rushwa kwa kutoa elimu kwa umma na kubaini mianya ya rushwa kwa lengo la kuiziba. Elimu hiyo itatolewa kupitia vikao mbalimbali vya Wizara na Taasisi zake na maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Wiki ya Utumishi wa Umma, Sabasaba na Nanenane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 tutaendelea kutoa mafunzo juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari. Pia, tutaendelea na jitihada za kuwawezesha wafanyakazi waishio na virusi vya UKIMWI kupata huduma ya virutubisho *(food suplements)* lishe na usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ujao wa 2011/2012, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 80 kwa kada mbalimbali ili kuziwezesha idara na vitengo vyote kutoa huduma nzuri na kwa ukamilifu. Pia Wizara inatarajia kuwathibitisha kazini watumishi watatu na kuwapandisha vyeo jumla ya watumishi 67 baada ya kupima utendaji kazi wao kupitia *OPRAS* na kuzingatia muundo wa Utumishi wa Umma *(scheme of service).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambao wametoa misaada mbalimbali kusaidia Wizara yangu. Misaada na michango yao imechangia kwa kiasi kikubwa Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija. Nchi hizo ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na *ARIPO,* Benki ya Dunia, *CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA,* Jumuiya ya Madola, *KOICA*, *SIDA, UNCTAD, UNDP, UNIDO, USAID, WIPO* na *WTO. (Makofi)*

Maombi ya fedha katika mwaka 2011/2012, Matumizi ya Kawaida katika mwaka 2011/2012 Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya shilingi 30,052,589,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ili iweze kutekeleza majukumu niliyoelezea ya kuendeleza sekta ya viwanda, viwanda vidogo na biashara ndogo, biashara na masoko. Kati ya fedha hizo, shilingi 21,503,769,000 ni kwa matumizi ya mishahara na shilingi 8,548,820,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi zake. *(Makofi)*

Katika mwaka 2011/2012 Wizara inaomba jumla ya shilingi 27,676,129,000 kwa ajili ya shughuli za Miradi ya Maendeleo katika Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha hizo shilingi 16,387,859,000 ni fedha za ndani ambazo zitatumika katika shughuli za maendeleo katika taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 11,288,270,000 ni fedha za nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHIRIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Dkt. Cyrill Chami kwa hotuba yako. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa. *(Makofi)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusoma maoni ya Kamati naomba Bunge lako Tukufu kuongeza dakika 30 zilizotumika kwenye Miongozo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tumia muda wako uliopewa vizuri. *(Makofi)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Naomba utumike kwa wajumbe kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hayo tutayaamua kuchangia baadae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 99 (7) na 114 (11) Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2010/2011, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, afya na kuniwezesha kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Kabla sijawasilisha maoni ya Kamati, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sitawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa kunichagua kwa kauli moja kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge, nawaahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote kuwatumikia na wala sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa wanakamati kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao kwa sauti moja na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia bila kujali itikadi za vyama vyetu, pia namshukuru Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, kwa ushirikiano anaonipa na kwa namna ya kipekee namshukuru sana Waziri Kivuli Mheshimiwa Lucy Owenya, kwa ushirikiano wake mkubwa katika Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa kwa Wizara kwa mwaka 2010/2011. Katika mwaka wa fedha uliopita Kamati ya Viwanda na Biashara ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo 11. Nasikitika kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali haijatekeleza maagizo ya Kamati. Hivyo Kamati yangu inaendelea kusisitiza na kuagiza Serikali kutekeleza maagizo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara iliidhinishiwa na Bunge, kiasi cha shilingi 64,260,505,500/=, kati ya fedha hizo fhilingi 31,542,839,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 32,717,666,500/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hata hivyo mpaka kufikia mwezi Aprili 2011, Wizara ilipokea shilingi 13,303,713,331/= tu kwa ajili ya Maendelao, ambayo ni sawa na asilimia 41% tu ya fedha yote ya Maendeleo ambayo iliidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mapungufu makubwa sana na athari zake kiuchumi ni kubwa, Kamati yangu inaiagiza Serikali kuipa Wizara ya Viwanda na Biashara fedha yote inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2010/2011 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, tarehe 31/5 hadi 2/6/2011 Jijini Dar es Salaam, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Waziri wa Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hiyo Waziri alieleza kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Dira, dhima na majukumu ya Wizara;

(ii) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya mwaka 2010/2011;

(iii) Utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2010/2011;

(iv) Changamoto zinazoikabili Wizara; na

(v) Maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Makadirio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba jumla ya shilingi 57,728,718,000/= kati ya hizo shilingi 30,052,589,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 27,676,129,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu haikuweza kukamilisha na kupitisha Bajeti ya Wizara katika vikao hivyo kutokana na Bajeti hiyo kuwa ndogo sana ukilinganisha na majukumu ambayo Waziri aliyaainisha mbele ya Kamati kwamba Wizara yake imepanga kuyatekeleza na hivyo Kamati kupanga kuonana na Waziri Mkuu ili kuona uwezekano wa Wizara kuongezewa Bajeti, Kamati ilimwona Waziri Mkuu na kuahidiwa kuwa Bajeti hiyo itaongezwa, lakini hadi tarehe 30/07/2011, Kamati ilipokutana Dodoma na Wizara ili kupitisha Bajeti hiyo hapakuwa na mabadiliko yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imesikitishwa sana na Bajeti iliyopangiwa Wizara hii. Pamoja na ushauri wa Kamati uliotolewa mwaka jana kuhusu umuhimu wa Wizara hii na kutaka iingizwe kwenye Wizara za vipaumbele ikiwa ni pamoja na kuongezewa fedha bado Bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana. Cha kusikitisha zaidi ni kwamba badala ya Bajeti ya fedha za Miradi ya Maendeleo kuongezeka mwaka huu imepungua zaidi kutoka shilingi 32,717,666,500/= kwa mwaka wa fedha 2010/2011 hadi shilingi 27,676,129,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Wakati Wizara hii ina jukumu kubwa la kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuifanya Tanzania kufikia kiwango cha kati cha Maendeleo ya Uchumi wa Viwanda *(Semi Industrialized Economy)* ifikapo mwaka 2025, hii ni pamoja na kutekeleza na kusimamia Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inajiuliza hivi Serikali ina dhamira ya kweli ya kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuisaidia Wizara hii kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na kuifanya isimamie kikamilifu Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda na kuifikisha Tanzania kiwango cha kati cha maendeleo ya uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Kamati inashauri Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili iweze kutekeleza azma hii. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kama zilivyoidhinishwa kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kodi za Serikali kuwa nyingi na kutozwa kwa kiwango kikubwa sana na kwa makundi machache ya watu na hivyo kodi kugeuka kuwa mzigo kwa wawekezaji na wajasiriamali wadogo kwa ujumla na kufanya wafanyabiashara wengi kukwepa kulipa kodi na Serikali kukosa mapato. Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa ili kulinda maslahi ya nchi na kuwahamasisha wafanyabiashara wote kulipa kodi bila kukwepa, ni vyema mfumo wa kodi uangaliwe upya kwa lengo la kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejikita kwenye kaulimbiu ya Kilimo Kwanza ikiamini kuwa ndicho kitakachowakomboa Watanzania zaidi ya asilimia 80% wanaotegemea kilimo na kwamba kitawatoa kwenye hali ya umaskini na kuwawezesha kuwa na maisha bora, Kamati yangu inaamini kuwa bila kuweka mkazo na nia ya makusudi kwenye viwanda, azma hii ya Kilimo Kwanza haiwezi kufanikiwa kwa kiwango cha juu kwa sababu kilimo kinategemeana sana na viwanda, Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa ili kufanikisha azma hii ya Kilimo Kwanza bado kuna umuhimu mkubwa wa sekta hii ya viwanda kupewa kipaumbele. Aidha, Kamati yangu inaamini kuwa Serikali inatakiwa kuhamasisha wananchi wawekeze katika viwanda vya kusindika mazao, ili

kuongeza thamani ambayo kwa hakika itaongeza bei ya bidhaa zetu na kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ina taasisi 17 zenye miradi mbalimbali na kwa kuwa Bajeti ya Wizara haitoshi kutekeleza mipango yote kwa wakati mmoja, Kamati yangu inashauri Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka vipaumbele ndani ya Wizara kwa kuanza na Taasisi nne tu kwa mwaka huu ambazo zikiwezeshwa zitaleta ufanisi wa hali ya juu na kuepukana na utegemezi wa Bajeti unaojitokeza kila mwaka. Aidha, utekelezaji wa miradi husika utaiwezesha Tanzania kukua kiuchumi na hatimaye kuondokana kabisa na umaskini. Kwa mwaka huu, Kamati yangu inapendekeza Mashirika yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC).* Shirika hili katika mipango yake limekusudia kutekeleza Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Ngaka, Chuma cha Liganga, Mradi wa kuangamiza Mazalia ya Mbu na mradi wa Magadi Soda. Endapo miradi hii itatekelezwa nchi itaweza kutekeleza miradi mikubwa ambayo ni chachu ya uanzishwaji wa viwanda vikubwa, kati na vidogo kutokana na upatikanaji wa mali ghafi muhimu ya chuma na upatikanaji wa umeme wa uhakika. Miradi hii ya makaa ya mawe inatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa *Mw 1,000* ifikapo mwaka 2014 na kutengeneza chuma tani 1,000,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

Kamati yangu kwa msisitizo inaamini kabisa kuwa, kama Serikali ina nia ya kweli ya kutatua tatizo sugu la umeme ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kwa uchumi katika nchi yetu, Shirika la *NDC* kupitia Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Ngaka, Kiwira na mradi wa umeme wa upepo Singida ndio suluhisho la uhakika na la haraka. Kamati yangu imesikitishwa sana na taarifa za urasimu ilizozipata juu ya uanzishwaji wa mradi wa umeme uliopo Mkoani Singida, Kamati yangu inakusudia kumwita Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* ili atupe sababu za msingi kwa nini mpaka leo hajasaini mkataba wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi imejifunza kwa njia ngumu kuelewa kwamba sasa hatuwezi kuweka mategemeo yetu yote katika umeme unaotokana na maji. Duniani kote mitambo ya umeme inayotumia makaa ya mawe inachangia 41% ya umeme, wakati mitambo ya maji inachangia 16%, gesi 20%, nguvu za nukilia 15% na mafuta 6% tu. Katika nchi ya Afrika ya Kusini mitambo ya makaa ya mawe huchangia umeme kwa 93%, India 69% na Moroco 55%. Tanzania tuna maeneo kumi yenye makaa ya mawe na yanapatikana Kusini Magharibi mwa nchi yetu. Maeneo haya yanakadiriwa kuwa na makaa ya mawe zaidi ya tani bilioni 1.2. Kati ya maeneo haya yaliyokwishafanyiwa uchunguzi ni Mchuchuma – Katewaka, Songwe – Kiwira na Ngaka – Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* kwa kushirikiana na Kampuni ya *Intra Energy* ya Australia wameunda Kampuni inayoitwa *TANCOAL ENERGY LTD.* inayoendesha Mradi wa Ngaka Wilayani Mbinga. Lengo ni kujenga mitambo ya kufufua umeme wa *MW 400* kwa kutumia makaa ya mawe. Kwa kuwa kwa sasa Mkoa wa Ruvuma haujaunganishwa na Gridi ya Taifa na kwa vile Serikali ya Sweden inafadhili mradi huo toka Makambako hadi Songea kwa kujenga njia ya umeme ya *132 kV.* Kamati yangu inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuzungumza na Wahisani hawa ili kuharakisha ujenzi wa mradi huu ili umeme utakaozalishwa Ngaka uingizwe kwenye grid ya Taifa; na

(ii) Serikali kwa kushirikiana na Wadau wake ijenge njia ya umeme kutoka Ngaka mpaka Songea. Mradi unakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani 46 milioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* inahusika sana pia kuendeleza miradi ya chuma cha Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka china. Kwa kuwa miradi hii ni yenye faida na maslahi makubwa kwa Taifa na imezungumzwa kwa muda mrefu. Kamati yangu inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuipa fedha zaidi *NDC* ili iweze kuwa na nguvu ya kimaamuzi na utekelezaji;

(ii) Kuhakikisha miradi hii inaanza vizuri kwa kuangalia maslahi ya wananchi pale wanapotakiwa kupisha uchimbaji wa madini hayo kwa kuwalipa vizuri, lakini pia kuwapimia na kuwaandalia makazi ya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kuangamiza mazalia ya mbu. Mradi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kuangamiza mazalia ya mbu chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni sita kwa mwaka. Utekelezaji wa kiwanda hiki utaleta suluhisho la kudumu la ugojwa sugu wa malaria kwa Watanzania na kuondoa tatizo la kupoteza nguvu kazi inayopotea kila mwaka kutokana na vifo vya malaria. Aidha, mradi huu utaweza kuiondolea Serikali adha ya kuendelea kupata msaada wa vyandarua ambavyo hata hivyo siyo suluhisho la kudumu la tatizo la malaria, kwani tumeendelea kuona na kushuhudia watanzania wakiendelea kupoteza maisha kutokana na ugojwa wa malaria pamoja na juhudi za Serikali za kugawa vyandarua kila kaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO).* Mataifa mengi duniani yamekuwa na uchumi mzuri na kuondokana na umaskini kwa kuwawezesha wajasiriamali wadogo kupitia Viwanda Vidogo vidogo *(SIDO).* Endapo *SIDO* itawezeshwa na kutumiwa vizuri itasaidia sana kuondoa tatizo la ajira kwa vijana na Pato la Taifa kukua kwa kiwango kikubwa na hivyo kuondoa tatizo la umaskini na kuboresha maisha ya kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili *SIDO* iweze kutekeleza mipango yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 itahitaji shilingi 11,232,000,000/=. Katika Bajeti hii imetengewa shilingi 1,759,322,360/= tu, fedha ambayo haiwezi kutekeleza hata mradi mmoja. Suluhisho la kudumu la ajira kwa vijana linapatikana hapa. Tatizo la ajira ni bomu linasubiri muda, linaweza kulipuka wakati wowote. *SIDO* imedhamiria kujenga mitaa ya viwanda kila Wilaya kwa kuandaa maeneo kwa ajili ya wazalishaji wadogo na wa kati. *SIDO* isaidiwe kwa kupewa mtaji wa kutosha ili kutengeneza ajira za kutosha nchi nzima. Maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana kama Taifa litaamua kwa dhati kuwekeza *SIDO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wameshindwa kujiajiri kutokana na ukosefu wa maeneo ya kufanyia kazi na mitaji. Wakopeshaji wanakuwa na hofu kutokana na vijana hao kutofikika kirahisi na kutojulikana kwa shughuli zao. Matokeo yake wengi wa vijana wahitimu wa vyuo wamejikuta wakianzisha biashara zisizo na tija au kuishia kuwa vibarua wa wageni. Kamati yangu inaishauri Serikali kutumia fursa za mitaa ya *SIDO* na maeneo huru ya uwekezaji *(EPZA)* kutenga maeneo maalum kwa ajili ya vijana hususan wanaomaliza Vyuo Vikuu na *VETA,* ili kuwajengea mazingira mazuri ya kujiajiri. Aidha, tunashauri vijana waanzishiwe benki yao maalum kama ilivyo kwa wanawake ili kuwawezesha kupata mitaji ya biashara rasmi inayofanana na elimu yao. Hali kadhalika vijana hao wakijiajiri wanaweza kulipa mikopo yao ya benki na ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wameshindwa kujiajiri kutokana na ukosefu wa maeneo ya kufanyia kazi na mitaji. Wakopeshaji wanakuwa na hofu kutokana na vijana hao kutofikika kirahisi na kutojulikana kwa shughuli zao. Matokeo yake wengi wa vijana wahitimu wa vyuo wamejikuta wakianzisha biashara zisizo na tija au kuishia kuwa vibarua wa wageni. Kamati yangu inaishauri Serikali kutumia fursa za mitaa ya *SIDO* na maeneo huru ya uwekezaji *(EPZA)* kutenga maeneo maalum kwa ajili ya vijana hususan wanaomaliza Vyuo Vikuu na *VETA,* ili kuwajengea mazingira mazuri ya kujiajiri. Aidha, tunashauri vijana waanzishiwe benki yao maalum kama ilivyo kwa wanawake ili kuwawezesha kupata mitaji ya biashara rasmi inayofanana na elimu yao. Hali kadhalika vijana hao wakijiajiri wanaweza kulipa mikopo yao ya benki na ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maeneo Huru ya Kukuza Uchumi *(EPZA),* Mkutano uliopita wa Bunge tulipitisha marekebisho ya Sheria ya *EPZA* ili kuipa mamlaka hiyo nguzu zaidi ya usimamizi wa Maeneo Huru ya Uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kupata wawekezaji kwa maeneo yaliyokwishaainishwa likiwemo eneo la Bagamoyo ambalo wawekezaji wako tayari kuwekeza wakati wowote likikamilika. Ili uwekezaji uweze kuendelea katika maeneo yaliyoainishwa, *EPZA* inatakiwa kulipa fidia ya shilingi 65,000,000,000 kwenye maeneo yafuatayo:-

Bagamoyo shilingi 55,000,000,000/0, Songea shilingi 3,100,000,000/=, Tanga shilingi 4,200,000,000/=, Kigoma shilingi 1,500,000,000/= na Mara shilingi 1,200,000,000/=. Aidha *EPZA* inatakiwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika eneo la Bagamoyo na Benjamin Mkapa. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Mamlaka imetengewa kiasi cha shilingi 4,106,164,640/= tu, kiasi hiki cha fedha hakiwezi kulipa fidia wala kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika eneo moja. Endapo *EPZA* itawezeshwa na kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika eneo la Benjamin Mkapa na Bagamoyo tu, litaweza kupata wawekezaji, hivyo kuliongezea Taifa fedha za kigeni, kuongeza ajira kwa wananchi wengi pamoja na kuongeza kipato chao na hivyo maisha bora kwa kila Matanzania yatawezekana. Aidha, kukamilika kwa mradi wa Bagamoyo kutasaidia kuondoa msongamano wa kibiashara uliopo Dar es Salaam ikwemo Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZA* imetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji katika Mikoa yote ya Tanzania isipokuwa Tabora na Dodoma na maeneo hayo yalikuwa yanamilikiwa na wananchi hivyo inatakiwa kulipwa fidia. Wananchi wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu ili kulipwa fidia yao na thamani ya fedha inashuka kila kukicha je, wananchi hao watalipwa fidia yao pamoja na riba? Ni vyema Serikali iipatie *EPZA* fedha ya kutosha ili wananchi husika waweze kulipwa fedha zao la sivyo Serikali iache maeneo ya wananchi ili wafanyie shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na nyumba nyingi za wananchi wanaohamishwa kuwa duni hivyo kusababisha walipwe fidia ndogo ambayo haiwezi kwenda kujenga nyumba nyingine, Kamati yangu inashauri Serikali kuona utaratibu mzuri wa kuwasidia wananchi hawa kwa kuwajengea nyumba nyingine mahali pengine *(settlement). (Makofi)*

Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CARMATEC)* kina kazi kubwa ya kubuni, kuunda na kueneza teknolojia za zana za kilimo vijijini. Endapo *CAMARTEC* itawezeshwa kifedha itaweza kuinua hali ya maisha ya wananchi wa vijijini kwa kutengeneza na kueneza teknolojia ya zana bora za kilimo. Kwa sasa *CAMARTEC* imejikita katika utengenezaji wa trekta. Kamati imebaini kuwa trekta hizo ni bora na zina uwezo mkubwa kuliko *power tillers* ambazo kwa sasa nchi yetu inazieneza kwa kasi. *(Makofi)*

Kwa kuwa Serikali inahamasisha kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, Kamati yangu inashauri Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya kununua trekta kutoka *CAMARTEC* ili kuiwezesha kukuza mtaji wake, kusambaza teknolojia yao na kujiendesha yenyewe hivyo kuipunguzia Serikali mzigo *(Commercialization of Tractor Project).* Aidha, wananchi watakuwa wamefaidika na teknolojia iliyogunduliwa hapa nchini na Watanzania wenyewe na hivyo kuharakisha mapinduzi ya viwanda. Ili kukamilisha mipango yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 *CAMARTEC* inahitaji shilingi 4,406,691,795/=; kwa sasa imetengewa shilingi 850,000,000/= tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa hapo juu, Kamati yangu inaendelea kusisitiza Wizara iongezewe Bajeti na kupatiwa angalau shilingi 50,000,000,000/= kwa matumizi ya maendeleo ili Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC),* Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO),* Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uwekezaji *(EPZA)* na Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini *(CAMERTEC)* ziongezewe fedha kwa lengo la kutekeleza angalau sehemu ya miradi iliyopangwa kutekelezwa na Taasisi hizi kwa maslahi ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, Kamati yangu iliahidiwa kuwa Bajeti hii itaongezwa wakati wa kufanya mapitio ya Bajeti *(Mid Year Budget Review).* Kamati yangu inaamini kwamba kwa umakini wa Serikali yetu ahadi hii itatekelezwa kwa muda muafaka kama ilivyoahidi na hivyo kupitia Bajeti hii Kamati inaomba kauli ya Serikali kuhusu *commitment* yake juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia utekelezaji wa mfumo wa soko huru, Tanzania imekuwa jalala la bidhaa zote zisizo na ubora na bandia, Serikali bado haijadhibiti mianya yote inayotumiwa kuingiza bidhaa zisizo na ubora na bandia ambazo zimekuwa na athari kubwa kwa Taifa na watu wake. Kwa mfano uingizaji wa tairi na *tube* za pikipiki aina ya *Vee Rubber* Thailand ambazo huuzwa kwa bei ndogo na kusababisha ushindani usio wa haki katika biashara kwa viwanda vyetu vya hapa nchini. Mipira hii bandia imetapakaa sana Dar es Salaam na maeneo mengi ya mipakani kama Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Bukoba na Musoma. Athari za bidhaa hizi bandia ni kubwa sana kwa Taifa letu ikiwemo:-

(i) Ajali za mara kwa mara zinazosababishwa na kupasuka kwa tairi na kusababisha vilema vya kudumu au kupoteza maisha kwa waendesha pikipiki na watembea kwa miguu, hivyo kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

(ii) Wananchi kudanganywa kulipia bidhaa bandia kwa bei kubwa sawa na bidhaa halisi kutokana na kukosa uelewa wa kutofautisha kati ya bidhaa bandia na halisi kwani bidhaa hizi kwa kawaida zinakuwa zinafanana sana na siyo rahisi kutofautisha.

(iii) Kutokana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya Maofisa wa *TRA* kwa kushirikiana na wafanyabiashara wadanganyifu wanaoingiza bidhaa hizi bandia kutoka nje, Serikali inakosa mapato mengi ya haki. Aidha, hali hii inawavunja moyo na kuwakatisha tamaa wafanyabiashara waaminifu ambao wanaingiza bidhaa halisi na kulipia kodi kama wanavyotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inakusudia kuunda Kamati ndogo ili kulifanyia uchunguzi jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ina shangazwa sana na Serikali kwa nini mpaka leo Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine inahusu ukaguzi wa bidhaa kabla hazijaingia nchini *(Pre-shipment Verification of Conformity to Standard – PVoC)* haijaanza kutumika, sheria hii ingeweza kudhibiti uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora na bandia na kusaidia udhibiti dhidi ya wafanyabiashara na baadhi ya Maofisa wa *TRA* wasiowaaminifu kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa zote zinazoingia nchini huko huko nje zinakotoka. Suala la kufanya ukaguzi wa bidhaa hizi zikiwa tayari zimeingia nchini linaleta hasara na machungu mengi kwa wahusika kwani zinapothibitika hazina kiwango au ni bandia, Sheria ya *TBS* inataka bidhaa hizo ziteketezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inashauri utaratibu wa *Pre-shipment Verification of Conformity (PVoC)* uanze kutumika haraka kwa kuwa Sheria hiyo ilishapitishwa na Bunge lako Tukufu tangu mwaka 2009. Aidha, inapotokea bidhaa zimekamatwa ambazo hazifai, wahusika waamriwe kuzirudisha kule walikozitoa badala ya utaratibu wa sasa wa kuziteketeza kwa moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tamko la Waziri wa Fedha lililotolewa wakati akiwasilisha Bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kuhusu Serikali na Taasisi zake kuacha kununua bidhaa ikiwemo samani kutoka nje na kutoa agizo kuwa samani zote zinunuliwe kwa wenye viwanda hapa nchini, Kamati inaipongeza Serikali kwa tamko hili ambalo wananchi wamekuwa wakisubiri kusikia kwa muda mrefu sasa. Kwa vile bado tunashuhudia kununuliwa kwa samani za nje, Kamati yangu inashauri kuwa ni wakati muafaka sasa Serikali ilete Muswada wa Sheria hapa Bungeni ili kurahisisha utekelezaji wa azma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria na Sera ya uvunaji malighafi za viwandani ya mwaka 2006, iliwekwa kwa nia nzuri ya kuzuia watu wa nje wasiendelee kuvuna magogo na mbao na kuzisafirisha nje ya nchi, lakini kwa bahati mbaya Sheria hii haikuangalia wawekezaji na watumiaji wa malighafi hii katika viwanda vyetu vya ndani ambapo imesababisha urasimu na usumbufu katika kupata vibali vya uvunaji wa malighafi pamoja na usumbufu katika usafirishaji kutokana na vizuizi vya barabarani na usumbufu wa polisi. Kutokana na sheria hii viwanda vingi vya samani vinalazimika kununua malighafi (magogo) nje, kutoka Msumbiji, Congo, Gabon na Afrika ya Magharibi ambako bei yake ni ndogo kuliko bei ya hapa nchini. Mfano *cubic metre* ya mbao kutoka nje hadi kufika Dar es Salaam ni dola za Kimarekani 500 hadi 600 wakati hapa nchini ni 900 hadi 1,000 na kupoteza fedha nyingi za kigeni ambazo zingetumika kwa matumizi mengine kuendeleza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyote vilivyokuwa vya Serikali *(Tanzania Wood Industry Corporation – TWICO)* vilivyonunuliwa na wawekezaji kama *Mang'ula Sawmill Morogoro*, *Mkata Sawmill Co. Ltd.* na *Sick Sawmill (T) Tanga, Kill Timber* Moshi, *Mingoyo Sawmill Co. Ltd.* Lindi na Tabora Misitu vimekufa. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara husika kupunguza gharama ya malighafi hii ya magogo na mbao ili kunusuru viwanda vya samani ambayo bado vinaendelea, ikiwemo kufufua viwanda nilivyovitaja hapo juu. Aidha, Sheria ya Uvunaji Malighafi za Viwandani

ya mwaka 2006 ifanyiwe marekebisho haraka. Kuchelewa kufanya marekebisho kwa sheria hii kutasababisha viwanda vingi kufungwa na hivyo kuathiri ajira ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za makusudi zinazotakiwa kufanywa na Serikali kwa lengo la kuvilinda viwanda vya ndani, Kamati yangu inatoa angalizo katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kulinda viwanda vya ndani kusisababishe kuwaumiza wakulima wadogo, kwa wenye viwanda kupanga bei ndogo ya mali ghafi ambayo itaweza kuwathiri.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana linalojitokeza katika uagizaji wa sukari nje ya nchi. Lengo la Serikali ni zuri lakini, inatakiwa iruhusu uagizaji wa sukari mwaka mzima baada ya kufanya tathmini ya kweli na kujua mapungufu ambayo yatakuwepo katika mwaka huo husika. Hii itasaidia sana kufanya bei ya sukari kutobadilika badilika badala ya kutoa leseni na vibali vya kuingiza sukari pale inapogundulika kuwa kuna mapungufu, kwani wafanyabiashara ambao sio waaminifu hutumia mwanya huo kuwaumiza wananchi walio wengi kwa kupandisha bei ya sukari bila mpangilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa juhudi za makusudi za kuhamasisha na kuchochea uwekezaji wa viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi ndani ya nchi vinavyotumia ngozi zilizosindikwa na viwanda vya usindikaji vilivyopo hapa nchini, hii ni pamoja na kazi nzuri ya uanzishaji na uzinduzi wa kituo cha mafunzo kwa wajasiriamali wa ngozi kilichozinduliwa hapa Dodoma tarehe 18 Juni, 2011 na Waziri wa Viwanda na Biashara. Hatua hii ya Serikali ni muhimu sana na inaonyesha kwamba inajali watu wake pamoja na rasilimali zilizopo nchini. *(Makofi)*

Hata hivyo kituo hiki hakitakuwa na maana endapo Serikali itaendelea kuruhusu ngozi ghafi kuendelea kusafirishwa nje ya nchi. Tanzania ina uwezo wa kuzalisha ngozi ghafi zenye futi za mraba milioni 92 kwa mwaka, lakini wastani wa makusanyo ya ngozi ghafi nchini ni futi za mraba milioni 51.2 kwa mwaka. Uwezo uliosimikwa kwa mwaka kwa viwanda vyote kama vingekuwa vinafanya kazi ni futi za mraba milioni 74.0 lakini kwa tathmini ya mwaka 2010, uwezo uliotumika ulikuwa futi za mraba milioni 34.3, hata hivyo kumekuwa na ongezeko kubwa kwani mwaka 2005 uwezo uliotumika ulikuwa futi za mraba takribani milioni 6.0 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu mojawapo ya viwanda vya usindikaji wa ngozi nchini kutotumia uwezo wao wote kama takwimu zinavyoonyesha ni kukosekana kwa mali ghafi ambapo sehemu kubwa inaendelea kuuzwa nje ya nchi, hii inaonyesha kwamba endapo ngozi zote zingekusanywa kikamilifu *(potential production)* na endapo viwanda vyote vya usindikaji vitafanya kazi kwa uwezo uliosimikwa, ngozi zinazokusanywa hazitatosheleza mahitaji ya ngozi ghafi, kutakuwa na upungufu wa ngozi ghafi wa futi mraba takribani milioni 23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara watiwe moyo kuongeza thamani ya zao la ngozi hata kwa kusindika kwa kiwango cha awali tu *(Semi processed leather)* na kuuza nje bila ushuru kwa lengo la kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wanabadilisha mfumo wa sasa wa kuuza ngozi ghafi badala yake wauze ngozi iliyosindikwa hapa hapa nchini na hii italeta faida kubwa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulinda na kuimarisha sekta hii ya ngozi, Kamati yangu inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kuongeza ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje *(Export Levy)* kutoka 40% inayotozwa sasa hadi 90%. Hii itasaidia ngozi ghafi kutosafirishwa nje kwa wingi na hivyo viwanda vyetu vya ndani kupata mali ghafi ya kutosha kwani kwa sasa ngozi ghafi nyingi inauzwa nje kwa sababu bei ya nje ni kubwa. Aidha, Serikali itaongeza mapato zaidi na fedha hizo zitarudi kusaidia sekta ya ngozi.

(ii) Kamati yangu imegundua udanganyifu mkubwa katika biashara ya ngozi ghafi zinazouzwa nje hasa kwa Maofisa wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanaotoa vibali vya usafirishaji

wa ngozi ghafi nje ya nchi kwa kushirikiana na baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu. Udanganyifu huo upo katika vipimo na uzito na bei ya kuuzia ambapo wafanyabiashara huwasilisha nyaraka zao Wizara ya Mifugo na Uvuvi zikiwa tayari zina udanganyifu na kwa bahati mbaya maafisa wanaohusika hupitisha na kutoa vibali, hii inawezekana ni kutokana na kukosa umakini kwa maafisa hao au ni kwa kusudi maalum.

Kamati yangu inaishauri Serikali iunde Kamati maalum itakayohusika na uchambuzi wa nyaraka za wafanyabiashara na kutoa mapendekezo kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili waweze kutoa vibali kwa kuzingatia mapendekezo na ushauri wa Kamati hiyo. Hii iatasaidia kunusuru mapato ya Serikali yanayopotea kutokana na ubadhilifu huu.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko la uingizwaji wa viatu kutoka nje, mwaka 2005 ziliingia jozi za viatu vya plastiki 18,042,000 na viatu vya ngozi 140,000 tu, mwaka 2009 viliingizwa viatu vya plastiki 33,999,000 hivi vyote vinaongeza ushindani usio wa haki kwa viatu vya ngozi vinavyotengenezwa hapa nchini. Ili kupunguza ushindani usio wa haki, Serikali itoze ushuru maalumu *(specific import duty)* kwa bidhaa za plastiki kama mabegi na viatu zinazoingizwa nchini kutoka nje ambazo zinafananana na ngozi halisi. Hii itasaidia sio tu kupunguza ushindani usio wa haki bali kuvilinda viwanda vya ndani na Serikali kupata mapato.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kusimamia na kudhibiti ngozi ghafi zinazosafirishwa nje kupitia mipaka yetu kwa njia za panya. Aidha, Serikali ishirikiane na wadau wa ngozi kwa maana ya Chama cha Wadau wa ngozi *(Leather Association of Tanzania - LAT)* na Chama cha Wasindikaji wa Ngozi Tanzania *(Tanzania Tanner's Association-TTA)* kuhamasisha wenye viwanda vya usindikaji wa ngozi kuandaa na kutekeleza mipango thabiti ya kuongeza utumiaji wa uwezo wa viwanda vyao na kufanya upanuzi zaidi kwa lengo la kusindika ngozi zote zinazozalishwa hapa nchini.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na nchi yetu kutokuweka utaratibu unaoeleweka kwa wafanyabiashara kumekuwepo na maduka kila mahali na yasiyo na mpangilio na wakati mwingine kuonekana kama uchafu. Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa maduka ya aina moja kuwa katika mtaa mmoja. Hii itasidia sana kudhibiti bidhaa bandia na zisizo na ubora pia itakuwa rahisi kwa Serikali kukusanya kodi. Aidha, Kamati inashauri maduka ya magari yatengewe eneo moja nje ya mji kuliko utaratibu wa sasa wa kila mahali katikati ya mji kuna maduka ya magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu na Wabunge wote kwa ujumula wamekuwa wakizungumzia kwa uchungu kuhusu ufufuaji wa kiwanda cha matairi cha *General Tyre East Africa Ltd.* Kamati yangu inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa kiwanda hiki kinafufuliwa na kuanza kufanya kazi kwa kuiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kuanza mchakato huo. Kamati yangu inaiagiza Wizara kufanya kazi hiyo kwa haraka na kwa kuzingatia maoni ya Kamati ndogo ya Bunge iliyoundwa kuchunguza Kampuni ya *General Tyre East Africa Ltd.,* taarifa ya Kamati ndogo itawasilishwa na Kamati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mwanzo huu mzuri wa kukifufua Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre*, Kamati yangu inaiagiza Serikali kuchukua hatua thabiti juu ya viwanda vilivyobinafsishwa lakini havifanyi kazi au matumizi/malengo yake yamebadilishwa bila kibali cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Maonesho ya 35 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo ilifarijika sana na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzanaia *(TanTrade)* ambayo ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 2009 iliyopitishwa na Bunge lako kwa lengo la kuratibu na kusimamia biashara ya ndani na nje, shughuli ambazo zilikuwa zinafanywa na Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET)* na Bodi ya Biashara ya Ndani *(BIT).* Ikiwa katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Kamati yangu iliweza kushiriki uzinduzi wa Mamlaka ya *TanTrade* uliofanywa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Gharib Bilal. Kuzinduliwa kwa Mamlaka hii kutaiwezesha kuendeleza na kukuza biashara ya ndani

na nje, kutoa ushauri wa kitaalam kwa wazalishaji ili waweze kuzalisha kwa kuzingatia mwenendo na mahitaji ya soko na hatimaye kuwaunganisha na masoko ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa *TanTrade* Mheshimiwa Ramadhan Khalfan pamoja na watendaji wote walio chini yake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kuyaboresha maonesho hayo mwaka hadi mwaka na hata kuyafanya kuwa kivutio kikubwa kwa washiriki wa ndani na nje. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la washiriki. Jumla ya nchi 17 zilishiriki katika maonesho ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa bidhaa nao umeongezeka, mazingira yameboreshwa hakuna vumbi, milango ya kuingilia iliongezeka, mapato nayo yameongezeka kwa kipindi cha 2000 hadi 2010 mauzo ya papo kwa papo yaliyofanywa na makampuni na taasisi zilizoshiriki yamefikia shilingi 141,000,000,000, maulizo ya mauzo ya nje ya nchi *(export orders)* yalikuwa dola za Marekani milioni 1,176.5 na maulizo ya manunuzi toka nje *(import orders)* yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,064. Hata hivyo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kuwepo mitaa maalum ili kuweza kupata kirahisi bidhaa ambazo wananchi waliziona wakati wa maonyesho na wanataka kuzinunua.

(ii) Kuwepo utaratibu wa kuwa na vifungashio vizuri ambavyo kwa bidhaa zinazofanana vinafanana ili kuwavutia wanunuzi.

(iii) Kutokana na urasimu na usumbufu uliopo mipakani na bandarini na hivyo kucheleweshа mizigo ya wafanyabiashara wanaokuja kwenye maonesho Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuondoa kero hizi kwani kuna wafanyabiashara wanasumbuliwa na kucheleweshewa mizigo yao na kujikuta wamechelewa kwenye maonyesho hivyo kuwakatisha tamaa.

(iv) Kuwepo na maonesha ya Kanda ya wajasiriamali wa ndani, wadogo na wa kati kabla ya Maonesho ya Kitaifa na wale watakaoonekana wanafanya vizuri wawe wanateuliwa kwa kusaidiwa kwenda kwenye Maonesho ya Kitaifa kwani tutakuwa na uwezo wa kupata washiriki wengi wa ndani.

(v) Kamati inaipongeza Wizara kwa kutenga eneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara wenye ulemavu, hata hivyo mazingira ya kufika maeneo hayo hayakuwa wezeshi kwa watu wenye ulemavu. Hivyo tunashauri kipindi kijacho Wizara iangalie namna ya kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu ili nao wapate kufaidika na maonyesho kama watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu pia ilishiriki katika uzinduzi wa *GS1. GS1* ni Asasi isiyo ya Kiserikali inayohusika na utoaji wa mfumo wa utambuzi wa bidhaa *(bar codes)*. Nchi yetu imekuwa ikipata huduma hizi kutoka nchi za Kenya na Afrika Kusini na hivyo kufanya bidhaa zetu kuonekana zinazalishwa nchi hizo, kwa sababu hiyo, Kamati yangu inaipoingeza Serikali na wajasiriamali wote waliofanikisha zoezi hili muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya mazuri, Kamati imepata taarifa kuwa wapo wadau wengine hawajaridhika na namna mchakato wa kuipata Kampuni itakayoshughulikia na utambuzi wa wa bidhaa *(bar codes)* na kwa vile taarifa hizi zimewafikia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kupitia vyombo vya habari kama magazeti. Kamati yangu inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina ili wananchi waweze kuelewa nini kinaendelea kuhusu suala hili. Aidha, wananchi waelimishwe vya kutosha juu ya matumizi ya mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuhusu majukumu ya yanayofanywa na Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, Kamati yangu inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa kuweka vipaumbele ndani ya taasisi chini ya Wizara ili kuziwezesha kwa mwaka huu Taasisi za *SIDO, NDC, EPZA* na *CAMARTEC* ziweze kutekeleza vema majukumu yake na baadaye kuweza kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru tena wewe binafsi, Spika Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika Mheshimiwa Job Ndugai, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba kwa kuendesha vikao vya Bunge lenye machachari mengi vizuri na kwa kufuata Kanuni zilizowekwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Naibu Waziri Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Katibu Mkuu Bibi Joyce Mapunjo, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Shabani Mwinjaka, pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara na taasisi zake kwa maelezo na ufafanuzi walioutoa mbele ya Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wao katika kuchambua Bajeti ya Wizara na kutoa maoni haya ya Kamati. *(Makofi)*

Kwa heshima kubwa naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mwenyekiti, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Abuu Jumaa, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Salim Hassan Abdallah Turky na Mheshimiwa Mohamed Dewji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Aidha, namshukuru Katibu wetu wa Kamati Bibi Angelina Sanga kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati wakati wote ikiwa ni pamoja na kuandaa maoni haya ya Kamati kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kuwatakia kila la heri Waislamu kokote duniani ambao wako katika mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu awabariki sana na awatakabalie swaumu zao. Amin. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba Bunge lako Tukufu liyapokee maoni haya na kuyajadili. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LUCY P. OWENYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hotuba yangu ni ndefu sana na sitaweza kuimaliza, naomba inukuliwe kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa leo asubuhi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu leo na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti ya Viwanda na Biashara mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7), Toleo la 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Namshukuru kwa miongozo yake na uongozi thabiti akishirikiana na Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zitto pamoja na Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa kuendelea kuonyesha imani kwangu. Naahidi nitaendelea kuifanya kazi niliyotumwa na chama changu kwa moyo mmoja na uaminifu mkubwa. Sina budi sasa kuwashukuru sana wapiga kura wa Tanzania kwa kuongeza sana imani yao kwa chama

changu cha CHADEMA na kukipa kura nyingi ambazo bado sura ya kukubalika kwa chama imeendelea kung'aa sana siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru familia yangu hasa wanangu Caroline, Yahone na mume wangu mpenzi Dkt. Fidelis Owenya kwa kuendelea kunivumilia kwa kunipa ushauri, upendo na mwongozo visivyokoma hasa kipindi kigumu cha kuuguzwa baada ya kupata kipigo cha polisi huko Jjijini Arusha Januari mwaka huu. Ninakiri kuwa donda la unyama niliofanyiwa na askari wa polisi nikiwa kama mama, Mbunge na raia mwema wa nchi hii lingenitesa zaidi kama nisingepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa familia yangu hasa wazazi wangu, Mama Ndehorio Makomu na Mzee Philemon Ndesamburo pamoja na marafiki. Ninachoweza kusema, nawapenda, Mungu azidi kuwalinda na kuwatimizia yote mnayoyatarajia kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa masikitiko makubwa wakati tunajiandaa kutimiza miaka 50 ya Uhuru wa nchi yetu, sekta ya viwanda na biashara imeathirika sana na hasa viwanda kushindwa kuzalisha au kuzalisha chini ya uwezo wake kutokana na matatizo ya nishati ya umeme na hivyo kupelekea wafanyakazi kuachishwa kazi kutokana na kukosa kazi za kufanya. Hii ni aibu kwa Taifa letu ambalo viongozi wake wakuu ambao mara zote wanatafuta wawekezaji katika sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zetu kwa Serikali kwa kupunguza bei ya mafuta kama ilivyoahidi, Kambi ya Upinzani ilisikitishwa na tabia ya kiburi, dharua iliyoonyeshwa na wafanyabiashara wa nishati hii ya mafuta. Aidha, tunaishauri Serikali isimamie kikamilifu na kutekeleza agizo la Bunge lako Tukufu lililoitaka Serikali kuwa na akiba kubwa ya mafuta ili kudhibiti soko la nishati hii ikiwa ni pamoja na kufufua kiwanda cha kusafishia mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikawachukulia hatua wote waliohusika katika mgomo wa kuuza mafuta. Haya ndiyo matatizo ya soko huria ambalo Serikali haisimamii kwa makini na hatimaye kuwa soko holela. Aidha, Kambi ya Upinzani inapendekeza biashara ya mafuta inabidi iangaliwe kwa jicho pana zaidi kwani inaweza kutishia usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya Wizara hii ni kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya sekta za viwanda, biashara na masoko kwa njia ya kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na biashara, kujenga na kuimarisha ujuzi katika biashara na kuweka msukumo zaidi kutumia fursa za masoko na kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza dhima hii Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kuna changamoto kubwa ambayo inatokana na mfumo wetu wa Viwanda na Biashara ambao ulikuwa umejengeka katika dhana nzima ya kukabiliana na bidhaa na huduma toka nje ya nchi. Viwanda vinajitahidi kuzuia bidhaa za nje kwenye soko la ndani badala ya kujitahidi kufungua milango kwenye masoko ya nje sambamba na kuongeza ubora wa bidha hizo. Hili ni tatizo kubwa na jambo hili limechangia kwa kiasi kikubwa sekta ya Viwanda na Biashara kutokuwa shindani katika sura ya Kimataifa na hivyo kutokutoa tija inayohitajika ya kuleta uchumi ulioendelevu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Kambi ya Upinzani inaona kuwa ili kuwa na sekta endelevu ya viwanda inatakiwa kurekebisha mfumo mzima wa sekta ya fedha na sekta ya nishati kama vichocheo muhimu ili kufanya sekta ya viwanda kuwa shindani Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kubadlisha mfumo wa sekta ya fedha kwa dhana kuwa mikopo inayotolewa kwa wawekezaji wa viwanda uwe tofauti na ule unaotumiwa na wafanyabiashara wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi kupitia vyombo vya habari pamoja na baadhi ya watu binafsi kuhusiana na usajili wa kampuni ya kutoa huduma ya kutambua bidhaa *(bar codes)*. Kadhia hii inatokana na kusajiliwa kwa kampuni mbili tofauti lakini zenye maudhui sawa na Katiba za kampuni hizo zikiwa zinafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvutano wa kampuni hizi umezua mashaka makubwa kwa kuwa umeihusisha Serikali ikiwemo Ikulu pamoja na watendaji wake chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mvutano huo Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu kuhusu barua yake yenye Kumb. Na. BC.407/533/01 ya tarehe 16 Machi, 2011 aliyomuandikia Mkurugenzi Mkuu wa *BRELA* akimtuhumu kuhusika na sakata hili huku ikionyesha wazi kuwa kuna mashaka juu ya taratibu zilizotumika kuanzisha kampuni hizo mbili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi, je, taratibu za sheria na utawala bora zilifuatwa katika usajili wa kampuni hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa zinazoikabili Wizara kwa ujumla ni kutokutengewa Bajeti ya kutosha ili kuendesha taasisi zilizo chini yake. Jumla Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 39.97 wakati mahitaji halisi kulingana na shughuli zinazotakiwa kutekelezwa na Wizara pamoja na mashirika yake iliomba jumla ya shilingi bilioni 114.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti kati ya fedha zilizotolewa na zile zilizoombwa na Wizara ni shilingi bilioni 74.13 ambayo ni sawa na asilimia 64.96. Lazima ifahamike kwamba duniani kote viwanda mama ni jukumu la Serikali kuvianzisha, ni ukweli uliowazi hakuna mwekezaji hata mmoja aliyekuja na kujenga kiwanda hata kimoja bali wamerithi vile vilivyokuwepo. *(Makofi)*

Kwa Bajeti hii ni kweli Serikali ina nia ya dhati ya kufanya mapinduzi ya viwanda? Japokuwa Bajeti ya Wizara imekuwa finyu mno kwa kulinganisha na mahitaji halisi bado Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 175.9 kama posho za vikao. Kambi ya Upinzani inauliza umakini uko wapi katika kupanga na kusimamia vipaumbele vyetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* ana mamlaka ya usajili wa biashara na leseni kama jina lenyewe linavyosadifu lakini cha kushangaza mpaka sasa Wakala huyu hajihusishi na usajili wa leseni. Kambi ya Upinzani tunapenda kutoa ushauri kwa Serikali kuwa wakala huyu apewe jukumu la kusajili leseni kwa kuwa watakuwa katika nafasi kubwa ya kujua vizuri taarifa mbalimbali za wafanyabiashara kuliko ilivyo sasa ili kupunguza urasimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Usajili wa Biashara namba 14 ya mwaka 2007 na kuridhiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Machi, 2007. Hata hivyo pamoja na sheria hiyo kuwepo muda mrefu bado haijaanza kutumika mpaka sasa, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa sheria hiyo itaanza kutumika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hiyo inatoa mwanya wa kuanzisha kanda za usajili ambapo itasaidia wananchi wanaoishi mbali na Msajili Mkuu lakini mpaka sasa Kanda hizo hazijaanzishwa na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi wanaotoka maeneo ya pembezoni. Pia Sheria hiyo inamtaja Msajili Mkuu wa Biashara *(Chief Registrar)* ambapo wadhifa huo mpaka sasa haupo na badala yake bado wadhifa wa Mkurugenzi Mkuu bado unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini sheria hiyo haijaanza kufanya kazi na kuleta tija kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ambao wamekuwa wakihangaika kupata usajili wa majina ya biashara kutokana na urasimu uliopo *BRELA* kwa sasa, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda ina changamoto nyingi zinazosababisha sekta hii ishindwe kuwa kiongozi katika kuchangia kwenye Pato la Taifa na pia kutoa ajira nyingi na za uhakika. Moja ya sababu kubwa ni ughali katika uzalishaji kwa kulinganisha na uzalishaji viwandani kwa nchi za nje. Ughali huu kwa kiasi kikubwa unatokana na nishati umeme na maji. Sababu ya pili na ya msingi kutokuwepo kwa taasisi za fedha zinazotoa mikopo maalum kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya changamoto hizo kuna tatizo la uingizwaji wa bidhaa zenye ubora hafifu kwenye soko letu na kusababisha ushindani mkubwa wa bei na bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu

bidhaa hizi zinaingiaje nchini mpaka zinamfikia mlaji kupitia bandarini mpakani na viwanja vya ndege wakati maeneo hayo yana wakaguzi? Kwa nini wahusika wasichukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona changamoto zote tulizoeleza hapo juu sio za lazima bali zimetokana na mfumo mbaya wa Serikali uliojaa ukiritimba katika mipango inayoweka mazingira wezeshi kwa viwanda. Udhaifu uliopo katika kutekeleza sheria au sheria kutengenezwa kwa lengo la kuangalia baadhi ya watu na kwa muda fulani. Aidha, ni kwa Serikali kutunga sheria kutokana na msukumo toka nje bila ya kuwepo kwa sera na hivyo kusababisha wajanja kunufaika na sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa viwanda vyetu sisi ndio wenye jukumu la kuvilinda na sio nchi za nje ambazo nazo zinawajibu wa kulinda raia wake na viwanda vyao. Udhaifu wetu kushindwa kupanga matumizi bora ya rasilimali zetu pamoja na kutunga sheria bora na kuzisimamia itaendelea kuitesa nchi na kupelekea miaka yote sekta ya viwanda kushindwa kutoa matunda tarajiwa. Jibu la tatizo hili ni kubadilisha mfumo wa utawala tulionao kwani toka Uhuru hadi sasa imedhihirika wazi kuwa umeshindwa kuleta tija kwa Watanzania kutokana na kuwa viongozi wabovu wanalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mfumo mbovu nilioutaja hapo juu Kambi ya Upinzani inaamini kwamba marekebisho yanayotaka kufanywa na Serikali kwenye Sheria ya Manunuzi *(Public Procurement Act)*, yanalenga kuruhusu ufisadi kuendelea kwenye ununuzi wa mali za Serikali, hivyo tunaishauri Serikali kuangalia upya sheria hiyo na kuachana na kununua mali zilizotumika ili kulinda viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haiamini kabisa kama nchi nyingine inaweza kutoa fedha ili tutengeneze sheria, ni dhahiri kuwa sheria itakayotungwa haiwezi kuwa na maslahi ya wananchi wetu, kwa vyovyote vile kutakuwa na mwanya kwa ajili ya wale waliotoa fedha za utungaji wa sheria hiyo. Mfano mzuri ni Muswada uliorudishwa wa Sheria ya Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Bill), IMF* wanadai ni kwa nini Muswada uliletwa Bungeni bila ya wao kutoa ridhaa. Swali la msingi ni kwa nini wao wakubali na sio sisi wenye nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha *General Tyre,* kutokana na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza kiwanda hiki cha *General Tyre* kimetegemewa kutoa mchango mkubwa katika sekta ya usafirishaji hasa vijijini kwa kutengeneza mpira unaohimili barabara zetu. Mipira inayoagizwa toka nje imeshindwa kukidhi mahitaji ya barabara zetu kutokana na hali ya hewa na pia bei zake kuwa za hali ya juu kupita kiasi. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Kiwanda cha *East African General Tyre* cha Arusha kifufuliwe ili kikidhi mahitaji ya nchi ikiwa na pamoja na kupunguza ajali za barabarani zitokanazo na matairi yasiyokidhi viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko yaliyofuatiwa na matamko ya Serikali kuhusu Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre East Africa Ltd.* hivi sasa Kiwanda hiki kimefungwa na hakifanyi kazi yoyote. Tatizo mojawapo ambalo limechangia kufilisika kwa kiwanda ni ubadhirifu wa kuuza mali za kiwanda zikiwemo nyumba na viwanja kadhaa viliuzwa na uongozi wa Kiwanda katika mazingira tata. Vilevile takwimu zinaonyesha kuwa hadi mwaka 2009 kampuni ilikuwa ina madeni yanayofikia shilingi bilioni 38.3. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni sababu zipi zilizosababisha mbia mtarajiwa *(Continental AG)* kubadilisha mawazo na kuamua kutotoa mtaji kwa mujibu wa makubaliano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mkopo ambao Kampuni ilipewa na Taasisi ya *NSSF* Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo kadhaa. Kiwanda cha *General Tyre* kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 74 na *NSSF* ni taasisi inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, *NSSF* ndiyo iliyotoa mkopo kwa *General Tyre.*

Kambi ya Upinzani inataka kujua ni katika mazingira gani yalipelekea kuwepo kwa dalali toka Marekani aitwaye *Debt Advisory International - DAI* kushughulikia mkopo huo? Baadaye dalali huyo kulipwa dola milioni moja sawa na asilimia 10 ya mkopo wote wa dola za Kimarekani

milioni 10. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu Kampuni hiyo ya *DAI* na hatua za kisheria zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa kiwanda cha *East African General Tyre* cha Arusha kifufuliwe haraka iwezekanavyo na kisifilisiwe kama ambavyo Serikali na wadai wa Kiwanda wakifikiria la kufanya. Kwa kuwa Taasisi ya *NSSF* ni ya umma na kuna mahusiano chanya kati ya kufufuka kwa kiwanda na kufaidika kwa taasisi hii (wafanyakazi kuwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na hivyo kuongeza michango na faida kwa uchumi mpana kwa ujumla), Serikali iiombe Taasisi hii kubadili deni lake kuwa mtaji katika Kampuni ya *GTEAL* na kisha kutafuta mbia *(Strategic Investor*) kukifufua kiwanda. Katika kukifufua kuwe na mkakati makini wa kuhakikisha kuwa mashine zilizokuwa zinatumika kabla ya kufungwa kwa kiwanda hicho zimerejeshwa na kupatiwa uwezo wake wa kuzalisha na kufungwa katika kiwanda hicho ili uzalishaji uanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatoa pendekezo hili baada ya kujiridhisha kuwa nchi yetu imekuwa soko la magurudumu yasiyokidhi kiwango. Watengenezaji wengi wa magurudumu kutoka katika nchi za Asia na Ulaya wamekuwa wakizalisha magurudumu ambayo hayawezi kuhimili barabara zetu na hali ya joto katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi kwamba magurudumu haya hayamudu changamoto za barabara zetu na hali ya hewa huku kwetu ni kutokea kwa ajali nyingi ambazo zinagharimu maisha ya Watanzania wengi na kuwaacha wengi wakiwa na ulemavu wa kudumu mara kwa mara, baada ya tairi hizo kupasuka ovyo au kuyeyuka barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kwamba Kamati ndogo iliyoundwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma *(POAC*) itakuwa imemaliza kazi yake, hivyo Kambi ya Upinzani inataka taarifa yake iwasilishwe Bungeni haraka na hatua za utekelezaji zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Nguo Mwanza *(Mwatex),* kiwanda hiki ni mojawapo ya viwanda vilivyofunguliwa na Muasisi wa Taifa letu kwa lengo la kutoa ajira na kupata soko la wakulima wa pamba. Mwaka 1999 wafanyakazi zaidi ya 1500 waliachishwa kazi ghafla kwa kisingizio kuwa kiwanda hakina uwezo wa kujiendesha. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wafanyakazi hatma ya maslahi yao, ina mkakati gani wa makusudi wa kukirejesha kiwanda hicho katika hali yake ya awali ya uzalishaji ili kuepuka kuuza pamba ghafi nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 1980 viwanda vya magunia vilikuwa vikifanya kazi kwa asilimia 100 na kupata tija kubwa sana. Ajira ilipatikana viwandani humo kwani Watanzania wengi waliajiriwa katika mashamba ya mkonge na viwanda husika. Serikali ilipata fedha nyingi za kigeni kutokana na biashara ya magunia na kamba za katani katika soko la dunia.

Kambi ya Upinzani inasikitishwa na namna sera ya uwekezaji inavyotekelezwa kwa kuua kabisa zao hili muhimu. Mathalani kiwanda cha magunia cha Mjini Moshi kilikabidhiwa kwa mwekezaji ambaye sasa amekifanya kiwanda hicho kuwa *godown*. Mashine zote zimeng'olewa katika kiwanda hicho na kuliacha jengo lile kuwa ghala tu la kuhifadhia mali. Mwekezaji analalamikia Serikali kuweka ugumu kwake kupata soko baada ya kufungua soko la magunia kuingia nchini kwa bei rahisi sana. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kutoa waraka wa kuyataka mashirika yote yanayofungasha mazao ya chakula kama vile mahindi, mchele, kahawa, korosho, mbaazi, maharage na kadhalika kuwa yafungashwe mazao hayo katika magunia ya katani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kuhifadhi nafaka kwa kutumia magunia yatokanayo na mkonge na viwanda vya hapa nchini ni nyingi. Nitaelezea chache tu, kwanza tutaendeleza kaulimbiu ya Kilimo Kwanza kwa vitendo kwa kuwaendeleza wakulima wetu kwa kupata ajira katika mashamba ya mkonge, pili, wananchi watapata ajira katika viwanda vinavyozalisha magunia na Serikali itapata fedha kutokana na kodi na viwanda hivi na kulioongezea Taifa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa angalizo kwa wenye viwanda vya magunia hapa nchini kwa kupata fursa ya kuuza magunia ya kuhifadhi nafaka wasichukulie ndio njia ya kuuza magunia kwa bei wanayoamua. Lazima bei iweze kulingana na bei ya soko. Kwa upande mwingine Serikali ichukue jukumu la kutoza kodi kubwa kwenye magunia yanayotoka nje ili kulinda masoko ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wetu kama watunga sheria na wawakilishi wa wananchi kuhakikisha tunaweka Utaifa wetu mbele na mengine yafuate baadae. Kama nchi hii tunaweza kuagiza magunia kutoka nje ya nchi kwa nini sisi tusiwe ndio tunapeleka magunia hayo nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Serikali ya Tanzania inamiliki hisa asilimia 49% na Serikali ya watu wa China wanamiliki hisa 51%. Kiwanda cha ubia kilianza kazi rasmi tarehe 01/04/1997. Asilimia 49 ni nyingi mno hivyo kukosekana kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara katika masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji ni kosa ambalo limesababisha Serikali kupata hasara kubwa. Katika hatua ya kukiimarisha kiwanda Serikali ya China ilitoa mkopo wa *USD* 27,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni kwamba fedha hizo zilitumika kununua mitambo mikuu kuu. Aidha, wafanyakazi waliendelea kupunguzwa badala ya kuongezwa kutokana na kufufuliwa kwa mitambo, jambo ambalo kama kweli mitambo ingelikuwa ni mipya ajira zingeongezeka na siyo kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inafahamu kuwa baadhi ya mitambo imekuwa ikiuzwa kama vyuma chakavu? Aidha, Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ukaribu wa Serikali kwa ujumla na uendeshaji wa Kiwanda chetu ukoje? Kwani Serikali ndiyo iliingia ubia na Serikali ya watu wa China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, msuguano mwingine unatokana na ukweli kwamba wakati Bodi ya Pamba ilivitaka viwanda vyote vinavyotumia bidhaa ya Pamba kama malighafi muhimu katika uzalishaji wa bidhaa zake kuipelekea mahitaji yao ya pamba kutokana na kupanda kwa mahitaji ya pamba kwenye soko la dunia, menejimenti haikupeleka mahitaji ya kiwanda kwenye Bodi hiyo na matokeo yake, Bodi hiyo ikauza pamba nyingi kwenye soko la dunia. Matokeo yake ni kiwanda hicho kukosa malighafi ya kutosha na hivyo kupunguza wafanyakazi kwa kisingizio cha kutokuwa na malighafi (pamba) ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na wimbi kubwa la ukosefu wa ajira, hivyo basi ninaiomba Serikali kupitia kwenye Bodi ya Mamlaka ya Pamba kuweka kipaumbele katika mauzo ya pamba kiwe ni viwanda vya ndani kwanza kabla ya kuuza nje ya nchi, hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa mtafaruku wa bei ya pamba ulioko hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Viberiti cha Mjini Moshi *(Kibo Match)* ni kati ya viwanda vyenye kuzalisha ajira zisizopungua 600. Hali ya kiwanda hiki kwa sasa iko taabani, punde kitafungwa kutokana na kukosa uwezo wa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa mkubwa uliokikumba kiwanda hiki ni ushindani usiodhibitiwa. Viberiti vingi kutoka nje vimevamia soko letu na kutokana na kutokuwepo kwa kodi maalum kwa waagizaji ikiwa ni pamoja na tatizo la kutokuwa na umeme wa uhakika. Kwa lengo la kukinusuru kiwanda basi kiwanda kimejikuta kikishindwa kabisa kumudu ushindani katika soko hili holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutoa njia mbadala za kuokoa kiwanda hiki ambacho kimeajiri mamia ya Watanzania ambao ajira zao zinakuwa si za uhakika mara kwa mara kutokana na kusuasua kwa soko la viberiti ambapo hali hiyo husababisha kiwanda kushindwa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, Kiwanda hiki kilibinafsishwa mwishoni mwaka 1998 katikati ya mabishano na upinzani wa wafanyakazi wa

kiwanda, wakulima na Serikali; hoja za wafanyakazi na wakulima wa miwa ilikuwa kwamba kiwanda hakina matatizo yoyote ya kujiendesha na hivyo hakihitaji ubinafsishaji. Hata hivyo kiwanda kilibinafsishwa kwa nguvu ya Serikali na siyo kuwa kilikuwa na matatizo ya kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kubinafsishwa kiwanda hiki kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara na endelevu hadi sasa:-

(i) Migogoro kati ya Kiwanda na Wakulima wa miwa;

(ii) Migogoro kati ya kiwanda na wafanyakazi wake;

(iii) Migogoro kati ya kiwanda na wafanyakazi wastaafu; na

(iv) Migogoro kati ya Kiwanda na vijiji majirani zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wananchi wa Mtibwa matatizo haya yataisha lini? Hadi sasa kiwanda hiki kinadaiwa jumla ya shilingi milioni 421 ikiwa kodi stahiki ya 0.3% kwa Halmashauri ya Mvomero kutokana na mauzo ya sukari, je, fedha hizi zitalipwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maonesho ya Sabasaba ya 34 ya mwaka 2011; Kambi ya Upinzani inapenda kuwapongeza *TanTrade* kwa maonesho ya mwaka huu 2011 ambayo yalikuwa yameandaliwa vizuri sana. Utaratibu wa kuingia katika maonyesho ulikuwa mzuri ikiwa ni pamoja na suala zima la ulinzi na usalama wa raia na usafi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo Kambi ya Upinzani bado tunatoa ushauri ili kuweza kuongeza kipato katika viwanja vya Sabasaba kuwe na maonesho endelevu tofauti, kila baada ya miezi mitatu. Kwa mfano maonesho ya vyakula pekee, maonyesho ya magari na mwisho yaje yale ya jumla ya Sabasaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza pia kuwa maonesho kama yale ya Sabasaba yafanyike Kikanda kwa lengo la kuwakutanisha wazalishaji mbalimbali na wadau pamoja na kuwapatia masoko kwa wale wasioweza kufika Dar es Salaam kwenye maonesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaishauri Serikali iweke mkakati wa kuwaorodhesha wazalishaji wote wa viwanda vidogo vidogo ili iwezekane kuwashirikisha katika maonesho hayo mbalimbali ndani na nje ya nchi kama vile maonyesho ya Jua Kali Afrika Mashariki. Lengo la maonesho haya pia liwe kutoa mafunzo ya kuongeza tija katika uzalishaji wa bidhaa zao za viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari za Tanzania zinalalamikiwa sana kutokana na ucheleweshaji katika kutoa mizigo iliyoko forodhani. Mathalani inachukua si chini ya siku sita kutembeza karatasi za kutoa mizigo bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika tatizo la kucheleweshwa kwa utoaji wa bidhaa bandarini halitokani na ubovu au uduni wa miundombinu bali ni ukiritimba unaotokana na mlolongo wa madawati yanayotakiwa kupitiwa hadi kufikia hatua ya kutoa mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kutoa mizigo bandarini na kuondoa kabisa mianya yote ya ukiritimba bandarini hapo ili kuwawezesha wafanyabiashara kutovunjika moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko mengi yalikuwepo kipindi cha Sabasaba kwa waonyeshaji *(exhibitor)* kushindwa kukomboa mizigo yao bandarini hadi maonesho kukaribia kufungwa, hili siyo jambo zuri kwa nchi yetu. Nchi inayoyatangaza maonesho nchi za nje zije

wakifika wanakutana na kero tele za kukomboa mizigo yao. Hii ni aibu kwa Serikali na hivyo tunaitaka kuchukua hatua za kurekebisha kero hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu ni biashara. Uendelezaji wowote ni biashara, kufanya kitu kiwepo ni biashara, uhai wa watu ni biashara, kuulinda huo uhai pia ni biashara. Kambi ya Upinzani imejiridhisha kuwa Serikali haina mpango wa kuwawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kufanikiwa kufanya biashara kwa mafanikio na tija kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kwamba Serikali haijawa tayari kubeba mzigo wa kuwawezesha kiujuzi wajasiriamali pamoja na kuweka sera zitakazozilazimu taasisi za mikopo na benki zilizoko nchini kutoa mikopo rafiki kwa wajasiriamali wetu, ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira mazuri kwa wazawa kumudu biashara na ushindani katika biashara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ikiwawezesha wananchi wake kufanya biashara zenye tija, uchumi utainuka kwa kasi kubwa. Tatizo la ajira litapungua sana kama si kutoweka kabisa na soko letu la ndani litakuwa na bidhaa zenye uhakika wa ubora kwa usalama wa walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa hili linawezekana kabisa. Imekuwa ikionekana bayana kwamba wawekezaji kutoka nje ya nchi wanaingia nchini na *briefcase* tu yaani wanakuja bila mtaji hata kidogo ama wanakuja na mtaji kidogo sana lakini kama vile tumerogwa, mabenki yote yanafungua milango na Serikali inawapa wawekezaji hao fursa za kukopa na kuendesha biashara zao kwa mafanikio makubwa. Hatimaye wanaondoka nchini wakiwa wamepata faida nono mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa kwa nini milango inayofunguka mbele ya wawekezaji wa kigeni haifunguki kwa wajasiriamali wazawa? Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri masharti ya uwekezaji yawe ya usawa baina ya wageni na wazawa, kwani ilivyo wazawa wanaumia zaidi. Mfano mzuri ni katika ulipiaji wa ankara za umeme na maji wote wanalipa sawa lakini wageni wanapata unafuu wa kulipa kodi, jambo linalopelekea kutokuwepo kwa mazingira sawa katika ufanyaji wa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaonekana kuwa Taifa lisilojali watu wake kwa kuwapendelea sana wageni na kuwatelekeza wazawa. Maandiko matakatifu yanatanabaisha kuwa nchi yenu itakuwa imelaaniwa mtakapowapa wageni heri na kuwafanya wana na mabinti wenu kuwa watumwa katika nchi yenu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaacha changamoto hii kwa kuitaka Serikali kuonyesha kwamba ina nia ya kweli ya kuondoa umaskini kwa Watanzania na kwa Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ndiyo nguvu ya biashara, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itambue kuwa mawasiliano ya simu, posta, *internet, fax* na kadhalika ni nyenzo muhimu sana katika kufanikisha biashara. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali sasa ione umuhimu wa kusaidia upatikanaji wa mawasiliano ya simu posta, benki, *internet* kwa wingi hadi vijijini. Ijulikane kuwa *internet* si anasa bali ni zana za kazi katika kuwezesha biashara kufanyika kwa ufanisi. Kambi ya Upinzani inapenda kuipongeza Serikali kwa kuendelea na juhudi za kufunga mkongo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, nchi zilizopiga hatua kubwa katika uchumi kama vile Malaysia, Indonesia, Trinidad na Tobago zilichukua hatua za makusudi kuwawezesha wazalendo kuanzisha viwanda vidogo vidogo vyenye tija, kuanzisha ama kwa ushirikiano au kibinafsi *(individually)* viwanda vya kati na vile vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo, vya kati na vikubwa havitokani tu na bidii ya wananchi na au wawekezaji. Ni sharti Serikali itengeneze sera nzuri na kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya kuwezesha uanzishaji, uendeshaji, ukuaji na usalama wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tija katika sera ya Kilimo Kwanza haiwezi kuonekana hadi pale ambapo tutakuwa tunawawezesha wananchi wetu kuzalisha na kuuza mazao ambayo yameongezewa thamani katika viwanda. Kama kilo moja ya pamba inayouzwa shilingi 800 – 1,100 inatengeneza mashati manne na kila shati likauzwa shilingi 10,000 tu, basi tukiwezesha Watanzania kutumia pamba yote nchini kwa kuwawezesha kujenga na kuendesha kwa tija viwanda vya nguo pamba kilo moja ingepanda thamani hadi kufikia shilingi 20,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano ambao Waheshimiwa Wabunge wote hapa Bungeni wanaujua na wana uchungu nao na dhana ya Mheshimiwa Rais ya maisha bora kwa kila Mtanzania yatafanikiwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO);* naipongeza *SIDO* kwa jitihada inayofanya kuwawezesha wajasiriamali lakini *SIDO* ingeweza kufanya vizuri zaidi kama Serikali ingeamua kuchukua hatua za makusudi kuwawezesha kifedha zaidi ili waweze kutengeneza viwanda vidogo/vya kati katika kila vijiji ili wakulima waweze kusindika na kuongezea mazao thamani kulekule kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji huu kwa kiasi kikubwa utaondoa tamaa ya vijana kukimbilia mijini ambako wakifika huko badala ya kupata ajira wanaishia kupigwa mabomu ya machozi na kupigwa kwa kuambiwa wamevamia maeneo yasiyoruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji kwa kiasi hiki cha shilingi bilioni 1.6 walichopewa *SIDO,* kweli Serikali ina nia thabiti ya kuwakomboa wajasiriamali au ni fedha za kulipa wafanyakazi mishahara? Ukizingatia kuwa walikuwa wameomba kupatiwa jumla ya shilingi bilioni 11.23? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* pamoja na kuwa na umuhimu mkubwa katika ukuaji wa uchumi kwa shirika hili, imekuwa kawaida kuona kuwa *NDC* inaendeshwa kama shirika linalogharamiwa na Serikali kwa miradi yake yote. Ni pendekezo la Kambi ya Upinzani kwamba kuanzia sasa *NDC* iendeshwe kibiashara, ikifanya miradi yake kibiashara na kwa utaalamu zaidi ili kupata faida na kuweza kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa ubia baina ya Shirika la *NDC* na Kampuni *Sichuan Hongda* toka China ili kuendeleza Mradi wa Mchuchuma - Liganga ni muhimu usainiwe sasa kwa haraka na Serikali ishauriwe kutimiza wajibu wake kwa hatua ambayo *NDC* imefikia ikizingatiwa faida za kiuchumi za mradi huu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa ya utekelezaji kuhusiana na mradi huo. Mazingira ya sasa ya uchumi wa dunia na mahitaji ya Taifa ni muafaka kwa miradi ya makaa na chuma. Kuchelewa kuanza kwa miradi hii kunaweza kusababisha miradi isifanyike kabisa kwani uchumi wa dunia kwenye bidhaa za chuma huwa unayumbayumba sana *(fluctuations). (Makofi)*

Mradi huu ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, ni vema tukaweka utaratibu wa kupata taarifa kila Mkutano wa Bunge juu ya utekelezaji wa mradi huu kama Kauli za Mawaziri kuhusu utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni tanzu itakayoundwa ili kuendesha miradi hii ifuate taratibu zote za uchimbaji ikiwemo kusainiwa kwa Mkataba wa Uendelezaji Migodi *(Mineral Development Agreements-MDA)* kwa madhumuni ya kulinda maslahi ya Serikali, watu wa Ludewa na kampuni yenyewe. Hapa tunasisitiza, faida kwa wananchi wa Wilaya ya Ludewa na badala ya kuwa na kinachoitwa *win-win situation* katika ya Serikali na mwekezaji, tuite *win-win-win situation* na hii *win* ya mwisho ni wananchi wa Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la ubia limeishaamuliwa, ni bora kuangalia namna ya kufanya marekebisho ili ubia uzingatie kanuni ya faida *(profitability and pay back period)* au baada ya mwekezaji kurejesha mtaji wake basi hisa za Serikali zipande. Kwa mfano, *NDC* waanze kuwa na hisa 20% lakini mara baada ya mradi kulipa *(payback period)* umiliki wa hisa uwe ni sawa kwa sawa. Pendekezo hili pia lizingatiwe kwa mradi wa Ngaka ambapo *NDC*

wanahisa 30% kwenye Kampuni tanzu ya *TANCOAL Energy*. Miradi mingine yote inayohusu rasilimali madini ya Taifa iwekewe utaratibu wa aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyotengewa *NDC* ya shilingi bilioni 7.06 wakati wao waliomba jumla ya shilingi bilioni 24.35, kwa utekelezaji wa miradi minne mikubwa ambayo ni Liganga, Magadi Soda, Mradi wa kuangamiza mazalio ya mbu Wilayani Kibaha, ili kuingia kwenye ubia wenye faida ni lazima uweke mchango wako. Hivyo basi katika miradi ambayo *NDC* inaingia ushirika na makampuni toka nje mchango wa shirika hilo kwenye ubia ni muhimu zaidi, vinginevyo nchi yetu itaendelea kuwa wasindikizaji na kuwatengeneza faida wabia wetu na sisi tukibakia masikini bila kupata faida yeyote kwenye ubia huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Magadi Soda ni mradi mkubwa na muhimu kiuchumi (ukitekelezwa Taifa letu litapanda chati duniani kwa kuwa wazalishaji wakubwa wa Magadi - Soda duniani, watu watapata ajira, Bandari ya Tanga itapata biashara kubwa na uchumi wa Taifa utakua). Lakini kulitokea kutokuelewana baina ya Serikali na wanaharakati wa mazingira. Kambi ya Upinzani inataka Serikali kutoa kauli kuhusiana na je, mradi huo unaendelea au umesimama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme na viwanda; viwanda ni moja ya sekta zinazoathiriwa sana na janga la ukosefu wa umeme linaloikumba nchi yetu kwa sasa. Tayari Umoja wa Wamiliki wa Viwanda umeshatangaza athari mbalimbali wanazozipa kutokana na janga hili ambalo mwisho wake ni kuathirika kwa uchumi wa nchi kwa wenye viwanda kushindwa kulipa kodi kwa Serikali kama inavyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashindwa kuona ni jinsi gani Serikali itawezesha kuendeshwa kwa sekta ya viwanda bila kuwepo kwa umeme wa uhakika. Tunaishauri Serikali kuona kwamba sasa umefika wakati suala la umeme lipatiwe suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba vipo vyanzo vingi vya umeme ambavyo vinaweza kabisa kutumiwa na kupata umeme wa uhakika na pengine kuwa na ziada ya kuuza nje. Lakini inaonekana kwamba Serikali haipo makini katika suala hili na tunawashauri wazingatie mapendekezo kama yalivyowasilishwa na Waziri Kivuli wa Nishati na Madini Mheshimiwa John Mnyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZA* ni mpango mzuri wa kuwavutia wawekezaji. Lakini ni lazima izingatie maslahi ya wazawa kwenye haki zao kama malipo ya fidia pindi wanapowapisha wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi ya kulipwa fedha kidogo kwa wananchi wale ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya uwekezaji huu, mathalani Wilaya ya Bunda mradi wa *EPZA* ulifanyiwa tathmini tarehe 17/10/2007 ukihusisha vitongoji vinne katika kijiji cha Tairo ambavyo ni Kitongoji ch Kirumi waliofanyiwa tathmini ni 404; Kitongoji cha Mabatini "A" waliofanyiwa tathmini ni 220 na Kitongoji cha Bushigwamara waliofanyiwa tathmini ni 203. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini hii kufanyika mnamo mwaka 2008 baadhi ya vitongoji ambavyo viligundulika kuwa havimo kwenye mradi vilipewa ahadi ya kulipwa fedha za usumbufu kutokana na kuacha kuendeleza maeneo yao navyo ni Kitongoji cha Mabatini "A" na kitongoji cha Bushigwamara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa vitongoji tajwa hapo juu wahusika 220 kutoka Kitongoji cha Mabatini na wakazi 203 kutoka Bushigwamara hawajalipwa chochote. *EPZA* iliamua kuchukua Kitongoji cha Kirumi ili kitumike kwenye mradi na kuhamisha wakazi 404 kutokana na tathmini, lakini malipo ambayo hayalingani na tathmini ya maeneo yaliyochukuliwa yalifanyika kwa wakazi 116 tu, aidha, wakazi waliolipwa fedha kiduchu wanasubiri kupewa maeneo mapya jambo ambalo hadi sasa halijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuonesha mambo tatanishi katika zoezi hilo, eneo la Ndugu Kichele Nyasawanga lenye ekari 32, tathmini ilifanywa kwa ekari 25, tarehe 28/10/2011

alipokea hundi kupitia NMB ya shilingi 8,012,792 *PV No. 9000458* kama fidia ya ekari 32 pamoja na mali zilizokuwemo wakati wa tathmini, suala ni kwa vipi walilipa ekari 32 wakati tathmini ilikuwa kwa ekari 25? Sambamba na hilo kuna wakazi halali wa kitongoji hicho majina yao hayakuonekana katika wale wanatakiwa kupewa fidia na kupatiwa maeneo mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tathmini ifanyike hadi sasa ni muda wa miaka mitatu, ambapo ekari moja ilitathminiwa kwa shilingi 300,000 lakini hali halisi ni kwamba thamani ya ardhi imepanda. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni kwa nini wananchi wasilipwe fidia kwa bei ya soko ambayo ni tofauti na wakati wa kufanya tathmini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna madai kama hayo Wilayani Bagamoyo ambapo wananchi walichukuliwa mashamba na makazi yao kwa ajili ya kupisha mradi wa *EPZA* lakini hadi sasa mwaka umepita tangu kufanyika kwa tathmini lakini hawajapewa fidia na kupewa maeneo mbadala. Wananchi hao walizuiwa kufanya shughuli yoyote ya maendeleo katika eneo hilo, jambo linalowaletea umaskini na kuwa ombaomba. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli katika suala hili na kama wakilipwa walipwe kwa kuzingatia thamani ya sasa na sababu zipi zimepelekea kutolipwa kwa mrefu kiasi hicho tangu mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha *EPZA* imetengewa fedha za ndani kwa ajili ya kuendeleza maeneo maalumu ya *EPZ* na *SEZ,* lakini haionyeshi fedha za kulipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kupisha mradi huo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali inapoingia mikataba na wawekezaji maslahi ya wananchi yawekwe mbele, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa kipaumbele cha Serikali ni kwa wananchi wake au kwa uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Ushindani, Ubora wa Bidhaa za Huduma *(TBS);* Kambi ya Upinzani inapokea kwa mikono miwili hatua ya Tanzania kuingia katika *bar code system*. Hii itawawezesha wazalishaji wa Tanzania kuuza bidhaa nje ya nchi kwa halisi ya bidhaa zao bila kuonekana kuwa bidhaa zetu zinazalishwa nchi jirani. Mfano mzuri ni *Tanzanite* katika soko la Kimataifa Tanzania haijulikani kama ni mzalishaji mkubwa na pekee duniani wa madini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* inahitaji kuharakisha uanzishaji wa kituo cha ufungashaji *(Packaging Technology Center)* ili iwezeshe kuwepo kwa ushindani mzuri hasa katika nyakati hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, izingatiwe pia kuwa Tanzania inaingia katika Soko la Afrika Mashariki hivyo ni lazima tuzalishe bidhaa zenye uwezo wa kushindana katika soko kwa mafanikio. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa kasma ya shilingi milioni 80 iliyotengwa kwa ajili ya *TBS* iongezwe ili kuipa uwezo wa kufanya kazi zake kwa tija, kwani kasma hiyo ni kwa ajili ya kuendeleza teknolojia ya vifungashio bidhaa tu, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa *TBS* inatakiwa kufanyakazi nyingi zaidi za maendeleo zaidi ya hii ya vifungashio, mfano mazao ya kilimo hasa matunda na mboga mboga kwa minajili ya soko la nje ya nchi yawe katika viwango vipi na yazalishwe kwa utaalam upi? Hii yote ni changamoto inayoikabili *TBS*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti, mafunzo na maendeleo ya teknolojia, moja ya jukumu la msingi la Wizara hii ni kusimamia taasisi zinazofanya utafiti na maendeleo ya teknolojia katika sekta za kilimo na maendeleo vijijini *(CAMARTEC),* taasisi nyingine ya *TEMDO* inaonyesha kuwa msisitizo wa utendaji kazi wake umewekwa katika kubuni mitambo na vifaa vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo, mitambo na vifaa kwa ajili ya nishati mbadala pamoja na mitambo na vifaa kwa ajili ya sekta ya madini. Uanzishwaji wa Taasisi hii ilikuwa ni maalum kwa ajili ya utafiti na maendeleo ya uandisi kwa ajili ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maudhui mazima ya utendaji kazi wa taasisi hizi mbili ni dhahiri kuwa zinafanya kazi zinazofanana, japokuwa uanzishwaji wa *TEMDO* ulikuwa maalum kwa ajili ya utafiti wa teknolojia kwa ajili ya viwanda ambavyo Muasisi wa nchi hii alifanya juhudi kubwa sana kuvianzisha. Kambi ya Upinzani kwa kuliona hili la muingiliano wa shughuli baada ya taasisi moja kujitoa katika kazi zake za msingi jambo ambalo kwa kiasi kikubwa viwanda vyetu vimeishia kubinafsishwa kutokana na teknolojia iliyokuwa inatumika viwandani kupitwa na wakati.

Ni vyema taasisi hizi zikaunganisha nguvu zake badala ya kuendelea kufanya kazi za kurudufiana, mfano, taasisi zote zinatengeneza mashine za usindikaji wa mazao kama kupukuchua mahindi, kukamua mafuta na matunda na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi Maghalani, mfumo huu umekumbana na changamoto nyingi hasa kwa mazao ambayo ni mazao ya chakula kutokana na wakulima kutokupatiwa elimu ya kutosha juu ya utendaji kazi wa mfumo huu. Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka Bajeti ya kutosha kwa Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania ili watoe elimu ya kutosha Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuhitimisha hotuba yangu hii kwa kutoa tena shukrani zangu kwa Watanzania kwa kuendelea kuwa wavumilivu wakati huu mgumu ambao maisha yamezidi kuwa magumu na hatuoni hatua za haraka za makusudi zinazofaywa na Serikali ili kuwaondolea mzigo huu. Hata hivyo sisi tutaendelea kuwatetea Bungeni kwa kutoa hoja zenye nguvu na zinazokusudiwa kuishauri na kuitaka Serikali kutekeleza vyema wajibu wake kwa wananchi. Kazi hii tutaifanya kwa upole, uhakika, umakini, bidii kubwa na hakuna kulala mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda kuishukuru Wizara na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa pindi yanapotokea majadiliano yahusuyo Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wadau wote wa maendeleo na wananchi kwa ujumla nashukuru sana kwa kunisikiliza Mungu awabariki wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Viwanda na Bishara Mheshimiwa Lucy Owenya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, aliombwa miongozo mbalimbali hapa na miongoni mwa Mwongozo mmojawapo kulikuwa kuna jambo la dharura na ilimpasa kuitisha Kikao cha Kamati ya Uongozi inaonekana kikao hicho kimeisha. Kwa hiyo, basi ninaomba nimpe nafasi ili aje aendelee na utaratibu unaoendelea. *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kwamba asubuhi ya leo niliombwa miongozo mbalimbali lakini Mwongozo mmojawapo wa Mheshimiwa January Makamba ulihusu jambo la dharura kufuatana na Kanuni ya 47. *(Makofi)*

Baada ya muda wa Maswali kumalizika Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kwa shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge jambo halisi la dharura. Ukiitazama Kanuni ya 47(4) inasema; "Iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura, halisi na lina maslahi kwa umma, basi aturuhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala huu wa hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa." *(Makofi)*

Mimi nikaona ni busara nipata ushauri wa Kamati ya Uongozi wa Bunge, nisiamue jambo hili peke yangu. Katika kuamua Kamati ya Uongozi ya Bunge imezingatia Kanuni ya 48(3) na (4) ambayo inasomeka kama ifuatavyo; "Jambo linaloletwa kwa hoja chini ya Kanuni hii litahesabiwa kuwa ni jambo la dharura iwapo; (a) athari zake ni dhahiri na linaweza kutokea wakati wowote;" Kamati ya Uongozi imeona kwamba jambo hili athari zake ni dhahiri. Ikakubaliana na hoja iliyotolewa kwamba limetokea siku hiyo au siku za karibuni na limeletwa bila kuchelewa imeonekana kwamba hoja hii inakidhi kipengele hicho na hakutatokea fursa ya kujadili siku za karibuni kwa njia ya kawaida ya kushughulikia mambo ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika siku za karibuni hatuna ajenda ya kujadili jambo hili la *crisis* ya mafuta kwa hiyo, imekidhi. Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake. *(Makofi)*

Kamati ya Uongozi imeona kwamba jambo hili kwa jinsi lilivyo linahitaji hatua zaidi. Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi imekubaliana na mtoa hoja kwamba jambo hili linahitaji lipewe fursa ya kuweza kujadiliwa kwa utaratibu wa kidharura. Kwa jinsi hiyo, muda mfupi ujao nitatoa fursa hiyo kwa Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kufanya hivyo kwa utaratibu kwamba Wabunge watakaotaka kuchangia watasimama mahali pao nitachukua majina yao halafu itategemea na muda tulionao tutaendelea na uchangiaji. Lakini uchangiaji wenyewe utakuwa ni Mbunge mmoja atachangia si zaidi ya dakika tano ili kutoa nafasi kwa Wabunge wengi zaidi katika muda mdogo tulionao. Kwa hiyo, naomba sana watakaopata fursa hiyo wajitahidi kutumia mwanya huo mdogo tulioupata kuweza kutusaidia katika jambo hili. *(Makofi)*

Lakini tutaanza na Mheshimiwa January Makamba ambaye ndiye alilileta jambo hili, yeye nitampa dakika 10 hadi 15 itategemea na alivyojipanga. Halafu baada ya hapo tutaendelea na Mheshimiwa Naibu Kiongozi wa Upinzani Mheshimiwa Kabwe Zitto na Waheshimiwa Wabunge wengine kadri nitakavyoorodhesha tutafuata kwa dakika tano tano.

Naomba tuzingatie Kanuni kwa wale ambao wana maslahi katika sekta hiyo katika kuchangia kwao basi kwa sentensi moja wa-*declare interest* ili tuweze kwenda vizuri. Hauzuiliwi hata kidogo ni kuweka tu mambo sawa ili tuweze kwenda vizuri. Baada ya maelezo hayo sasa moja kwa moja naomba nimuite Mheshimiwa January Makamba. *(Makofi)*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hoja niliyoitoa ya kujadili tatizo la mafuta nchini kama jambo la dharura. Nitajitahidi kutumia muda mfupi zaidi ili na wenzangu wapate nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haihitaji maelezo marefu na ya kina kujua kwamba nchi ipo kwenye dharura. Tumekuwa kwenye mgao wa umeme katika kipindi cha muda mrefu sasa. Tumekuwa tunalalamikia nishati ya umeme. Lakini kwa maendeleo ya nchi yetu, usalama wa nchi yetu, ustawi wa nchi yetu, nishati ya mafuta ni muhimu zaidi kuliko nishati ile ambayo tumekuwa tunaipigia kelele siku zote. Sasa maana hata umeme vilevile unazalishwa kwa mafuta. Mgao wa umeme ni adha lakini mgao wa mafuta ni kiama. Mama Anne Kilango Malecela alitumia neno zuri wakati tupo kwenye Kamati ya Uongozi kwamba nchi itasimama ni kweli nchi itasimama. *(Makofi)*

Sasa tangu tarehe 3 mwezi huu baada ya *EWURA* kutoa tangazo la bei mpya kabla ya tangazo mafuta yalikuwa yanatosha mambo yalikwenda vizuri watu wananunua wanafanya shughuli zao, siku ya pili ghafla mafuta yakakauka vituoni. Sasa sisi hapa Bungeni kazi yetu tunatunga sheria, lakini kuna wenzetu tunawapa kazi ya kuzisimamia hizi sheria. Katika mazingira ambapo mafuta yalikuwepo siku moja na kesho yake hayapo nchi nzima hapo kuna tatizo la udhaifu katika usimamizi wa sheria. *(Makofi)*

Sasa maamuzi ya kushusha bei ya mafuta msingi wake ilikuwa ni mmoja tu kwamba na sisi Bungeni hapa tulikubaliana kwamba katika mipango yetu na sisi kwenye Chama chetu cha Mapinduzi katika mipango yetu yote tunayofanya lazima tuhakikishe kwamba gharama za maisha ya watu zinashuka. Hatua ya kushusha bei ya mafuta ni hatua ya kuelekea huko kwenye kushusha gharama za maisha. *(Makofi)*

Sasa wenzetu mnapofanya uamuzi wa kutekeleza sheria lazima vilevile muwe mmejiandaa kwenye kusimamia uamuzi ule wa kisheria. La sivyo sisi hapa tunakuwa tunatunga sheria tunawapa wenzetu hamuwezi kuzisimamia sasa kuna haja gani ya kutunga sheria kama hakuna uwezo wa kuzisimamia? Wenzetu wa *EWURA* unapotoa tamko kama lile ambalo lazima utekelezaji wake unahitaji uwezo mkubwa wa kiutawala na uendeshaji unatoa tamko halafu kesho yake mambo yanaharibika unasubiri wiki nzima kana kwamba hakuna kitu. *(Makofi)*

Sasa sisi hapa ni viongozi tumekuja kuwawakilisha watu hatuwezi kukaa humu tunaendelea na Bunge wakati mambo yanaharibika huko watu wanahangaika, wanapata adha tunaendelea tu na Miswada na vitu vingine kana kwamba hakuna tatizo. Hili ni tatizo kubwa lazima tulijadili, lazima wenzetu kwenye Serikali hebu waonyesha kabisa kidogo kwamba Serikali jamani ipo na ina uwezo wa kusimamia Sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu haiwezekani maana yake hili jambo la mafuta nadhani kila Mbunge ana historia yake jinsi alivyoli-*experience.* Sasa zinakuja simu hapa na *message* kwamba sasa hivi mafuta sawa mmeshusha bei, lakini kwa matokeo ya kutosimamia sheria na kutosimamia tangazo lile sasa hivi watu wananunua mafuta kwa shilingi elfu tatu au elfu nne, elfu tano. Sasa hata ile hatua ya kushusha bei kwa sababu usimamizi wake haukuwa mzuri matokeo yake ni kwamba bei zimekwenda juu zaidi. Kuna foleni kubwa sana kwenye vituo vya mafuta Dar es Salaam. Ukikaa kwenye foleni upo mwisho mtu anakuja na dumu la lita 20 anakuambia nipe 25,000 kwa sasa watu wananunua mafuta badala ya bei ile ambayo tumesema tumeshusha wananunua maradufu. Nimepata ujumbe sasa hivi Korogwe shilingi 3,000; Handeni naambiwa hapa na Mheshimiwa Dkt. Kigoda ni shilingi 4,000. Sasa nchi nzima mafuta yamepanda maradufu kuliko ile bei ambayo mmetuambia mmeishusha na Tabora naambiwa hakuna. Najua Wabunge wote sehemu mbalimbali za nchi hii watu wanapata shida. Sasa jamani tusiruhusu tuonekane kana kwamba sisi viongozi hatupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake sisi tupo kusimamia haya mambo. Sasa kama watu wanapata adha, wanahangaika, wanasumbuka halafu kana kwamba hatujali, hatuoni tamko, hatuoni hatua hasa tunapata shaka.

Kwa hiyo, tunaomba wenzetu wa Serikali mkiweza basi jioni leo njooni na tamko hebu wahakikishieni umma huu kwamba jamani nchi haiendi kwa sababu mafuta, nadhani mnafahamu Waheshimiwa Wabunge jinsi mafuta yalivyo muhimu kwenye usalama na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu spika, leo yakikosekana mafuta watu wanaweza waka-*riot* kule barabarani na Serikali haiwezi kusema unajua hicho ni kiburi cha waagizaji mafuta, ni kweli lakini sasa mmewasimamia vipi? Kwa hiyo, mimi nataka Serikali hebu ijaribu kuonesha kama ipo ili watu warudishe imani kwa Serikali. *(Makofi)*

Sasa kuna jambo lingine, bei ya mafuta inafikiwa vipi hasa, inakuwaje mpaka ile bei elekezi inatangazwa imepatikanaje kwa sababu inaelekea hapo ndio chanzo. Maana hizi bei za mafuta zimekuwa zinatangazwa kutoka mwezi wa kwanza mwaka 2009 kwa nini sasa hivi imekuwa tatizo? Sasa wenzetu wa Serikali watueleze kama kumekuwa na tatizo la ukokotoaji leo kuliko ilivyokuwa mwezi uliopita basi tuambiwe tatizo liko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Niabu Spika, lakini sisi tungependa kuona hali ya mafuta inarudi kama ilivyokuwa kama siyo leo jioni, kesho asubuhi. Tuiokoe nchi yetu kwenye janga kubwa ambalo linaweza kupatikana kama umeme utakuwa haupatikani. Kwa sababu hata mawasiliano nadhani mnafahamu kwamba mitambo ya *towers,* mitambo ya kurusha simu, mawasiliano mengi yanatumia jenereta, jenereta zinaendeshwa na mafuta.

Sasa kama *delivers* za mafuta hazifika mikoani ambapo mitambo hii mingi ipo vijijini tutashindwa hata kufanya mawasiliano ya simu jambo ambalo tumeliona ni kawaida. Kwa hiyo, tunaposema nchi itasisima ni kweli itasimama na watu watatuchukua sote sisi hawatawachukua tu waagizaji mafuta hata sisi tuliomo humu tutachukiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Chama cha Mapinduzi tumeunda Serikali ili isimamie haya mambo. Jinsi ilivyokuwa *handled* kwenye jambo hili sivyo ambavyo wanachama cha Chama cha Mapinduzi wanategemea na sivyo ambavyo wananchi kwa ujumla wanategemea.

Kwa hiyo, kwa kumalizia naomba niwasihi tena wenzetu Serikalini onyesheni mpo, onyesheni mnajali. Mheshimiwa Waziri sema kitu, Mheshimiwa Waziri Mkuu sema kitu kwa sababu *EWURA* ipo, lakini Serikali ipo na hili jambo linawahusu. Haiwezekani siku saba nzima hatujasikia Waziri Mkuu amesema kitu, hatujasikia Waziri amesema kitu, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo limekera sana naomba nikae nisiseme maneno mabaya lakini kwa kweli tunaomba muoneshe kwamba mpo na mnafanyakazi na mnajali maisha ya Watanzania kwa sababu chama chetu ndiyo kilichotutuma tuje tufanye hapa mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nakuomba utoe hoja na kama hoja yako inaungwa mkono ili niweze kuona kama kweli…*(Makofi)*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Naomba kutoa hoja rasmi kwamba jambo hili lijadiliwe kama dharura. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Sasa nimepata waombaji kadhaa kwa maandishi. Naomba wale ambao mngependa kuchangia msimame mahali penu ili niweze kuchukua majina yenu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Muda wetu ni mdogo kweli mtapata nafasi wachache sana. Lakini tujitahidi kuutumia kama nilivyosema dakika sizizozidi tano. Mheshimiwa Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kawaida tumezoea kuona wafanyakazi wakigoma kudai maslahi yao pale ambapo wanapoona maslahi yao hayatekelezwi na waajiri. Wanaita *industrial action.* Hatujawahi kuona kwa muda mrefu wafanyabiashara wakifanya *industrial action* na tulipoamua ku-*liberalize* kufungua uchumi wetu kuwa uchumi wa soko tulitoa haki kwa wafanyabiashara kufanya kazi kwa mujibu wa soko. Lakini kamwe hatukuondoa uwajibikaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado *responsibility* ya Serikali kulinda raia wake ilibakia ni jukumu la Serikali. Wafanyabiashara kwa kutumia *cartel* yao wameamua kukiuka maagizo ya chombo cha Serikali. Hatupaswi kuwa na maneno matamu ya aina yoyote dhidi yao. Ni lazima ionekane kuna Serikali, ni lazima ionekane kuna dola na ni lazima ionekane kuna uwajibikaji ambao vyombo vya Serikali inafanya kulinda raia. Sheria ya *EWURA* imetoa nafasi, imetoa hadhi ya *EWURA* kulinda walaji na imesisitiza kulinda walaji wa hali ya chini. Kifungu cha 6(B) cha Sheria ya *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wananchi wetu Dar es Salaam na miji mingine ya nchi wanahangaika. Hawawezi kwenda makazini kwenda kufanya kazi za kuzalisha mali. Wakienda kwenye daladala hivi sasa nasikia daladala zimepandisha bei. Kule Kigoma leo ni siku ya nne hakuna umeme kwa sababu hakuna mafuta. Wafanyabiashara wa mafuta wanai-*hold* nchi, hatuwezi kukubali. Kama nilivyosema *in a democracy* wafanyabiashara wana haki zao kama wafanyabiashara, lakini Serikali ina majukumu yake na wajibu wake kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba na napenda nilishawishi Bunge, kwamba *EWURA* leo watoe *order,* wafanyabiashara wote wa mafuta wa-*release* mafuta. Atakayepinga anyang'anywe leseni mara moja. Natoa ujumbe kwa wananchi wetu, inawezekana maamuzi haya yakawaletea shida. Haitakuwa mara ya kwanza wananchi wetu kupata shida. Tulikwenda vitani kupigana na Nduli Iddi Amini, hatukuwa na uwezo, hatukuwa na vifaa kama alivyokuwa navyo yeye, hatukuwa na wakubwa wanaotuunga mkono kama alivyokuwa anaungwa mkono yeye. Wafanyabiashara binafsi walitoa magari yao. Wanajeshi na mgambo walikuwa *mobilized* tukaenda vitani, tukampiga Nduli tukamtoa na tukamtoa Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi watapata shida lakini ni lazima tutoe fursa ya kufanya *enforcement* ya Sheria zetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wafanyabiashara wa mafuta wana maneno matamu sana, watakwambia kuhusu *profit margins* zao lakini waulizeni wakati tumeamua bei ya mafuta ya taa ipande *the next day* walipandisha bei. Hawakutueleza masuala ya *profit margins* zao, hawawezi kutueleza sasa masuala ya *profit margins. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria imeshatoka, *EWURA* wana kazi ya ku-*enforce* na sijasikia kama wafanyabiashara wamefuta wamekata rufaa, sijasikia kama Tume ya Ushindani imekaa kuangalia rufaa ya wafanyabiashara ambao wamefutwa. Wanataka kutuonyesha ubabe wao, wanataka kutumia jeuri yao ya fedha. Watanzania siku zote ni maskini jeuri. Leo mafuta yatoke. *EWURA* watoe *oder,* mafuta yatoke. Ikifika saa 12 jioni wafanyabiashara wamegoma wanyang'anywe leseni mara moja. Jeshi la Wananchi liingie, wafungue vituo, wafungue ma-*godown* mafuta yatoke watu wetu wapate mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wachumi wa Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha, wakae waangalie hilo suala la *profit margin* la wafanyabiashara wakati raia wanapata mafuta. Hatuwezi kukaa hapa tunajadiliana mambo ya nchi huku kuna watu wachache wamekaa, wanaamua kutokana na maslahi yao ya kibiashara. Hatuwezi kukubali hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba nichangie hayo na naomba Bunge lako Tukufu likubaliane nami *EWURA* wafanye kazi hiyo na tuwape nguvu *EWURA*, vijana wetu wanapokuwa kazini tusiwakatishe tamaa. Tusiwaone *EWURA* ni wakosaji wakati wanatekeleza maagizo ya Bunge. Ni sawasawa na askari wako yuko jeshini, kuna matatizo, unaanza kumlaumu. Tuwalaumu baadaye, tuwape nguvu *EWURA* wafanye *enforcement,* mafuta yapatikane ili wananchi wetu wafanye kazi kama jinsi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto, Kiongozi wa Upinzani CHADEMA. Sasa tusikie *CUF*. Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya *CUF*, Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nizungumze machache kuhusu kadhia hii ya mafuta. Kwanza, nielekeze mchango wangu kwa wafanyabiashara wa mafuta. Lakini pamoja na Serikali. Nasema hivyo kwa sababu kubwa sana ya msingi, kwamba inawezekana Serikali ina matatizo, ina makosa waliofanya, lakini makosa hayo yanatokana na humu humu Bungeni, Bunge lako Tukufu kushindwa kuisimamia Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge la Tisa iliweza kupendekeza kwa Serikali mara nyingi sana kuhusu suala la *TPDC* kupitia kampuni tanzu ya *COPEX* kuanzisha biashara ya mafuta. Kamati ya Nishati ya Bunge la Tisa ikazungumzia pia *Bulk Procurement* pia *Strategic Reserve.* Bunge lako Tukufu kwa bahati mbaya na hii ni moja katika kasoro kubwa ambayo kuanzia mwaka huu ningeomba irekebishwe. Katika Kamati zote zilizopo za sekta hakuna Kamati ambayo inafuatilia maazimio ya Bunge ili Serikali kusimamiwa kwa zile ahadi au maazimio tuliyoyapitisha hapa Bungeni kufuatiliwa barabara na kusimamiwa vilivyo, hatuna Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa tunayo Kamati hiyo isingefika *stage* hii leo tukapata mhadhara huu wa wafanyabiashara wa mafuta wakaweza kutuadhiri wakaleta mgomo wa namna hii, ingekuwa *COPEX* ya *TPDC* inayo biashara ya mafuta, wangeuza mafuta. Tatizo la pili, tuweze kubaini kama Serikali kwamba kumbe maagizo yote ya *IMF* na *World Bank* siyo kwa manufaa ya nchi zetu. Serikali kujitoa *a hundred percent* katika biashara ilikuwa ni kosa hatuwezi kujitoa katika kila kitu kwa maana hiyo kama Serikali ina-*think tank* madhubuti, ifikirie na ijue kwamba hayo maagizo ya kufuata hao wakubwa *IMF* kwa mashauri wanayotupa siyo kwamba yote yako sahihi katika mfumo wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano halisi tumeuona hata wao Marekani walipopata matatizo ya kiuchumi ya mabenki yao, Serikali iliweza ku-*inject* fedha na wakaweza kuingilia kati. Kwa maana hiyo hili liwe fundisho na tutafute njia ya kujikwamua. Hiyo *EWURA* tumeshaipa meno na *EWURA* tunataka i-*act* mara moja iwe na meno. Lakini si hilo tu umefika wakati sasa kwamba ile Sheria ya Tume ya Maadili ifanye kazi yake. Kwa sababu pamoja na mambo mengine inasemekana kwamba ndani ya wafanyabiashara wa mafuta wakubwa wamo viongozi wa Serikali ndiyo wanaokwamisha masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata tatizo la reli vile vile Februari, 2007 hapa Bungeni. Bunge hili lilipendekeza katika yale maazimio ya *Richmond* kwamba mikataba mipya na mikataba mikubwa isipitishwe kabla haijapitiwa na Bunge na Serikali hii hii ikaweza kupitisha mkataba wa *RITES* wakati huo ulikuwa haujasainiwa na matokeo yake leo tunayaona. Kwa maana hiyo, tatizo la reli kuwa halishughulikiwi pia kunasemekana kwamba pana wafanyabiashara wakubwa wenye ma-*truck* ambao hawataki reli ifufuke. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ile Tume ya Maadili sasa iko haja ya kuchunguza, kupitia Tume ya Maadili, viongozi wanaojihusisha biashara kubwa na huku wana vyeo vikubwa Serikalini (Mawaziri).

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ni kengele ya pili?

**MHE. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA:** Aidha, katika biashara ya mafuta au katika biashara ya *transport*. Lakini ifike mahali *EWURA* ichukue hatua yake na Serikali iwe na *think tank*, siyo kwamba tujitoe katika biashara *totally.* Ahsante sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Naomba ku-*declare interest* ni mjasiriamali lakini sio wa mafuta. Wafanyabiashara wote wana lengo moja. Lengo la mfanyabiashara ni kutengeneza faida, mfanyabiashara atakayekwambia kwamba nia yangu ni kumfurahisha mlaji si kweli, mfanyabiashara yoyote duniani nia yake ni kutengeneza faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sifa ya mfanyabiashara duniani mfanyabiashara mzuri ni yule anayekubali kuchukua *risk*, mfanyabiashara akubali kwamba, wakati mwingine apate hasara. Kwa sababu katika sisi wafanyabiashara pamoja na mimi kuna wakati unapata faida kubwa sana. Kuna wakati unapata faida ya kati, kuna wakati unapata hasara. Sasa ni vema wafanyabiashara wa mafuta wakubali kwamba kuna wakati walipata faida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakubali kuwa wafanyabiashara wazuri ni wale ambao wanachukua *risk,* wana-t*ake risk* inapobidi. Mfanyabiashara mzalendo, chukua *risk* inapobidi na sikubali wala sina uhakika kwamba bei hii mpya tuliyoipitisha sasa hivi inawafanya wapate hasara, sina uhakika. Lakini ninawasihi wafanyabiashara wenzangu na mimi ni mfanyabiashara, tukubali kuchukua *risk.* Sasa hivi twende tukubali kwamba, katika nchi ni lazima Serikali isikilizwe *then you are taking risk*, unachukua *risk* sasa hivi, lakini kuna wakati ulibeba faida kubwa. Sasa naomba nimuunge mkono hoja Mheshimiwa Zitto Kabwe bila ya kuzunguka kwamba, leo hii ikifika jioni wafanyabiashara wakubali kwamba unapokuwa mfanyabiashara ukubali kwenda kwenye *risk taking*, chukueni *risk,* fungueni vituo vyote mafuta yauzwe na nchi itoke kwenye hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi upande wa Serikali, wafanyabiashara wasidhani wako juu ya Serikali wala wako juu ya Sheria. Warudi wakubali kwamba nchi ina Serikali. Walipokubali kuingia kwenye biashara sifa ya kwanza walioikubali ni *risk taking*. Hata nilipoingia kwenye biashara ya kuuza ninavyouza nilikubali *risk taking*. Kwa hiyo na wao wauze mafuta wakikubali kuna wakati wanachukua *risk* kwa nini wanakataa. Tulipopandisha bei ya mafuta ya taa walikubali mara moja asubuhi yake wakasimama pale. Sasa tunapoteremsha wakubali kama walivyokubali wakati ule tulipopandisha bei ya mafuta. *(Makofi)*

Naomba niunge mkono hoja kwamba *EWURA* leo ionyeshe meno yake. Serikali ionyeshe meno yake. Tupo hapa ndani kwa ajili ya wananchi na pamoja na hao wafanyabiashara ni wananchi wetu, lakini wafikirie mlaji wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama chini ya Kanuni ya 150 ambayo inahusu kutengua Kanuni pamoja na maelezo yake yote ya sehemu ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne. Sababu yangu ni kwamba kwa sababu jambo hili Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo linawagusa wananchi na ni jambo muhimu sana ambalo tunalijadili na kwamba wananchi wetu wanaumia. Sisi kama Wabunge nikiambatana na wote ambao wamesema, sidhani kama ni busara tukiachilia jambo hili tukaenda kula eti kwa sababu tunataka kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza tuendelee na mjadala mpaka tutakapomaliza wasemaji wote tulioomba kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Sijawaona. Ahsante sana, nitatoa mwongozo wangu baadaye. Tuendelee. Mheshimiwa Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote naomba nitangaze maslahi, mimi ni *Marketing and Trading Consultant* katika *field* ya mafuta. Niliwahi kuwaeleza kwamba nina uzoefu wa miaka 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, nilizungumza mlivyotoa taarifa *EWURA* kwamba kazi waliyokuwa wakiifanya ingeleta matatizo. Nikaenda kwa Waziri wa Nishati, nikamwambia kazi waliyokuwa wanaifanya ilikuwa inakwenda kutuweka katika matatizo. Ilikuwa siku kumi kabla ya Wizara ya Nishati na Madini kufanya kazi yake ya bajeti ambayo mliirudisha. Wakati tatizo lilipotokea *indicative price* Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati aliniita Dar es Salaam, saa tano usiku nikaondoka kwenda Dar es Salaam, tukakusanya nyaraka zote kuangalia tatizo liko wapi? Masikitiko yangu ya kwanza leo ni siku saba Serikali haijachukua hatua yoyote. *(Makofi)*

Tatizo liko hapo, siku saba tatizo limetokea *no action taken.* Mtu anakwambia maji ya sumu unachukua siku saba, watu wanachota, *no action taken,* tatizo hapo ndipo ninapoliona. Nakubaliana na yote. Waheshimiwa Wabunge mimi kama mtaalam tatizo si bei. Nimeshawaambia nimeshayapitia makabrasha haya na Waziri nimemwambia. Nilikuwa nawasiliana na Waziri wa Nishati saa nane usiku, tatizo liko kwenye Kanuni, Kanuni inayopanga bei, niliiona siku kumi kabla Waziri hajawasilisha na nikamwambia na akawaambia watu wa *EWURA.* Mimi ni *trader,* katika mamlaka ile hakuna mtu mwenye uwezo kama mimi! *I am a trader. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ndipo lilipotokea, kwa hiyo Serikali imepotoshwa. Nimemsikia kiongozi mmoja wa Serikali akizungumza, hawa watu wa mafuta walikuwa ni watu wa kukamatwa. Siku ambayo tumepandisha mafuta ya taa, niliwaambia watu wa *EWURA,* pima matenki yote tujue *stock* ni kiasi gani. Halafu baada ya kujua *stock,* tuweze kujua ile *windfall profit* wanayopata ni kiasi gani! Hatukupata mrejesho nyuma! Tumekuwa tukihangaika, kama mnavyosema, tatizo ni ile *feedback.* Kwa hiyo, hili suala linakwenda hovyo hovyo! Watu wamekwishaumia siku saba! Tumewaonesha hapa kuna kasoro, hawajachukua hatua! Hatujaambiwa *windfall profit* waliyopata kwenye *kerosene* ni kiasi gani? Hatujaambiwa! *Kerosene* ipo kwenye matenki, hatujaambiwa, kwa hiyo, tatizo liko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, pamoja na maamuzi ya Wabunge mliyopitisha, hizi pande zote mbili tuziite hapa, kusudi watuoneshe ni kipi kilichokwenda kando, kama Kampuni za mafuta zimekiuka, zitaifishwe asubuhi. Kama watendaji wamekosea, usiendelee kumbeba mtu ambaye amekosea, kitu kiko *obvious* au ataifishwe! Lakini na huyo mpe mbeleko umbebe basi, hatuwezi kushabikia kitu ambacho kitakuwa hakiko waz, Hatumbembelezi mtu, aje atukamue hapa kwenye nchi yetu. Kanuni ni ya mahesabu, aliyekiuka agizo la Serikali na kuidhalilisha, achukuliwe hatua. Awe ni mtendaji, awe ni mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tumefika hapa tulipo kwa sababu ya udhaifu na ulegelege wa Serikali, lakini sitaki kuzungumzia tulipofika, nataka kusema tunatokaje hapa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tumia ile *next*

*(Hapa Msemaji alihamia sehemu nyingine, kutokana na microphone yake kutoa sauti ya mwangwi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya sasa pamoja na kauli za Wabunge, Bunge letu lina pande mbili; upande mmoja ni Wabunge na upande wa pili ni Rais. Kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu, Ibara ya 34 na Ibara ya 35, Mamlaka makubwa zaidi ya Kisera, ya Kiutendaji, ya Kisheria, yako mikononi mwa Rais. Kwa hiyo, kwa ushauri wowote atakaouchukua, pamoja na kuiagiza *EWURA,* pamoja na kuagiza Wizara, lakini mimi binafsi natoa wito kwa Wabunge wenzangu kwamba, pamoja na yote Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, anapaswa kuingilia kati katika jambo hili kwa kutumia mamlaka yake ya Urais. Ibara ya 35, imempa mamlaka ya kutoa maagizo kwa maana ya *Decrees* na masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono moja kwa moja maoni yote yaliyotolewa na Naibu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu jambo hili, tusiiadhibu *EWURA.* Binafsi ninayo mawasiliano ya ndani ya Serikali, *EWURA* ilitekeleza wajibu wake. Katika hili, pamoja na Mamlaka ya Rais na kila kitu, kama jambo la dharura vilevile, *TAKUKURU* inapaswa kuingilia kati kuchukua hatua kwa upande wake. Nina ushahidi wa baadhi ya Maafisa wa Serikali kuhongwa katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme vilevile kwamba, tunamiliki 50% ya hisa kwenye *BP* na leo *BP* nayo inaweka kiburi cha kuuza mafuta! Sisi tuna hisa 50%, Serikali yetu iko wapi? Kwa kampuni ambayo tunaimiliki! Inakataa kuuza mafuta kwa wananchi wake, Serikali yetu iko wapi? Tunamiliki 50% ya *TIPER,* hifadhi ya mafuta pale Kigamboni, tunaambiwa mafuta hakuna! Serikali yetu iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ushauri vilevile kwa mamlaka zote za Kiserikali zinazosimamia *TIPER,* zinazosimamia *BP,* kuingilia kati vilevile kama jambo la dharura. Kama wafanyabiashara ikifika muda ambao Naibu Kiongozi ameueleza hapa, hawajatekeleza agizo, pamoja na kuwachukulia hatua tunahitaji vilevile kuendelea kuwahudumia wananchi, tuna *BP* tuna *TIPER,* pamoja na kuwa hatuna *strategic reserve,* tunaweza tukashikilia hata mafuta yaliyoko *on transit* hivi sasa kwa sababu, ni hali ya dharura; tuna uwezo kabisa wa kufanya wananchi wakaendelea kupata mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niseme tu kwamba, tunapigania hapa, tunazungumzia tu tozo. Ubishani wote huu ni tozo ambayo ni 5% mpaka 10% tu ya bei. Hata tukiwa na ufanisi wa namna gani, kama hatutarudi kwenye hoja ya msingi kama Taifa, ya kupunguza kodi kwenye mafuta, bado hata tukishikilia msumari kwenye hii tozo maana ni 5% tu ya bei! Bado hatutachangia kwa kiwango kikubwa kwenye kupunguza gharama kwa wananchi; tutatatua tu dharura ya mafuta, lakini hatutapunguza gharama. Natarajia Serikali, majibu watakayoleta jioni ni pamoja na kutoa ahadi, kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, inayorudishwa Jumamosi tarehe 13, Serikali ikubali mapendekezo tuliyoyatoa kwenye hotuba ya Kambi, ya kufanya

marekebisho ya Sheria ya Fedha ili kwenda kushughulikia lengo la msingi bila kuleta mzozo, fujo na mambo mengine katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba niseme kwamba, nimefanya kazi na nafanya kazi ya biashara ya mafuta na nina kituo cha mafuta. Kwa hiyo, nina-*declare interest.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa uagizaji wa mafuta ndio unatuletea tabu hapa. Kwanza, hao wenye vituo vya mafuta wanaoambiwa wanagoma, utaratibu ule *channel of distribution,* inawezekana kabisa hao wenye vituo hawana mafuta na hawatayapata mafuta. Kwa sababu, kuwa na kituo sio unamiliki kampuni ya mafuta, wewe ni msambazaji wa mwisho katika ile *channel of distribution.* Kwa hiyo, inawezekana nikawa na kituo Muheza, nanunua mafuta yangu kutoka kwenye kampuni ya *GAPCO, GAPCO* amefunga! Mimi Muheza, nitakwenda kununua wapi mafuta? Nina kituo lakini hakitakuwa na mafuta. Kwa hiyo, ni lazima tuiangalie ile *channel of distribution,* badala ya kudhani wenye vituo ndio wakorofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo mnaviona vina nembo, vimeandikwa *BP,* vimeandikwa *GAPCO,* vimeandikwa *TOTAL,* sio vyote mali ya makampuni ya mafuta! Hivyo wamejenga watu binafsi wenyewe lakini wakaweka nembo ya *TOTAL,* wakaweka lebo ya *BP* na kwa hivyo hawezi kuuza mafuta mpaka aende kwenye *depot* ya *BP* akachukue mafuta alete kwenye kituo chake. Hilo tukishalielewa tutajua wapi penye matatizo. Ambalo wenzetu wameanza kulizungumza ni kweli tuna 50% ya umiliki wa kampuni ya *BP.* Ni lazima twende *BP* tukaangalie, hivi kweli *BP* amekataa kujaza mafuta kupeleka kwenye vituo vya *BP* vilivyopo? Hilo ndilo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli amefanya hivyo, lawama haziwezi kumwendea mwenye kituo cha mafuta! Lawama ni lazima zimwendee mwenye *depot;* lazima mwenye *depot* ndio ahukumiwe. Hili lazima tuliangalie sana na kwa makini. Nimeagiza mafuta katika nchi hii kwa zaidi ya miaka 12 hadi 15 iliyopita! Naujua mfumo mzima wa kuagiza mafuta kutoka kwa *suppliers* mpaka yanapofika kwenye *depot.* Kwa hiyo, ndugu zangu hapa tuangalie; ile *profit margin* ina mgawanyo wake vilevile. Yule *supplier* ana-*profit margin* yake, lakini na huyu anayeagiza pia ana-*profit margin,* huyu mwenye kampuni *depot* ana-*profit margin* lakini huyu mwenye kituo cha mwisho pia ana *profit margin* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimkandamiza mwenye kituo cha mwisho kwamba, yeye ndiye anayeuza kwa dakika za mwisho, halafu *profit margin* yake yeye ndio unayoikaba katika *pricing system!* Hata huyu mwenye kituo atajiondoa, hatafanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa mchango mdogo ambao nimeweza kuutoa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewekwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Sehemu ya 8, inasema wazi kwamba: “Serikali inawekwa na wananchi”. Kama Serikali imewekwa na wananchi inapaswa Serikali hii kuelewa matatizo ya wananchi na kusimama imara katika kuwasaidia wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni hapa tatizo liko wapi! Siwezi kuliona tatizo liko wapi hata kidogo! Kwa sababu, huu ni mfumo wa biashara wa kisheria na ni mfumo wa kibiashara wa kisheria unaosimamiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ndani ya Nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako lilifanya maamuzi ili kuwasaidia wananchi Watanzania waepukane na tatizo la ugumu wa maisha, ndio maana tukapitisha maamuzi humu na naweza kusema ilikuwa ni maamuzi mazito ya kuangalia ni namna gani nauli zitashuka ili Watanzania waweze kusafiri kwa kutumia nauli ambazo ziko ndani ya uwezo wao. Lakini tukasema kwamba, viwanda vinatumia mafuta, uzalishaji wa bidhaa uweze kushuka na wananchi wa Tanzania waweze kupata bidhaa zao kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wafanyabiashara wanapogoma ku-*supply* mafuta katika nchi yetu na Serikali isipochukua maamuzi sahihi ya kusimama imara! Hakika Serikali yetu haitakuwa na heshima katika nchi yetu. Naomba kabisa hilo lieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali yanaweza kuwa yako matatizo ya kiutekelezaji katika kufikia hatima hii ambayo leo imetufanya tujadili kama suala la dharura! Lakini Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba hapa leo tusijadili hayo ambayo ni wajibu wa Serikali huko ndani! Tujadili umuhimu wa Serikali kusimama kwenye maamuzi na wananchi wapate nafuu ya maisha kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano ambao mmenipatia mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata Mwongozo wa Mheshimiwa Simbachawene, ni Mwongozo mzuri, lakini nashauri Bunge likubaliane na mimi, tuendane na ile Kanuni ya 47 (4) ya kuniachi kuendesha mambo haya kadri ninavyoona inafaa, kama nilivyopewa mamlaka na Kanuni hii. Kwa hiyo, kwa ushauri wangu sasa ni muda wa kusitisha shughuli za Bunge, hadi saa 10.00 kamili jioni, tutakapoendelea na jambo hili na mambo mengine yataendelea baada ya hapo.

Niwakumbushe tu CHADEMA saa 09.00 wanakutana Ukumbi Namba 219 na CCM tukitoka hapa, moja kwa moja tunakwenda katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, basi nasitisha shughuli za Bunge, hadi saa 10.00 kamili jioni hii.

*(Saa 7.15 mchana, Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni.)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea kuhusiana na ile hoja yetu ya dharura iliyotolewa asubuhi na Mheshimiwa Makamba. Sasa tunaendelea na utaratibu wetu ule ule wa dakika tano, tano. Naomba nianze na Mheshimiwa Lekule Laizer.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie suala hili la dharura ambalo ni la dharura kweli kweli. Namshukuru Mheshimiwa Makamba, kulileta jambo hili hapa Bungeni ili tulijadili na tuangalie kama tutapata muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosa mafuta katika nchi hii au nchi yeyote ni kama vita, hata vita ikitokea wakati wowote, huwezi kwenda vitani kwa sababu unatumia mafuta, kila jambo linatumia mafuta. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue jukumu hili haraka sana iwezekanavyo. Kwa sababu ukiangalia jambo hili limetokea muda wa wiki nzima, Serikali ilikuwepo na imenyamaza kimya. Sasa narejea usemi wa Rais aliyesema wakati mmoja kwamba, inapasa kutenganisha kofia ya biashara na uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linawezekana likawa na wafanyabiashara na viongozi, siwezi kusema wapo hapa lakini inawezekana ni viongozi na huwezi kabisa ukachukua jukumu ambalo una maslahi nalo. Kuna mambo ambayo yanasikitisha kidogo, niliwahi kusikia kwa mara ya kwanza tangu niwe mtu mzima, Mhindi mmoja kuipa Serikali masaa 24, sijawahi kusikia, pale pale bado Serikali haijajibu, wamepewa masaa 24 na mtu. Nadhani ni mtu binafsi tu ndiyo anapewa masaa 24, lakini sijawahi kusikia dharau kubwa kama hiyo ya Serikali kupewa masaa 24 halafu wakanyamaza kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kuona Serikali ambao ni waoga wa aina hii, kupewa masaa 24 na mtu ambaye ni Mhindi, ukanyamaza kimya, yeye ndiyo mtawala. Kwa hiyo, wakati mwingine viongozi wawe na ujasiri, huwezi kuongoza nchi kama wewe siyo jasiri, utakanyangwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili haliwezi kufanya kazi ya Serikali, sisi tumechaguliwa na wananchi, wananchi ambao wanateseka sasa, Rais amechaguliwa na wananchi ambao wanateseka sasa kwa ajili ya baadhi ya watu. Kama kuna mtu ambaye ana maslahi na yuko Serikalini, huyo awe wa kwanza kujiuzulu na Serikali isifumbie macho jambo hili, kama ni mtu yeyote kwa kweli Serikali ichukue hatua haraka sana iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mmenisikia lakini Serikali ichukue hatua haraka sana hasa kwa hawa wafanyabiashara. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kimsingi nakubaliana na hoja iliyotolewa kuwa kunahitajika maamuzi ya dharura. Katika hali ya kawaida, binadamu wanatakiwa kurudisha wema wanaofanyiwa. Sote tunakumbuka hapa ulipotokea mtikisiko wa uchumi Rais, ambaye ndiye kiongozi wa Serikali ambayo inalaumiwa sasa hivi, alitoa mamilioni ya pesa kwa ajili ya kitu kilichoitwa *stimulus package,* madhumuni yake ilikuwa ni kuwasaidia watu waliopata matatizo. Sasa inapofikia mahali ama wao mara moja kwa moja, au waliohusiana nao nchi inafika katika wakati mgumu kama huu wanatokea watu kama alivyosema kaka yangu pale Mheshimiwa Lekule Laizer, wanaambiwa punguzeni au tumieni bei mpya wanaipa Serikali masaa 24, *this a kind of the subordination to Government* na haiwezekani hata siku moja Serikali ikawa laini kiasi hicho. Kama hilo ni kweli basi hiyo ni aibu kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko vitu vinavyoweza kustahmilika, lakini huwezi kustahmili shida ya watu wengi kwa manufaa ya watu wachache, hata siku moja. Naamini Serikali inaelewa mfanyabiashara mmoja, mmoja inaelewa kampuni moja, moja kiwango cha mafuta waliyoleta kuanzia kabla ya bajeti mpaka ilivyopitishwa bajeti. Kama Serikali haijui hivyo mpaka leo Mwezi Agosti, 2011 haijaweza kuchunguza ikajua idadi ya mafuta yaliyopo ni jambo la kusikitisha sana. Kwa sababu mie ni miongoni mwa watu waliopata fursa ya kutembelea pale bandarini, inaonesha wanajua kila kinachoingia wale watu wa bandarini. Sasa mfanyabiashara anapokwambia hawezi kuuza kwa sababu ana mafuta mengi aliyoyanunua kwa bei kubwa. Kwa nini mafuta mengi hayawi wakati inapopandishwa bei, hasemi kuwa mie nilikuwa sina mafuta nasubiri mafuta mapya niuze, anapandisha bei *immediately* kwa sababu anajua jambo lile lina maslahi. Lakini kwa sababu hili linaangusha huu Mfuko wake wanaamua kuwatesa wananchi pasipo sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali kwa hili, tutasema Wabunge mpaka jioni kama Serikali haikufanya maamuzi ya kijasiri, bora ilaumiwe kwa hili lakini iweze kuwaokoa wananchi wenye shida. Ni kawaida uhuru unapotolewa watu wengine wanautumia vibaya mpaka tunakufuru na tunaona mambo mbalimbali hapa, vyombo vya habari na magazeti mara nyingine kwa sababu ya uhuru tu wanakufuru, wanaandika vitu vya ajabu, ajabu, wafanyabiashara ndiyo hawa wanapata fursa kama hii wanaitumia vibaya, basi wao hawafikiri kuwa nchi yetu ina tatizo, wanahitaji angalau kutoa mchango wao katika hili wanaangalia kunenepesha mifuko yao tu, hii ni aibu, na mie nasema hii ni *challenge* ya mwanzo ya Serikali hii ya Awamu ya Nne, tokea tumeanza 2006, ni *challenge* ya kwanza. Kama wakiyumba kwa hili wakawaruhusu watu wachache wakachezea mamlaka ya dola kiasi hicho, maana yake ni kuwa wengine watatakiwa wafanye zaidi ya hivyo, watu wanajifunza kulinga na wenzao, ukimuachia mtoto leo akakuvuta sikio, kesho atachukua kisu akuchome tumboni na ndiyo utakapojua kuwa mtoto wako ulikuwa unampenda alipokuvuta sikio ukamwachia au ulikuwa unamuumiza na mwisho anakuumiza wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, yuko mwandishi mmoja maarufu wa Nigeria bwana Chinua Achebe, yeye alisema katika kitabu chake kimoja, anasema *the Fox must be faced away, then the hen might be warned against wandering in the bush. A Kings' men in trouble should be saved and not blamed,* wananchi wana shida sasa hivi wasaidiwe, haya masuala ya kuwa sijui wafanyabiashara watapata hasara, sijui hivi, sijui hivi lugha hii haiwezi kueleweka. Na wananchi tunaitazama Serikali itafanyaje katika muda huu mchache uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, kwa hakika hali ilivyo huko nje na wananchi kwa ujumla hali ni mbaya sana, ni kama vile Taifa lina tishio la usalama wa nchi. Sasa tunapokutana na jambo kama hili ni lazima tuoneshe siyo tu uzalendo wetu lakini pia ukakamavu katika kuonesha uzalendo huo. Dhana ya ushirikiano wa kuendesha uchumi ya *PPP*, kwa maana ya *Public Private Partnership* inaingia doa na hawa wafanyabiashara wa mafuta ndiyo wa kwanza kuonyesha doa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa Taifa lolote sasa duniani ni nishati na kama mtu anacheza katika eneo la nishati amekugusa amekushika pabaya. Usalama wa nchi haulindwi tu kwa kununua madege ya kivita, kununua bunduki, ni kumiliki nishati. Jambo hili ni fundisho tosha, hatuhitaji tena mwalimu mwingine juu ya jambo hili, nadhani sasa ule uamuzi wetu wa kuirudisha *TPDC*, ulikuwa ni wa busara, ni vizuri ukachukua sura ya haraka sana kuanzia sasa tunapofundishwa na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hawa wafanyabiashara wa mafuta wamevunja sheria, sheria ya ushindani wa kibiashara kwa sababu tunapata taarifa kwamba wanawatishia hata wenye nia ya kutaka kutoa huduma hiyo. Wamefunga magodauni yao ya mafuta, hawataki yule anayetaka kujitolea kuendelea kufanya biashara kwa kukubali na kutii agizo la *EWURA,* wanataka kumshughulikia, huku ni kukiuka sheria iliyopo inayo *control* masuala ya ushindani wa kibiashara katika soko huria. Kwa hiyo, kabla ya yote haya tunayosema na waliyosema wenzangu juu ya nini kifanyike, ningeshauri tuanze mkakati wa kuwafungulia mashtaka watu hawa, maana hili halizuii ni suala la kuwepo kwa ushahidi tu, *EWURA* watapaswa kufuata sheria kwa sababu ni taasisi ya Serikali na sheria ndiyo inasema kwamba baada ya kuwapatia ile notisi ya wao kufuata kutekeleza jambo walililoliagizwa watapaswa kusubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati tunaposubiri, wananchi wanaumia, maumivu haya ni lazima tuwashtaki hawa watu, wamekiuka sheria, si watu wema, wametishia usalama wa nchi na kwa hiyo, tunapaswa Serikali kuonesha ujasiri na ukakamavu katika jambo hili. Niwaombe tu Watanzania katika kipindi hiki, pengine tutapata shida sana kwa sababu sekta hii ya binafsi ndiyo inayoingiza mafuta kwa kiasi chote karibu tunachokitumia, tuwe wavumilivu lakini tuoneshe uzalendo wa nchi yetu hata kukubali kuteseka kwa ajili ya kuonesha uzalendo na heshima ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, nakushukuru, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na jambo hili na kwa ujumla Serikali nzima msiogope katika jambo hili, chukueni hatua zozote tupo tayari kwa jambo lolote. Tukizembea katika jambo hili, tutafuata mambo ya sukari, wata-*curtail*, watakuja na masuala ya *cement* wata-*curtail*, tutaingia kwenye matatizo makubwa, tuonyeshe mfano katika jambo hili ili sekta ya binafsi ijue inapaswa kuheshimu sekta ya umma maana hizo ni fursa tunazotoa kwao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nioneshe kwa kweli masikitiko yangu ya dhati ya moyo kwa jinsi nchi hii inavyotaka kuyumbishwa na kundi la watu wachache wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu kama tumesahau nchi yetu mwishoni mwa miaka ya 70 na mwanzoni mwa miaka ya 80 ambapo wafanyabiashara walitaka kuitia nchi ya kwetu katika matatizo makubwa wakati ule Marehemu Hayati Moringe Sokoine akawa jemadari wa kuhakikisha kwamba heshima ya nchi inarejeshwa kutoka kwa wafanyabiashara waliokuwa wamehodhi bidhaa muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tukumbuke, kwamba tukiruhusu wafanyabiashara hawa wakajiunga wanaweza kutengeneza nguvu ambayo itaiyumbisha nchi hii, tusifike huko, lazima Serikali ichukue hatamu. Ilifikia wakati wafanyabiashara wanasema Serikali wameiweka mfukoni. Hivi ndiyo kuiweka mfukoni, wiki nzima Watanzania wanahangaika wanatembea kwa mguu kwenda kazini, magari yamesimama kwa sababu ya watu wachache

waliopewa dhamana ya kuleta bidhaa hii muhimu katika nchi yetu. Naomba Serikali ichukue uamuzi wa haraka na nafikiri wakati huu sasa tunapojadili hili suala, vyombo vya dola vingekuwa kwenye visima, vyombo vya dola sasa hivi vingekuwa kwenye maghala ya bidhaa hii, vyombo vya dola sasa hivi vingekuwa vinawafuatilia hawa wote waagizaji na wasafirishaji wa mafuta, mawasiliano yao yote, kuhakikisha kwamba hii njama yao haiendelei zaidi. Vyombo vifike huko sasa hivi, viwe kazini, kwa sababu tukisubiri wao sasa hivi wanaanza kufanya mawasiliano hata na *suppliers* wa nje ili sasa bidhaa hii iweze kuadimika katika nchi yetu, kwa sababu tu eti wameingiliwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishaji katika biashara katika maamuzi haina maana ya kudharau Serikali. Sasa naomba sana Serikali ichukue uamuzi madhubuti na wa haraka, sasa hivi hatua zianze kuchukuliwa kuwafuatilia. Hatuwezi tukaruhusu watu wachache na bahati mbaya nafikiri tulivyoingia kama nchi katika soko huria la biashara, tuliachia milango mipana hata bidhaa muhimu ambazo ni za usalama wa Taifa. Inatakiwa Serikali iwe nazo mamlaka. Hata wakati tunachangia kwenye Muswada wa Madawa, nilizungumza sana nilihofia sana sekta ya madawa, ikiwa huru sana ni hatari kwa sababu huo ni usalama, madawa yataingizwa ya ajabu ajabu na siyo watu wanaugua wanapunguza maisha kwa sababu ya huria hii, na hii huria ya mafuta sasa ndiyo inataka kutupeleka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ichukue hatua na vyombo vifanye kazi kwelikweli ili iwe fundisho kwa wafanyabiashara wengine tusiende kwenye sukari, tusiende kwenye bidhaa zingine muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni yanayofanya biashara ya mafuta katika nchi yetu, hayana haki ya kufanya biashara hiyo yana *privilege* tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi hii, si haki kufanya biashara ya mafuta, *is only a mere privilege,* ndiyo maana sheria iliyounda *EWURA*, inasema utafanya biashara ya mafuta ukipewa leseni tu. Kwa mujibu wa sheria za Tanzania hiyo *privilege* ya kufanya biashara ya mafuta unaweza kunyang'anywa wakati wowote uki-*abuse*. Ndiyo maana sheria hiyo imesema moja ya mamlaka iliyonayo *EWURA*, ni pamoja na kunyang'anya leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kama ukinyang'anywa leseni baada ya kui-*abuse* na hujaridhika na kunyang'anywa hiyo *privilege* ya kufanya biashara ya mafuta kukata rufaa kwenye *Fair Competition Tribunal* na hakuna kampuni ya mafuta hata moja ambayo imekata rufaa mpaka sasa hivi, juu ya maamuzi ya *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria za Tanzania *EWURA* ina mamlaka ya kutoa amri inaitwa *complies order*, amri ya kuyataka haya makampuni kuuza mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa mujibu wa sheria za nchi hii, *EWURA* ina wajibu wa kuhakikisha kwamba mafuta yapo na yanauzwa kwa watumiaji. Sasa Taifa letu limekuwa *held to ransom*. Makampuni ya mafuta yametuwekea bastola kichwani, yanasema tufanye tunavyotaka au vinginevyo tunavuta ile kitu inaitwa *trigger*, tunawalipua. Taifa huru linapaswa kuwaambia hamna haki ya kufanya biashara, *you are only enjoy your privilege* na Taifa huru hili lina mamlaka kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuchukua hatua za haraka na za dharura kuyanyang'anya makampuni haya, hiyo *privilege* na Serikali ikifanya hivyo itakuwa haivunji haki za kibinadamu kwa mujibu wa Ibara ya 30(2)(a), (c) na (f) kwa sababu makampuni yanataka kuathiri uchumi wetu, yanataka kuathiri ustawi wa jamii yetu na yanataka ku-*undermine* uchumi wa Taifa. Tuna wajibu, Mamlaka na uwezo kisheria wa kuwanyang'anya hiyo *privilege* kama hayawezi kufuata utaratibu wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, Serikali isipepese macho, *the Government should not blink*, mchukue hatua zote katika *arsenal* yake na zinatosha kabisa, tusichezewe, inaweza kuwa walituchangia wakati wa kampeni lakini huu si wakati wa kupepesa macho kwa sababu tukiruhusu tukapepesa macho Taifa letu litaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na nataka kuchangia kidogo katika suala hili.

Nianze kwa kuwapa pole sana wananchi ambao kwa sasa hivi wanahangaika na adha hii ya mafuta. Lakini vilevile niseme kwamba Serikali yetu imechelewa sana kufanya maamuzi. Ni vema basi, kunapotokea jambo kubwa la Kitaifa kama hili, Serikali iwe nyepesi kuchukua hatua mapema iwezekanavyo. Kwanza, nilipongeze sana Bunge kwa kuliona hili na kuja kuleta mjadala kama huu mchana wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inatakiwa iwe imara, thabiti na iwe jasiri katika suala hili. Huu umoja wa wauza mafuta umeonesha jeuri kubwa sana kwa Serikali yetu, wameonyesha jeuri ya fedha, ubabe, tamaa na vilevile wanataka kuonesha kwamba wako juu ya Serikali, hili halikubaliki hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wasemaji wote waliopita na waliosema kwamba Serikali sasa inabidi ichukue hatua, ikiwezekana ndani ya saa 24 wananchi ambao wanapata adha hii waweze kupata haya mafuta. Ikiwezekana wale ambao watakaidi amri hii leseni zao zifutwe na wale ambao wanasema hawana mafuta, tukakague matanki yao na mafuta tutakayoyakuta yawe ni mali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha mpito Serikali iamue na kujipanga ili tuwe na kampuni yetu sisi wenyewe ya mafuta na tuiwezeshe ili iweze kufanya shughuli hii ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile katika suala la soko huria hatuwezi kuruhusu biashara ya masuala ya muhimu kama mafuta na vyakula tukaacha yakawa yanakwenda kihivyohivyo tu. Kuna umuhimu sasa Serikali ikajipanga kuwa na udhibiti mzuri wa bidhaa muhimu na nyeti kwa usalama wa Taifa letu. Lililotokea leo halikubaliki, halivumiliki na ni wakati muafaka sasa Serikali ikachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia hapo. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na kuipongeza Serikali kuruhusu jambo hili lijadiliwe kwenye Bunge hili Tukufu, nashukuru kwa mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru jambo hili limepata nafasi ya kujadiliwa kwa niaba ya Watanzania na pia niwapongeze Wabunge wote kwa sababu hii inaonesha kwamba Wabunge wanawatetea sana wananchi na mimi naunga mkono kabisa maana hili jambo ni *serious*. Tukiwa kama wawakilishi wa wananchi tunasimama kinagaubaga kulitetea jambo hili kwamba siyo sawa wafanyabiashara wa nishati hii ya mafuta kutouza mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli jambo hili ni lazima tuwe makini na nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, hiki ni kinyume kabisa na utaratibu wa nchi na nasema kila nchi ni lazima iongozwe kwa Sheria. Lazima nchi iwe na utaratibu wake sasa, hawa watu ambao wanakwenda zaidi ya maelekezo ambayo yanatolewa na vyombo husika siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunashuhudia wanafunzi kusafiri na vibasi vimepandisha gharama, imekuwa ni kubwa sana, akina Mama kwenda hospitalini na watu wengine wanatakiwa kwenda hospitali za rufaa, imekuwa ni gharama kubwa sana na mzigo huu wote ni hata kwa wale wanaojitahidi kusafirisha bidhaa, yaani mwananchi ndiye analaliwa kwa sababu mwisho wa siku usafiri unapokuwa gharama, zile bidhaa zikifika madukani kwa mtumiaji wa mwisho bei inapandishwa. Nitumie nafasi hii kuwapongeza wale ambao wanafanya biashara hii ya mafuta hadi leo ambao wamesimama ngangari kukubali kwamba sisi tutauza mafuta.

Nimeshuhudia baadhi ya Taasisi kama *GBP, Engine, Oil Com* na wengine mwendelee kuruhusu kuuza mafuta. Nchi lazima iongozwe kwa utaratibu, hiyo nchi ambayo haieleweki utaratibu wake ukoje na niiombe sana Serikali katika hili isimame kabisa kidete kuhakikisha kwamba jambo hili linafikia muafaka na ni muafaka unaoeleweka.

Lakini pia tunajifunza kwamba kumbe huu utaratibu tunaousema hapa na kila siku tunaimba *Public Private Partnership* tushirikiane na wafanyabiashara na wadau binafsi kuendeleza nchi yetu. Sasa hawa wadau binafsi wanatufundisha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake tunajifunza kwamba kila eneo lazima Serikali tuwe na *shares*, maana yake Serikali ikiicha sekta binafsi sekta binafsi wakati mwingine inagoma na wananchi wetu wanaumia watu milioni 40 Watanzania leo....

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa namna ya pekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa January Makamba kwa kuleta hoja hii pamoja na Kamati yake na hii inaonesha kwamba bado Serikali ilikuwa imelala. Kama si Mheshimiwa January kuleta hoja hii wala tusingepata nafasi ya kuzungumzia suala hili. Lakini huko mtaani hali ni mbaya sana lakini Serikali mmekuwa kimya tu, hamna hatua mnayochukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtindo huu wauza mafuta hawa wataendelea kuiendesha Serikali yetu na wamekuwa wakisema siku zote kwamba Serikali imewekwa mfukoni na hii inaonekana. Wametusumbua kwenye uchakachuaji wa mafuta, tumepelekana nao mbio sana, wameyumbisha uchumi wa nchi yetu kwa sababu ya kuchakachua lakini na leo tena wanaiyumbisha nchi yetu kwa sababu ya kuuza mafuta. Mafuta wanayo yako kwenye maghala lakini wameyazuia hawataki kuyatoa kwa sababu bei imepunguzwa, laiti bei ingekuwa imepandishwa saa hiyo hiyo bei ingepanda lakini kwa sababu bei imeteremshwa kidogo wanakuwa wazito na Serikali imekaa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali kwa hili ambalo limetokea na kwa hali ambayo ipo mtaani hivi sasa tunataka kuona Serikali inachukua hatua haraka sana na tatizo hili mpaka ikifika kesho muda huu tunapozungumza liwe limeshakwisha, kinyume cha hayo na ninyi Mawaziri wala hamstahili kukaa huko ondokeni kwa sababu mnashindwa kufanya kazi, mnaidhalilisha Serikali yetu lakini pia mnadhalilisha na chama chetu kwa sababu hamfanyi kazi inavyotakiwa, mmekuwa mkifanya kazi kwa uogauoga, hamko *serious* na hata kuingia Bungeni hapa umeona wakati wachangiaji wa mwanzo wanaanza kuchangia kulikuwa na Mawaziri wawili yaani Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu Waziri wa Nishati na Madini lakini wote hawakuwepo na kila mmoja anaingia anavyotaka hapa. Hii inaonyesha ni jinsi gani hawapo *serious* na jambo hili. Tunaomba sana ifikapo kesho, tatizo la mafuta nchini kwetu liwe limekwisha ili wananchi wetu wapate huduma ya mafuta na waende kazini kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge Idd Azzan pamoja na kwamba ni Mbunge wangu Kinondoni lakini nawajibika kusimamia hapa kuwatetea Mawaziri kwa sababu asubuhi ya leo nilipewa jukumu la kukaimu shughuli za Serikali Bungeni na mimi mwenyewe nilikuwepo angalau hata angekumbuka jina langu basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapokuwa hapa Bungeni Mawaziri wanakuwa na majukumu mengine kwa ajili ya Bunge hilihili na wale wanaokuwa huku ndani wanasimama kwa niaba ya wale ambao wako nje. Naomba Waheshimiwa Wabunge waone kwamba sisi ni Wabunge wenzao na tunapokuwa nje hatuendi kwenye mambo mengine bali ya kuimarisha Bunge hili na kutekeleza majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru lakini kwa taarifa hii bila shaka Mheshimiwa Azzan atapokea taarifa yangu kama mimi nilivyomsikiliza yeye.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana tumepokea sote, Mheshimiwa Nassir atafuatiwa na Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nichukue fursa hii kwanza kuwapa pole Watanzania wote kwa ujumla wao. Kadhalika labda kwa kila mjumbe aliyechangia hapa ingekuwa ana-*declare interest.* Nimelelewa kwenye sekta ya mafuta, lakini nina uhakika na wenzangu wengi hapa kwa sababu ni watumiaji wa nishati hiyo basi, pia na wao wanapaswa ku-*declare interest.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika Taifa limeingia mahali pazito sana, tumeshuhudia kitendo ambacho sasa kinaitwa cha Makampuni ya Mafuta kuiweka nchi hii mahali pagumu, kitendo ambacho kiukweli kabisa kwa mazingira tuliyokuwa nayo ya Kimataifa au hata kwa utashi wa Taifa hakikubaliki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutumie fursa hii kuyaambia Makampuni ya Mafuta kwamba nchi hii ina utawala wa Sheria, nikubaliane kabisa na hoja za msingi zilizotolewa na ndugu yangu Zitto Kabwe na *ceiling* aliyokuja kuifanya ndugu yangu Tundu Lissu pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Kuna mahali hapa mambo hayakwenda sawa na labda niseme hivi kutokuwepo kwa *EWURA* ndani ya Wizara ya Nishati na Madini, inawezekana ikawa ndiyo sababu iliyopelekea viongozi wa kisiasa au Makada wetu tuliowaweka kwenye Wizara ya Nishati na Madini kuwa wakimya au kuifanya Serikali kwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini ikanyamaza kabisa au tuone basi kuna umuhimu wa kuigatua sasa *EWURA* iwe *answerable* kwa Wizara ya Nishati na Madini ili tusije tukafikia hapa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya sana, wananchi wa Korogwe Mjini leo wananunua petroli kwa shilingi 3,000/=, ina maana tumewarejeshea ulanguzi. Sasa tuseme ulanguzi huu umerejeshwa na Makampuni ya Mafuta au umerejeshwa na chombo kinachosimamia dhamana hii au umerejeshwa na Serikali kwa kukaa kimya pamoja na kupata taarifa hii kwa kiasi cha siku saba au siku kumi leo? Haya mambo hayakubaliki! Tufike mahali kama Bunge tutoke na kauli ya pamoja na tutoke na azimio la pamoja leo, kabla ya kuliahirisha Bunge kwamba, msimamo wa Serikali na maamuzi yaliyopo ni haya na niwasihi sana wafanyabiashara wa mafuta kwamba mnacheza na nyakati tunajua faida mnavyoipata na tunajua ni jinsi gani mnavyoji-*invoice* mara mbili ndani na nje kwa mzigo ule ule unaokuja nchini, tukiambiwa *BP Tanzania* ana *BP Afrika* kama *Sister Company*, ukiambiwa *Total Tanzania* ana *Total International* kama *Sister Company,* sijui makampuni kama *Oil Com* na kampuni nyingine ila mnao mfumo thabiti wa kubania *hedge funds* kwa kuji-*invale* mara mbili.

Pia tunajua *system* nzima ya kulinda maslahi yenu msicheze na chombo hiki, msicheze na Kamati hii na msicheze na Serikali, nendeni mkatekeleze wajibu wenu na sisi tuko kwa maslahi ya Taifa hili pamoja na kulinda nafasi yenu ninyi kama wafanyabiashara na kama wawekezaji. Mmepewa *margin* ipokeeni, angalieni na tutaliangalia suala hili la mafuta kwa mtazamo si wa kisiasa tu peke yake, tuliangalie kiuchumi na pia tuliangalie hata kimahesabu. Njooni na *template* yenu na *EWURA* waje na *template* yao na hatimaye tupate *consensus* ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na naunga mkono hoja hii ya dhamira mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Nishati na Madini kwa kuliona hili na kulileta hapa Bungeni ili tuweze kulijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni usaliti kwani wafanyabiashara wamelisaliti Taifa ambalo kwayo ndiyo linalowalinda wafanye biashara hii kwa amani kabisa. Kama kusingekuwepo na Serikali biashara yao ingekuwa ngumu na pengine wasingefanya hapa Tanzania. Hili lisichukuliwe kama ni jambo la mzaha mzaha tu bali lichukuliwe kama kuna usaliti katika nchi hii tayari tunaona dalili ndiyo hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ingetangazwa kwamba bei ya mafuta imepanda leo basi leo hii hii jioni tayari wangekuwa wameshapandisha bei ya mafuta, lakini kwa vile utaratibu mzuri umetumika tena kwa taratibu kabisa za kutangazwa Bungeni kuwa ndugu zetu wafanyabiashara hali ya maisha ya Watanzania inakuwa ngumu kwa sababu bei ya mafuta iko juu tumezungumza kwa muda mrefu na tumefikia hatua kuwa kwa kiwango hiki sasa angalau Watanzania wanaweza wakapumua, tukapandisha bei ya mafuta ya taa ambayo kwa kweli bado wananchi wanalalamikia na hii kwao ilikuwa bado ni faida lakini hawakusema kitu. Sasa leo tumesema tu-*balance* maisha ya Watanzania wanaopata shida, wenzetu kwao imekuwa nongwa. *(Makofi)*

Naomba kama vyombo vingine vyote, *EWURA* na kadhalika vimeshindwa basi Serikali ichukue hatua ya mwisho, haifai kuendelea kujadili hapa, tunataka kuona wale wamekamatwa na wengine wamefungiwa leseni zao. Hiyo ndiyo hatua pekee ambayo Serikali inatakiwa kuchukua lakini tofauti na hivyo hao watatukalia, wanachotaka kitokee hapa ni kitu kibaya sana na wananchi waki-*react* huko mitaani Serikali itakimbilia wapi?

Kwa hiyo, sipendi kuona huu mjadala unaendelea lakini ningependa kuona Serikali leo hii hii inachukua hatua na mnapochukua hatua ya kunyang'anya leseni tayari kuwe na Askari kukagua visima vyao walikoficha mafuta na yauzwe kwa sababu hakuna sababu ya kuendelea kuwabembeleza hawa wafanyabiashara. Mazungumzo mnayotafuta na hawa mnatafuta balaa tu kwani hawabembelezeki hawa, ni kuchukua hatua tu! Kama ningekuwa mimi leo hii, hawa wangekuwa wameshanyang'anywa leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kweli kama kuna sehemu ambayo Serikali inatakiwa kujisafisha na kuwaonesha Watanzania kwamba siyo legelege ni kuchukua hatua sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipeleke lawama zangu kwanza kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga uswahiba na matajiri hasa wakati wa kampeni wakawa wanachangiwa fedha na wafanyabiashara wa mafuta mpaka wafanyabiashara hao wamefikiria kwamba wao ni sehemu ya Serikali na wanaweza kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuko kwenye amani wanakataa kutoa mafuta, vipi tungekuwa vitani? Hali ingekuwaje? Hatuhitaji kusema mengi sana tunahitaji utekelezaji wa Serikali. Kama huu mgomo ungefanywa na wanafunzi wa vyuo vikuu basi *Field Force* ingekuwa kule, hivi leo wanasubiri nini? Haya mambo wamekaa wakayapanga, taarifa za kiintelijensia hapa zilikuwa wapi? Au ziko kwenye maandamano ya CHADEMA peke yake? Tunahitaji kuona makali ya Serikali sasa kama kweli siyo legelege. Leo ndiyo Watanzania watajua kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni legelege au siyo legelege?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Rai yangu ya kwanza ni kuliomba Bunge hili kurudisha ile Sheria ya amri ya kuwekwa watu kizuizini ambayo Bunge lako Tukufu iliifuta na ndiyo maana leo tunachezewa kama mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kifungu cha 9 cha Sheria namba 8 ya mwaka 2003 na kifungu namba 20 cha Sheria za *EWURA*, kitendo chochote cha wafanyabiashara kufanya

kikao na kuamua ni haramu na adhabu yake imeelezwa kabisa pale aidha ni 5% ya *turnover* au 10% ya *turn over.* Leo ni siku ya saba hawa watu hawajachukuliwa hatua hata kidogo na hivi vitu viko *very straight.*

Kwa hiyo, natoa ushauri mwingine wa kurahisisha ili Watanzania wasiendelee kupata tabu. Kule Tabora leo hakuna mafuta siku ya tatu, siyo kwamba wako kwenye foleni kama Dar es Salaam, hapana! Jana nilisahau kutia mafuta katika gari lakini nilipofika Chalinze nikaambiwa Mkoa wa Pwani hakuna mafuta lakini bahati nzuri gari yangu ilikuwa na bendera ya Ubunge, nilipokwenda kituo cha pili kabla ya kufika Mdaula waliponiona, nikapata mafuta kwa kuhofia ile bendera tu, ni lazima niseme ukweli! Lakini watu walikuwa wanaambiwa hakuna mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukomesha huo ujinga naomba kama Ma-*DC* wananisikiliza wa nchi nzima waende wakaangalie kwenye *petrol stations* wakikuta mafuta yapo waagizwe wale watu wanaouza wauze na wenye mafuta yale wakamatwe kwa sababu DC ana Mamlaka ya kumweka ndani mtu bila sababu masaa 48 ili iwe fundisho wakati mwingine watu wasirudie huo mchezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo napenda sana kumshukuru ndugu yangu na mdogo wangu January Makamba kwa kuleta hoja hii na naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeuri waliyoonesha wafanyabiashara, ya kuwatesa Watanzania bila huruma inaonesha ni kwa jinsi gani ambavyo Serikali inaonesha udhaifu na inaonesha ni jinsi gani Wizara husika imeshindwa kutekeleza wajibu wake kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku kama tano zilizopita yupo mfanyabiashara aliyesimama akasema kwamba, naipa Serikali saa ishirini na nne (24), iongeze bei ya mafuta, sisi tulitegemea Serikali ingeamka ikachukua hatua mapema, lakini wametulia kimya mpaka sasa hivi tumefikia hapa tulipo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni kawaida wafanyabiashara kutaka *super profit*, hakuna uzalendo wala upendo. Tunaomba Serikali leo ichukue hatua na wafanyabiashara hawa ambao wanaonekana kama ni sehemu ya ubia kwenye Serikali, wanaongoza Serikali pamoja, haiwezekani! Ni akinamama wangapi wamepoteza maisha tangu juzi mpaka leo? Ni watoto wangapi wameshindwa kwenda hospitalini kwa muda na wamefariki? Ni watoto wangapi wamekwama kwenda shuleni? Ni tabu kiasi gani Watanzania wameipata? Yote haya tunairudishia Serikali kwa sababu kwa siku saba wameshindwa kuonesha kwamba wao ni Serikali. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wengine wote waliozungumzia suala hili kwamba, tunataka hatua za haraka jioni ya leo, tusisubiri kesho. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niungane na wenzangu kutoa masikitiko yangu juu ya tatizo hili la mafuta kutokana na mgomo baridi wa wauzaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida tunapokuwa na changamoto kubwa kama hii, kwa upande mwingine ni lazima tuwe makini sana. Nchi yetu sasa hivi inakabiliwa na tatizo la umeme, kuna giza na sasa hivi kuna hili la mafuta ambalo ni zito sana kwa uchumi wa nchi. Lakini kubwa zaidi, Bunge lilitoa mamlaka kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*) na tukaipa namna ya kufanya ili haki itendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mnivumilie sana wapendwa! Wanasema ushauri unaweza ukawa mzuri na mkubwa sana kwa watu wengi, lakini hata mmoja naye umsikilize. Hata mtu anapokuwa ameua, anawekewa Wakili. Leo naomba niwe Wakili wa wauzaji wa mafuta. Naomba mnisikilize kwa sababu ni muhimu, tuangalie hayo yote kwa makini. Suala ninalotaka kulisemea hapa ni hivi, kwanza tunawaomba wauzaji wa mafuta kama kuna jambo ambalo

linawaumiza kiasi cha kuweka mgomo baridi, basi waliache ili tuweze kulitatua kwa njia ya maafikiano mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kwamba pia kuna tatizo kubwa sana la uingizaji wa mafuta katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Hayo yote hayajazungumzwa. Kwa hiyo, itakuwa ni vema sana tusiangalie upande mmoja tukaacha upande mwingine. Ushauri wangu ninautoa leo, ni kuiomba sana Serikali tusifanye maamuzi ya jazba, badala yake tukae kwa kuhakikisha kwamba tunafanya maamuzi mazuri kwa faida ya Watanzania. Haitoshi tu kuwapa *pressure* bali kwa maamuzi yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na kwamba wachangiaji wengi wamenifilisi yale ambayo nilikuwa nataka niyazungumzie, lakini binafsi ningeiomba sana Serikali kupitia sheria zilizopo ichukue hatua ya haraka sana kwa sababu pamoja na kwamba tunayo *EWURA* kama ndiyo chombo ambacho kinasimamia na kuendesha biashara zote zinazohusiana na nishati, pia tunalo Baraza la Ushindani (*Fair Competetion Tribunal*) ambalo linasimamia ushindani wa kibiashara. Sijui mpaka sasa hivi wamechukua hatua gani kwa sababu ikiwa mara zote mnufaikaji anakuwa ni yule muuzaji wa mafuta, leo hii muuzaji wa mafuta hakubali mtumiaji naye anufaike, hili jambo inabidi liangaliwe kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mlivyosema biashara ya mafuta inataka kuuweka uhuru wa nchi yetu rehani. Ni jambo ambalo Serikali inabidi iliangalie kwa makini sana na hatua ambazo zinatakikana zichukuliwe ziwe ni zile ambazo ni madhubuti kabisa kwa sababu ni Bunge hili hili ndiyo tulikaa tukakubali kuongeza bei ya mafuta ya taa ili kuweza kudhibiti uchakachuaji. Leo hii uagizaji wa mafuta ya *Jet - A1* umepanda zaidi ya mara kumi ya mahitaji ya kawaida, kwa maana kwamba badala ya kutumia mafuta ya taa, sasa hivi yanatumika mafuta ya ndege. Sasa wafanyabiashara hawa hawa tutaendelea kuleana nao mpaka lini na Serikali imekaa kimya haitoi matamko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wote tunasema kwamba Serikali ikubali kuingia katika baadhi ya biashara muhimu. Suala la mafuta hatuwezi tukaliacha likaenda huru tu! Leo asubuhi wachangiaji walianza kusema kwamba mara zote tuwe tunaangalia hizi *policy support instruments* tunazoletewa. Moja kati ya uamuzi mbaya sana ambao tumepewa na mashirika ya kimataifa ni ku-*shut down plant* yetu ya *refinery* pale *TIPPER.* Kwa nini tuliua *TIPPER*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndiyo maana tunakaa hapa tunajadiliana bei ya mafuta. Bei ya mafuta Tanzania ambao tuko na bandari, inashindana na bei ya mafuta ya Zambia. Zambia wao wana *refinery plant*, sisi tunaagiza mafuta yanakuja kama *fresh product*. Siku zote kwa nini tusingekuwa tunaagiza mafuta kama *crude*? Kungekuwa hakuna mambo yote haya! Sasa tunahitaji hatua za haraka ziweze kuchukuliwa, lakini hatua za kudumu Serikali iingie kwenye biashara ya mafuta ili kuwe kuna ushindani wenye uwiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba niunge mkono hoja na nimpongeze mtoa hoja kwa kuleta hoja hii ndani ya Bunge lako. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita mchangiaji wa mwisho kwenye hoja hii. Kama mnavyojua mwenye hoja ni Mheshimiwa January Makamba, kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kama mchangiaji wa mwisho kwenye hoja hii.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili kuweza kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kulishukuru Bunge lako Tukufu, kama nilivyosema kwa kunipa fursa hii ya kutoa taarifa kwa njia hii ya uchangiaji kuhusu hali ya biashara ya mafuta ya petroli hapa nchini kama vile ambavyo mjadala unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, mafuta ya petroli ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu kwani viwanda, vyombo vya usafiri na huduma nyinginezo nyingi hutegemea mafuta na bidhaa zake. Bei ya mafuta inapopanda, bei zingine nyingi hupanda kwa mfano, bei za usafiri, bei za vyakula, bei za bidhaa za viwandani na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22 Juni mwaka huu wa 2011, Serikali kupitia kwa Waziri wa Fedha wakati akihitimisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/12, ilitoa maagizo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*), kuchukua hatua mbalimbali zitakazochangia kupunguza bei za mafuta. Hatua ambazo ziliagizwa kuchukuliwa ni pamoja na:-

(a) Ukokotoaji wa thamani ya shilingi kwa kuioanisha na dola ya Marekani (yaani *exchange rate*);

(b) Kuondoa au kupunguza wigo wa asilimia 7.5 ambayo makampuni yaliruhusiwa kuweka ili kufidia baadhi ya gharama;

(c) Kupitia upya misingi ya ukokotoaji wa viwango vya tozo mbalimbali za Taasisi za Umma, kwa lengo la kubakia na tozo stahili na kwa viwango stahili bila kuathiri majukumu ya udhibiti na usimamizi yanayofanywa na Taasisi hizo;

(d) Kupunguza tozo za kampuni za mafuta ikiwa ni pamoja na gharama za kibenki (yaani *financing charges*); na

(e) Upotevu wa mafuta yanayosafirishwa kwenye meli na gharama ya ukaguzi (yaani *inspection fee*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali. Serikali kupitia *EWURA* ilianza mara moja mchakato wa kurekebisha kanuni ya ukokotoaji wa bei za mafuta hapa nchini kwa lengo la kuleta unafuu wa bei kwa mlaji. Hatua ya kwanza ilikuwa kuandaa hoja (*discussion paper*) ambayo ilitoa mapendekezo ya maeneo mbalimbali yanayofaa kurekebishwa ili kupata maoni ya wadau wa sekta ya mafuta. Mapendekezo hayo yalizingatia maagizo ya Serikali pamoja wa ushauri mbalimbali wa wadau katika sekta ya mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wadau. Mchakato wa kupata maoni ya wadau (taftishi) ulianza tarehe 4 Julai, mwaka huu wa 2011 na kukamilika tarehe 26 Julai, mwaka huu 2011. Kwa kawaida, mchakato huo ungechukua siku 81 lakini kutokana na unyeti wa suala hili, Mamlaka ililazimika kuufupisha hadi siku 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano wa wadau uliitishwa tarehe 22 Julai, 2011 ili kupitia rasimu ya kanuni pamoja na jedwali la uchambuzi wa maoni ya wadau lililoandaliwa na *EWURA*. Wadau walioshirikishwa katika taftishi hiyo ni pamoja na makampuni ya mafuta, Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na *EWURA* (*Consumer Consultative Council*), Baraza la Ushauri la Serikali, Taasisi za Umma kama vile *TRA, TBS, WMA, TPDC, TPA, SUMATRA,* na *TIPER*. Maoni mbalimbali ya wadau yalipokelewa na kuchambuliwa na *EWURA*, ikiwa ni pamoja na kupata maoni ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali zikiwemo Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Uchumi, Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (*TPDC*), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *EWURA* na Makampuni ya Mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 23 Julai, mwaka huu wa 2011, *EWURA* iliitisha kikao cha wawakilishi wa wadau wakubwa ambao ni pamoja na *CCC, TPDC, TPA*, Wizara ya Nishati na Madini, Mwanasheria Mkuu na baadhi ya makampuni ya mafuta kupitia mapendekezo yaliyokuwepo na kutoa maoni ya mwisho kabla ya kuwasilishwa kwenye Bodi kwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 26 Julai, mwaka huu wa 2011, Bodi ya Wakurugenzi ya *EWURA* ilikaa na kupitia mapendekezo ya marekebisho ya vipengele mbalimbali vya kanuni ya kukokotoa bei ya mafuta. Maamuzi hayo ya Bodi yamepelekea punguzo la bei za mafuta kwa viwango vifuatavyo: Petroli Sh. 202.37; Dizeli Sh. 173.49 na Mafuta ya Taa Sh. 181.37. Mabadiliko haya ya bei ni sawa na punguzo la asilimia 9.17; 8.31; na 8.70 kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa sawia. Kanuni hii ya kukokotoa bei za mafuta imeanza kutekelezwa kuanzia tarehe 3 Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 na 4 Agosti, 2011 makampuni ya mafuta yaliwasilisha kutoridhishwa na maamuzi yaliyofanywa na *EWURA* hususan kuhusu kupunguzwa kwa wigo wa asilimia 7.5; *margins* za makampuni ya mafuta na gharama za kuchelewesha meli bandarini *(demmurage charges)*. Haya ndiyo mambo ambayo yaliwasilishwa *EWURA*, makampuni yakiwa yanaelezea kutoridhishwa na huo ukokotoaji uliokuwa umefanywa na *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia vikao hivyo vya Serikali, makampuni pamoja na *EWURA* siku ya Ijumaa tarehe 5 mwezi huu wa Agosti 2011, Mamlaka ya *EWURA* ilifanya marekebisho mengine katika vipengele vifuatavyo:-

(a) Gharama za ucheleweshaji meli bandarini (*demmurage charges*) ziliongezwa kutoka wastani wa Sh. 1.85 kwa lita hadi Sh. 8.76 kwa lita.

(b) Viwango vya faida kwa kampuni za mafuta *(OMCs margins)* ziliongezwa kutoka Sh. 108.69 kwa lita hadi Sh. 110.57.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji na usambazaji mafuta baada ya kuanza kutumika kwa kanuni mpya. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini imeendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa biashara ya mafuta hapa nchini. Ufuatiliaji uliofanywa kwenye maghala ya kuhifadhia mafuta umedhihirisha kuwa kuna mafuta ya kutosha hapa nchini na pia kuna meli kadhaa ambazo zipo nje ya gati zikisubiri kupakua mafuta. Aidha, makampuni ya mafuta yameuza mafuta kwa wingi siku ya Ijumaa tarehe 5 Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Ijumaa tarehe 5 Agosti, 2011 kiasi cha mafuta yaliyokuwepo katika maghala ya baadhi ya Makampuni ya Mafuta yaliyokaguliwa ni lita milioni 191.813 ambayo inakidhi matumizi ya nchi kwa kati ya siku 8 hadi 67 kulingana na aina ya mafuta kama inavyoonekana kwenye hapa chini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta yaliyoko nchini tarehe 5 Agosti, 2011; Akiba iliyopo: Mafuta ya Petroli ni lita 41,934,139; Mafuta ya Dizeli ni lita 92,650,300; Mafuta ya Taa ni lita 41,227,870; Mafuta ya Ndege ni lita 4,384,297 na Mafuta Mazito ni lita 10,805,070. Wastani wa Matumizi kwa siku: Mafuta ya Petroli ni lita 875,000; Mafuta ya Dizeli ni lita 3,100,000; Mafuta ya Taa ni lita 615,240; Mafuta ya Ndege ni lita 560,500 na Mafuta Mazito ni lita 1,087,695. Makadirio ya siku za kutumika: Mafuta ya Petroli ni 48; Mafuta ya Dizeli ni 30; Mafuta ya Taa ni 67; Mafuta ya Ndege ni 8 na Mafuta Mazito ni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya mafuta kwenye maghala ya jumla. Takwimu zilizowasilishwa *EWURA* na mkandarasi anayeweka vinasaba katika mafuta yauzwayo hapa nchini (*GFI*) na kuhakikiwa na wakaguzi wa EWURA zinaonesha kuwa kwa siku ya Ijumaa tarehe 5 Agosti, 2011 mauzo ya mafuta kutoka kwenye maghala *(depots)* yalikuwa ni malori 329 kwa aina mbalimbali za mafuta kwa ajili ya soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Agosti, 2011, walipakia malori 40 wakati tarehe 4 Agosti yalipakiwa malori 185. Kwa kawaida, wastani wa mauzo kwa siku ni takriban malori 250 hadi 300. Takwimu hizi zinadhihirisha kuwa kuanzia tarehe 5 Agosti, 2011 mauzo ya mafuta yaliongezeka na kufikia kiwango cha kawaida. Katika hali ya kawaida, Makampuni mengi ya mafuta hayafanyi kazi katika siku za mapumziko na hasa haya ambayo yanatoa mafuta kwenye *depots* sio kwenye vituo vya kawaida. Kwa hiyo, siku ya Jumamosi tarehe 6 Agosti, 2011, jumla ya malori 115 yalipakia mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya mafuta kwenye vituo vya mafuta vya rejareja. Ukaguzi uliofanywa na *EWURA* kwenye vituo vya mafuta Jijini Dar es Salaam na baadhi ya Mikoa unaonesha kuwa vituo vingi vilianza kuuza mafuta kama kawaida kwa wiki iliyopita. Ukaguzi huu pia umehusisha kupata takwimu za mafuta yaliyopo kwenye vituo ili kuhakikisha kuwa hakuna kituo kinachohodhi mafuta na kuacha kuuza. Kuna baadhi ya vituo vilikuwa vikisubiri kupata mafuta kwa vile walikuwa wameishiwa kwa sababu Makampuni ya Mafuta hayakuuza mafuta kwa kiwango cha kawaida siku ya tarehe 3 na 4 Agosti, 2011. Makampuni mengi yaliendelea kupakia malori ya mafuta mpaka usiku wa tarehe 5 Agosti, ambapo ilikuwa ni siku ya Ijumaa. Hivyo ilitarajiwa kwamba kungekuwa na usambazaji mwingi zaidi kwenye vituo kuanzia Jumamosi tarehe 6 Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya bei. Ukaguzi uliofanywa na *EWURA* unaonesha kuwa bei za mafuta kwenye vituo vinavyouza mafuta zimezingatia bei kikomo zilizotolewa na Mamlaka ya *EWURA* tarehe 3 Agosti, 2011. Ukaguzi huo umefanyika katika Miji ya Arusha, Moshi, Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, hakuna taarifa zilizopokelewa na *EWURA* kutoka Mji wowote kuhusu kukiukwa kwa bei kikomo iliyopo sasa kwa wale ambao walikuwa wanauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali, bidhaa za mafuta ya petroli zinatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi katika nchi zote duniani. Upatikanaji wa uhakika wa mafuta na kwa bei stahili vitafanya uchumi wa nchi yetu kukua kwa kasi zaidi na kuwa endelevu. Serikali inachukua hatua zifuatazo ili kuhakikisha kuwa mafuta ya kutosha yanapatikana sehemu zote nchini.

Kwanza, Serikali kupitia *EWURA* inafuatilia mwenendo wa usambazaji wa mafuta kwa karibu kutoka katika maghala ya Kampuni ya Mafuta kwenda kwenye vituo vya mafuta.

Pili, Serikali kupitia *EWURA* itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa Kampuni zilizokiuka masharti ya leseni na kusababisha uhaba wa mafuta kwenye vituo vya kuuza mafuta nchini.

Tatu, leo hii tarehe 9 Agosti, 2011, Serikali kupitia *EWURA* imeipa leseni Kampuni ya *COPEC* ambayo ni Kampuni Tanzu ya Serikali kupitia *TPDC* kuanza kufanya biashara ya mafuta mara moja. Naomba kurudia. Leo hii tarehe 9 Agosti, 2011 Serikali kupitia *EWURA* imeipa leseni *COPEC* ambayo ni Kampuni Tanzu ya Serikali kupitia *TPDC* kuanza kufanya biashara ya mafuta mara moja. *(Makofi)*

Nne, Serikali kwa kupitia *EWURA* imekamilisha taratibu za uagizaji wa mafuta kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa mafuta yanapatikana na kwa gharama nafuu zaidi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia *EWURA* leo hii tarehe 9 Agosti, 2011 imetoa *Compliance Order* kwa Makampuni manne ambayo ni *BP, ENGEN, OILCOM* na *CAMEL OIL* ambapo wanatakiwa watekeleze hatua zifuatazo. Nirudie hapo kufuatia hali iliyojitokeza leo hii tarehe 9 Agosti, 2011, *EWURA* imetoa *Compliance Order* kwa Makampuni manne ambayo *ni BP, ENGEN, OILCOM* na *CAMEL OIL* ambapo wanatakiwa watekeleze hatua zifuatazo.

Kwanza, mara moja wanatakiwa kuanza kutoa huduma katika maghala yao ikiwa ni pamoja na kuanza kuuza mafuta katika vituo vya rejareja ikiwemo vituo vilivyo chini ya milki zao. Narudia, mara moja wanatakiwa kutoa huduma katika maghala yao ikiwa ni pamoja na kuanza kuuza mafuta katika vituo vya rejareja vikiwemo vituo vilivyo chini ya milki zao.

Pili, Makampuni yanaagizwa yaache mara moja kitendo chochote kitakachosababisha upungufu wa makusudi wa mafuta ya petroli katika soko la Tanzania. Katika kipindi cha masaa 24 tangu amri hii ilivyotolewa, wajieleze kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria dhidi yao kwa kukiuka matakwa ya Sheria ya Mafuta pamoja na Sheria ya *EWURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuisha kwa muda uliotolewa na *EWURA,* adhabu stahiki zitatolewa kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kusitisha ama kufuta kabisa leseni zao. Katika

hali ya kawaida na kwa mujibu wa Sheria, mtu ama Taasisi ama Kampuni yoyote isiporidhika na maamuzi ya *EWURA* anapaswa au Kampuni au Taasisi hiyo inapaswa kukata rufaa katika Baraza la Ushindani yaani *Fair Competition Tribunal*. Hatua hii kwa mshangao mkubwa haijafuatwa hadi sasa na haya Makampuni yanayokaidi na Serikali inaelekeza kwamba masuala kama haya ni vyema yakafuata taratibu za Kisheria kufanya vinginevyo ni kujitafutia matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madin, Mheshimiwa Ngeleja, sasa naomba nimwite mtoa hoja kwa kifupi sana tumalizie hoja yake.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kukushukuru wewe na uongozi wa Bunge kwa kukubali kwamba hoja hii ijadiliwe. Napenda kuwashukuru Wabunge wenzangu na wenyewe kwa kukubali na kuchangia kwa moyo wa uzalendo na kwa ufasaha kabisa na sote bila ya kujali itikadi za Vyama, tunakubaliana na udharura wa jambo lenyewe na uharaka wa hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha mjadala huu kwa kuzungumza mambo mawili, matatu kwa maana ya maoni na mapendekezo. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kutoa leseni kwa Kampuni ya Serikali ya *COPEC* na yenyewe iagize mafuta, jambo hili litatuhakikishia usalama wa mafuta. Vilevile kama Kampuni ya Serikali inaagiza mafuta tutajua biashara hii inaendeshwaje, vitu gani vinaendelea huko na faida inapatikana vipi na ni kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napendekeza sasa kwamba kutoa leseni ni jambo moja, lakini kuiwezesha Kampuni hii kuagiza mafuta ni jambo lingine. Tulivyopitia bajeti yetu ya Wizara ya Nishati na Madini, *COPEC* ilikuwa imepangiwa shilingi milioni 20. Kwa hiyo, kwa uamuzi huu wa kuipa leseni, tunapenda Serikali ifanye jambo kubwa la msingi kwa manufaa ya nchi. Aidha, ipewe fedha zaidi kutoka kwenye bajeti kama walivyofanya kwenye bajeti ya Uchukuzi kwamba zitafutwe pengine au iwezeshwe sasa kwa maana ya dhamana ili ikope na kuweza kuagiza mafuta. Hilo la kwanza kwamba leseni ni vyema, lakini uwezeshaji wa kuagiza mafuta ndilo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba kwa kuwa sasa mgogoro huu na hii dharura tuliyonayo sasa imetokana na kutokuelewana kuhusu kanuni au *formula* ya kukokotoa bei ya mafuta, napendekeza kwamba *formula* hiyo au kanuni ya bei ya mafuta iwekwe wazi kwamba bei inayotangazwa na *EWURA* wanaipatapata vipi, ni *formula* au kanuni gani inatumika? Nashauri kanuni au *formula* hiyo sasa iwekwe wazi, Bunge lijue na umma ujue, isiwe ni bei ambayo watu wanadhani imedondoka, hata mjadala kuhusu bei haulengi hasa bei hiyo imefikiwa vipi. Kwa hiyo, napendekeza Serikali ipate fursa ya kueleza kupitia Kamati ya Nishati na Madini au Kamati ya Fedha na Uchumi au Bunge zima kwamba bei ya mafuta inafikiwaje na udhibiti wake ni vipi, hilo jambo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, mafuta ambayo tunayatumia sisi, mafuta ya Tanzania kama nchi, yako katika sehemu tatu na yanahifadhiwa katika sehemu tatu. Kwanza, ni yale yaliyopo kwenye visima vya mafuta kwenye vituo vya kujazia mafuta. Pili, ni yale yaliyopo kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta na tatu ni yale yaliyopo kwenye meli ambazo zinakuja Tanzania, ni oda. Kwa kuwa tunafahamu kwamba katika sehemu hizo tatu, hii sehemu ya kwanza, mafuta yamekauka au yanaelekea kukauka na kweli tunafahamu kwamba kwenye maghala yapo kama alivyotoa takwimu Mheshimiwa Waziri lakini vilevile zipo taarifa ambazo mtoa hoja anazo kwamba hadi sasa meli nne zilizokuwa zinaleta mafuta Tanzania zimekuwa *diverted* tani 120,000, kwamba oda imekuwa *cancelled* hayaji tena Tanzania. Kwa hiyo, tunaweza tukafanya uamuzi leo ambao ni mzuri wa kuamrisha Makampuni yatoe mafuta kwenye maghala, lakini kama ambavyo yameisha kwenye vituo kwenye maghala na kwenyewe yataisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna meli zinazoleta mafuta Tanzania ambazo bado zinaagizwa na haohao wauza mafuta, kwa hiyo ni tatizo kubwa zaidi kuliko ambavyo tunalizungumza. Pendekezo langu ni kwamba Serikali ijiridhishe na uuridhishe umma kwamba meli zinazoleta

mafuta Tanzania zitaendelea na safari za kuleta mafuta Tanzania. Kwa sababu kuamrisha tu wauze kwenye maghala na yenyewe yataisha, kubwa ni meli zinazoleta mafuta Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba inawezekana kwamba nafuu ikapatikana kwa hatua hizi ambazo Serikali imesema. Nafuu ya upatikanaji wa mafuta Tanzania ikapatikana na naamini itapatikana, lakini sote tunajua kwamba ikipatikana nafuu inaanza Dar es Salaam wakati tatizo la mafuta sasa hivi ni nchi nzima. Kwa hiyo, napendekeza kwamba mara pale dalili za nafuu zitakapoanza kuonekana kwa maana ya upatikanaji wa mafuta nchini, Serikali iandae mpango wa dharura wa usafirishaji wa mafuta Mikoani haraka sana ili wenzetu kule wa Tabora, Rukwa, Kagera, Kilwa, Shinyanga na kwenyewe wapate mafuta kwa haraka kama ambavyo watu wa Dar es Salaam watayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba kama unavyofahamu, uhaba huleta ulanguzi na uhaba wa mafuta umeshaanza kuleta tatizo la ulanguzi. Kwa sababu wananchi wengi sasa hivi wanauziwa mafuta bei ya juu kuliko hata ile iliyokuwepo mwanzo ambayo *EWURA* waliishusha. Kwa hiyo, sasa tumekuja kwenye tatizo kubwa zaidi la ulanguzi. Ulanguzi unaendana na kuficha bidhaa, ukitaka kulangua kitu unakificha kionekane hakipo halafu ndio unasema bei yake ikiwa ni ya juu zaidi. Sasa tunajua kwamba mafuta yanahifadhiwa kwa namna ya kipekee ya usalama. Ulanguzi wa mafuta una hatari tu sio kwa uchumi, lakini hata kwa usalama kwa maana ya moto na mambo mengine. Kwa hiyo, napendekeza kwamba Serikali itoe tahadhari kwa umma, kwanza ichukue hatua kali dhidi ya ulanguzi wa mafuta ambao umeanza kujitokeza lakini itoe elimu kwa umma na kwa jamii kuhusu hatari ya kuhifadhi na kuficha mafuta. Kwa sababu katika mazingira haya, mtu ana hela zake anaweza kununua mapipa mawili ahifadhi ndani ya nyumba petroli kwa shaka tu kwamba mafuta yanaweza yasipatikane kwa muda mrefu. Sasa Serikali itoe elimu kwamba hili ni hatari, wanaweza wakaunguza Magomeni nzima, Mungu apishie mbali, kwa sababu tu watu wameficha petroli ndani ya nyumba zao, kwa hilo na lenyewe ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala alilolizungumza Mheshimiwa Waziri hapa la *Compliance Order,* naipongeza Serikali kwa jambo hilo, hizo ndio hatua ambazo tunazitaka kwamba sheria ifuate mkondo wake. Kwa kuwa *Compliance Order* hii ni masaa 24, ambacho tunataka Serikali ijitayarishe nacho ni kuitekeleza *order* hii mara pale itakapokuwa haijatimizwa, maana wakati ule tangazo la bei lilivyotoka inaelekea Serikali ilikuwa haikujitayarisha kuhakikisha kwamba bei hiyo inatimizwa, lakini sasa tumejifunza, *Compliance Order* imetoka ndani ya masaa 24 watu hao wawe wameuza mafuta. Sasa watakapokuwa hawajauza na naamini ndani ya masaa 24 tutakuwa bado tuko Bungeni kesho, kwa hiyo, tunapenda kuona sasa hatua zinazostahili zinachukuliwa kwa hao ambao watakuwa wamekiuka amri ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa January Makamba kwa hoja yako. Sasa utaratibu unanitaka Waheshimiwa Wabunge niwahoji na hoja iliyo mbele yetu kufuatana na maelezo ya Mheshimiwa Makamba na *Compliance Order* kwamba Serikali ihakikishe huduma ya mafuta inapatikana nchi nzima na ni endelevu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA**: Hongera sana Mheshimiwa Makamba na hongereni Waheshimiwa Wabunge wote kwa fursa hii iliyopatikana ya kutumia Kanuni zetu vizuri kuweza kujadili jambo ambalo kwa kweli linaathiri jamii ya Watanzania wote bila ya kujali tofauti zao za Vyama vya Kisiasa, dini, rangi, kabila, jinsia, ni jambo ambalo linawaathiri watu wote. Tunaomba basi wahusika wote wajitahidi kuhakikisha kwamba jambo hili ambalo linaweza likatuharibia uchumi kwa haraka linarekebika. Tunaitakia mema Serikali yetu katika kushughulikia jambo hili ambalo liko mbele yetu na tunaamini kabisa kwamba inawezekana.

Baada ya hapo sasa tunaendelea na utaratibu kama kawaida.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mwongozo wa Spika. Kwa kutumia Kanuni namba ...

**NAIBU SPIKA:** Naomba nikupe nafasi mwishoni, univumilie kidogo tuendelee kidogo tu, tuitendee haki Wizara ya Viwanda na Biashara. Nitakumbuka wakati utakapowadia.

Tulifika wakati wa uchangiaji, naomba Mheshimiwa Hasnain Murji aanze na Mheshimiwa Gaudence Kayombo atafuatia.

**MHE. HASNAIN M. MURJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenifikisha salama na kuweza kusimama na kuchangia leo. Pia naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wapigakura wangu ambao wamenipigia kura nyingi na kura za kishindo lakini pia niwashukukru kwa kunipa Madiwani wote wa CCM ndani ya Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, tumekipitia vizuri kitabu chake, kwa kweli inatia moyo na nampongeza kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia, naomba na mimi ni-*declare interest* kwamba na mimi ni mjasiriamali. Kitabu hiki nimekisoma na nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri lakini nimesikitika kuona kwamba hakuna takwimu za aina yoyote za viwanda vya sukari. Viwanda vyote tumepata takwimu zake, kwamba mwaka 2009 tulizalisha kiasi gani na mwaka 2010 walizalisha kiasi gani lakini nilipopitia vizuri katika Kitabu, sikuona eneo lolote ambalo viwanda vya sukari vimeonyeshwa kwamba mwaka 2009 vilizaliswa kiasi gani na mwaka 2010 vimezalishwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mfupi uliopita tulikuwa na hoja ya mafuta hapa na tuna tatizo kubwa la mafuta na mimi niseme kwamba tatizo la mafuta linafanana kabisa na tatizo la sukari sasa hivi nchini, tuna tatizo kubwa sana la sukari sasa hivi. Tuna viwanda ambavyo si chini ya vinne lakini kati ya viwanda hivyo, kiwanda kimoja ndiyo kinachozalisha sukari cha Kilombero. Pamoja na kiwanda hicho kuzalisha sukari lakini mgao wa sukari kutoka kiwandani ni wa upendeleo mkubwa sana. Inaelekea hii biashara ya sukari imechukuliwa na inaendeshwa na wafanyabiashara wachache tu wenye uwezo, basi! Hali hii ndiyo inayosababisha leo kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba kuna magari yapo Dar es Salaam leo karibu siku ya kumi yanasubiri kupakia sukari kwenda Mikoani lakini hawajapata hiyo sukari. Magari yako *godown* na sukari hakuna. Sasa hatuelewi kwa sababu kipindi hiki ndiyo kipindi cha uzalishaji wa sukari, hatuelewi kwa nini hawa watu wa viwanda hivi wanafanya hivyo, wanafanya makusudi au wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichukue nafasi hii nimwombe Mheshimiwa Waziri aongee na Mheshimiwa Waziri Mkuu angalau atoe tamko kwamba hivi viwanda sasa vi-*release* sukari na kwa nini viwanda hivyo vimefungwa, tujue kwa nini viwanda vingine havifanyi kazi. Leo tuna kiwanda cha Mtibwa kimefungwa, tuna *TPC* kimefungwa, tuna Kagera pia kimefungwa lakini hatuelewi sababu ya hivi viwanda kufungwa wakati huu ndiyo wakati mwafaka wa viwanda hivi kufanya hiyo biashara ya sukari!

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kuna wakati kulikuwa kumetokea tatizo la sukari lakini ilipotokea Serikali ilitoa kibali kwa wafanyabiashara waagize sukari kutoka nje lakini cha ajabu Serikali hii ilitoa vibali kwa viwanda vilevile vinavyozalisha sukari, vikapewa vibali kuagiza sukari. Tuliona ajabu sana kwamba hivi viwanda ndivyo vinavyopewa vibali vya kuagiza sukari na ndiyo vinavyozalisha? Sasa hapa kuna kitu wanatengeneza hatujui ni nini? Kwa hiyo, tunaomba sana mtakapotoa vibali basi hivi vibali vitoke kwa wafanyabishara wote, msilenge kwamba kuna wafanyabiashara watatu, wanne mnaowapa vibali, ni hatari kwa nchi hii pia. Sisi tulio pembeni na wananchi hawaelewi kwa nini haohao tu ndiyo wanapewa vibali kila mwaka? Hapo kunakuwa hakuna maana tena ya biashara huria. Mnapoamua kutoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje kila mtu mwenye uwezo mpeni kibali aagize sukari lakini utakuta ninyi mnachagua wafanyabiashara watatu ndiyo mnawapa, hatuelewi kuna nini na kunaelekea kuna jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimeagizwa na wapigakura wangu ambao ndiyo wafanyabiashara wengi wapo pale Mtwara eneo la sokoni kwamba wanatoa ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri kwamba na wao wanaomba sasa sukari, pale Msumbiji ipo na kutoka Mtwara kwenda Msumbiji ni tofauti, kutoka Mtwara kuja Kilombero ni mbal lakini wao wakivuka tu, wakienda Mweda mpaka Pemba wanapata sukari na kuweza kuja kuuza pale na kwa bei nafuu kuliko hii sukari inayopatikana sasa hivi. Kwa hiyo, tunaomba sana, ninajua kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ni wasikivu, mara nyingi nimekwenda kwao kila ninachoomba wananisikiliza. Kwa hiyo, naomba sasa kwa hili wawaruhusu wafanyabiashara wa Mtwara wakachukue sukari pale Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine sisi watu wa Mtwara tuna historia na watu wa Msumbiji. Vile vita walivyopigana kule na sisi tuna mchango mkubwa sana. Sasa haina maana leo kwamba kuna sehemu ambayo tumetoa mchango wetu na tunaweza tukapata kitu tukakileta kwa manufaa ya wananchi wa Mtwara *and then* ikashindikana. Kwa hiyo, naomba sana Waziri atakapokuwa ana-*windup*, atoe vibali au aruhusu na wafanyabiashara wa Mtwara kwa tatizo hili waende wakachukue sukari pale Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwenye hiki kitabu kwamba kuna viwanda vinakuja Mtwara. Kuna kiwanda cha mbolea, kuna kiwanda cha saruji na kuna viwanda vingi. Mheshimiwa Rais wiki moja iliyopita alikuwa ziarani Mkoani Mtwara, ametutia matumaini makubwa sana kwamba Mtwara inakua na tutegemee Mtwara tutapokea wageni wengi na viwanda vingi lakini hivi viwanda vitakapokuja Mtwara tuna matatizo makubwa sana. Leo wamekuja hawa wachimbaji wa gesi pale Mtwara, ukienda kuangalia na ukienda kufanya tathmini wafanyakazi wanaofanya kazi pale hata asilimia tano ya vijana wa Mtwara hawamo. Ni tatizo kubwa sana. Sasa nina mashaka sana kwamba hivi viwanda vinavyokuja kweli tutavipokea, tutawalea lakini sasa wasije wakatufanyia kama hawa wachimbaji wa gesi walipokuja kwamba wale vijana wetu wasipate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha ajabu hata Askari wa kulinda nyumbani wanamtoa kutoka sehemu nyingine na kumleta pale Mtwara, hata Madereva ambao sisi tunao na vijana wetu wana sifa unakuta wanakosa ajira hiyo wanakwenda kuwachukua kutoka mbali. Sasa hii ni hatari, watu wa Mtwara hawatakubali na watashindwa kufanya hizi biashara zao kwa amani. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba hivi viwanda vitakapokuja basi kaeni nao na miongoni mwa masharti basi watoe nafasi fulani au asilimia fulani kwamba ajira ya pale itolewe kwa vijana wa Mtwara, maana hili ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kulitokea nafasi za ulinzi, ninaambiwa kwamba Walinzi Mtwara wapo lakini wameshindwa kuchukuliwa pale na wameenda kuchukuliwa mbali ili waje walinde pale Mtwara. Ni aibu sana na naomba sana kwamba hivi viwanda vinapokuja vije lakini tunaomba sana wazingatie na kuwe na masharti ya vijana wetu waliokuwepo Mtwara waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba tuna viwanda ambavyo viko nchini vinazalisha kwa mfano Viwanda vya Saruji, cha ajabu utakuta viwanda hivi vipo lakini hawaangalii sana maslahi ya Watanzania, wanaangalia maslahi yao wenyewe. Nitoe mfano, leo ukienda kuangalia saruji inayoagizwa kutoka nje ambayo ina ubora wa 42.5% ambayo hapa haizalishwi,

inazalishwa kwa ajili wa ujenzi wa madaraja, leo utakuta saruji inayotoka nje ni rahisi kuliko saruji inayozalishwa hapa Tanzania inakuwaje? Leo ukinunua saruji ya nje unafyatua matofali arobaini lakini saruji ya kwetu unafyatua matofali thelethani lakini bado utakuta kwamba hivi viwanda ni vyetu, viko hapa lakini bei ya saruji ya Tanzania ni ghali kuliko saruji inayotoka nje. Mheshimiwa Waziri na hilo nalo naomba atupe majibu wakati atakapo-*windup*, inakuaje saruji kutoka nje ambayo ubora wake ni zaidi kuliko saruji inayozalishwa hapa inakuwa rahisi kupita saruji inayozalishwa hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye hotuba, Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza kwamba mwaka huu kumepatikana tani laki moja na ishirini za korosho na ni kweli mwaka jana uzalishaji ulikuwa mzuri. Mheshimiwa Waziri nataka kumwambia mwaka huu kuna kila *possibility* ya kuweza kushuka kwa zao hili. Ninajua kwamba hii ni Wizara ya Viwanda na Biashara na nitakayoongea ni ya Wizara ya Kilimo lakini lazima mshirikiane ninyi wawili ili tuweze kuondoa tatizo hili. Tuna tatizo kubwa sana la pembejeo. Leo *sulphur* inayoagizwa nje na wafanyabiashara haitoshi na hatujui sababu gani, leo wafanyabiasha wamegoma kuleta *sulphur* hatujui ni kwa nini. Kwa hiyo, tani laki moja na ishirini zilizozalishwa mwaka jana nina imani mwaka huu tunaweza tuka-*drop down* mpaka *half of it* lakini kwa sababu hakuna dawa, watu hawajapuliza. Leo bei ya *sulphur* ni shilingi 26,000/- bei ya ruzuku ni shilingi 13,000/- lakini leo mfuko mmoja wa *sulphur* umefika shilingi 45,000/- kweli tunamtendea haki mkulima wa zao la korosho? Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo washughulikie suala hili, ni aibu na hili ni tatizo sugu, tunaomba mliondoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tena niongelee Viwanda vya Korosho. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri katika ziara ya Mheshimiwa ya Rais alikuwepo na alitembelea kiwanda pale Tandahimba ameona. Hivi viwanda vinafanya kazi nzuri na hivi viwanda kwa kweli vinatoa ajira kubwa sana kupita viwanda vingine vya aina yoyote. Hivi viwanda vya kubangua korosho ni viwanda ambavyo vinatoa ajira kubwa sana na Mheshimiwa Waziri ameona lakini kwa mfumo huu wa biashara uliopo, Mheshimiwa Waziri vile viwanda havitaweza kufanya kazi. Kwa sababu leo unakwenda...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Murji kengele ya pili tayari.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji. Kabla sijamwita Mheshimiwa Gaudence Kayombo, niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba wale wote walioalikwa futari kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar jioni ya leo, basi litakuwepo nje hapo baada ya kuahirisha kikao kinachoendelea saa kumi na mbili na nusu jioni hii. Kwa hiyo, naomba wale wote ambao mmealikwa huko usafiri wa uhakika utakuwepo. Tangazo hili linaratibiwa na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, Kamishna wa Tume.

Mheshimiwa Gaudence Kayombo atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kuwapa pole ndugu zangu Watanzania kwa ukosefu wa mafuta, kule Mbinga nimepata taarifa sasa hivi lita moja ni shilingi 6,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuwa na mgonjwa yupo *ICU* kunakuwa hakuna sababu ya kupeana pongezi hata kama yule Daktari amefanya vizuri, ukifika ni kumuuliza anaendeleaje na ile kazi ili kuhakikisha kwamba mgonjwa anapona. Nchi hii kwa miaka miwili, mitatu inajikuta katika tatizo la umeme, hili la mafuta limekuja leo lakini mimi nataka kuzungumzia habari ya umeme. Mimi naamini Wizara ya Viwanda na Biashara wana mchango mkubwa na wanaweza wakatatua tatizo hili kwa haraka zaidi kama Serikali iko tayari kutoa fedha za kutosha. Tumeongea na Shirika la *NDC*, limetupa mpango wao, sina maana kwamba katika Wizara hii Mashirika

mengine hayafanyi kazi, *SIDO* wanafanya kazi nzuri sana, *TEMDO* wanafanya kazi nzuri sana, lakini tunaye mgonjwa ambayo yuko *ICU*, tatizo la umeme, *NDC* hana fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko rafiki yangu mmoja amenipa kitabu kinaitwa *'Bad Samaritan'* na mimi naomba ninukuu maneno machache na yameandikwa kwa Kiingereza na huyu mwandishi wa kitabu hiki ni Mchumi na amesoma *Cambridge* kule London anasema hivi:-

*"The world's wealthiest countries and major institutions such as the IMF and the World Bank wants to see all nations becomes modern thriving societies, in practice though those at the top are kicking away the radar to the wealth that they themselves climbed".* Tafsiri yake isiyo rasmi inasema haya mataifa makubwa yanataka kuona haya mataifa yanaendelea na yanajifanya yanasaidia lakini kwa wakati huohuo haya mataifa yakitaka kupanda ile ngazi ambayo haya mataifa yalipandia wao, ile ngazi wanaisukuma inaanguka. Kwa msingi huu, mimi sitaki kumlaumu mtu lakini tulifanya makosa tukabinafsisha kila kitu. Tulifanya makosa, inawezekana hata na mimi pia lakini ukisoma hiki kitabu anaonyesha wazi kabisa zile zote ni hila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa mwingine anasema *"privatisation sometimes works well but can be a recycle for disaster especially in developing countries that lacks the necessary regulatory capabilities even when the privatisation is the right solution it may be difficult to get thriving in practice".* Anasema ni kweli ubinafishaji unaweza ukafanya kazi lakini wakati mwingine unaweza ukaleta maafa makubwa kama haya ambayo tunayapata kwenye mafuta leo. Kwa hiyo, viko vitu vya kujifunza na mimi nataka kuishiwishi Serikali na ndugu zangu Wabunge tuhakikishe kwamba Wizara hii inapata fedha zaidi na kwa msingi huu siwezi kuunga mkono hoja mpaka pale nitakapopata majibu ya Serikali ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Nchi hii kwanza kihistoria haijawahi kuwa na umeme wa msingi, wanasema *load base* yaani umeme ambao upo kama kuna matatizo unasaidia, hatuna na umeme wa uhakika wa namna hiyo unatokana na umeme wa makaa ya mawe peke yake. Sasa Wakoloni walipokuwa wanachimba makaa kule Songea miaka ile ya 1947 na 1956 na yale makaa yapo mpaka leo, pale kuna tani nyingi tu za makaa ya mawe, ndugu zangu wa *NDC* wameingia ubia na kuunda kampuni inaitwa *TANCOAL* ambayo wanashirikiana na Kampuni kutoka Australia lakini Serikali haijatoa fedha hata senti tano. Matokeo yake ni nini? Kampuni ya *Intra Energy,* kampuni mama ambayo iko Australia ndiyo inayofanya maamuzi kutoka Australia na yanaletwa kwenye Bodi ya *TANCOAL* kwa utekelezaji, mwaka 2007 waliamua kujenga *power station* Ngaka kule Mbinga ya *Megawatt 400,* waliamua kujenga Chuo cha Ufundi cha mambo ya Madini kikubwa pale Ngaka, waliamua watajenga *transmission line* kutoka pale Ngaka kwenda Mufindi kwa kuzingatia kwamba umeme utakaozalishwa ni *megawatt 400* hautaweza kubebwa na *line* zozote zilizoko sasa. Wamemfukuza aliyekuwa Mkuu wa lile Shirika akaja mwingine wakamfukuza amekuja mwingine. Huyu mwingine amekuja na maamuzi tofauti, hayuko tayari kujenga hizo *megawatt 400* mara anaamua kujenga Kyela na sasa kuna taarifa anataka kujenga Dar es Salaam na aanze kusafirisha makaa ya mawe kutoka Ngaka kwenda Litui, kupanda vyombo kwenye maji kwenda Kyela, kupanda lori kwenda Mbeya, kupanda treni kuja Dar es Salaam, biashara gani hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali haipo, haina mkono, tumeachia watu binafsi. Waswahili huko mitaani wanasema "dezo alishakufa". Serikali hatuwezi kukubali iwe inapenda dezo tu. Kwa nini haiwekezi kwenye mradi huu? Kwa nini haitoi fedha kwenye mradi huu umeme ukapatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema *Quick Wins* ni kujenga *MW120* ili kufikisha Songea kwa matumaini kwamba ule mradi unaofadhiliwa na *SIDA* utakuja mpaka Songea kwenda Mbinga, kwa hiyo unaweza ukabebwa pale. Tatizo ni kujenga *transmission line* kutoka Ngaka kwenda Songea, zinatakiwa *USD* milioni 46. Serikali inashindwa kutoa fedha hizi?

Waheshimiwa Wabunge, sitaki kubeza mradi wa vitambulisho, lakini kuna bilioni 300 ya kujenga Ofisi kila Wilaya ya Vitambulisho kabla hatujapata umeme. Mambo haya ya vitambulisho

yote ni *computerized*, hizo *computers* zitakwendaje bila umeme? *Why are we putting the cart before the horse? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuisaidia Serikali yangu kuona kwamba tunaondoka katika janga hili la umeme. Nataka kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba anapata fedha za kutosha aweze kuendesha Wizara hii na ionekanae. Nataka Mheshimiwa Waziri atakapoondoka hapo na Serikali ya Awamu ya Nne itakapoachia ngazi kupisha awamu nyingine, iwe imeacha alama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Konokono ni mnyama mdogo sana na ana maisha mafupi, lakini njia atakayopita tu inaonekana kwa nini kwa sababu anaacha alama. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne imeacha alama, *UDOM*, imeacha alama Sekondari, iache alama kwa kuhakikisha tatizo la umeme linaondoka na litaondoka tu kwa kuisaidia *NDC*, kwa kuhakikisha kwamba mradi wa Ngaka unaanza kufanya kazi na mimi naomba Waheshimiwa Wabunge, katika hili mtuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mbinga wanasema wana hamu kubwa ya kuchangia maendeleo ya nchi hii. Tulipokuwa hatuna Fedha za Kigeni, wakulima wa Kahawa wa Mbinga, wa Mbeya, wa Kilimanjaro, wa Arusha, wa Bukoba, Kahawa yao ndiyo ilikuwa inaulizwa, mna tani ngapi, ndiyo mafuta ya nchi yanaingia. Mbinga ilishiriki hapo, leo tena wananchi wa Mbinga kwa nafasi tu waliyopewa na Mwenyezi Mungu wana makaa ya mawe, wanataka kushiriki katika kuondoa tatizo la umeme bado hawajafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mbinga wanachoomba ni kuhakikisha kwamba Serikali inatoa fedha, kama ni kwa *Quick Wins* hii ya kujenga *transmission line* kutoka Ngaka mpaka Songea, sawa. Sasa hivi hao wenzetu wa *SIDA* wanatusaidia kujenga *transmission line* kutoka Makambako kwenda Songea mpaka Mbinga ili ku-*link Grid* ya Taifa kwa sababu Magharibi ya Nchi na Kusini hakuna hiyo *Grid* lakini tunapeleka nini kule? Hakuna umeme, uko Dar es Salaam! Hiyo *Grid* ya Taifa unapeleka nini? Kwa hiyo, *logic* ni kujenga *transmission line* kutoka Ngaka mpaka Mufindi ili kutoa umeme Ngaka na kuleta huku na siyo Dar es Salaam kuupeleka kule kwa sababu haupo! Mimi nafikiri hii ni hesabu rahisi sana na nafikiri Serikali itaichukua hesabu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uko mpango wa kukarabati *transmission line* kutoka Iringa kwenda Dar es Salaam, kwa ajili gani? Mimi nafikiri ungekuwepo mpango wa kujenga *transmission line* kutoka Ngaka mpaka Mufindi ili iweze kuchukua na kubeba ule umeme wa *MW400*. Makaa yaliyoko kule, *capacity* yake ni kubwa zaidi, wanaweza wakatoa hata *MW1000*. Hawa wawekezaji wanasema sisi tunahangaika hivyo kwa sababu tumejaribu kwenda *TANESCO* hatupewi jibu, tunajaribu kwenda Wizara ya Nishati, hatupewi jibu. Sasa tukaamua pengine tupeleke makaa Dar es Salaam, halafu tuweze kufanya hiyo biashara, Serikali ikisema tu *yes*, *they are ready*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu aliyeko kwenye msiba hazungumzi maneno mengi, anachotakiwa ni kupewa sanda na jeneza akazike. Naiomba Serikali itoe fedha kwa ajili ya *NDC* ifanye kazi hii, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii adimu na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tujiulize sisi Watanzania, je, tuna uzalendo na nchi yetu? Tunaipenda nchi yetu au tumerogwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sikujiandaa lakini nasema kuwa nina masikitiko makubwa. Tujiulize tuliomo humu ndani, tunaipenda nchi yetu au tuko tu, tunaona nchi yetu ikidhalilika katika mazingira ambayo hata hatuwezi kuifananisha na Kenya wala Uganda, huu ni ugonjwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze, sekta yote ya viwanda na biashara, ni sekta mtambuka, ina-*deal* na kila sekta, iwe kilimo, iwe viwanda vyenyewe, iwe uchukuzi, iwe madini na kadhalika lakini, tujiulize hapa tulipofika ni wapi na tulikotoka ni wapi? Tunazidi kwenda kubaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nianze kuangalia sekta ya kilimo na tulivyoathirika. Tanzania kuna kundi dogo la matajiri wanaiyumbisha nchi na hawa hawayumbishi peke yao, tunawasaidia sisi wenyewe Watanzania kwa kutokuwa na uzalendo na kuipenda nchi yetu. Niulize kwa nini? Katika miaka ya nyuma tulikuwa na Shirika la *GAPEX* katika Wizara ya Kilimo, basi lile Shirika lilifanyiwa vurugu mpaka likafa. Yale majengo yakachukuliwa, wakakaa nayo, wao wameridhika na wanaona wametajirika kwa kupitia *GAPEX*, wanauza mazao nje, lakini nchi inapata kidogo, nchi inapata Sungura wao wanapata Tembo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niulize kwa nini naongea hivi? Kuna siku Naibu Waziri wa Viwanda alikuwa anazungumzia suala la *AGOA* na Tanzania ni mojawapo kati ya nchi ambazo ziliridhia kuingia katika *AGOA*, wenzetu Kenya wanafaidika kwa bilioni 200, Tanzania tunafaidika kwa bilioni moja, kwa nini? Mazao yanayotoka Tanzania yanakwenda India, yakitoka India yanakwenda Marekani, kwa faida ya nani? Tujiulize! Ni sisi wenyewe tumetengeneza mtandao kuhakikisha tunakuwa duni na tunawatajirisha makabila mengine na wafanyabiashara wengine wako humu ndani wanatuchanganya akili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali tujiulize, je, tuna uzalendo? Tunaipenda nchi yetu? Kama ni ugonjwa, tukakae majumbani, tukafanye ibada na sala kwamba tuiokoe nchi yetu kwa dhamira ya dhati, kwa kuipenda, siyo kuangalia watu binafsi wanafaidika katika kundi hilo kwa kuhakikisha nchi inaingia katika janga zito.

Mheshimiwa Naibu Spika Wizara ya Kilimo kwa mfano tulikuwa na Viwanda vya Korosho, vyote vilihujumiwa. Masasi kilikufa, Mtwara kilikufa, Lindi kilikufa, Mbagala kilikufa, Kibaha kilikufa lakini sasa hivi baadhi ya wale ale wajanja wamechukua vile viwanda wanaviendesha wao kwa namna wanavyotaka kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, inanisikitisha mpaka nashindwa kusema, tumefikia hivi Tanzania? Wataalam wetu wanaisaidia nini nchi hii? Hawana upendo na nchi hii. Wataalam hawana upendo na Tanzania, wanaangalia binafsi atafaidika nini yeye na watoto wake lakini wanawaacha walalahoi wa Tandahimba, wanamwacha mlalahoi wa Kigoma, wanamwacha mlalahoi wa Rukwa akihangaika! Kama wangekuwa na upendo, wangeangalia kwanza, je, Tanzania tunataka tufaidike na sisi kama ngozi nyeusi tunafaidikaje? Sijapenda kubagua na kuna watu wengine wenye ngozi nyeupe wenye upendo, lakini kuna kundi dogo limeikamata nchi, wao wameshika uchumi. Kama ni kisu, wao wameshika mpini, sisi tumeshika ncha, wanatuburuza wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika sekta ya uchukuzi. Tanzania tulikuwa na reli moja inatoka Dar es Salaam kwenda Bara yote iwe Mwanza mpaka Kigoma. Kulikuwa na reli ya Tanga, kulikuwa na reli ya kwenda mpaka Kilimanjaro, mpaka Nairobi. Reli imehujumiwa kwa makusudi ili bidhaa zao zipite katika barabara ambazo kila siku Serikali inatenga pesa kwa ajili ya barabara ambazo hazitusaidii. Wanafanya vile kwa kuhakikisha mizigo yao itapita katika magari ili wananchi wanaopita kandokando ya reli wasifaidike, hii ni kwa faida ya nani? Wao wanakaa pembeni wanatuangalia Watanzania kama katuni. Imefika mahali tujiulize kulikoni Watanzania tukafikia hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wetu walitusomesha katika mazingira ya kimaskini, lakini tumekuja kuwahujumu na kuwaacha wakiwa wanadhalilika Vijijini, kuacha kundi dogo likinufaika katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia tena katika sekta ya maliasili. Maliasili yetu inahujumiwa kwa kushikwa na ma-*investors* wachache ambao ni haohao. Wanahakikisha wanaivuruga hii nchi hata ile *concession fee* wasilipe mle ndani. Hii ni kwa faida ya nani? Tujiulize Watanzania, tuna moyo wa kuipenda nchi yetu? Tuko hapa kwa ajili ya nini? Haiwezekani! Leo tuangalie hata kati ya sisi Wabunge, kuna Wabunge wanakuja humu ndani kuangalia biashara zao zinasema nini. Siku

akimaliza biashara yake, anaenda nje! Je, Mbunge huyu hapa anasaidia nini zaidi ya kuhakikisha biashara zake zinakwenda vizuri, siku ikimalizika anaondoka zake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imefikia mahali tujiulize, kulikoni Tanzania? Uchumi wa Uganda unakua kwa kuwa unamilikiwa vizuri na wazawa. Uchumi wa Kenya unakua kwa vile unamilikiwa vizuri na wazawa na wazawa wao wana uzalendo na nchi yao, Tanzania ni ziro, kwa nini? Tufike mahali tujiulize, tunafanya haya kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika sekta ya madini. Madini yote yanamilikiwa na kundi dogo hilohilo ambalo linaiyumbisha nchi na wanafaidika wao wakituangalia Watanzania tunahangaika kutafuta Visungura, sijui wao wana Tembo, mpaka lini? Tufike mahali tujiulize, wataalam wa Tanzania soma yao yote inamsaidia nini Mtanzania ambaye ni maskini? Hakuna maana yoyote. Wafikie mahali watubu, waende Makanisani, wakatubu, waende Misikitini wakatubu ili angalau waje waisaidie Tanzania lakini kwa mtindo huu, baada ya miaka mitano itakuwa kama Greece. Uchumi umeshikwa na watu wachache, wao wanajiona ndiyo Vifaru wa nchi hii, wao wanaiburuza nchi hii, kama wameshindwa kuisaidia watoke, sisi tutaanza tena ziro. Haiwezekani leo hii nchi inakaa gizani, lakini wao wanatuburuza kwa ajili ya mafuta ambayo wanayo, lakini wanajua tutaiyumbisha nchi hii ikae katika aibu. Kulikoni Tanzania? Watanzania je, ni lini Mwenyezi Mungu atatupa roho za kurudi kwenye uzalendo na kuiangalia nchi yetu na kuweza kuisaidia nchi yetu? Kwa kweli nimefikia mahali ambapo nashindwa hata jinsi ya kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nasema nasikitika, naunga mkono hoja kwa vile bado ni mzalendo wa Tanzania. Ahsante Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Viwanda. Zaidi ya hapo, namshukuru Mungu pia ambaye amenipa uzima na ametupa uzima wote na ndiyo maana tuko hapa tunaweza tukatoa michango yetu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza katika Wizara hii, nataka nizungumzie kidogo kuhusu Kiwanda cha Nyama cha Mbeya *(Tanganyika Parkers)*. Kiwanda hiki kimejengwa miaka karibu 30 iliyopita au 40 iliyopita, wakati Mwalimu anatawala nchi hii mpaka leo hii hakuna hata ng’ombe mmoja amewahi kuchinjwa pale, lakini mabilioni ya pesa yamemwagwa pale kwa ajili ya kujenga kiwanda. Serikali wala haina mpango wowote!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kusoma hotuba ya Waziri wa Fedha, nikaangalia tena kwenye Mpango wa Miaka Mitano, lakini inaonyesha kwamba katika Mpango wa Miaka Mitano hakuna utaratibu wowote ambao unazungumzia kuhusu kufufua kiwanda kile. Kiwanda kile kimekaa zaidi ya miaka 30 pale na wanalinda tu na mapesa yanazidi kumwagwa pale kwa sababu kuna watu ambao wanalinda kiwanda. Sasa najiuliza, Serikali ina mpango gani wa kufufua kiwanda kile? Naomba nipate jibu kwa sababu katika hotuba ya Waziri Mkuu pia nilizungumzia kuhusu kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua pale Mbeya kinajengwa kiwanja kikubwa cha ndege. Nafikiri Serikali ingekuwa na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinafunguliwa, kinaanza kuzalisha na kutoa nyama ambayo pengine kwa kutumia kiwanja kile wangeweza kusafirisha nyama kupeleka nchi za nje. Lakini mpaka sasa sijajua kwamba Serikali ina mpango gani. Kwa hiyo, naomba labda Waziri atakapokuwa anahitimisha hotuba yake, basi anieleze kwamba Serikali ina mpango gani wa kufufua kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hekta zaidi ya 600 ambazo zinakaa bure, ziko *idle*, watu wangeweza kulima na hata hivyo, wananchi wanajaribu kwenda kuomba kulima pale, lakini bado wananyimwa. Kama Serikali haina mpango wa kufufua kiwanda hiki, yale mashamba wapewe wananchi walime. Kuna haja gani kukaa miaka na miaka? Kama katika Mpango wa Miaka Mitano hakipo, sasa mashamba haya yanakaa bure, kwa nini yasizalishe? Kwa hiyo, naomba, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha aniambie kuhusu masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili au mchango wangu wa pili ni kuhusu Wakala wa Vipimo. Mwaka jana katika Bunge lililopita, nilikuwa nimejaribu kulieleza Bunge kwamba kumekuwa na malalamiko makubwa sana kuhusu kufungasha vyakula katika makontena, kwa mfano, magunia. Imeonekana kwamba Serikali imeshindwa kusimamia hatua hii kwa sababu watu wanafunga malumbesa katika viazi, katika mahindi, katika mkaa na vyakula kadha wa kadha. Naomba niiulize Serikali inatoa tamko gani kuhusu mambo ya lumbesa kwa sababu limewaumiza sana wakulima na wananchi wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Serikali walitoa taarifa, wakatoa tamko lakini halifuatwi, ni kitu gani kinafuata baada ya hapo? Naomba suala hili la Wakala wa Vipimo, wawe makini kuhakikisha kwamba mazao yetu ambayo yanalimwa hapa yasiwe ya kuwaumiza wananchi. Wanapakia kwenye vifurushi bila hata mpango wowote, wala hamna kilo zinazohesabika. Hakuna nchi yoyote Duniani inaweza ku-*pack* vyakula namna hiyo jamani. Unaenda *South Africa*, Botswana, Namibia na wapi, kuna mpango maalum, wanaweka makontena maalum, vyakula vinawekwa na vinapimwa kwa kilo lakini vyakula vyetu, wananchi wetu, wakulima wetu wanateseka vibaya sana. Gunia moja wanaongeza zaidi ya theluthi ya vyakula ambavyo vinatakiwa viwekwe mle ndani, jamani, tunawasaidia wakulima au tunawachezea wakulima? Naomba kwa hilo kwa sababu nilipokuwa nimeongea na Waziri wa Kilimo, akasema kwamba suala la viwango au vipimo ni suala ambalo linahusu Wizara ya Viwanda, lakini na wenyewe pia wanahusika. Mimi nafikiri mtakaa kwa pamoja na kisha mtoe tamko ambalo kwa kweli litawasaidia wakulima wasinyang'anywe mazao yao hivihivi tunaangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la tatu ambalo naomba niliongelee, nalo niliwahi kuliongelea. Nashangaa kuona kwamba bei ya *cement* Mbeya ambako inazalishwa (Tembo) iko juu zaidi kuliko *cement* ya Tembo ambayo inauzwa hapa Dodoma! Wale watu wanaathirika na vumbi na *cement* inasafirishwa mpaka hapa, lakini bei ya hapa iko chini. Naomba Serikali inieleze ni kwa sababu gani bei ya *cement* Mbeya iko juu zaidi kuliko hapa Dodoma au na maeneo mengine. Hiyo ni pointi namba tatu na naomba Serikali inijibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne ni kuhusu ununuzi wa pareto. Tulipokuwa tunaanza miaka miwili iliyopita, wanunuzi walikuwa wengi, ilikuwa ununuzi holela na bei ya pareto ilikuwa juu sana lakini mwaka huu nasikia kwamba, kwa taarifa ambazo wananchi wangu wananipigia simu, amepewa mnunuzi mmoja tu ambaye yeye ndiye anaye-*determine* bei na bei ya pareto imekuwa chini kuliko ambavyo walikuwa wanauza mwaka jana, ni kwa sababu mnunuzi yupo mmoja. Naomba Serikali inieleze pia katika soko inakuwaje mambo haya yanakuwa hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba niliongelee hapa ni kuhusu sukari. Mimi kwa miaka zaidi ya thelathini sijawahi kuona sukari ya Tanzania, nikija Dar es Salaam ndiyo naona sukari ya Tanzania inauzwa hapa, lakini huko Mbeya kwetu, Sumbawanga na sehemu zingine sukari yote inatoka Zambia, Malawi ndiyo ambayo nimezoea kununua, sijawahi kununua sukari inayotoka Tanzania kwa miaka zaidi ya thelathini.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua sukari ya Malawi na sukari ya Zambia hata leo hii ukienda hutakuta sukari ya Tanzania inauzwa Mbeya lakini kitu ambacho kinanisikitisha ni kwamba hawa watu ambao wanaleta sukari wanavyofukuzana na watu wa *TRA.* Kuna wauzaji wadogowadogo wanakwenda kuchukua sukari kule, lakini wamekuwa na msuguano mkubwa sana na *TRA*. Sijajua ni kwa nini Serikali inashindwa kufanya utafiti wa kuweza kuwaruhusu hawa watu hata kama ni wafanyabiashara wadogowadogo walete sukari, ambao kwa miaka yote sisi ndiyo tunapata sukari kutoka kwao, nashangaa kwa nini Serikali hawajafanya utafiti. Je, hakuna watu wanashughulika na mambo hayo kuliko kuendelea kufukuzana na hawa wafanyabiashara wadogo? Ni afadhali Serikali iweke uhuru lakini uhuru huo uwe unatoa vibali ambavyo vitasaidia wafanyabiashara wadogowadogo waingize sukari kwa wingi hapa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itusaidie vijana hawa wapewe vibali vya kuleta sukari ili mradi tu wapite katika njia ambazo ni nzuri. Nashangaa kwa nini wasifanyiwe hivyo kwa sababu ni uhuru, kuliko tukaacha sukari labda inaagizwa na watu wakubwa, lakini hawa wadogo wanachukua sukari Zambia, Malawi, wanatuletea na sisi ndiyo ambayo tumekulia, hata leo mtu

wa Mbeya ukimwambia sukari ya Tanzania atakuwa anakushangaa tu maana hawaijui. Mimi nikiishiwa sukari naenda Kasumulo, nanunua sukari yangu, naenda Tunduma pia nachukua sukari yangu naileta pale nyumbani tunatumia lakini sukari ya Tanzania sijui Mtibwa, sijui Kilombero sijui TPC, hatuijui.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefanya kazi *TPC* miaka mitano, nilikuwa msimamizi wa mambo ya *irrigation* pale, sukari wakati ule ilikuwa inazalishwa sana, lakini sasa baada ya miaka mingi sijaona tena sukari inakuja. Kwa hiyo, naomba Waziri atusaidie kujibu kuhusu tatizo hili la sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba katika Wizara hii ya Viwanda ni kwamba, Mbeya tulikuwa na viwanda vingi sana, kulikuwa na Kiwanda cha Zana za Kilimo, kulikuwa na Kiwanda cha Sabuni, *Hisoap*, ambacho sasa hivi sijui mwekezaji gani ameweka pale kama ghala tu la kutunzia vitu vyake, lakini *Hisoap* nao wametoa vitu vyote pale. Naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda vile? Ni kweli kwamba pengine tumeacha kwa ajili ya kubinafsisha, watu binafsi wachukue, lakini kama hatua hizo zimeshindikana kwa nini Serikali isiwe na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinafufuliwa na vinazalisha, kwa sababu kuna majengo, mashine na kila kitu. Mashine zinakufa, kila kitu kinakufa na hakuna kitu kinachoendelea, kwa nini Serikali isisaidie?

Mheshimiwa Naibu Spika, zana za kilimo zingeweza kuzalishwa kwa wingi sana Mbeya na zilikuwa zinatusaidia sana kwa wakulima hasa wa Nyanda za Juu. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Viwanda na Biashara atusaidie kueleza kwamba je, kuna mpango wowote wa kufufua viwanda vile au ndiyo vimekufa? Sasa hivi nakumbuka tulikuwa tunazungumzia mambo ya kuwaachia watu binafsi, kwa kweli hawa watatupeleka pabaya sana. Naomba Serikali iwe makini kuhakikisha kwamba mambo haya mengine ni lazima iyachukue, huwezi ukaacha kila kitu, mwisho tutakufa hapa. Watu huko nje wanatusikiliza kwa hamu sana kwa sababu wanataka kujua kwamba Serikali na Wabunge wanasema nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hoja lakini nikiwa na matumaini kwamba Serikali itatoa majibu ambayo yataridhisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Simwoni Mheshimiwa Mpina, sasa nitamwita Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine atajaribu kutumia dakika zitakazokuwa zimebaki.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Awali ya yote, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuagiza mafuta, lakini pia kwa namna ambavyo imekubaliana na mawazo ya Wabunge kwamba makampuni haya ya mafuta yaweze kutoa mafuta ili Watanzania wasiendelee kuteseka.

Mhehsimiwa Naibu Spika, napenda pia niipongeze Serikali kwa kupitia Wizara ya Viwanda kwa kusajiliwa na *GS1 (Global Standard One).* Kusajiliwa huku kwa kunazipa utambuzi bidhaa zetu za Tanzania, kwa hiyo *Barcode* yetu ambayo tumepata ni rahisi sasa kwa mtu yeyote aliyepo nje ya nchi au mtu yeyote kuangalia *details* za bidhaa ambazo zinatengenezwa Tanzania. Naipongeza sana Serikali kwa kupata *Barcode* kwa sababu wananiambia zamani ilikuwa wanaenda kununua *Barcode* ya Kenya au ya South Africa. Baada ya kupata *Barcode* yetu ni vema sasa iwe kama kichocheo kwa ajili ya Watanzania kuzalisha bidhaa zaidi na naomba pia watumiaji kama *TCIA* ambao ndiyo wadau wakubwa, *CTI* na wengineo, lakini pia wakulima wanaozalisha bidhaa kwa mfano kahawa, chai na wenyewe wapewe elimu wafahamu *GS1* ni nini. Itakuwa ni vizuri sana iwe kama changamoto kwao kuweza kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ambayo Wizara hii imepewa kwa kweli ni kidogo, shilingi bilioni 30 ni kidogo na hasa kwa sababu Wizara hii inabeba Wizara zingine zote, kwa sababu kilimo bila biashara kitakuwa hakina tija, uchukuzi bila kwenda kwa namna ya biashara itakuwa haina tija na hata uwekezaji. Kwa hiyo, kwa vile bajeti hii ni ndogo sana, Serikali iangalie ni namna gani tunaweza kuinusuru ili iweze kusimamia hizi idara zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali pia kwa kuja na mpango wa *EPZ*, mfumo huu unaweza kweli kuvutia *Foreign Direct Investment* lakini sasa *EPZ* tumetenga maeneo ambayo mengi yanahitaji fidia kwa wale wananchi waliopo kwenye maeneo hayo. Maeneo mengi pia hatujaanza kutengeneza miundombinu, naiomba Serikali kwa sababu mpango wa *EPZ* ni mpango ambao unaweza kweli kubadilisha uchumi wa nchi kwa njia ya ajira lakini pia kwa njia ya kipato na kwa njia ya kodi kwa Serikali, itilie mkazo katika hili ili tuweze kurekebisha kwa kuweka miundombinu kwa ajili ya kuweza kubadilisha uchumi wetu.

Mhehsimiwa Naibu Spika, *EPZ* inaweza pia kusaidia katika kulitimiza soko la *AGOA* ambalo tunalo muda mrefu na hatujaweza kulitimiza. Yapo pia masoko ambayo ni *Prime* ambayo yanatengeneza bidhaa muhimu kwa mfano bidhaa za michezo kama *Reebok*, Adidas. Viwanda hivi vikiwepo kwenye *EPZ*, vikitengeneza bidhaa kama hizo na *quality* ile ambayo inatakiwa, kwa uhakika tutakuwa tumetengeneza ajira kwa Watanzania lakini pia na kipato kwa nchi ya Tanzania. Watanzania wanahitaji ajira na Serikali inahitaji fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yalipobinafsishwa Watanzania wote tuliamini kwamba wale watu waliooneshа nia wanaweza kabisa kuendeleza yale mashirika, kitaaluma na kifedha, lakini kumbe sivyo. Wengi waliochukua viwanda kwa mfano Kiwanda cha Magunia Mkoani Kilimanjaro, Kiwanda cha Ubungo *Garments*, Kiwanda cha Morogoro *Ceramics*, *Steel Rolling Mills* kilichokuwa Tanga, lakini pia kuna Kiwanda kama Morogoro *Shoe*, viwanda hivi vyote malighafi zake kwa sehemu kubwa zinaweza kupatikana Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Morogoro Shoe tunasema tuna mifugo ambayo ni nusu idadi ya Watanzania wote yaani milioni kama ishirini. Morogoro *Ceramics* pia tunaambiwa kwamba Singida inawezekana kuna madini kabisa ambayo yanaweza kupatikana kwa ajili ya kutengeneza *tiles*. Pia hata tukisema magunia kwamba yalikuja magunia ya *jute* kwa hiyo magunia ya katani yakakosa soko, lakini tungeweza pia kutengeneza kwa ajili yetu sisi wenyewe, tunalima mahindi mengi Ukanda wa Kusini, ambapo pia magunia haya tungeweza kuyatumia. Tukiangalia pia kiwanda cha *TANGOLD*, tunasema kipo chini ya Wizara ya Kilimo, lakini ukiangalia magari yaliyopanga foleni Namanga Arusha kwa ajili ya kupeleka matunda haya Kenya, chungwa likienda Kenya asubuhi, jioni unaambiwa limefika Frankfurt lakini Watanzania wangeweza kabisa kufanya biashara hii.

Mhehsimiwa Naibu Spika, naomba sasa *Consolidated Holding Corporation* ambao ndiyo wameshikilia mikataba ya viwanda hivi wako wapi na wanafanya nini na mikataba hiyo mbona wamekaa nayo kimya? Wale ambao hawakutimiza masharti au hawakufufua hivi viwanda kwa nini mikataba isipitiwe upya na viwanda hivi vikaingia mikononi mwa Serikali na wawekezaji wanaoweza Watanzania au watu wa nje wanaoweza wavichukue kwa ajili ya kuviendeleza. Nimesema tena kwamba Watanzania wanahitaji ajira lakini na Serikali inahitaji kodi na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri pia Serikali ianze sasa kulinda bidhaa zetu na viwanda vyetu. Vipo viwanda kwa mfano Kiwanda cha Kibo Match kilichopo Kilimanjaro, Kiwanda cha *TPC* kinachotengeneza sukari, Mtibwa Sugar na Kagera, vipo viwanda vingi ambavyo tunaweza tukavilinda, kwamba tupunguze uagizaji wa bidhaa hizi kutoka nje. Zipo nchi nyingi kwa mfano Malyasia ambao wanalinda viwanda vyao, kwa hiyo kama kuna bidhaa ambazo viwanda vinatengeneza nchini basi ile bidhaa haiagizwi kutoka nje. Nadhani umefika wakati sasa Serikali ilinde viwanda vyake na hata ikiwezekana Bunge hili Tukufu linaweza likatunga Sheria ambayo inazuia bidhaa nyingine kuingia nchini kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu.

Mhehsimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kui-*support SIDO. SIDO* ni shirika ambalo linasaidia sana wajasiriamali, wanatengeneza bidhaa nyingi lakini pia wanatoa mafunzo ya aina nyingi na mojawapo ni mafunzo ya usindikaji wa mazao mbalimbali ambayo yanafanywa sana na wajasiriamali wadogowadogo na hususani wajasiriamali wanawake. Mimi naamini kabisa kwamba mafunzo haya ndiyo yanasaidia lakini mafunzo peke yake bila mashine itakuwa ni vigumu. Naomba Serikali iliangalie hili kwamba kama kweli tunataka tuwasaidie hawa wajasiriamali wasindikaji waongeze thamani katika kile wanachotengeneza, iweze kui-*support SIDO* ili iweze kuwasaidia hawa wajasiriamali. Tukumbuke kwamba wajasiriamali wetu Tanzania

watashindana na wajasiriamali wengine kutoka Afrika ya Mashariki na kwa hivyo soko litakuwa la ushindani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze *Fair Trade Competition.* Wamekuwa wanadhibiti bidhaa feki na nimeona nyingine wanachoma. Naomba waendelee kusaidiwa ili waendelee na kazi hiyo kwa kasi kubwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni *TFDA* wanaodhibiti dawa feki, naomba tafadhali waendelee lakini pia na *TBS* naomba na wao waendele kwa ajili ya ku-*check quality* ya vitu ambavyo vinatengenezwa na viwanda vyetu lakini na vingine ambavyo vinaagizwa kutoka nje.

Mhehsimiwa Naibu Spika, mara nyingi najiuliza mbona simu au bidhaa fulani zinatengenezwa pale China na ukienda Marekani kila kitu unakuta ni Made in China, lakini ile *product* ya *Made in China* iliyopo Marekani ni tofauti kabisa na iliyopo hapa kwetu. Ni nzuri kabisa na wala haiharabiki hovyo, lakini ukija Tanzania *product* hiyohiyo ya Kichina siku mbili inaharibika. Nataka kuamini kwamba inawezekana siyo biashara pekee isipokuwa kuna mikataba ambapo kuna makubaliano kwamba viwanda hivi visitengeneze bidhaa feki. Naomba Serikali ya Tanzania kama tunaweza hivyo na sisi tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee jambo la mwisho kwamba tunajiunga katika Soko la Afrika ya Mashariki na naomba Maafisa Biashara wa Wilaya na hasa ile Mikoa ambayo inapakana na hizi nchi kama Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kigoma, wapewe elimu, waende wakatangaze hizi fursa za soko hili kwa wanakijiji, waondoke Maofisini waende vijijini kuwaeleza Watanzania soko la Afrika Mashariki lina faida gani na fursa gani ambazo zipo. Wakenya wanabeba machungwa, wanabeba maparachichi, matunda haya inawezekana kabisa kubebwa na kuuzwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Betty Machangu. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, lakini nitamwomba atumie dakika kumi nina shughuli kidogo na zile dakika tano za mwisho, jitahidi kutumia dakika kumi.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, natoa shukrani kwa Wizara na Waziri husika pamoja na Naibu Waziri kwa kuandaa bajeti ambayo kwa kiasi fulani inaweza ikakidhi haja au isikidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hapo, naomba niweke jambo moja wazi ambalo nilikuwa nimeliombea Mwongozo. Jana kilichotokea, nilikuwa naenda Nyamongo kuangalia mambo ambayo yanafanyika kutokana na ule mgodi, lakini nilipopata taarifa kwamba Mwekezaji ndiye amekodi zile ndege kuwapeleka Wabunge pale nilikataa. Kwa hiyo, sikuachwa na nilisema kabisa kwamba niliacha kwenda makusudi kwa sababu Mwekezaji yule anawanyanyasa na kuwaonea wananchi wa Tarime kitu ambacho ni kinyume cha Sheria na ningepanda hizo ndege ningekuwa nimewasaliti wananchi wa Tarime, lakini wananchi wa Tarime ninawapa ahadi kwamba lazima huyo Mwekezaji atatekeleza yale yote ambayo aliyaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba kuchangia hoja, nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Wizara hasa Waziri kwa sababu ya kutambua umuhimu wa kutumia nembo za mstari *Barcodes.* Kama wenzangu waliotangulia walivyosema. Hizi *Barcodes,* nashauri zitumike haraka iwezekanavyo ili kutambulisha bidhaa za Tanzania hususani Tanzanite yetu inayozalishwa kutoka Mkoa wa Arusha lakini inaonekana kwa kiasi kikubwa kwamba inatoka Kenya na Afrika Kusini, naomba jambo hilo lifanikiwe kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimuulize Waziri anayehusika kuhusu viwanda vilivyopo Tanzania ambavyo vimeuzwa na kubinafsishwa. Je, ni vingapi vimeuzwa, vingapi vimebinafsishwa, vingapi vimo mikononi mwa Serikali na vinafanya nini na vitainuaje uchumi wa Tanzania? Je, kuna mkakati gani wa kuinua viwanda vya ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niongelee suala la *EPZA* hasa katika Wilaya ya Bunda, kijiji cha Tairo ambapo ekari elfu tatu zimechukuliwa. Ekari hizi elfu tatu ni za wafugaji. Kaya zaidi ya mia nne haziendelezi hayo maeneo kwa sababu walishalipwa fidia nusu ambapo fidia ilikuwa zaidi ya shilingi bilioni mbili, malipo ambayo yalishalipwa hadi sasa ni shilingi bilioni moja na mengine bado. Sasa wakulima wale na wafugaji wanashindwa kuendeleza maeneo yao. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inawalipa fidia halali wale wafugaji wa Bunda wa Kijiji cha Tairo ili hilo eneo litumike kwa ajili ya *EPZA?*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sisi Wilaya ya Tarime tumebahatika kupakana na nchi ya Kenya ambayo kwa kiasi kikubwa ina viwanda vidogovidogo kama ambavyo tunavyoviita hapa Tanzania *SIDO*. Nimemwomba Waziri mara nyingi tu kwamba afike Tarime aangalie fursa ambayo anaweza kuitumia tukaanzisha viwanda vidogovidogo. Sasa Waziri atakapokuwa anajibu hoja hii atuambie ni lini atafika Tarime na kuangalia namna tutakavyoweza kushirikiana kuanzisha Viwanda vidogovidogo ili kuwasaidia wakulima hususan wale wanaolima mazao ya chai, tumbaku, kahawa pamoja na ndizi. Kuna uwezekano mkubwa kwamba tukaanzisha kiwanda cha juice, mvinyo na kadhalika. Hii ni pamoja na Wilaya ya Serengeti ambayo kwa kiasi kikubwa inategemea mazao ya kilimo katika kujipatia riziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile pamoja na mambo yote ambayo tunazungumzia hapa mimi naamini kabisa kwamba Watanzania ni wajasiriamali na wanajitahidi kwa kiasi kikubwa kufanya biashara hata ukitembea katika baadhi ya nchi kama Dubai, ukienda China, ukienda sasa hivi Turkish wengi sana wanafanya biashara lakini elimu ya biashara hawana. Mimi naishauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu ihakikishe kabisa kwamba somo la biashara linafundishwa kuanzia Darasa la Tano mpaka Vyuo Vikuu hii itasaidia zaidi Watanzania kujiajiri na naamini kabisa kwamba itawawezesha kufanya biashara ya uhakika pasipo kudhulumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Mkoa wa Mara kuna Kiwanda kikubwa cha Nguo kilichokuwa kinaitwa *MUTEX*. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu aniambie hatma ya kiwanda hicho kwa sababu hicho ni Kiwanda kikubwa cha Nguo kilichokuwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, sasa pale yamebaki magofu tu hayana kitu na sijui hatma yake ni nini. Naomba tufikiri zaidi kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika hebu tuangalie namna ya kufanya biashara hususan katika nchi yetu tuna makabila mengi ambayo tunaweza tukaanzisha *cultural tourism*. Katika nchi nyingine ukienda kwa mfano South Africa hata Kenya watu wanaingiza hela nyingi sana kupitia hii *cultural tourism*. Sasa sisi Watanzania tuna mbuga, tunachonga vinyago vya kila aina mfano vya wanyama, naomba tuangalie namna tutakavyowezesha vijana wetu hasa wale wa Kimasai waanzishe hii *cultural tourism* iwasaidie kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kitu kimoja kwamba katika nchi yetu ya Tanzania biashara au bei ya bidhaa mbalimbali zinapangwa na mzalishaji au muuzaji. Mtu anaweza akaenda China akanunua simu kwa dola 20 akifika hapa anaipiga shilingi 200,000. Ni kwa nini katika nchi yetu ya Tanzania hatuna Tume ya Bei? Hilo suala naomba Mheshimiwa Waziri alifikirie, tuangalie ni kwa nini katika nchi ya Tanzania hatuna Tume ya Bei. Kila mtu anajipangia tu anavyotaka. Hili suala kwa kweli linahitaji tufikiri zaidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie *TBS*. Mimi nimeshangaa kwa mfano wale wanunuzi wa magari, wakishanunua magari Dubai yakikaguliwa kule Dubai mtu analipa dola 150 lakini ukifika Tanzania kama umeagiza gari kutoka Dubai au Japan bila kulifanyia ukaguzi ili upate *certificate* kwa Tanzania unalipa asilimia 20 ya *value* ya gari lile. Nashangaa ni kwa nini hiyo? *TBS* ipo kwa makusudi ya kuwaumiza wafanyabiashara au kuwatetea? Naomba hilo Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuchangia kuhusu bandari ya Dar es Salaam ambayo ingeweza kutumika kuwainua wafanyabiashara lakini matokeo yake wafanyabiashara wananyanyasisika, wanaonewa, wakileta mizigo yao inachukuliwa kwenda kutunzwa kwenye

magodauni ya Wahindi. Kwenye yale magodauni ukifika pale unaweza ukalipa bandarini dola 200 lakini bidhaa zako zikipelekwa kwenye magodauni ya Wahindi unalipa dola mara tatu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kupewa majibu ya uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyambari Nyangwine kwa mchango wako. Kesho baada ya maswali tutaendelea na uchangiaji wa Wizara hii.

Nina matangazo yafuatayo. Wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Inspector General wa Polisi aliahidi kugawa vipeperushi kwa Waheshimiwa Wabunge wote vinavyoelezea kampeni inayoendelea sasa ya kushawishi utii wa sheria bila kushurutishwa ili kudumisha amani, usalama na utulivu nchini. Kutokana na ahadi hiyo, Ofisi ya Bunge iliona ni vema kumpa nafasi *IGP* ya kukutana na Waheshimiwa Wabunge na kutoa maelezo ya ziada kuhusu kampeni hiyo ambayo imeonyeshwa kwenye vipeperushi hivyo. Hivyo basi nawafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba *IGP* atakutana nanyi kesho saa 7.20 katika Ukumbi wa Pius Msekwa ambapo *IGP* atatumia muda wa saa moja kuwaelezea Waheshimiwa Wabunge juu ya Kampeni hiyo. Waheshimiwa Wabunge wote tunakaribishwa na kesho tutawakumbusha pia.

La pili, tulipata maombi ya kufafanua miongozo minne naomba basi Chini ya Kanuni ya 68(1) na (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 nitoe ufafanuzi ya baadhi ya mambo yaliyoombwa kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, leo wakati wa kipindi cha asubuhi cha majadiliano ya Bunge, nilipokea maombi ya Mwongozo wa Spika kutoka kwa Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Ismail A. Rage na Mheshimiwa Idd M. Azzan na Mheshimiwa January Makamba jambo ambalo tumeshalishughulikia.

Nikianza na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, yeye namnukuu aliyoyasema. Alisema:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wanatakiwa kutoa uthibitisho juu ya kauli zao wanazozitoa. Kwa mfano, mimi kuna kauli niliyoitoa tarehe 04/7/2011 hapa Bungeni nikatakiwa kuthibitisha na nilifanya hivyo kwa kuzingatia matakwa na masharti ya Kanuni za Bunge.*

*Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujua, Mbunge anapothibitisha kauli yake anahitaji kusubiri kwa muda gani ili Ofisi ya Spika iweze kumpatia uthibitisho kuhusiana na kauli yake?"*

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu kuhusu jambo hilo ni ufuatao:-

Kanuni ya 63(6) inaelekeza kwamba "*Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni, atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, papo hapo au katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili ya kufanya hivyo"*

Vilevile, Kanuni ya 68(4) inaelekeza kwamba, *"Spika anaweza, ama papo hapo kutoa Uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu au kuahirisha Uamuzi ili alifikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi baadaye."*

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kwamba, kutokana na Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli aliyoitoa Bungeni kuwa na wajibu wa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, Spika pia ana wajibu, baada ya kupokea uthibitisho huo kutoka kwa Mbunge Mhusika, wa kujiridhisha kuwa uthibitisho husika ni wa kiwango cha kuliridhisha Bunge. Kwa sababu hiyo na kwa kutumia busara zake, Spika ameahirisha kutoa Uamuzi kuhusu suala la Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, kwa kufuata masharti ya Kanuni ya 68(4), ili aweze kulifikiria zaidi jambo hilo, kwa maana ya kujiridhisha kuwa uthibitisho husika ni wa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hakuna Kanuni yoyote inayoweka muda wa Spika kutoa Uamuzi wake. Hata hivyo, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, hana haja ya kuwa na hofu

yoyote; Spika yuko safari lakini wakati muafaka atalitolea Uamuzi suala lake baadaye, kama Kanuni hiyo inavyoelekeza.

Suala la Mheshimiwa Idd M. Azzan, ninanukuu amesema:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, Kanuni ya 68 (7). Tarehe 3 na 4/8/2011 wakati wa mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Uchukuzi, mambo mengi yalizungumzwa, likiwemo suala la uuzwaji kinyemela wa hisa za Shirika la Usafiri Dar-es-Salaam, yaani UDA. Serikali ilitoa tamko kuhusu hatua zilizochukuliwa, lakini cha kushangaza, tarehe 5 Mstahiki Meya wa Jiji la Dar-es-Salaam alifanya kikao na Waandishi wa Habari na katika maelezo yake amenukuliwa akitamka kwamba Waheshimiwa Wabunge wameshindwa kufikiri kwa kutumia akili na badala yake wanatumia makalio yao kufikiri. Kauli hiyo si kwamba tu imewadhalilisha baadhi ya Wabunge, bali pia imelidhalilisha Bunge Zima. Kwa kuwa huo ni ukiukwaji wa kinga na haki za Bunge, naomba Mwongozo wako kwa jambo kama hilo"*

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu**,** masharti ya Ibara ya 100(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sura ya 2 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania inayoweka kinga na haki za Bunge na Wabunge, inaelekeza wazi kuwa, *"uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge haupaswi kuvunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge." (Makofi)*

Vilevile, Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania, Toleo la 2002, imetamka wazi kuwa:-

"*There shall be freedom of speech and debate in the Assembly and such freedom of speech and debate shall not be liable to be questioned in any court or place outside the Assembly."*

Aidha, Kanuni ya 71 ya Kanuni za Bunge imeweka utaratibu mzuri kuhusu haki ya raia wasio Wabunge, ya kujitetea na kujisafisha dhidi ya kauli zinazotolewa na Wabunge Bungeni. Kanuni hiyo inaelekeza, pamoja na mambo mengine kwamba:-

*"Mtu yeyote asiye Mbunge ambaye atajisikia kuwa amekwazwa au amepata athari hasi kutokana na kauli au maneno au shutuma zilizotolewa Bungeni kumhusu yeye binafsi anaweza kupeleka malalamiko pamoja na maelezo yake ya kujitetea kwa Spika".*

Kwa kuzingatia ufafanuzi huo na ili niweze kujiridhisha pasipo mashaka yoyote kwamba suala hili linahusu kinga na haki za Bunge, nimeamua, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 68(5), kulipeleka kwenye Kamati ya Madaraka, Maadili na Haki za Bunge ili iweze kulichunguza na kulishauri Bunge hili ipasavyo kuhusiana na jambo hili. *(Makofi)*

Mwongozo wa mwisho, ni wa Mheshimiwa Ismail A. Rage naomba kumnukuu kama ifuatavyo:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa zimeandikwa katika vyombo vya habari leo kwamba, Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikwenda North Mara kwa kufadhiliwa na ndege za Barrick. Naomba nipate Mwongozo wako kwamba je, utaratibu huo ni sahihi? Kama si sahihi, ilikuwaje hata Waziri wa Mazingira naye akawemo kwenye msafara huo? La kushangaza zaidi, Mbunge anayetoka Tarime akaachwa uwanja wa Ndege. Inakuwaje? Naomba maelezo."*

Mwongozo wangu Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 68(4) na (7), nimeona ni busara niahirishe Mwongozo wangu kuhusu suala hili ili nilifikirie zaidi na kuutoa hapo baadaye. Mwongozo huu umetolewa Bungeni leo Jumanne tarehe 9 Agosti, 2011.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, napenda kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12. 32 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 10 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)*